Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 24 Julai, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika, (Mhe.Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Mtumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 245

**Ukosefu wa Mafuta ya Gari la Ukaguzi wa Shule Wilayani Ngara**

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

Wilaya ya Ngara yenye shule za msingi zipatazo 114 imekuwa haitembelewi kwa muda mrefu na wakaguzi wa Idara ya Elimu kwa sababu ya gari lao kukosa fedha za mafuta ya kuzungukia shule hizo:-

Je, ni lini Serikali itaipatia Idara hiyo ya Elimu fedha za mafuta ili shule hizo ziweze kukaguliwa na kuwa na elimu bora?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Aloys Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, hutenga fedha katika Bajeti yake ya kila mwaka kwa ajili ya ukaguzi wa shule. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti, fedha hiyo imekuwa haitoshelezi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Ukaguzi wa shule ilitengewa kisasi cha shilingi 6,270,837,656 kama fedha za matumizi mengineyo. Hata hivyo, kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 3.85 tu ambapo shughuli za ukaguzi zilipata kiasi cha shilingi 248,601,393.60 ambacho kiligawanywa katika Halmashauri 133 na Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha huo huo 2011/2012 Idara ya Elimu ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilikagua shule za msingi ishirini na nane (28) kati ya 114 ambapo jumla ya shilingi 3,100,000/= zilitolewa kwa ajili ya ukaguzi na ununuzi wa matairi ya magari. Kwa msingi huo, kiasi cha fedha kinachotengwa na kutolewa hakitoshelezi kukamilisha ununuzi wa mafuta ili shule zote ziweze kukaguliwa kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya ukaguzi wa shule kadiri ya upatikanaji wake kutoka Hazina.

Aidha, kwa sasa Wizara yangu imeandaa andiko ambalo litawezesha Idara kuwa Wakala ili kuimarisha shughuli za ukaguzi. Nachukua fursa hii kuziomba Halmashauri zote nchini ziendelee kusaidia shughuli za ukaguzi wakati Serikali ikiendelea kujizatiti kuimarisha ubora wa elimu nchini.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Mheshimiwa Spika, tunaposema kiwango cha elimu kimeshuka Tanzania, moja ya sababu kubwa ni hiyo ya kwamba shule nyingi hazikaguliwi. Idara ya ukaguzi Ngara ina gari, lakini halina mafuta na gari hilo linatumiwa na Idara za Halmashauri ambazo zina mafuta. Ni lini Wizara itaona umuhimu wa Idara hii ya Ukaguzi ambayo lengo lake ni kuhakiki ubora wa elimu inayotolewa mashuleni na ikiwezekana kutumia pikipiki wakati wa kiangazi?

(b) Ni lini Wakala huo utaanzishwa yaani *executive agency* kwa ajili ya kuboresha ukaguzi na kuondoa matatizo ambayo yameanza kujitokeza ambapo Wakuu wa shule za *private* wanasajili vijana ambao hawakushinda kuingia *form one* ili wajipatie fedha? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deogratias Aloys Ntukamazina, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa shule zimekuwa nyingi yapata shule za msingi sasa ziko 16,001 na idadi ya wakaguzi iko pale pale takribani miaka mitano iliyopita, shule za sekondari ziko 4367, shule hizi ukizijumlisha kwa pamoja na Idara ni ile ile zimekuwa ni shule nyingi sana, ndiyo maana Wizara sasa imeamua Serikali kwa pamoja sasa kuwa na andiko la kubadilisha hii Idara ya Ukaguzi kuwa Wakala ili ijitegemee iweze kufanya kazi vizuri sana.

Lakini suluhisho hilo si kwamba ndiyo inapelekea sasa ubora wa elimu nchini kushuka kama ulivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kabisa huko Mikoani na Mawilayani na mimi natembea sana naona kabisa ubora wa elimu unashuka. Lakini si kwa sababu tu shule

hazikaguliwi ni sababu tu ya hata ya uaminifu wa Wakuu wa Shule na uaminifu wa wazazi pamoja na wanafunzi. Yamejitokeza matatizo mbalimbali hata ya wizi wa mitihani wote tunayaona. Lakini nataka niseme kwamba leo asubuhi nilikuwa naangalia taarifa ya habari, nimeona hata kule Mwanza Kanda ya Ziwa Mkaguzi Mkuu wa Kanda amebaini, tulimwagiza watembelee shule Wakaguzi Wakuu wote wa Kanda kubaini wanafunzi wanaoingia sekondari bila kufaulu na wengine wanaingia hata bila kuwa na *selection* kutoka kwa Afisa Elimu wa Mkoa. Tumeagiza Kanda zote zituletee na tayari Kanda ya Ziwa wameanza na leo tumepata hiyo taarifa.

Wakuu wa Shule sio waaminifu na ndiyo maana hata nilipokwenda kule Kigoma nikawaweka ndani na kesi ziko Mahakamani na hapa naahidi kwamba hata huko Mwanza nitakwenda kuchukua hatua zinazoweza kustahiki ili fundisho hili liweze kuwafikia Wakuu wa Shule nchini, wasiweze kufanya mambo ya ajabu kama haya. Kwa hiyo, tusisingizie tu Idara ya Ukaguzi kwamba haitembelei lakini hata uaminifu wa wazazi, wanafunzi na uaminifu wa Wakuu wa Shule. *(Makofi)*

**MHE. GOSERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa iliyokuwa Wilaya ya Karagwe imegawanywa kuwa Wilaya mbili Wilaya ya Karagwe pamoja na Kerwa na Wakaguzi ambao wako pale Karagwe hawana gari wala mafuta na kwa kuwa hotuba ya Waziri wa Elimu inakuja tarehe 14 na 15 mwezi wa nane.

Je, kwa nini Mheshimiwa Waziri asitenge fedha ya dharura kwa ajili ya kuangalia Wilaya hizi mbili za Karagwe na Kerwa?

**SPIKA**: Haya anatenga kutoka Bajeti gani? Haya Naibu Waziri jibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Ni kweli Wilaya zimeongezeka na hivi Bajeti za ukaguzi vile vile zimeongezeka na si kwa Wizara ya Elimu tu nadhani ni Wizara zote kwa ujumla kwamba kila Wizara imeongeza Bajeti kwa ajili ya Mikoa kuongezeka na Wilaya kuongezeka. Hata sisi Serikali kwenye Wizara ya Elimu, tumeongeza Bajeti mwaka huu maana yake ili Idara ya Ukaguzi iweze kufanya kazi, tunahitaji kuwa na bilioni 13.6 na mwaka jana kama nilivyosema kwamba tulitenga bilioni 6.3, mwaka huu tumeongeza fedha ili angalau Halmashauri zote ziweze kukaguliwa hata hizo zilizokuwa zimeongezeka.

Kwa hiyo, nina matumaini kwamba Karagwe na Kerwa nao watapata mahitaji maalum ya ukaguzi katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha. (*Makofi*)

**SPIKA**: Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Naibu wa TAMISEMI, Elimu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake mazuri yanayohusu hasa kitengo cha Ukaguzi ambacho kwa kweli ni muhimu kwenye sekta yetu ya elimu.

Kumeulizwa suala la Kitengo cha Ukaguzi kuwa na magari yaliyoko kwenye Halmashauri zetu na bado hayana huduma wakati Wizara ya elimu inajipanga vizuri na kitengo hicho, Ofisi ya Waziri Mkuu tumeendelea kutoa maagizo kwa Wakurugenzi wote nchini kwa kuwa magari yale yako kwenye Halmashauri zetu na magari yale pia yanatumika pia kwenye huduma za Halmashauri kwa ujumla wake bado Wakuregenzi wanatakiwa wahudumie magari ya Wakaguzi, waweke ratiba nzuri ya Idara ya Ukaguzi ili Idara ya Ukaguzi iweze kufanya kazi ya ukaguzi kwenye shule zetu ziweze kupata mafanikio.

Bado hilo tunalisisitiza na Wakurugenzi tulishawaagiza na bado tunasisitiza waendelee kuhudumia magari yale ili Kitengo cha Ukaguzi kifanye kazi yake wakati Wizara ya Elimu ikijipanga vizuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 246

**Madai ya Walimu na Upungufu wa Vifaa Mashuleni**

**MHE. SUSAN A. LYIMO** aliuliza:-

Elimu bora inapatikana kama kuna walimu, wanafunzi na vitendea kazi kama maabara madawati, chaki na vitabu.

(a) Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu upungufu wa vitendea kazi katika shule nyingi nchini?

(b) Kwa kuwa walimu ndiyo kichocheo kikubwa cha elimu yote. Je, kwa nini bado wanadai malimbikizo yao licha ya kauli ya Mheshimiwa Rais ya kutaka walipwe?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikikabiliana na changamoto ya upungufu wa vitendea kazi kadri hali ya fedha inavyoruhusu; kwa mfano mwaka 2011/2012 Seriklai ilipeleka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kiasi cha shilingi bilioni 20,891,703,247 kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika shule za sekondari ikiwemo ukarabati wa shule kongwe 63 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.2, ununuzi wa maabara hamishika kwa gharama ya shilingi bilioni 3 na ujenzi wa hosteli kwa gharama ya shilingi bilioni 14.6.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huo huo wa 2011/2012 Seriklai kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imefanikiwa kujenga miundombinu ya shule yenye thamani ya shilingi bilioni 30 zikiwemo nyumba za walimu 614, vyumba vya madarasa 1,801, maabara 127, vyoo 1,916 na madawati 185,218. Vile vile katika mwaka huu, mwaka wa fedha 2012/13, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II), imetenga jumla ya shilingi bilioni 56.3 kwa ajili ya kukamilisha miundombinu muhimu ya shule 264 zikiwemo maabara, maktaba, madarasa, nyumba za walimu, vyoo na kuweka umeme. Aidha, Serikali imewaelekeza wakuu wa shule kutumia asilimia 50 ya fedha za ruzuku ya uendeshaji (*Capitation Grand)* kununulia vifaa kama vitabu na kemikali kwa ajili ya maabara za shule za sekondari.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la swali namba 205 la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, tarehe 16/07/2012, kwamba zipo changamoto nyingi zinazokabili ulipaji wa malimbikizo ya madai mbalimbali ya walimu zikiwemo:-

(c) (i) Walimu kuchelewa kutuma madai yao hivyo kulazimika kusubiri mwaka wa fedha unaofuata;

(ii) Baadhi ya walimu kutowasilisha vielelezo muhimu kama vile fomu za madai, stakabadhi, tiketi, hati za kuzaliwa na hati za ndoa na barua za kukubali madaraja na kadhalika pamoja na barua za kuripoti kituo kipya; na

(iii) Lakini vile vile baadhi ya vielezo kuwa na dosari za kiuhasibu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kulipa madeni mbalimbali ya walimu kadri yatakavyowasilishwa baada ya kufanyiwa uhakiki.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika,ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Pamoja na majibu hayo, nilikuwa naomba kuliza maswali mawili.

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba bado kuna upungufu mkubwa sana wa walimu hususani maeneo ya pembezoni lakini hata Mijini kuna tatizo kubwa sana la walimu wa shule za msingi pamoja na wa sekondari.

Lakini hivi karibuni mwezi wa tatu, Wizara imetoa *secular* kwamba wale wanaotaka kujiunga na uwalimu *certificate* wawe na pointi 27 wakati siku za nyuma ilikuwa ni *division four* lakini ya pointi 28.

Tangazo hili limekuja wakati tayari matokeo ya kidato cha nne mwaka 2011 yameshatoka na wanafunzi hao walijua kabisa wangeweza kujiunga na vyuo hivyo suala ambalo limepelekea vyuo vingi hususan vile vya *private* kukosa wanafunzi na hapa ninapoongea kuna vyuo ambavyo vilikuwa vipate wanafunzi kama 500 lakini sasa hivi wana wanafunzi 30 tu. Je, Mheshimiwa haoni kwamba *secular* hiyo ni kutowatendea haki wahitimimu wa mwaka jana?

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii inahusika na elimu na elimu tunajua ndiyo suala muhimu sana katika nchi yeyote ile. Lakini mwaka jana kuna baadhi ya wanafunzi wamemaliza darasa la saba, wamefaulu kwenda shule za sekondari, lakini wamegundulika kwamba hawajui kusoma wala kuandika na wala kuhesabu. Nilikuwa naomba kujua, kwa kuwa Wizara hii ndiyo inasimamia Baraza la Mitihani, ni sababu zipi zilizopelekea wanafunzi hawa kufaulu wakati hawajui kusoma wala kuandika? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nitangulize kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa na naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

(a) La kwanza ni kuhusu ufaulu wa wale ambao wanahitaji kwenda kuchukua *course* ya uwalimu. Ni kweli tumepandisha mwaka huu imefikia pointi 27 badala ya *cut off* ya point 28 ya mwaka jana na tumefanya hivyo kwa sababu kazi hii ni muhimu sana.

Taifa hili litaweza tu kufanikiwa ikiwa itaweza kuzalisha wananchi ambao wamesoma vizuri na tunataka walimu ambao wenye sifa ili kuweza kuingia darasani hatutoweza kuchukua wale ambao wameshindwa katika masomo yao ndiyo wawe walimu wa watoto wetu, hata kule Kijijini kwetu, jimboni Bagamoyo kuna mtu anauliza wewe hata uwalimu umekosa?

Maana yake kwamba walimu ndiyo ambao unachukua mtu ambae ameshindwa kila kitu, hapana. Kwa hivyo, tutaendelea kuongeza daraja la ufaulu kwa wale wanaokwenda kujifunza uwalimu mpaka tufikie kiwango ambacho wanaokwenda kujifunza uwalimu ni wale ambao wana uwezo huo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hili halitaleta athari kwa sababu, wale wenye madaraja ya juu kwa mfano daraja la 25, 26 mpaka hiyo 27, safari hii ambao wameomba ualimu ni karibu ni karibu 16,000 na nanafasi ambazo tunazo ni katika Vyuo vya Ualimu ni 5,000 na kidogo.

Hamna namna ambayo, tungewaacha hawa waliofaulu madaraja ya juu, tukaenda tukachukua wale ambao wamefaulu madaraja ya chini kwa hiyo, tutaendelea, tutakazia hapo hapo na tutaendelea kuboresha madaraja ya wale ambao wanahitaji kwenda kwenye kazi hii ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Wanafunzi wa Darasa la Saba, ambao wamekutwa kwamba, hawajui kusoma na kuandika; hii ni kadhia kubwa, inatusikitisha mno. Kama Mheshimiwa Naibu Waziri, alivyozungumza kabla wakati najibu maswali, inatokana na matatizo kadhaa na makubwa ni ya uaminifu, walimu, wazazi na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hawa ambao wanaambiwa wameenda *Form One,* hawajui kusoma na kuandika, kubwa ni kwamba, wameingia kwa njia za udanganyifu kama wale wanafunzi 9,000 ambao tumewafutia nafasi ya kuendelea kwenda *Form One.* Wamepata nafasi ambazo sio za halali yao. Tumechukua hatua ya kuhakikisha kwamba, tunahakiki, tujue ni wepi hao na hilo

limeingia mikingamo mikubwa, kiasi kwamba, mpaka hivi sasa hatujaweza kutoa kauli ya kuweza kuwaondosha kabisa wale ambao wamegundulika hivyo.

Mheshimiwa Spika, tuseme ni wachache. Mimi mwenyewe nimeenda katika shule zile walizoambiwa hawajui kusoma na kuandika, nikawakuta kumbe kusoma anajua, kuandika anajua, lakini kiwango chake hakifanani na mtu wa *Form One.* Kwa hiyo, sio kwamba, hajui kabisa kusoma wala hajui kuandika. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Na. 247

**Sera ya Michezo Nchini**

**MHE. IDDI M. AZZAN** aliuliza:-

Sera pamoja na Sheria ya Baraza la Michezo ya Mwaka 1972 kwa pamoja, vimepitwa na wakati:-

(a) Je, ni lini Sera ya Michezo itawekwa sawa?

(b) Je, ni lini Sheria ya Baraza la Michezo Tanzania itahuishwa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Iddi Azzan, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali katika Mwaka huu wa Fedha 2012/2013, inatarajia kukamilisha mchakato wa marekebisho ya Sera ya Maendeleo ya Michezo Toleo la mwaka 1995.

Wakati tukianza mchakato huo Wizara yangu, ilipata kujua kwamba, wadau wengi walipo Mikoani na Wilayani, walikuwa hawaifahamu vyema Sera ya maendeleo ya Michezo na Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kugundua mapungufu hayo, Wizara yangu ilichukua hatua za makusudi za kuwashirikisha wadau wa michezo katika Mikoa na Wilaya, katika kuwaelimisha kupata maoni na mapendekezo yao kuhusu maendeleo ya michezo kwa ujumla hapa nchini, kupitia Mijadala iliyoendeshwa katika Wilaya na Mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, hivi sasa tumefikia hatua nzuri ambapo Wizara imekamilisha Rasimu ya mwisho ya Sera na Rasimu hiyo, itawasilishwa kwenye Vyombo vya Uamuzi wakati wowote kuanzia sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya baraza la Michezo la Taifa *(BMT)* ya Mwaka 1967 na Marekebisho yake katika Sheria Namba 6, ya Mwaka 1971, mchakato wake umekwishaanza kwa kuainisha maeneo yenye mapungufu na pia kupokea maoni kutoka kwa wadau.

Hata hivyo, mchakato huo, utakamilika rasmi mara baada ya kukamilika kwa marekebisho ya Sera ya maendeleo ya Michezo, ili kuepuka mkinzano kati ya Sera na Sheria.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza nioneshe tu masikitiko yangu makubwa juu ya majibu ya Waziri, majibu haya, yamekuwa yakijirudia kila mwaka. Tumeanza kuomba Marekebisho ya Sera tangu mwaka 2006 na kila mwaka Wizara, inakuja na majibu haya haya. Kwa kweli, amenisikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tu sasa Waziri, atueleze hiyo Sera ambayo wamepeleka kwenye vyombo vya juu, ni lini itawasilishwa kwenye vyombo vya uamuzi, ili tujue? Kwa sababu,

hapa amesema tu itawasilishwa; ni lini sasa itawasilisha kwenye vyombo vya uamuzi wa hiyo Sera?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ningependa kufahamu pia, ni wadau gani ambao mmewashirikisha? Kwa sababu, kusema tu mmekwenda kwenye Wilaya na Mikoa, haileti maana na wala siyo kweli. Sasa niambie ni wadau gani mmewashirikisha kwenye suala hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu Maswali Mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Idd Azzan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka tu nimhakikishie kwamba, nia ya Serikali, ya kufanya marekebisho ya Sera ya Michezo, iko palepale na ninataka niseme tu kwamba, tayari kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi ni kwamba, tumekutana na wadau na tayari tunataka kupeleka katika *Secretariet Cabinet,* ili kufikisha jambo hili katika Baraza la Mawaziri na hatimaye lipate uamuzi na litarudishwa tena kwa wadau na Kamati na hatimaye Bungeni, tuweze kukamilisha suala hili ambalo limechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nilitaka nimhakikishie tu kwamba, ni kweli, Wizara, kupitia *BMT,* tumeshakutana na wadau. Mathahalan, tayari ma-*DAS,* Wilaya zote, wamekutana na Viongozi wa Vyama vya Michezo, Maafisa wa Michezo katika Wilaya zote, ma-*DAS* wote. Ma-*RAS* wote wameshakutana na ma-*DED* wote na Viongozi wa Vyama vya Michezo.

Lakini pia *BMT,* imeshafanya mijadala na vyama vya michezo mara tatu (3), kuanzia mwaka 2009 Septemba, Mei 2010 na Aprili, 2012, *BMT* imekutana na Vyama vya Michezo. Lakini zaidi, *BMT,* imekutana na Wizara ya Afya, Jeshi la Polisi na Wadau mbalimbali na Vyama vya Michezo, katika kushughulikia jambo hili.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa, Serikali, imerudisha Sera ya Michezo Mashuleni na tumeona mbali na kwamba, imerudi Sera ya Michezo Mashuleni, imekosa hamasa kutokana na matatizo ya Bajeti. Sasa je, Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ikishirikiana na Wizara ya Elimu, imejipanga vipi kuhakikisha michezo mashuleni inarudi kama ilivyokuwa zamani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali, imeweza kurudisha sasa hivi michezo katika Shule za Msingi na sekondari. Ni kweli kwamba, Wizara ya elimu na wizara yangu, zitaendelea kushirikiana kuona kwamba, tunaendeleza michezo. Lakini pia, jambo hili ni lazima litafsiriwe pia katika Bajeti.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tu, leo ndio tunawasilisha Bajeti. Basi, muipitishe, ili tuweze kuendeleza michezo vizuri zaidi.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, baadhi ya Wasanii wetu au Wanamichezo wetu nchini, hupenda kuiga Wasanii wa Marekani, hata wale ambao hawakubaliki nchini humo. Sasa Serikali, inachukua jukumu gani la kuwaelimisha wasanii wetu nchini, ili waweze kuzingatia maadili yetu na kuboresha Michezo na Usanii wa aina yoyote?

**SPIKA:** Wizara ni ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa hiyo, swali la mwanzo lilikuwa la michezo. Haya.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la dada yangu Leticia Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba, ni kweli, yanajitokeza mambo hayo ambayo Wasanii wetu wengine wanaiga utamaduni ambao si utamaduni wetu na kupotoka katika maadili. Nataka kusema tu kwamba, tushirikiane. Sisi kama Serikali, tutaendelea kutoa Miongozo, kuona kwamba, Wasanii wetu, hawaigi tamaduni ambazo hazipo katika maadili yetu ya Kitanzania.

Na. 248

**Visima Virefu na Vifupi Vinavyochimbwa Kutokutoa Maji**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Visima Virefu na Vifupi, vinavyochimbwa na Serikali, havidumu kwa kutoa maji kwa mwaka mzima:-

Je, Serikali, inasemaje katika hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji chini ya ardhi hutegemea aina ya miamba, kiasi cha mvua kwa mwaka na urefu wa visima katika eneo husika. Visima vinavyochimbwa kwenye miamba aina ya mchanga na miamba yenye mipasuko, hutoa maji mengi.

Visima vinavyochimbwa kwenye miamba ya mchanga uliochanganyika na udongo wa mfinyanzi, mchanga laini na miamba migumu yenye mipasuko kiasi, hutoa maji ya wasatani. Wakati visima vinavyochimbwa kwenye miamba migumu, isiyo na mipasuko, hutoa maji kidogo au havitoi maji kabisa.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa sababu za visima vifupi kutokuwa na maji wakati wote wa mwaka, ni pamoja na:-

(i) Visima hivyo kuwa na vina vifupi kama mita 15, ambavyo mara nyingi huwa na maji yaliyovia *(recharged)* eneo dogo, kipindi cha mvua.

(ii) Mapungufu katika kubaini eneo linalofaa kuchimbwa visima na uchimbaji kufanyika wakati wa kipindi cha mvua.

(ii) Kuongezeka kwa matumizi ya maji, hasa wakati wa kipindi cha kiangazi.

(iv) Matumizi mabaya ya pampu za maji; na

(v) Visima kutopata matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya visima vinavyochimbwa kutopata maji Serikali, imeelekeza mambo yafuatayo kuzingatiwa wakati wa uchimbaji wa visima:-

(i) Wataalam kufanya utafiti wa kina kubaini miamba yenye maji ya kutosha;

(ii) Kuchimba kisima cha uchunguzi chenye kipenyo kidogo cha inchi 4, ili kuona kama sehemu inayochimbwa ina maji yakutosha;

(iii) Visima vifupi vinavyochimbwa visipungue kina cha mita 15; na

(iv) Visima kufanyiwa majaribio ya uwezo wa kutoa maji *(pumping test)* baada ya uchimbaji kukamilika.

Visima virefu vilivyochimbwa na kufanyiwa majaribio na kubainika kuwa na maji ya kutosha, huwa havikauki kipindi cha kiangazi.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ninapenda tu kutoa shukrani kwa Naibu Waziri, kwa majibu yake ya wazi kabisa yanayoonesha jinsi gani Wataalam wetu, wanavyokuwa wazembe katika kutafuta haya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; kwa vile basi, kumejitokeza hivyo ndani ya Halmashauri zetu ninaamini. Kwa nini, sasa kusiweko agizo kutoka Serikalini, kwamba, kila Halmashauri sasa, ifanye sense ya hivyo visima ambavyo havitoi maji kwa sababu, ni uzembe wao, wavifufue kwa gharama zao kwa kila Halmashauri? Swali langu hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili. Wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Maji, Waziri, alizungumza kwamba, Wataalamu, wale Wataalamu wenye kuijua miamba halisi ya maji, wapo, lakini ni wachache. Je, Serikali, sasa inaweza ikawabaini hawa Wataalam, kuwa wazi kwetu ndani ya Bunge hili, ili tuweze basi, kuwagawa walao kimkoa, ili kusaidia tatizo hili kupungua? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu Maswali Mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maria Hewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Maria Hewa, kwa namna anavyofuatilia miradi hii ya maji, inayogusa wananchi wengi, hasa pale alipoamua kuliondoa swali lake aliposafiri na kwamba, liulizwe yeye mwenyewe akiwepo ili aweze kuuliza maswali ya nyongeza. Tunampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa agizo kwamba, Halmashauri zifanye sensa na pale itakapoonekana kwamba, uzembe ulifanyika, wanaohusika wachukuliwe hatua na kwa gharama zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba, hili tumelichukua. Wakati wa Bajeti yetu tulisema kwamba, sisi wenyewe kama Wizara, tutafanya ziara kutembelea visima vyote ambavyo vimechimbwa kwenye Halmashauri, ili kujionea hali halisi.

Lakini pamoja na hayo, tunakubaliana kwamba, Halmashauri zifanye sensa na pale itakapoonekana kuna uzembe ulifanyika, zichukuliwe hatua kama ilivyofanyika kwenye Wilaya ya Muheza, ambapo yule Mkandarasi, alichimba kisima kwenye eneo ambalo halikuainishwa kwenye utafiti wa awali. Halamashauri, inamchukulia hatua za kumwajibisha, ikibainika kwamba, ni kweli, aweze kutumia gharama zake kuchimba kwenye eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu kwamba, wataalamu ni wachache; ni kweli Wataalamu ni wachache, lakini kwa sasa hivi tunachopenda kuagiza ni kwamba, wale Wakandarasi, wanaokuwa wamepewa kazi za kuchimba visima kwenye Halmashauri, watumie Ofisi zetu za Mabonde ya Maji, ambazo ziko chini ya Idara ya Rasilimali za Maji. Kwenye Ofisi zile, kunakuwa na takwimu mbalimbali zinazohusu tabia na mienendo ya maji katika yale maeneo.

Mheshimiwa Spika, na kwenye Ofisi zile, wanatakiwa Mkandarasi anapokuwa amepata kazi, kabla hajaanza ile kazi kwenye ile sehemu, ni lazima zile Ofisi zetu za mabonde ya Maji, zitakagua uwezo wa yule Mkandarasi. Zitakagua uwezo kitaalamu na zitakagua uwezo wa vifaa, baada ya hapo, ndipo atakapoanza kuchimba.

Sasa akishaanza kuchimba, bado Ofisi zetu za Mabonde ya Maji, zinatakiwa zifuatilie mwenendo mzima wa uchimbaji hadi wakati wa kutoa maji. Hata baada ya kutoa maji, wanatakiwa wapime na Ofisi zetu ziridhike.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya hayakuzingatiwa awamu ya kwanza. Lakini suala la kuweka mkazo kwa kupata Wataalamu, hili tunalichukua kwa ajili, ya kufanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Kanda ya Ziwa, miaka 10 iliyopita kulikuwa na Mradi wa *HESAWA.* Mradi huu, zaidi ulichimba visima vifupi na hasa katika Wilaya ya Magu. Visima hivi sasa vimekauka na wananchi wanahangaika sana na maji.

Mheshimiwa spika, Je, Mheshimiwa Waziri, atakubaliana na mimi kwamba, Mradi huu wa *HESAWA* ulikuwa umeshindwa? Na kwamba, Waziri, yuko tayari kuja katika Wilaya ya Magu, ajionee shida iliyopo kubwa pamoja na shida ya maji katika mji mdogo wa Magu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Nyongeza, la Mheshimiwa Dkt. Festus Bujiku Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunakubali mualiko wake wa kwenda kutembelea Jimbo la Magu, ili kujionea hali halisi ya maji katika Kanda ya Ziwa Viktoria. Lakini pili, hiyo miradi, kama tulivyosema kwenye jibu la msingi kwamba, huenda wakati wa uchimbaji wa vile visima vifupi, vilichimbwa chini ya kiwango kinachotakiwa, kwa maana ya chini ya mita 15 wakati zinatakiwa mita 15 mpaka 30. Lakini inawezekana vilevile utafiti wa kina, haukufanyika.

Mheshimiwa Spika, ndio maana tunasema kwamba, wale wote ambao watakuwa wamepewa nafasi hizo hivi sasa, wafuate maelekezo ambayo tumeyaeleza kwenye jibu la msingi. Lakini vilevile, kwa upande wa Kanda ya Ziwa, tuna miradi mikubwa sasa ya maji ambayo inahusisha kutoa maji ziwa Viktoria na kuyapeleka maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la Magu. *(Makofi)*

Na. 249

**Kukamilika kwa Mradi wa maji wa Benki ya Dunia – Bahi**

**MHE. OMARY A. BADWEL** aliuliza:-

Karibu Wiloaya zote nchini ikiwemo Wilaya ya Bahi, zinatekeleza Mradi wa Maji wa Vijiji kumi wa Benki ya Dunia Mradi huo umechelewa sana kukamilika hadi sasa na hata visima vilivyochimbwa vimekosa maji:-

(a) Je, ni lini Serikali inawaahidi wananchi wa Bahi, juu ya kukamilika kwa mradi huo?

(b) Je, ni nini hatma ya visima vilivyochimbwa na kukosa maji katika Vijiji hivyo, kupitia mradi wa Maji wa Benki ya Dunia?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mradi wa Vijiji 10 Wilaya ya Bahi, Visima vilichimbwa katika vijiji 8 ambapo maji yalipatikana katika vijiji 4 vya Nondwa, Chiguluka, Mchito na Chimendeli. Kijiji cha Nkhulugana, kina kisima ambacho kitafanyiwa ukarabati.

Hivi sasa Halmashauri ya Bahi, inakamilisha taratibu za kumwajiri Mkandarasi aliyepitishwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye vijiji vilivyopendekezwa. Utekelezaji katika hatua ya kwanza, utaanza katika Vijiji vya Nondwa na Mchito na utakamilika katika Mwaka huu wa Fedha 2012/2013.

Aidha, ujenzi wa Miundombinu kwenye vijiji vilivyopata maji, lakini havipo kwenye hatua ya kwanza, miradi yake itatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha katika hatua inayofuata ya Programu.

(b) Mheshimiwa Spika, takwimu za utafiti zinaonesha eneo la Kiji cha Mnkhola, halina maji ya ardhini. Pia, visima vilichimbwa katika Vijiji vya Babayu, Mndemu, Ibhiwa na Nguji, lakini havikupata maji.

Hivyo, utafiti wa kina zaidi, utafanyika katika awamu ya pili ya program ya maendeleo ya Sekta ya Maji, kubaini vyanzo vingine vya maji ndani au nje ya Vijiji hivyo na uwezekano wa matumizi ya teknolojia nyingine, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini miongoni mwa Vijiji alivyovitaja ambavyo havikupata maji, kipo Kijiji cha Mndemu, ambacho sasa tumepata chanzo kipya cha maji cha Mzakwe, ambacho kipo karibu na Kijiji hicho.

Lakini katika utekelezaji wa mradi huo katika vijiji kumi ziko fedha zilizobaki ambazo Halmashauri ya wilaya ya Bahi ilikuandikia barua Mheshimiwa Waziri kukuomba tutumie fedha hizo kwa ajili ya kutoa maji katika hiki chanzo cha Mchito cha Mzakwe kwenda katika kijiji cha Mndemu. Lakini takribani mwaka mmoja umepita sasa Wizara yako haijatoa majibu kwamba inakubali au vipi tutumie hizo fedha.

Je, sasa Wizara yako iko tayari kutukubalia kutumia fedha hizo ili kutoa maji kutoka chanzo cha Mzakwe kwenda kijiji cha Mndemu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze jinsi alivyofuatilia suala hilo la maji ambapo amewasiliana mpaka na Mamlaka ya Maji Dodoma kuona namna ya kuwasaidia wananchi wake wa Bahi.

Lakini kuhusu suala hili lililoongelewa la kutoa maji kutoka Mzakwe kwenda Mndemu ni kwamba chanzo cha maji cha Mzakwe kipo chini ya Mamlaka ya Maji ya Dodoma na wilaya hii waliandika barua kuomba na Mamlaka ya Maji Dodoma imewaruhusu kutumia kile kisima.

Sasa kitu ambacho ningemshauri Mheshimiwa Mbunge, sasa tusiangalie barua kuchelewa kujibiwa au vipi tuone tunafanya nini sasa hivi kwenye *sealing* yao ya mwaka huu inaonyesha kwamba wana bilioni 1,700,000,000 wakati *sealing* ya awamu ya kwanza ilikuwa ni milioni 869.

Kwa hiyo, ni wazi kwamba kuna milioni 864 za nyongeza. Kwa hiyo ningemshauri kwamba kwa kutumia ruhusa ya mamla ya Maji Mjini Dodoma kwamba watumie kile kisima watumie hiyo nafasi kutoa maji kutoka Mzakwe kupeleka Mndemu na gharama za kutoa pale ni milioni 306 ambazo zitabaki nyingi tu kutoka zile milioni 800. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIEL WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona, ni kweli kwamba visima vingi vilivyochimbwa kwenye vile vijiji havikufanikiwa kutoa maji na ikiwemo Jimboni kwangu, Jimbo la Nyamagana.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni muda muafaka kwa jimbo la Nyamagana sisi ambao tuko karibu na Ziwa Victoria kwenye vijiji ambavyo waliainisha kuchimba visima kama Wanyema kule Fumagira, Igoma. sasa tuletewa maji kutoka Ziwa Victoria kuliko hivi visima ambavyo vimekataa kutoa maji?

**SPIKA:** Kutoka Dodoma kwenye visima vya kuchimba mpaka maji ya Victoria mbali kabisa lakini kwa sababu Waziri anayafahamu haya mambo ajibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama tulivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba visima vingi havikutoa maji na hasa vifupi kwa sababu havikufuata taratibu za uchimbaji kwa maana utaalam haukutumika hazikufuata. Sasa kupanga ni kuchagua tuna mpango wetu wa miaka mitano na tumeshaanza kutekeleza kupeleka maji maeneo mbalimbali ikiwemo kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Shinyanga Kahama, Magu, Bariadi na Meatu. Kwa hiyo, nina uhakika kabisa kwamba hata vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Wenje navyo vitafikiwa kwa awamu yake itakapokuwa iko tayari.

Lakini tunawaomba Halmashauri nao pia wawe na mikakati waviingize kwa kutafsiri ule mpango wa miaka yetu mitano kuhusu suala la maji waone namna ya kuvifikia vile vijiji ambavyo Mheshimiwa Wenje amevisema. *(Makofi)*

Na. 250

**Mkakati wa Chakula cha Kutosha Nchini**

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, Mkoa wa Shinyanga umeathirika kwa miaka mitatu mfululizo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mkao wa Shinyanga hauendelei kuwa ombaomba wa chakula?

(b) Je, Serikali itachimba mabwawa mangapi katika skimu zilizopo Shinyanga?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa naiba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hilali Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mkakati wa Serikali wa kuwa na chakula cha kutosha kutokana na mahitaji katika soko la ndani ni pamoja na:-

Kuiwezesha *NFRA* kununua tani 200,000 za nafaka katika msimu wa ununuzi wa mwaka huu wa 2012/2013 kutoka kwa wakulima mikoa iliyozalisha ziada, kwa maana ya Rukwa, Iringa, Mbeya na Ruvuma kuhamisha tani 100,000 za akiba ya nafaka iliyopo kwenye maghala yenye ziada ya chakula kwenda maghala ya mikoa yenye ziada ya chakula kwenda kwenye maghala yenye upungufu wa chakula.

Hatua hiyo itaiwezesha Serikali kukabiliana na upungufu wa chakula na mahitaji mengine ya soko kwa haraka zaidi na pia itatoa nafasi ya kuhifadhi nafaka zitakazonunuliwa msimu wa ununuzi wa 2012/2013 na kuhimiza wakulima kujiwekewa akiba ya chakula cha kutosha kwa ajili ya mahitaji ya kaya zao na kuuza ziada tu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imejipanga kutekeleza mkakati wa makusudi unaolenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kama mtama na uwele, mazao ambayo yanahimili ukame.

Mkakati huu utahusisha wilaya na tarafa ambazo zina historia ya ukame na mahitaji ya misaada ya chakula mara kwa mara. Hatua hizi ni pamoja na kuelekeza kwa kiwango kikubwa zaidi pembejeo za ruzuku kwa maana ya mbegu bora, mbolea na madawa katika maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na Mkoa wa Shinyanga kuwa mkoa wa Kame, ambao hauna mito ya kudumu, Serikali imekuwa ikiendeleza kilimo cha umwagiliaji mkoani humo kwa kutumia teknolojia ya kuvuma maji wakati wa mvua.

Kwa kutumia mfumo huu tayari zimeanzishwa *scheme* sita ambazo zinaendeleza kilimo cha umwagiliaji nyakati za mvua.

Aidha ujenzi wa mabwawa umefanyika pale ambapo sura ya ardhi kwa maana ya *land topography* inafaa.

Mheshimiwa Spika, kati ya *scheme* zilizopo *scheme* ya Masengwa peke yake ndiyo yenye eneo ambalo sura ya ardhi inafaa kwa ujenzi wa bwawa. Tayari usanifu wa bwawa hilo umekamilika na Serikali imetenga fedha za kuanza utekelezaji katika mwaka wa 2012/2013.

Maeneo mengine mawili yameabainishwa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa katika *scheme* mpya za Isholollo na Ngagamulwa. Kazi ya usanifu wa mabwawa hayo imekamilika chini ya mradi wa *DASIP* na inaendelea katika hatua ya zabuni kumpata mkandarasi wa kuyajenga mabwawa hayo.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa hata zao la Uwele na Mtama limekuwa likiathiriwa kwa kiasi kikubwa cha ukame uliopo Mkao wa Shinyanga. Kwa kuwa hali ya hewa ya Wilaya ya Kahama inaonekana kuwa nzuri kwa kilimo.

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuiwezesha wilaya ya Kahama kuweza kulima kwa wingi ili Wilaya ya Kahama iweze kulisha mkoa wa Shinyanga kwa ujumla?

Kwa kuwa wanawake wengi wa mkoa wa Shinyanga wamekuwa wakikimbiwa na waume zao wakati wa tatizo la chakula kama sasa hivi.

Je, Serikali inawasaidiaje wanawake hawa ambao wamekuwa wakibaki na familia wakihangaika kwa muda mrefu pasipo kusaidiwa na Serikali wakati waume zao wamewakimbia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Kikija chakula wanarudi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze na hili la pili la wanawake wanaokimbiwa na wanaume Wakisukuma. Mimi nadhani kama ulivyosema hili jambo kusema kweli ni jambo ambalo nadhani wenzetu jana wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto walikuwa wanalizungumzia ni jambo ambalo katika tabia hii halitakiwi tu linatakiwa likemewe tu na lipatiwe ufumbuzi kwa sababu huk wanakokwenda.

Je, inakuwaje, anatafuta mwanamke mwenye chakula?

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani hili ni jambo tu ambalo wanakimbia majukumu yao na kusema kweli tutaanza kuwakemea pia wanaume wa Kisukuma waliomo humu humu ndani Mheshimiwa Spika kwamba nao wakawaambie wenzao siyo tabia nzuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la kwanza kuhusu uwele na mtama, nadhani hili ametoa pendekezo Mheshimiwa Azza ni pendekezo zuri sana kwamba Kahama ijikite kuwa kama Wilaya ya chakula kwa Wilaya ya Kahama na Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Azza, mkakati huu Mkoa wa Tanga umefanya, Mkoa wa Tanga umeamua kwamba Handeni na Kilindi zi-*focus* ziwe wilaya za chakula.

Kwa hiyo, uongozi wenyewe wa mkoa kwenye *RCC* umejipanga hivyo umeleta taarifa kwenye wilaya na sisi tumekubali. Kwa hiyo, na sisi tunapeleka pembejeo mbolea bora na kadhalika na tuna *focus* kwenye zile wilaya mbili kwa ajili ya kulisha Mkoa wa Tanga wote.

Kwa hiyo, mimi nafikiri nimelipokea hili lakini namwomba Mheshimiwa Azza na wenzake wa Mkoa wa Shinyanga kwamba lianzie Mkoa wa Shinyanga nitakuja Mkoa wa Shinyanga tukutane na viongozi wa mkoa ili tuangalie namna ya kuifanya Kahama iwe kama ni *break basket* ya mkoa wa Shinyanga.

**MHE. RACHEL R. MASHISHANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Manispaa ya Shinyanga kuna mradi wa umwagiliaji katika eneo la Mambosheli, nilikuwa naiomba Wizara haioni sasa umefika wakati wa kuchimba bwawa katika eneo hilo ili mradi huo ukaendelea vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Mkoa wa Shinyanga kwa bahati nzuri kwa sababu ya hali ya ukame imekuwa inafanyiwa kazi na *analysis* ya muda mrefu. Hii kazi ya kufanya *land topography* kwa maana ya kupiga picha yale maeneo yameshafanywa na sasa hivi kuna *scheme* sita lakini tatizo la Mkoa wa Shinynga, ni kwamba mito yake inayoleta maji kwenye *scheme* ni mito ambayo inakauka. Kwa hiyo, ni *delicate* kidogo *analysis* yake.

Lakini nimelikubali hili naenda kuwapa wataalam waliangalie kama *analysis* kwenye tathmini hii ya kufanywa kama bwawa hili linaweza kutafutiwa fedha na kazi kwa sababu ziko namna nyingi za kufanyiwa mabwawa, yanaweza yakawa *scheme* za umwagiliaji zinatokana na maji kwa namna mbali mbali kutegemeana na ufanisi wa upatikanaji wa maji. Lakini wacha tukalifanyie kazi.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea na swali linguine muwe mnaangalia muda. Mheshimiwa Khatib Said Haji atauliza swali hilo.

Na. 251

**Msaada wa Mchele Kutoka Japan kwa Tanzania**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Kwa muda mrefu Japan imekuwa ikisaidia Serikali ya Tanzania Mchele kila mwaka:-

(a) Je, msaada huo ulianza kutolewa mwaka gani na kila mwaka tulipata kiasi gani cha mchele na wenye thamani gani?

(b) Je, utaratibu wa kuipa Tanzania Zanzibar mgao wa Chakula hicho ulianza lini na imekuwa ikipata kiasi gani na ni kampuni gani zilipewa?

(c) Taarifa za uhakika zinaonyesha kwamba awali mchele huo uligawanywa kwa mkopo kupitia wafanyabiashara na kampuni zilizoteuliwa na walilipa 30% tu na tulilipa deni lote katika muda maalum. Je, Kampuni zote zimelipa malipo yote, kama hazikulipa ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wahusika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Japan imekuwa ikiisaidia Serikali ya Tanzania mchele tangu mwaka 1979. Takwimu tulizonazo ni kwamba tangu mwaka 1992 hadi 2011 kiasi cha mchele uliotolewa ni jumla ya tani 183,000 wenye thamani ya Yeni kama bilioni 7.7 hivi.

Aidha, kati ya mwaka 1979 na 1990 mchele wa msaada kutoka Japan ulipokelewa na kusambazwa na Shirika la Usagishaji la Taifa la *(NMC Ltd.)* na kati ya mwaka 1991 kampuni ya biashara *Consumer Service (BCS)* lilikuwa shirika la Umma pia nalo lilipokea mchele wa msaada na kuusambaza kwa njia ya mauzo kwa niaba ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuipa Tanzania Zanzibar mgao wa chakula hicho ulianza mwaka 1995 kiasi ambacho Zanzibar imepata hadi mwaka 2011 ni jumla ya tani 7,220. Aidha, kati ya mwaka 1999 na 2005 hakukuwa na mgao rasmi kwa Zanzibar mchele uliopokelewa katika kipindi hicho ulianzwa kwa utaratibu wa zabuni ya wazi ambapo kampuni yoyote kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliruhusiwa kuomba zabuni na kununua na kusambaza mchele huo.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa awali Serikali iliuza mchele kwa mkopo na baadhi ya makampuni yalishindwa kurejesha fedha zote za mauzo. Baada ya kufuatilia madeni hayo bila mafanikio, Serikali iliingia mkataba na kampuni ya kukusanya madeni *(Msolopa Investment Company)* ambayo inaendelea na kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutumia vizuri fursa hii ya msaada wa mchele kutoka Japan kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania na ni matumaini yangu kwamba wafanyabiashara nao watazingatia haya ili kutokuharibu mfumo huu ambao una manufaa kwa Watanzania walio wengi.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Ahsante kwa kuwa Serikali ya Kijapan inatoa msaada wa chakula hiki kwa ajili ya Watanzania. Wakati mwingine au wakati mwingi chakula hiki tunapokipokea kunakuwa na mikoa ambayo inakuwa na ukame na njaa ya kutisha. Kwanini Serikali inaamua kuwauzia wafanyabiashara chakula hiki badala ya kupeleka kwa wananchi moja kwa moja?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali inakiri kushindwa kukusanya madeni kwa makampuni ambayo iliwapatia chakula hiki na makampuni hayo yapo na yanajiendesha kwa ufanisi mkubwa na yanajulikana. Serikali imefikia kuipa kampuni ya udalali ya Msolopa kukusanya madeni hayo.

Je, Serikali haioni kwamba kushindwa kwa Serikali na kuipa kampuni binasi hili ni jambo ambalo linaonekana wazi, Serikali haina nia kufuatilia madeni haya na kurudisha pesa za Serikali katika mfuko wa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba tukubaliane kwamba hizi pesa za Japani zinatoka na mfumo unaotokana na *KR1* ambao una *matching fund* kwa maana ya kwamba ule msaada unapokuja ili mwakani msaada ule uendelee ni lazima Hazina kwenye *matching fund* yake kila mwaka iweke hela ya kiasi fulani ili Wajapan nao waone kwamba kumbe na sisi Watanzania tunataka kuchangia kwenye utaratribu ule. Kwa siyo dezo ile, ile ina pesa fulani na sisi ambazo tunatoa, siyo bure. Sasa namna peke yake ya kuchangia kwenye mfumo huu wa mchele ni kwamba huu mchele ukija uuzwe kwa bei nafuu ili uweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kweli kwamba ziko kampuni na ni, nilitaka nimsahihishe tu hili ziko kampuni nane ambazo zinadaiwa lakini katika hizo ziko na kampuni za Umma nazo ambazo ni ma-*RTC.* Makampuni ya zamani ambayo nayo mengine yalishajifia huko ambayo nayo yanadaiwa.

Kwa hiyo, jumla pana madeni kidogo kiasi kikubwa lakini mwaka huu tulifika hatua ambayo kweli *KR1* kwenda kwenye *KR2* ilikuwa ina matatizo na tuliongea na Hazina na Hazina walitoa pesa kidogo kwa sababu mfumo huu siyo kwenye mchele unaingia pia kwenye pembejeo kwa maana ya mbolea. Lakini pia na kwenye mashine za kilimo kama matrekta na vipawa *tillers. K*wa hiyo, mfumo huu ni mkubwa kidogo lakini unataka na sisi wenyewe kuchangia kiasi fulani cha fedha ili Wajapan waendelee kuchangia.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha Bajeti yake alikiri kwamba mchele unaozalishwa Tanzania ni mchele mzuri sana na umekuwa ukitumika kupelekwa nje ya nchi. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni busara pesa ambayo inapatikana kutoka Japan badala ya kwamba watuletee chakula watuletee pesa ili tuzalishe nchini mchele ulio bora zaidi na tuweze kuuza?

**SPIKA:** Hata sisi tulipokwenda ndivyo walivyokuwa wanataka.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Ni kweli kwamba mchele wetu sisi haswa kama ukipikwa na nazi au na kitu kingine kile ni mchele mzuri sana. Kwa hiyo, ni kweli kabisa kwamba namna yoyote ile bado kwetu ni bora zaidi kuzalisha mchele humo ndani kuliko kuuagiza kutoka nje.

Lakini mwanzoni nilikuwa nazungumzia utaratibu wa *funding* ya *KR1* kwamba una makubaliano wawe wanaleta vifaa vyao na sisi tunachangia na wao wanachangia. Kwa hiyo, ule ulikuwa ni utaratibu wa *KR1.*

Mheshimiwa Spika, lakini tumejipanga pia kwenye utaratibu wa kuendeleza haya mabonde tuliyokuwa nayo, kwa sababu kwa namna yoyote ile bado inaonekana kwamba mchele tunaozalisha sisi *premium* zaidi kuliko mchele unaotoka nje.

Mheshimiwa Spika, yapo mabonde ambayo tumeainisha yanaanzia Morogoro mpaka Iringa mpaka Sumbawanga kwenyewe tumekwenda ambapo tumetenga maeneo haya kwa ajili ya uwekezaji. Lakini uwekezaji unataka sekta binafsi na Serikali tumekubaliana tutaweka hela kidogo ili kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kuongeza uzalishaji wa mchele ambao huo mchele wetu bado ni mzuri sana.

**SPIKA:** Tunaendelea jamani tumetumia dakika kumi kwa ajili ya mchele mtamu. *(Makofi)*

Na. 252

**Leseni za Utafiti wa Madini**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI** aliuliza:-

Leseni za utafiti wa madini zinazotolewa na Serikali huhusisha pia uchimbaji wa madini *(final mining).*

(a) Je, ni madini kiasi gani yameshachimbwa katika tafiti hizo na yamekwenda wapi?

(b) Je, Serikali inatumia mbinu gani kuhakikisha kuwa watu wanaochimba madini hayo hawaondoki nayo, wakati leseni zinazotolewa ni za miaka miwili na ni *renewable?*

(c) Je, Serikali inatumia mbinu gani kufuatilia tafiti hizo ili madini yasiibiwe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a), (b) n a (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, inatoa leseni za utafutaji mkubwa wa madini mbalimbali hapa nchini. Utafutaji huo unalenga kujua kiasi cha mashapoo ya madini yanayoweza kuchimbwa kibiashara. Katika hatua hii ya utafutaji wa madini kinachochimbwa ni kwa ajili ya kuchukua sampuli za udogo, mchanga au mawe ambavyo hupelekwa kwenye maabara ndani au nje ya nchi kwa ajili ya kujua kiwango cha madini katika eneo husika. Utaratibu huu hutumika kote duniani na maabara tulizonazo hapa nchini zinazofanya shughuli hizo ni pamoja na *GST, SEAMIC* na *SGS.*

(b) Mheshimiwa Spika, sampuli za Madini zinazochukuliwa katika maeneo ya utafutaji wa Madini husafirishwa kwa utaratibu wa vibali vinavyotolewa katika Ofisi za Madini zilizoko karibu na eneo la utafiti. Maafisa Madini hukagua sampuli hizo ili kuzihakiki kabla ya vibali kutolewa. Hakuna sampuli au mtu yeyote anayeruhusiwa kusafirisha sampuli za madini au madini ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Mamlaka husika kama Ofisi ya Madini na *TRA.* Hivyo, ikibainika kuwa kampuni au mtu yeyote amefanya hivyo hatua za kisheria zinatakiwa kuchukuliwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Maafisa Madini hufanya ukaguzi wa maeneo ya utafutaji na uzalishaji wa madini wakishirikiana na Wakalawa Ukaguzi wa Madini (*TMAA*) kuhakiki maendeleo ya shughuli hizo ili kudhibiti vitendo vinavyokiuka sheria.

Aidha, kulingana na sheria ya madini ya mwaka 2010 kampuni zinazofanya utafuta wa madini hutakiwa kuwasilisha taarifa kwa ushirikiano wa Wakala wa mwaka na taarifa hizo kuhakikiwa na Wizara kwa ushirikiano na Wakala wa Jiolojia Tanzania (*GST*). Lengo ni kujua kazi zinazofanywa na kampuni hizo.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa nini Serikali isitumie Taasisi zetu kama *STAMICO* au Chuo cha Madini kuwa zinafanya utafiti wa Madini ili mwekezaji anapokuja tuwe tunafahamu kwamba kuna Madini kiasi gani na tunaingia mkataba tukiwa tunajua kuna Madini kiasi gani?

Pili, kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba yapo Madini ambayo huwa yanachukuliwa sampuli na kupelekwa nje ya nchi kwenye maabara. Sasa tunaamini vipi utafiti ule unaothibitishwa na maabara za nje kwenye Madini yanayokuwa yamechimbwa wakati wa utafiti ndani ya nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sisi tunazo maabara ambazo zinafanya uchunguzi na tafiti za madini kama nilivyozitaja kwenye swali la msingi.

Wakala wa Jiolojia *GST* inafanya tafiti nyingi na hivi sasa inaendelea na kufanya tafiti katika maeneo ya Kanda ya Kati kwa teknolojia ya *Air Borne* kwa maana kwamba wanapiga picha kwa ndege na kuweza kujua kiwango cha maeneo ambayo yana Madini ambayo yapo hapa nchini.

Lakini pia tuna Taasisi ya Kusini na Mashariki mwa Afrika *SEAMIC* ambayo ipo Kunduchi inafanya tafiti na kupima sampuli mbalimbali zinazoletwa na makampuni ambayo yana leseni za utafiti hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili Mheshimiwa ameuliza kwa nini tusifanye wenyewe, ni kweli ni dhamira yetu Serikali kuhakikisha kwamba tunaziimarisha Wakala zetu na Maabara ili ziweze kufanya tafiti hizi kama nilivyoeleza kwamba tayari zinaendelea na kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali hapa nchini na takwimu tunazo nyingi, ukitembelea ofisi yetu ya Wakala wa Jilojia *GST* Dodoma utakuta takwimu nyingi tunazo za tafiti mbalimbali ambazo zimeshafanyika.

Kwa hiyo, tutaendelea kuziimarisha kwa maana ya kuzinunulia vifaa vinavyostahili kwa teknolojia ya sasa ili tuweze kufanya tafiti nyingi sisi wenyewe bila kutegemea makampuni ya nje.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba kujua kwamba je, Serikali inafahamu kwamba katika Tarafa ya Ndago, kijiji cha Luzilukulu kuna Silikoni inayopatikana kule na mtafiti aliyepo pale anachukua Madini kama Silikoni lakini kuna Almasi ndani yake? Ahsante sana.

**SPIKA:** Unafahamu hayo mambo? Si ndiyo amekuuliza kama unafahamu? Waziri wa Nishati na Madini!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Ukweli ni kwamba kijiolojia Silikoni haikai pamoja na *Diamond*, hiyo haiwezekani!

Kwa hiyo, Silikoni ni vito lakini ni vito ambayo inapatikana sehemu nyingi sana lakini Diamond inapatikana kwenye *Kimberlight pipes* ambazo zinatoka chini sana na tuna *Kimbelight pipes* zaidi ya 300 na ambazo zina Almasi hazivuki 10 kwa Tanzania hii. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba Silikoni na Almasi zipo pamoja.

**SPIKA:** Hayo ni mambo ya kitaalam na sasa twende kwenye swali linalofuata la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, kwa niaba yake Mheshimiwa Kaika Telele!

Na. 253

**Kusambaza Umeme Namanga na Longido**

**MHE. KAIKA S. TELELE (K.n.y. MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kabla ya kuuliza swali hili kwa niaba ya Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, napenda niwashukuru kwa niaba yake Waheshimiwa Wabunge ambao walipata nafasi ya kwenda kumfariji kutokana na msiba wa Mama yake.

Serikali imeleta umeme wa uhakika kutoka Kenya mpaka Namanga na Longido, lakini umeme huo haujasambazwa kwa wananchi.

(a) Je, ni lini nguzo na nyaya zitapelekwa Namanga na Longido?

(b) Je, usambazaji huo utachukua muda gani hadi kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mbunge wa Longido, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Longido unafadhiliwa na Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*). Gharama za mradi huu ni Shilingi bilioni 1.45. Mradi huu unatekelezwa na *TANESCO* kama Mkandarasi na umeanza mwezi Agosti, 2010. Aidha, nguzo zote 161 zilizokuwa zinahitajika ili kukamilisha mradi huu zilishapelekwa Longido. Tayari nguzo 141 zimekwisha simikwa na kufungwa waya mbili yaani *Single Phase.* Vifaa vyote vitaendelea kupelekwa ili kukamilisha mradi huu. Matarajio ya Serikali ni kwamba mraid huu utakuwa umekamilika ifikapo mwezi Septemba, 2012.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini tunazalisha nguzo za umeme hapa nchini, lakini soko la ndani limekuwa ni tatizo kubwa sana nguzo hizi tunauza nchi za nje kama Kenya, *DRC* na maeneo mengine. Kwa nini nguzo zinakuwa ni tatizo hasa maeneo ambapo Serikali inajitahidi kupeleka umeme?

Pili, kwa kuwa tatizo hili la upungufu wa nguzo linafanana sana na kule Loliondo kuna tatizo kubwa la nguzo, nyaya na mita. Ni lini sasa vifaa hivyo vitapelekwa ili kuweza kusambaza umeme katika mji wa Loliondo na mji wa Waswa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hapa nchini tunazalisha nguzo na ni kweli kwamba nguzo hizo zinauzwa hata nje ya nchi. Lakini kwa sasa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatuna tatizo la vifaa isipokuwa tu ni kwamba kwa kuwa mahitaji ni makubwa sana na kila siku miradi ya umeme na hasa baada ya kuleta mpango wa ujenzi wa miradi ya umeme vijijini mahitaji ya vifaa hivyo yamekuwa makubwa sana. Lakini changamoto hiyo tunajitahidi kupitia Shirika letu la *TANESCO* ili kuweza kupambana nazo na kwa sasa hatuna taarifa zozote kwamba kuna upungufu wa vifaa. Labda tu ni mchakato wa ujenzi wa miradi hiyo ndiyo inayochukua muda. Lakini kwa sasa kwa kweli tunajitahidi kwa kadiri inavyowezekana kuweza kuwa na vifaa hivyo mara zote.

Msimamo wa Serikali na Wizara kwa ujumla ni kwamba tunataka tuhakikishe kwamba mpaka ifikapo mwezi wa tisa hakuna mradi au mtu aliyeomba kufungiwa umeme ambaye atakuwa hajafungiwa. Kwa hiyo, ni kuhakikishie tu kwamba vifaa hivi tutajitahidi na vitaendelea kuwepo.

Kuhusu tatizo la nguzo, waya na mita Loliondo jibu lake ni lile lile kwamba kwa sababu sasa tumeamua kuwa vifaa vya kutosha na tumewaagiza *TANESCO* kuwa na vifaa hivi kwa idadi na kwa kiasi cha miradi inayotarajiwa kuwepo nchini basi nikuhakikishie tu kwamba vifaa hivi havitakuwa tatizo tena. (*Makofi*)

Na. 254

**Upanuzi wa Barabara ya Mtwara – Mnazimmoja Masasi**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2010 imeainisha kuwa barabara ya Mtwara – Mnazimmoja - Masasi itafanyiwa upanuzi na matengenezo makubwa.

Je, kazi hii inatarajiwa kuanza lini ili iweze kukamilika ifikapo mwaka 20152 kama inavyoelekezwa kwenye Ilani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya upanuzi na ukarabati mkubwa wa barabara ya Mtwara - Mnazimmoja – Masasi (km 200) imeanza. Mkataba wa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu ulisainiwa tarehe 5 Desemba, 2011 na kazi zilianza rasmi mnamo mwezi Januari, 2012. Muda wa utekelezaji ni miezi 9 na kazi zinatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2012 na zinafadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi ya usanifu kukamilika ujenzi utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kama nilivyouliza kwenye swali langu la msingi kwamba barabara hii ni mojawapo ya barabara ambazo zipo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba kazi ya ujenzi itaanza pale fedha zitakapopatikana.

Je, Serikali haioni ipo haja ya kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara zote nchini ambazo ziliahidiwa ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ikiwepo barabara hii ya Masasi Mtwara? *(Makofi)*

Pili, je, Serikali itaanza lini kuwalipa fidia wale wote watakaoathirika na upanuzi wa barabara ya kutoka Masasi – Mnazimmoja hadi Mtwara? Ahsante sana!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kasembe, kama ifuatavyo:-

Anaulizia ni kwa nini hatujaweka fedha za ujenzi, ni kwamba hatuwezi tukaweza fedha za ujenzi kwa sababu kwanza lazima usanifu ukamilike ndiyo utaonyesha gharama halisi ya kujenga barabara hiyo ni kiasi gani, ndiyo tutaweza kuweka *commitment* ya fedha. Lakini nimeahidi kwamba usanifu ukikamilika fedha zitapangwa na mwaka huu wa fedha tumepanga kwanza tumalize usanifu mwaka utakaofuata wa Bajeti tutakuwa na fedha za kujenga. Pili kuhusu suala la fidia, suala la fidia pia litajulikana baada ya usanifu kwamba fidia ni kiasi gani kuonyesha ni maeneo yapi ambayo yatakuwa *affected* na ile barabara ambayo inapanuliwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali pia yamekwisha. Lakini kwanza kabisa nitambue baadhi ya wageni tulionao ambao ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo Mheshimia Dkt. Fenella Mukangara, ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara Bwana Sethi Kamuhanda, Naibu Katibu Mkuu Bi. Sihaba Mkinga, Mkurugenzi wa Sera na Mipango Bwana Gasper Mwendezi, Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidia naomba kwa pamoja wasimame. Ahsanteni sana na tunawatakia kazi njema leo. (*Makofi*)

Pia wapo watendaji wakuu wa Asasi, Chuo na Taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara na hao pia wasimame kwa pamoja. Ahsanteni sana! Kuna Wenyeviti wa Bodi katika Wizara hizi nao wasimame walipo, kuna Katibu Mkuu wa Shirikisho la mpira wa miguu Tanzania *TFA* anaitwa Ndugu Angetile Hosea, yupo pia Afisa wa *TFF* Ndugu Raphael Matolla, nyie hawa hamwafahamu? Mnapaswa kuwapigia makofi. Yupo Dkt. Kasolele Nteve, huyu ni Mwenyekiti wa *Tanzania International Youth Fellowship.* Pia wapo wageni wa Msemaji Mkuu wa Upinzani Bungeni kwa Wizara hii yaani Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ambao ni Tusa Mwalwega, Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi. Yupo Ndugu Anselm Ngaiza, Msanii wa *Bongo Flavor. T*una wageni wa Waheshimiwa Wabunge wengine ambao ni Wageni wawili wa Mheshimiwa Mkanga, ambao ni Ndugu Henry Mutasiwa, yupo pia na Ndugu Pius ambaye ni Mkalimani.

Tuna wageni wengine nane wa Mheshimwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji, ambao ni Walimu na viongozi wa Umoja wa Vijana kutoka Kata ya Silop Hanang, wakiongozwa na Ndugu Salim Jumanne, karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tuna wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo hawa ni wanafunzi 39 pamoja na Walimu wao kutoka Shule ya *Elite* ya Ally Hassan Mwinyi Dar es Salaam, nafikiri wataingia baadaye. Dodoma, ahsnateni sana na karibuni sana lakini msome vizuri. Pia tuna wanafunzi wengine 50 pamoja na Walimu wao kutoka shule ya Sekondari Miyuji, Dodoma na Walimu wao, ahsante sana na msome kwa bidii. Tuna wanafunzi sita kutoka Taasisi ya Sanaa na Utamaduni, Bagamoyo na hao pia wasimame, ahsante sana na karibuni sana. Huwa tunaona mambo mnayoyafanya, ahsanteni sana. Wageni wengine wote pia mnakaribishwa.

Sasa ni matangazo kuhusu kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa Selemani J. Zedi anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na mkutano wa Kamati hiyo katika ukumbi namba 227. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimwa Mussa Zungu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao katika ukumbi namba 219.

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Idd Azzan, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wanamichezo kuwa Jumamosi, tarehe 28 Julai, 2012 kwenye uwanja wa Jamhuri Mjini Dodoma timu yetu ya Bunge yaani *Football* na *Netball* zitacheza na Benki ya *NMB Sports Club* na mpambano huo ni mkali na utakuwa wa ushindani mkubwa hivyo basi anawaomba wanamichezo wote wafike Mazoezini ili kujiandaa vilivvyo yaani waende bila kukosa. Kwa hiyo, mnakaribishwa huko.

Mwenyekiti wa *DRC* ambayo ni *Club* ya Bunge ya kulenga shabaha, Mwenyekiti wake naona ni Mheshimiwa Said Nkumba, anaomba niwatangazie wanachama wa *Bunge Range Club* kwamba zoezi la kulenga shabaha litafanyika Jumapili tarehe 29 Julai, 2012 huko Makutupora JKT, kuanzia saa 4 asubuhi. Aidha, mabasi yatakayowabeba Waheshimiwa Wabunge watakaohudhuria zoezi hilo yatakuwepo viwanja vya Bunge kuanzia saa mbili asubuhi. *(Makofi)*

waheshimiwa Wabunge, mimi nilikuwa member lakini nimejitoa. Kwa hiyo, wanaohusika wamesikia tangazo lao hilo. Katibu tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 - Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

**SPIKA:** Sasa nitamwita mtoa hoja Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama hapa mbele yenu leo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa rambirambi. Mimi mwenyewe kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, natuma salamu za pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa msiba mkubwa wa kuwapoteza Watanzania wenzetu takribani 76 kwa ajili ya kuzama kwa meli siku ya Jumatano tarehe 15 Julai, 2012.

Aidha, nawapa pole wale wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki katika ajali hiyo. Tunawaombea Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira wakati wa kipindi hiki kigumu cha msiba. Pia tunawaombea wale wote walionusurika na majeruhi wapone haraka ili warejee haraka katika kazi za kujenga Taifa letu. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu...

**SPIKA:** Waheshimiwa wanaotoka naomba muondoke kwa staha.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** ... kwa kuniokoa mimi na wafanyakazi wenzangu wawili katika ajali mbaya ya gari iliyotokea tarehe 29 Juni, 2012. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa upendeleo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya familia yangu na mimi binafsi naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapendwa wangu wote walionipatia salamu za pole zilizonifikia kwa namna mbalimbali. Nataka niseme tena, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, tulizungumza kwa kirefu. Pia nichukue nafasi hii kukushukuru Mheshimiwa Spika, kwa ujumbe wako, Waziri Mkuu, Wabunge, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Mkuu wa Mkoa wa Tabora na Ma-*DC* wa Igunga na Nzega, Wakuu wa Mikoa mbalimbali, Mwenyekiti wa UWT – Taifa, Mheshimiwa Sophia Simba, wanachama wa CCM, vijana mbalimbali, vijana wa Wilaya ya Nzega na wanachama wa CCM wa Nzega, Madiwani wa Serikali za Mitaa, nakumbuka walikuwa

wanaelekea Mwanza walikuwa wa kwanza kunikuta pale kwenye ajali na wakanipeleka pamoja na wenzangu kule Nzega kwa ajili ya kutibiwa.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Madaktari na Polisi walionisaidia kwa namna moja au nyingine, pamoja na wanahabari kwa ujumla. Nataka niseme kwa kifupi tu kwamba, nimefarijika sana kwa sala, salamu na dua mlizoniombea nyakati mbalimbali. Mungu awabariki sana. Naomba sana tuendelee kushirikiana, kupendana na kujenga nchi yetu kwa amani.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niendelee na kazi muhimu iliyoniweka hapa mbele yenu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Asasi zake katika mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Bunge lako Tukufu tukiwa wenye afya na uzima. Namshukuru pia kwa kuijalia nchi yetu kubaki katika hali ya amani na utulivu. Aidha, sina budi kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri mnaonipa unaoniwezesha kutekeleza kikamilifu majukumu niliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa heshima aliyonipa ya kuniteua kuwa Waziri anayesimamia Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na pia kumteua Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla (Mb), Mbunge wa Jimbo la Mvomero kuwa Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa ushirikiano na maelekezo yake ya kazi wakati akiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Nashukuru pia familia yangu, hasa mume wangu mpendwa, Prof. Daudi Mukangara na watoto wangu Cleopatra, Natasha na Jackson, kwa ushirikiano na uvumilivu wao muda mwingi ninapokuwa nikitekeleza majukumu ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Bunge lako Tukufu liliwapoteza Mheshimiwa Jeremia Sumari, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki (CCM), Mheshimiwa Regia Mtema, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA) pamoja na Mheshimiwa Mussa Khamis Silima aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini (CCM). Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa namna ya pekee niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri pamoja na Wakuu wa Mikoa na Wilaya walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pongezi za pekee ziwaendee Wabunge wote wapya waliochaguliwa na wananchi na walioteuliwa na Mheshimiwa Rais na ambao wamejiunga katika Bunge lako Tukufu kutoka katika Chama cha Mapinduzi, CHADEMA na NCCR - Mageuzi.

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteua wajumbe wa Tume ya Katiba wenye dhamana ya kuratibu maoni ya wananchi kuhusu Katiba Mpya. Vilevile, nawapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), kwa hotuba yake fasaha yenye maelekezo ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013. Waziri Mkuu ameainisha malengo ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kutokana na Dira ya Taifa ya Maendeleo, Malengo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II).

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Stephen Wasira (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa hotuba yake iliyoonyesha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2012/2013. Pia, nampongeza Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa (Mb), Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake nzuri iliyoainisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kwa namna ya pekee niwashukuru

Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba za Mawaziri walionitangulia. Maoni waliyotoa yamesaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali, zikiwemo Sekta ambazo ziko chini ya Wizara ninayoiongoza.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kutumia fursa hii kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ambayo inaongozwa na Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Makamu Mwenyekiti wake Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kusini, Mheshimiwa Juma Nkamia, kwa kuiongoza vizuri Kamati hii. Aidha, naishukuru Kamati ya Bunge lako Tukufu kwa kutoa ushauri na maelekezo wakati wa kujadili bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu manne kama ifuatavyo: Eneo la kwanza ni majukumu ya Wizara, eneo la pili ni Mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, eneo la tatu linahusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2012/2013 na eneo la nne ni hitimisho lenye kujumuisha shukrani, makadirio ya bajeti kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 na maombi rasmi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara hii ni haya yafuatayo:-

(i) Kuandaa na Kusimamia utekelezaji wa Sera za Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali;

(ii) Kuratibu na kusimamia masuala ya maendeleo ya vijana ili kuwawezesha kujiajiri na kujitegemea;

(iii) Kusimamia Vyombo vya Habari nchini;

(iv) Kuratibu tasnia ya utengenezaji wa sinema, maigizo, maonyesho na utoaji wa leseni;

(v) Kusimamia utendaji wa Taasisi, Mashirika ya Umma, Wakala, Miradi na programu zilizo chini ya Wizara; na

(vi) Kuendeleza, kuwezesha na kuratibu masuala ya kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012. Mapato na Matumizi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 766,907,385 kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2012 jumla ya Shilingi 682,374,217 zilikuwa zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 89 ya lengo la makusanyo ya mwaka. Kadhalika Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi 14,671,877,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zilijumuisha mishahara ya Wizara Shilingi 2,076,869,000 na ya Taasisi Shilingi 5,991,270,000; Matumizi Mengineyo *(OC)* ya Wizara Shilingi 3,806,163,200 na ya Asasi zake Shilingi 2,797,574,800. Hadi mwezi Juni, 2012 jumla ya Shilingi 14,671,877,000 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi 3,880,851,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Juni, 2012, Shilingi 3,600,000,000 zilikuwa zimetolewa na kutumika, sawa na asilimia 92.8. Miradi iliyotekelezwa ni ujenzi wa eneo Changamani la Michezo na Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa TBC, eneo la kuimarisha mitambo ya Radio na Televisheni.

Mheshimiwa Spika, sekta ya habari. Waraka wa mapendekezo ya Kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari umekamilishwa na kuwasilishwa kwenye ngazi ya juu kwa maamuzi ya Serikali na hatimaye Bunge lako Tukufu katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2012/13. Aidha, kutungwa kwa sheria hii kutaimarisha weledi na uwajibikaji wa vyombo vya habari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Idara ya Habari imeendelea kukusanya taarifa mbalimbali za Serikali, kuandika habari na kuzitoa katika vyombo vya habari, kupiga picha za matukio mbalimbali ya kitaifa, kuzitoa katika magazeti na kuzihifadhi katika maktaba ya kumbukumbu ya picha kwa njia ya elektroniki.

Mheshimiwa Spika, kupitia Tovuti ya Wananchi, wananchi wanaendelea kupata haki yao ya kikatiba ya kutoa maoni kwa uhuru katika masuala yanayowahusu. Tovuti imewawezesha wananchi kuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na Serikali. Aidha, katika kipindi cha mwaka ulioanza Julai, 2011 hadi Juni, 2012, jumla ya hoja 38,247 zimepokelewa. Hoja 36,466 zimeshughulikiwa kwa kupelekwa katika Wizara na Taasisi husika ili kupatiwa majibu na ufumbuzi. Hoja nyingi zilihusu ucheleweshwaji wa malipo ya pensheni, mgao wa umeme, ukosefu wa maji, ajali kazini hasa kwenye migodi na mabadiliko ya Katiba. Hoja 1,781 hazikushughulikiwa kwa sababu hazikuihusu Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza uhuru wa upatikanaji wa habari na vyombo vya habari, Wizara imeendelea na usajili wa magazeti na majarida. Hadi mwezi Juni, 2012 jumla ya magazeti na majarida 763 yalisajiliwa, hii ikiwa ni ongezeko la magazeti 52 kutoka mwaka jana. Magazeti yaliyosajiliwa kuchapishwa kila siku na yaliyo hai ni 14 na yale yanayochapishwa kila wiki ni 62. Aidha, magazeti matano (5) yaliyokiuka maadili ya uandishi wa habari yalipewa onyo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utangazaji imeendelea kukua kwa kasi na watu wengi wanazidi kuomba leseni za kuanzisha vituo vya utangazaji. Mpaka sasa kuna vituo 85 vya redio na vituo 26 vya televisheni. Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 vituo vipya 12 vya redio na kituo kimoja (1) cha televisheni chenye kutoa huduma ya matangazo ya malipo *(Subscription Sattelite TV)* vimesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* limeendelea kuwa chombo mahiri cha utangazaji nchini likiwa na Idhaa tatu (3) za redio na mbili (2) za televisheni. Aidha, limeendelea kuongoza kati ya vyombo vya utangazaji vilivyopo nchini kwa kueneza usikivu wa matangazo yake kupitia vyombo vyake vya redio na televisheni katika eneo kubwa zaidi la nchi yetu. Jumla ya mitambo 22 ya redio za mfumo wa *FM* imejengwa Zanzibar na katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Arusha, Dodoma, Manyara, Kigoma, Shinyanga, Singida, Tanga, Tabora, Rukwa, Katavi, Morogoro, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Iringa na Kilimanjaro. Mitambo hiyo inarusha matangazo ya Idhaa mbili za TBC-Taifa na TBC-FM.

Aidha, kwa upande wa redio kuna mitambo tisa (9) ya Masafa ya Kati inayorusha matangazo ya TBC-Taifa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Dodoma, Arusha, Kigoma, Mbeya, Mwanza na Ruvuma. Kwa upande wa Televisheni, mitambo ipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mwanza, Kagera, Mara, Lindi na Mbeya kwa mfumo wa analojia na Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Kilimanjaro kwa mfumo wa dijitali. Matangazo yake yanapatikana kwa satelaiti na kwenye mtandao wa DSTV ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, *TBC* ilishiriki kwa ufanisi mkubwa kufanikisha maadhimisho hayo. Aidha, vipindi vingi viliandaliwa na kurushwa. Matangazo ya kilele cha sherehe yalirushwa moja kwa moja kwenye redio na televisheni. Vilevile vipindi vya elimu kwa umma, burudani na biashara vimeendelea kurushwa kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika kupanua vyanzo vya mapato, Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)* imezindua Gazeti la Kiswahili la michezo la kila wiki, Spoti Leo, ambalo limepokelewa vyema na wasomaji. Aidha, Kampuni imekamilisha ukarabati na kuhamia Jengo lake la ofisi lililopo Barabara ya Mandela Jijini Dar es Salaam. Kukamilika kwa jengo hili, kunatoa fursa ya uendelezaji wa jengo la Mtaa wa Samora kama kitega uchumi. *TSN* imeendelea kuimarisha magazeti yake ya *Daily News, Sunday News* na Habari Leo. Kampuni hii inajiendesha kwa faida, ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12 imechangia gawio la Shilingi 16,000,000 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maudhui ilianzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* Na. 10 ya mwaka 2003. Kamati hii inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia

Sera ya Utangazaji ya mwaka 2003, Sheria ya Bunge Na. 3 ya mwaka 2010 pamoja na Kanuni za Utangazaji za mwaka 2005. Kamati hiyo inateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya utangazaji. Kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha sheria hiyo, Kamati ina jukumu la kumshauri Waziri kuhusu masuala ya Sera ya Utangazaji nchini, kufuatilia na kudhibiti maudhui potofu ya utangazaji. Kamati pia inasimamia na kuhakikisha kuwa maadili na kanuni za utangazaji zinafuatwa. Aidha, Kamati inashughulikia malalamiko yatokanayo na maudhui ya utangazaji kutoka kwa watumiaji wa huduma za utangazaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maudhui imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko yatokanayo na vipindi vinavyorushwa ambavyo vinakiuka maadili ya utangazaji na utamaduni wa Mtanzania. Kamati imekuwa ikiyafanyia kazi malalamiko yote na kuyatolea maamuzi. Ilipobidi Kamati ilitoa makaripio kwa vituo vilivyokuwa vikienda kinyume cha sheria na kanuni za utangazaji za mwaka 2005 na maadili katika utangazaji. Katika kipindi hicho, Kamati ya Maudhui ilisikiliza mashauri manne (4) ya ukiukwaji wa Kanuni za Utangazaji. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2011 hadi mwezi Juni, 2012 *TCRA* ilipokea jumla ya malalamiko kumi na nane (18) ambapo kati ya hayo kumi na tatu (13) yaliwasilishwa na wananchi na matano (5) yalitokana na ufuatiliaji wa wajumbe wa Kamati ya Maudhui. Vituo saba (7) vilipewa onyo na vituo viwili (2) vilipewa mwongozo. Aidha, Wizara yangu imeelekeza kuanzia sasa kila kituo cha utangazaji kiwe na Miongozo ya Sera za Uhariri *(Editorial Policy Guidelines).* Miongozo hii itasaidia kuweka misingi ya vituo vya utangazaji ili kuviwezesha kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni zilizowekwa. Vituo vitakavyokwenda kinyume na miongozo hii vitachukuliwa hatua na ikibidi kuvifungia.

Mheshimiwa Spika, *TCRA* kwa kushirikiana na Wizara yangu pamoja na wadau wa Sekta ya Utangazaji, imefanya marekebisho ya Kanuni za Utangazaji kufuatia kukua kwa Sekta ya Utangazaji na kubadilika kwa mfumo wa utangazaji hasa kuelekea kwenye mfumo mpya wa utangazaji wa dijitali. Aidha, naomba kuchukua fursa hii ya pekee kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Utangazaji kwa michango, mapendekezo na maoni yao katika kufanikisha zoezi lote la kuziandaa upya kanuni hizi. Kadhalika, shukrani zangu za dhati ziende kwa uongozi wa *TCRA* kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu mwaka 2011/2012, *TCRA* imefanya mikutano na wadau wa Sekta ya Utangazaji katika kutoa elimu kwa umma kuhusu mchakato wa kuhama kutoka teknolojia ya utangazaji ya analojia kwenda dijitali. Uhamaji huo unatakiwa uwe umekamilika ifikapo tarehe 17 Juni 2015, kwa mujibu wa makubaliano ya nchi wanachama wa Shirika la Mawasiliano Duniani *(ITU).*

Mheshimiwa Spika, nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki zimeazimia kusitisha matangazo ya analojia ifikapo tarehe 31 Desemba, 2012. Kiufundi, kusitisha katika kipindi hicho cha miaka mitatu kabla ya muda uliokubaliwa ulimwenguni, kutaziwezesha nchi wanachama kupata fursa ya kutathmini iwapo kutatokea matatizo ya kiufundi washirikiane kuyatatua mapema ili kuondoa usumbufu usio wa lazima. Pili, katika kipindi cha mpito makampuni yanayotoa huduma za utangazaji yatahitajika kuendelea kutoa huduma kwa mfumo wa analojia kwa maeneo ambayo mfumo mpya haujafika na pia kwa dijitali kwa mujibu wa Kanuni za *TCRA*. Hata hivyo, mchakato wa mabadiliko haya kutoka teknolojia ya analojia kwenda dijitali utagusa utangazaji kwa njia ya televisheni pekee na siyo utangazaji wa redio.

Mheshimiwa Spika, Mchango wa Vyombo vya Habari. Serikali itaendelea kuthamini mchango wa Vyombo vya Habari, ili kuimarisha Tasnia ya Habari nchini. Wizara yangu inaendelea kuhimiza Vyombo vya Habari kuhakikisha vinaajiri wahitimu bora wa taaluma ya uandishi wa habari na utangazaji. Umefika wakati kwa Vituo vya Televisheni kuwatumia wahitimu hao ili viweze kutoa matangazo bora kwa wasikilizaji na watazamaji. Kwa hili, nitaendelea kuhimiza ili kuhakikisha weledi wa uandishi wa habari unashamiri hapa nchini. Nahimiza pia matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu katika vituo vya televisheni na redio. Ni matumaini yangu vituo vyote vitawajibika katika matumizi bora ya Kiswahili sanifu na vitajiwekea utaratibu wa kutathmini mwelekeo mzima wa lugha hii ya taifa ambayo ndiyo inayotumika kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kulipongeza Baraza la Habari Tanzania *(MCT)* kwa mchango wake katika kuboresha mitaala ya Mafunzo kwa ajili ya Uandishi wa Habari. Mitaala hiyo ambayo iliandaliwa na kupewa ithibati na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* ni kwa ngazi ya 4 ya Cheti cha Awali cha Uandishi wa Habari *(Basic Certificate in Journalism),* ngazi ya 5 ya Cheti cha Uandishi wa Habari *(Certificate in Journalism)* na ngazi ya 6 ya Stashahada ya Uandishi wa Habari *(Diploma in Journalism)*. Kukamilishwa kwa mitaala hiyo na kupewa ithibati ya *NACTE* ni hatua muhimu katika kuimarisha mafunzo yanayotolewa kwa waandishi wa habari kwenye vyuo mbalimbali vya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutambua juhudi zinazofanywa na Vyama na Taasisi mbalimbali za habari katika kuimarisha weledi, uwajibikaji na maadili ya uandishi wa habari kwa kuwatambua na kuwatunza waandishi wa habari ambao wamefanya vizuri zaidi. Chini ya uongozi wa Baraza la Habari Tanzania, vyama mbalimbali vya uandishi wa habari vimekubaliana kutoa tuzo za pamoja ambazo zinaheshimika kwenye maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na habari za afya, mazingira, biashara, michezo, sayansi na teknolojia, watoto na jinsia. Katika kufanikisha hili, mwezi Machi, 2012, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alikuwa Mgeni rasmi katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari za mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuvipongeza kwa dhati Vyombo vya Habari kwa kushiriki kikamilifu katika Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Vyombo hivi vimehabarisha wananchi kuhusu maendeleo na mafanikio yaliyopatikana nchini mwetu katika kipindi hicho. Aidha, navipongeza vyombo hivyo kwa namna vilivyotoa taarifa kuhusu maafa makubwa yaliyotokana na mafuriko ya mwaka jana na kusababisha kupotea kwa maisha ya watu, mali zao pamoja na uharibifu wa miundombinu. Vyombo vya Habari vilikuwa bega kwa bega katika kutoa taarifa muhimu kwa wananchi, kuhamasisha uokoaji na utoaji wa misaada mbalimbali kwa wananchi walioathirika.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Wizara yangu kuwa juhudi hizi za pamoja kati ya Serikali na wadau wote wa habari zitaendelea katika kuimarisha Sekta ya Habari ili iendelee kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuharakisha maendeleo na ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Vijana. Wizara imeendelea kufanikisha utekelezaji wa Mwongozo wa Stadi za Maisha kwa vijana walio nje ya shule. Kupitia Mwongozo huu ambao utasaidia kukabiliana na changamoto za maisha, Wizara imewapa mafunzo ya kuwajengea uwezo Maafisa Vijana wote nchini ili waweze kuufahamu na hivyo kusimamia utekelezaji wake katika maeneo yao. Aidha, mtaala wa kufundishia stadi za maisha kwa waelimisha rika umeshaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imewezesha kuridhiwa kwa Mkataba wa Vijana wa Afrika wa mwaka 2006. Mkataba huu umeridhiwa na Bunge lako Tukufu mnamo tarehe 1 Februari, 2012. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imepeleka taarifa za kuridhiwa mkataba huo Makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU) ili nchi yetu iweze kuwekwa kwenye orodha ya nchi zilizokwisharidhia mkataba huo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanza kuchukua hatua za kuandaa Muswada wa sheria ya utekelezaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2011 zilizinduliwa tarehe 14 Oktoba, 2011 katika Kijiji cha Butiama Mkoani Mara. Mgeni Rasmi wakati wa uzinduzi alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal. Siku hii pia ni ya kuadhimisha kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa na Muasisi wa Mwenge wa Uhuru, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Aidha, Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2011 zilikuwa maalum kama sehemu ya maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara chini ya kauli mbiu "Tumethubutu, Tumeweza na Tunazidi Kusonga Mbele". Mbio hizo pia zilitumika kuwahamasisha wananchi na hasa vijana kushiriki katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI, kuepuka matumizi ya dawa za kulevya na vitendo vya rushwa. Sambamba na maadhimisho hayo Mwenge wa Uhuru pia ulipandishwa katika Kilele cha Mlima Kilimanjaro usiku wa kuamkia Desemba 9, 2011 kukumbuka siku ya uhuru wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Sherehe za Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru zilifanyika Mkoani Dar es Salaam tarehe 01 Desemba, 2011. Mgeni Rasmi katika sherehe hiyo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa mujibu wa taarifa zilizokusanywa kupitia Mbio za Mwenge, jumla ya miradi 273 yenye thamani ya Shilingi 232,357,556,185 ilizinduliwa na kuwekewa mawe ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2012 zilizinduliwa tarehe 11 Mei, 2012 katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine, Mkoani Mbeya. Mgeni Rasmi katika sherehe hizo za uzinduzi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. Kauli mbiu ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu ni, "Sensa ni Msingi wa Mipango ya Maendeleo Yetu Shiriki Kuhesabiwa 26 Agosti, 2012". Aidha, ujumbe huu unaambatana na kauli mbiu nyingine za uhamasishaji wananchi kuhusu mambo yafuatayo; Mabadiliko ya Katiba, Mapambano Dhidi ya UKIMWI, Rushwa na Matumizi ya Dawa za Kulevya. Sherehe za kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru 2012 zitafanyika tarehe 14 Oktoba, 2012 katika Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho ya Wiki ya Vijana yalifanyika sambamba na Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara yaliyoadhimishwa Mkoani Dar es Salaam. Vijana kutoka sehemu mbalimbali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walishiriki. Aidha, katika banda la maonyesho la kila Mkoa kulikuwa na uwakilishi wa shughuli za maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeadhimisha Siku ya Kujitolea Duniani Mkoani Dar es Salaam. Sherehe za mwaka 2011 ziliadhimishwa sambamba na maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru. Aidha, vijana kutoka sehemu mbalimbali nchini wameshiriki katika makongamano ya kimataifa nchini Marekani, Australia, Guinea ya Ikweta, Kenya na Rwanda.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni. Wizara yangu imeratibu mchakato wa kuridhia Mikataba miwili ya *UNESCO* ambayo ni Mkataba unaohusu Kulindwa kwa Urithi wa Utamaduni Usioshikika wa mwaka 2003 na Mkataba unaohusu Kulindwa na Kukuzwa kwa Uanuwai wa Kujieleza Kiutamaduni wa mwaka 2005. Aidha, hati ya kuridhiwa Mikataba hii ilipelekwa *UNESCO* Makao Makuu na kusainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa *UNESCO* tarehe 8 Agosti, 2011. Katika kutekeleza Mikataba hiyo, Wizara iliandaa mafunzo kwa wadau wa Sekta ya Utamaduni ili kujenga uelewa wa pamoja wa utekelezaji. Baadhi ya masuala yaliyomo katika Mikataba hiyo ni pamoja na utafiti, kuorodhesha amali na urithi wa utamaduni usioshikika, kuhifadhi, kusambaza na kukuza utamaduni kwa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imeendelea kutoa elimu juu ya Utamaduni wa Mtanzania kwa jamii katika kutambua, kupokea na kuheshimu maadili yetu ya Kitanzania. Elimu hii imekuwa ikitolewa kwa kuandaa na kurusha vipindi vya redio kuhusu 'Maadili ya Mtanzania' kupitia kituo cha TBC-Taifa. Katika kipindi hicho jumla ya vipindi 42 vilirushwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliunda Kamati ya kukusanya maoni ya wananchi kuhusu dhana ya kuwa na Vazi la Taifa. Maoni yalikusanywa kikanda na Wizara imepokea mapendekezo ya Vitambaa kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Mapendekezo yaliyowasilishwa na wengi ni kuwa na kitambaa mahususi kitakachoshonwa Vazi la Taifa. Kutokana na hatua hiyo, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utaratibu wa kupata Vazi hilo upo katika ngazi za ushauri Serikalini na matarajio yetu ni kukamilisha zoezi hili katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lilitekeleza kazi muhimu zifuatazo:-

(i) Miswada 46 ya vitabu vya taaluma ilisomwa na kupewa ithibati ya lugha;

(ii) Baraza lilitoa huduma ya tafsiri ya Miswada, brosha, hati mbalimbali kama vile vyeti vya shule, vyeti vya kuzaliwa, hati za ndoa na talaka. Pia lilithibitisha tafsiri mbalimbali zilizofanywa na wafasiri wa nje;

(iii) Baraza liliratibu na kutoa huduma ya ukalimani wa Kiswahili kwenye mikutano ya Umoja wa Afrika iliyofanyika mwezi Julai, 2011 huko Guinea ya Ikweta na Januari, 2012 huko Ethiopia. Aidha, Baraza lilitoa huduma ya tafsiri na ukalimani wa Kiswahili kwenye mikutano ya Bunge la Afrika iliyofanyika mwezi Oktoba, 2011 huko Afrika Kusini; na

(iv) Baraza lilichunguza makosa yanayofanywa na Vyombo vya Habari na watumiaji wengine wa Kiswahili. Jumla ya makosa 120 yalibainishwa na kuorodheshwa pamoja na usahihi wake. Makosa hayo yamekuwa yakisahihishwa katika vipindi vya redio na televisheni vinavyoshirikisha wataalamu wa BAKITA.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) lilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendesha midahalo 47 ya Jukwaa la Sanaa ambapo jumla ya mada 47 ziliwasilishwa kwa wadau 4,055. Midahalo hii inalenga kuwapa wadau uelewa mpana wa tasnia ya sanaa;

(ii) Kuendesha mafunzo kwa Walimu 54 kutoka shule za Msingi 20 katika Mkoa wa Morogoro. Mafunzo hayo yamewajengea uwezo Walimu wa kuwapa stadi za uchoraji na utambaji wa sanaa watoto shuleni;

(iii) Kusimamia uchaguzi wa viongozi wa mashirikisho manne (4) ya Sanaa za Maonesho, Ufundi, Muziki na Filamu kwa kupata viongozi wapya kwa mujibu wa katiba zao; na

(iv) Kushiriki katika Mkutano Mkuu wa Tano wa Shirikisho la Mabaraza ya Sanaa Ulimwenguni Australia na kujenga mahusiano na Mabaraza ya Sanaa ya mataifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza imekagua jumla ya filamu 98 ambapo filamu za ndani 48 zilikaguliwa na kupewa madaraja. Kati ya hizo, moja (1) ilipewa daraja R ikimaanisha filamu hiyo hairuhusiwi kuoneshwa mahali pa hadhara. Filamu zilizokaguliwa kutoka nje ya nchi ni 50, kati ya hizo, tatu (3) zilipewa daraja R ambapo moja ni kutoka Liberia na mbili kutoka Norway. Aidha, Bodi imeweka alama maalum kwenye filamu zilizokaguliwa ikiwa ni moja ya njia ya kuhakikisha filamu zote zisizokaguliwa zinajulikana na wahusika kuchukuliwa hatua. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2011 hadi Juni, 2012, Bodi ilitoa vibali 21 vya kutengeneza filamu kwa Watanzania na 84 kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza iliandaa na kufanya mafunzo elekezi kwa Maafisa Utamaduni wa Wilaya nchini kwa lengo la kuboresha Bodi za Filamu za Wilaya. Bodi ilisambaza Sheria na Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Wilaya nchini. Bodi imeendesha mijadala mitatu kwa wadau wakiwemo watengenezaji filamu na wasanii wa filamu. Vilevile, imefanya mkutano kuhusu Mustakabali wa Tasnia ya Filamu katika kuadhimisha miaka 50 ya Uhuru na mkakati kwa kipindi cha miaka 50 ijayo. Mkutano huu umesaidia wadau walioshiriki kubuni mikakati mbalimbali ya kuboresha tasnia hii. Mikakati hiyo ni pamoja na kuhakikisha kuwa filamu na michezo ya kuigiza vinalenga zaidi katika kutangaza utaifa, uzalendo, maadili na utamaduni wa Tanzania. Nia ni kuondokana na filamu ambazo zimemezwa na tamaduni za nje. Vile vile, kuhakikisha kuwa tasnia ya filamu inakuwa rasmi ili ichangie pato la taifa na la msanii binafsi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Filamu ilizindua Kanuni za Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ambapo nakala 4,200 za Kanuni na nakala 4,200 za Sheria zilisambazwa. Aidha, utafiti uliofanywa na Bodi kwa kushirikiana na wadau wa filamu umebaini kuwepo kwa Makampuni 127 yanayojihusisha na uongozaji, utengenezaji, uzalishaji na usambazaji wa filamu kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee. Makampuni hayo yameajiri watu kati ya watatu (3) na kuendelea na kwa pamoja yanatoa wastani wa ajira 508.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Michezo. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine wa Michezo, iliendesha kongamano maalum kuhusu Michezo kwa Amani na Maendeleo. Kongamano hilo lililenga kuonyesha fursa za kutumia michezo katika kufanikisha malengo ya maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika kushiriki mashindano ya Kimataifa, Timu za Taifa ziliandaliwa na kuwezeshwa kushiriki katika Michezo ya Afrika. Tanzania iliwakilishwa na zaidi ya wanamichezo 60 katika mashindano hayo yaliyofanyika nchini Msumbiji, mwezi Septemba, 2011. Katika mashindano hayo, timu ya Taifa ya Mchezo wa Netiboli ilishika nafasi ya pili na kujinyakulia medali ya fedha. Aidha, timu hiyo ya Netiboli ilishiriki katika mashindano ya Netiboli ya Kimataifa yaliyofanyika Dar es Salaam ambayo yalishirikisha timu nane (8) kutoka mataifa mbalimbali. Tanzania ilijinyakulia ushindi wa pili katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendesha mafunzo kwa wanachuo 38 katika fani za Stashahada ya Elimu ya Ufundishaji wa Michezo na Stashahada ya Uongozi na Utawala wa Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Mafunzo ya muda mfupi yalitolewa kwa wadau wa michezo zaidi ya 300 katika Vituo vya Michezo Kanda ya Kaskazini, Arusha na Kanda ya Kusini, Songea. Aidha, katika kupima ubora wa Walimu wa Michezo, mfumo maalum wa kitaifa wa kutathmini sifa na kutoa madaraja ya Walimu wa Michezo mbalimbali ulianzishwa. Mfumo huu umeanza kwa majaribio kwa michezo mitatu ya Riadha, Soka la Wanawake na Mpira wa Wavu kwa kushirikisha Walimu 86 katika hatua ya awali. Utekelezaji wa mfumo huu upo chini ya mradi wa kuboresha maisha ya watoto milioni mbili walioko shuleni kupitia michezo *(International Inspiration)* ifikapo mwaka 2014. Katika hatua ya awali, Mpango unaendeshwa kwa kujumuisha shule 15 zilizoko Zanzibar na Mikoa ya Arusha, Mwanza, Dar es Salaam na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa kitaalamu ulitolewa kuhusu miundombinu na vifaa bora vya michezo katika Mikoa ya Mara, Dar es Salaam na Dodoma. Ushauri huu ulitolewa kwa wadau mbalimbali wa michezo wakiwemo wamiliki na viongozi wa viwanja vya michezo zaidi ya 50. Sambamba na ushauri huu huduma ya kinga na Tiba kwa Timu za Taifa zilitolewa kwa Timu zilizoshiriki mashindano ya Nchi za Afrika huko Msumbiji, Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) na SHIMIWI iliyofanyika huko Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara imeboresha Uwanja wa Uhuru kwa kuufanyia ukarabati mkubwa na kuujenga katika umbo la "U". Ukarabati huu utakapokamilika Uwanja utakuwa na uwezo wa kukaa watazamaji elfu ishirini (20,000).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) lilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Baraza la Michezo la Taifa na Vyama vya Michezo vya Taifa kwa kuwaandalia mafunzo kulingana na mahitaji yaliyopo. Watumishi 12 wa Baraza walishiriki mafunzo ya Sheria ya Ununuzi yaliyoendeshwa na *PPRA*;

(ii) Kushirikiana na Halmashauri za Manispaa, Miji na Wilaya kuhamasisha na kuendesha matamasha ya michezo kwa jamii. Matamasha haya yalilenga kujenga mahusiano na kuboresha afya ya jamii. Halmashauri zilizoshiriki ni Musoma, Magu, Mpwapwa na Ngara;

(iii) Kuanzisha na kuendesha mafunzo ya ufundishaji michezo kwa viongozi vijana kwa ushirikiano na Vyama vya Michezo vya Taifa na Baraza la Michezo la Uingereza (*UK Sport International).* Vijana walioshiriki mafunzo hayo walitoka Dar es Salaam (800), Arusha (750), Mwanza (350) na Ruvuma (450);

(iv) Kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya ufundishaji kwa Walimu wa Michezo mbalimbali wapatao 500 katika Wilaya 10 za Tanzania Bara;

(v) Kuandaa, kusimamia na kuendesha mafunzo ya Uongozi kwa Vijana kupitia michezo kwa washiriki wapatao 1,200 na pia kuwashirikisha katika mabonanza wanafunzi wapatao 2,000 wa shule za Msingi na Sekondari; na

(vi) Kuanzisha mpango maalum wa mafunzo ya Uongozi wa Michezo kwa Wanawake.

Mheshimiwa Spika, Utawala na Rasilimali Watu. Hivi karibuni Serikali imeidhinisha miundo mipya ya kada za watumishi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Miundo hii imeainisha vizuri wajibu na sifa za Maafisa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na Halmashauri. Kupitia miundo hii, Wizara sasa itaweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi kwani itakuwa ni kiungo kizuri kati yake na ngazi za chini walipo wananchi. Nitumie fursa hii kuwaomba Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri kuhakikisha kuwa wanawawezesha Maafisa hao ili waweze kutumika ipasavyo katika kuleta matokeo tarajiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Utawala Bora na ushirikishwaji wa Wafanyakazi Sehemu za kazi, Wizara imekuwa ikifanya vikao vya Baraza la Wafanyakazi ili kutatua kero mbalimbali zinazowakabili watumishi wa Wizara. Aidha, Wizara imehakikisha kwamba Watumishi wapya waliojiunga na Utumishi wa Umma kwa mara ya kwanza wanapewa mafunzo elekezi ambayo lengo lake ni kuwapa mwelekeo wa utendaji katika Serikali ikiwemo kuwafahamisha matarajio ya mwajiri, taratibu za utumishi na maadili katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi wanaostahili kulingana na miundo ya utumishi ya kada zao na kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na 2008. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, watumishi 46 walipandishwa vyeo. Aidha, Wizara imewezesha kutoa mafunzo kwa watumishi 17, kati ya hao wawili (2) wamemaliza mafunzo na 15 wanaendelea.

Mheshimiwa Spika, mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu shughuli za Vitengo vya Habari vilivyomo katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali na kutoa mafunzo ya utoaji habari za Serikali kwa Maofisa Habari wa Vitengo hivyo;

(ii) Kuendelea na mchakato wa kuanzisha mtandao wa kulinda na kuuza picha za viongozi na matukio mbalimbali ya kitaifa popote duniani kupitia mradi wa *“e-commerce”.* Mtandao huo utawawezesha wadau kupata picha hizi popote kutoka katika maktaba ya picha;

(iii) Kuchapisha machapisho mbalimbali ya Serikali likiwemo gazeti la Nchi Yetu;

(iv) Kupokea maoni ya wananchi kupitia Tovuti ya Wananchi na kufuatilia hoja hizo; na

(v) Kukusanya na kuandika habari za matukio mbalimbali ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* linatarajia kuimarisha vituo vya televisheni ili kuongeza usikivu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)* inalenga kutafuta fedha za mradi wa upanuzi wa kiwanda cha uchapaji na kukamilisha mkakati wa ubia wa kuendeleza viwanja vyake vilivyopo Dodoma na Dar es Salaam. Aidha, kampuni itaendelea na juhudi za kuinua ubora wa magazeti yake na kuimarisha usambazaji, hasa Mikoani.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Vijana. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kumpata Mshauri Mwelekezi ili kufanya upembuzi wa mradi wa kuanzisha Benki ya Vijana. Mchakato huu utahusisha ukusanyaji wa maoni toka kwa wadau mbalimbali. Tayari mawasiliano ya awali yamefanyika kati ya Wizara yangu na uongozi wa Benki Kuu ya Tanzania na

Benki ya Wanawake, kwa lengo la kupata maoni ya kiufundi, uzoefu na mstakabali wa uanzishaji wa Benki hiyo. Lengo la kuanzisha Benki hii ni kuwa na chombo maalum cha fedha kitakachotoa mikopo nafuu na inayokidhi mahitaji halisi na uwezo wa vijana;

(ii) Kuendelea na maandalizi ya awali yanayohusiana na mapendekezo ya kutungwa kwa sheria ya uundwaji wa Baraza la Vijana Tanzania. Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri inayohusu suala hili tayari imeandaliwa na ipo katika ngazi za ushauri na maamuzi Serikalini;

(iii) Kuboresha utendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa kuzijengea uwezo *SACCOS* 242 ambazo tayari ni wateja wa mfuko huu. Inatarajiwa pia kwamba mara Benki ya Vijana itakapoanzishwa, *SACCOS* zilizopo na nyingine zitakazoanzishwa ndizo zitakazokuwa wateja wakubwa wa Benki hiyo; na

(iv) Kuwapatia mafunzo maalum ya muda mfupi ya kujiajiri, ujasiri na ujasiriamali wahitimu wa shule na vyuo mbalimbali. Moja ya mikakati ya kutekeleza lengo hili ni kwa kutumia vituo vyetu vya vijana vilivyoko Ilonga – Kilosa, Sasanda – Mbozi na Marangu – Moshi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia sekta hii itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kukamilisha utaratibu wa urasimishaji tasnia ya filamu na muziki ili wasanii wanufaike na kazi zao pamoja na kuchangia Pato la Taifa. Maelezo ya kina kuhusu utaratibu huu yalitolewa ndani ya Bunge lako Tukufu na Waziri wa Fedha wakati akiwasilisha Hotuba ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013;

(ii) Kuendelea kukusanya taarifa muhimu zinazohusu Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya vitambaa vya kushonwa Vazi la Taifa yaliyokusanywa Kikanda kwa kuhusisha Mikoa yote na makundi maalumu, wakiwemo vijana na wanawake;

(iv) Kufanya utafiti wa lugha za jamii 12 za Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Rukwa na Kagera kwa lengo la kukuza na kuhifadhi lugha za jamii zinazotafitiwa;

(v) Kusimamia na kuendesha Mkutano Mkuu wa Sekta ya Utamaduni unaofanyika kila mwaka kwa kuwashirikisha wadau na watendaji wa sekta hii. Lengo la mkutano huo ni kupokea, kujadili na kupitisha maazimio na mustakabali wa utamaduni nchini;

(vi) Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya redio kuhusu Maadili ya Mtanzania. Vipindi hivyo vina lengo la kuelimisha jamii kutambua nini ni maadili na nini sio maadili ya Mtanzania, ili kuelekeza vijana na Watanzania wote kwa ujumla kuthamini maadili ya taifa letu; na

(vii) Kuratibu na kusimamia maadhimisho ya Siku ya Utamaduni Duniani pamoja na vikundi vya ngoma za asili kushiriki katika maadhimisho ya Sherehe za Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya "Lugha ya Taifa", vipindi 52 vya "Kumepambazuka" katika redio na vipindi 52 vya "Ulimwengu wa Kiswahili" katika televisheni ili kupunguza matumizi ya Kiswahili ambayo siyo sanifu;

(ii) Kuendelea kusoma Miswada ya vitabu vya taaluma na kuipatia ithibati ya lugha;

(iii) Kuratibu na kutoa huduma za tafsiri na ukalimani katika mikutano ya kitaifa na kimataifa, shughuli za mashirika, makampuni na watu binafsi;

(iv) Kuendelea kuchunguza makosa ya Kiswahili yanayofanywa na Vyombo vya Habari na watumiaji wengine na kusambaza masahihisho yake;

(v) Kuhamasisha matumizi sahihi ya Kiswahili Sanifu katika mabango, matangazo na lebo;

(vi) Kuchunguza maneno ya lugha za makabila na lahaja za Kiswahili yanayoweza kusanifiwa katika Mikoa ya Kanda ya Mashariki, Magharibi, Kusini na Kati;

(vii) Kukarabati na kuboresha majengo yaliyonunuliwa kutoka Shirika la Bima la Taifa ili yaweze kukidhi mahitaji ya kiofisi kwa ajili ya matumizi ya BAKITA.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuratibu midahalo 52 kupitia Jukwaa la Sanaa kwa Wasanii, Waandishi wa Habari 4,500 ili kuwapa ufahamu, elimu na ujuzi katika masuala ya sanaa;

(ii) Kuhuisha kanzidata ya wasanii, vyama vya sanaa, mashirikisho na wadau. Lengo kwa mwaka huu ni kupata taarifa mbalimbali za wasanii 2,000, vyama vya sanaa 50, mashirikisho manne (4) na wadau 100 wanaojishughulisha na kazi za sanaa; na

(iii) Kuendesha Mafunzo kwa ajili ya utengenezaji wa batiki na uchapaji kwa Wakufunzi wa wasanii 20 kutoka Mkoa wa Dar es Salaam na Singida.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kupitia Miswada 105 ya filamu na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu maboresho ya miswada hiyo;

(ii) Kukagua filamu 105 na kutoa ushauri wa kitaalamu wa maboresho na kuziwekea madaraja na alama maalum filamu zote zitakazokaguliwa;

(iii) Kushirikiana na Kamati ya Taifa ya utoaji vibali vya filamu, kutoa vibali 25 vya kutengeneza filamu kwa raia wa Tanzania na vibali 100 kwa waombaji kutoka nje ya Tanzania;

(iv) Kutoa mafunzo ya kuongeza weledi kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya filamu;

(v) Kushirikiana na taasisi nyingine, kufanya msako maalum kukamata filamu ambazo hazijakaguliwa na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika; na

(vi) Kuimarisha Bodi na Sekretarieti yake kwa kuwapa mafunzo na kuweka vifaa vya kisasa vya ukaguzi vinavyoendana na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendesha mafunzo ya Stashahada kwa washiriki 150 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 200 walio kazini;

(ii) Kuendesha mafunzo ya cheti cha "*National Technical Award" (NTA)* katika fani ya uzalishaji na usanifu wa muziki;

(iii) Kukamilisha mitaala ya Shahada ya Kwanza ya Sanaa za Maonyesho na Sanaa za Ufundi na kuwasilisha *NACTE* kwa madhumuni ya kupewa ithibati; na

(iv) Kusimamia na kuendesha Tamasha la 31 la sanaa na Utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Michezo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali za Michezo kwa Walimu na viongozi wa michezo 400 katika Vituo vya Michezo Kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kanda ya Kusini (Songea);

(ii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa tafiti kuhusu fani mbalimbali za Maendeleo ya Michezo;

(iii) Kusimamia uanzishwaji na utekelezaji wa mikataba ya ushirikiano kati ya Tanzania na nchi marafiki kuhusu ushirikiano katika Sekta ya Michezo;

(iv) Kuendesha mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ufundishaji Michezo na Stashahada ya Uongozi na Utawala wa Michezo kwa wanachuo 40 wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya;

(v) Kuwezesha Timu za Taifa kushiriki katika michezo ya Olimpiki na Paralimpiki Uingereza; na

(vi) Kuendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya uendelezaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa eneo Changamani la Michezo la Taifa lililoko Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 Baraza la Michezo la Taifa (BMT) litatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa Walimu wa Michezo wapatao 3,000 nchini kwa kushirikiana na Halmashauri za miji na Manispaa;

(ii) Kutoa mafunzo ya elimu ya michezo na kupanga wataalamu wa michezo katika viwango stahiki (madaraja) kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo vya Taifa;

(iii) Kuendelea kutoa mafunzo ya Utawala Bora kwa Viongozi wa Vyama vya Michezo vya Taifa kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika Sekta ya Michezo;

(iv) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Baraza la Michezo la Taifa na Vyama vya Michezo vya Taifa kwa kuwaandalia mafunzo kulingana na mahitaji yaliyopo;

(v) Kuendelea kusimamia mafunzo ya uongozi kwa Vijana kupitia michezo kwa Walimu na vijana wa Shule za Msingi na Sekondari kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa; na

(vi) Kuimarisha ushiriki wa wanawake katika michezo na uongozi wa michezo kwa kushirikiana na Baraza la Michezo la Uingereza *(UK Sport International)* kwa kuandaa mfumo wa utambuzi na uendelezaji wa vipaji katika michezo mbalimbali kupitia Mradi wa kuboresha maisha ya watoto *(International Inspiration)*.

Mheshimiwa Spika, Utawala na Rasilimali Watu. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imepanga kuwaendeleza watumishi katika mafunzo. Wizara itaendelea kuwasomesha watumishi 21, kati ya hao kumi na tano (15) ni wa mwaka wa fedha 2011/2012, wawili (2) wapya, na wengine wanne (4) wanaotarajiwa kustaafu. Wizara itatoa mafunzo elekezi kwa watumishi ishirini (20), wanaotarajiwa kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, Wizara yangu itaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika sekta inazozisimamia ili ziweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. Hii ni pamoja na kuongeza ajira, kipato, kulinda mazingira, kuleta amani na furaha katika jamii. Pamoja na kutumia fursa hizo, bado kuna changamoto ambazo zinahitaji zipatiwe ufumbuzi ili kuzitumia ipasavyo katika kuleta maendeleo ya nchi. Matarajio yangu ni kwamba changamoto zilizopo zitaendelea kupatiwa ufumbuzi hatua kwa hatua hasa kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na wadau wengine wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, shukrani, kwa niaba ya Serikali na kwa niaba yangu binafsi, naomba kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 katika kutimiza malengo yetu. Mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yamewezekana kutokana na ushirikiano uliopo miongoni mwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara na wadau wengine walio nje ya Wizara. Shukrani zangu za pekee ziende kwa Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, (Mb), Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ambaye amekuwa msaada mkubwa kwangu, Bw. Sethi Kamuhanda, Katibu Mkuu na Bibi Sihaba Nkinga, Naibu Katibu Mkuu.

Aidha, nawashukuru Wakurugenzi, Wataalamu na Watumishi wote wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na Asasi zilizo chini ya Wizara kwa juhudi walizofanya kuhakikisha kwamba wanatimiza ipasavyo majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, nitumie fursa hii tena kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo ambao wametuunga mkono wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Shukrani hizi ziwaendee wahisani waliotusaidia nikitarajia kuwa wataendelea na moyo huo. Siyo rahisi kuwataja wote lakini nitaje wachache ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Finland, Uingereza, Denmark, Japan, Sweden, Norway, Iran, Cuba, Korea ya Kusini, Marekani na Ujerumani pamoja na Mashirika ya kimataifa ya UNESCO, CYP, UNV, ILO, UNICEF, UNFPA, IYF na UNDP. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuvishukuru vyombo vyote vya habari nchini ambavyo vimefanya kazi nzuri ya kuitangaza nchi yetu. Ninaamini kuwa vyombo hivyo vitaendelea na kazi ya kuhabarisha, kuburudisha na kuelimisha umma kwa kuzingatia maadili. Aidha, ninamshukuru sana Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati, bila kuvisahau vituo vya Televisheni na Radio ambavyo kwa namna ya pekee vinarusha hotuba hii hewani.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti Kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 714,209,000 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imetengewa bajeti ya Shilingi 16,210,999,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara), fedha hizo zinajumuisha:-

- Mishahara ya Wizara - Shilingi 2,410,357,920.
- Mishahara ya Asasi - Shilingi 7,761,301,000.
- Matumizi Mengineyo ya Wizara - Shilingi 4,635,340,080.
- Matumizi Mengineyo ya Asasi - Shilingi 1,404,000,000.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 3,096,600,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Fedha za ndani ni shilingi 2,740,000,000 na fedha za nje ni shilingi 356,600,000.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango wa mwaka 2012/2013. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa fedha 2012/2013, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 19,307,599,000 ambapo kati ya hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 16,210,999,000 na fedha za Miradi ya Maendeleo ni shilingi 3,096,600,000.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: www.hum.go.tz.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Hoja hii imeungwa mkono. Hatua inayofuata nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii au mwakilishi wake, namwona Makamu Mwenyekiti.

**MHE. JUMA S. NKAMIA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) na 114(11) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, napenda kukushukuru kwa dhati kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilikutana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika vikao vyake vilivyofanyika tarehe 05 na 06 Juni, 2011 Jijini Dar es Salaam na tarehe 14 Mjini Dodoma. Katika vikao hivyo, Kamati ilipokea na kujadili kwa kina utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 pamoja na Mpango wa Maendeleo, Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2012/2013, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha na kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa Fedha 2012/2013. Aidha, Wizara ilitumia fursa hiyo kuelezea utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika mwaka wa fedha uliopita wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Wizara imejitahidi kwa kiasi kikubwa kutekeleza maoni na ushauri uliotolewa na Kamati. Kutokana na utekelezaji huo, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Mchanganuo mzuri wa bajeti ambao umeainisha matumizi ya fedha kwa kila kifungu;

(ii) Kuandaliwa kwa rasimu ya mpango wa mafunzo ambao utawagusa watumishi wa ngazi zote katika Wizara; na

(iii) Kuanzishwa kwa programu mbili za maendeleo ya vijana; ya kwanza ikijulikana kama “Kazi nje nje” ambayo inakuza dhana ya ujasiriamali na ukuzaji wa biashara miongoni mwa vijana. Programu hii inahusisha vijana 74,000 na tayari 1,740 wamebuni miradi ya uzalishaji mali.

Programu ya pili ni ya stadi za maisha kwa vijana walio nje ya shule ambayo inalenga kuwaelimisha vijana kuhusu UKIMWI, afya ya uzazi na athari za mimba za utotoni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado yapo mapendekezo ambayo utekelezaji wake haujakamilika. Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kuongeza juhudi katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mapendekezo hayo unakamilika mapema.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania *TBC*, Wizara itanunua OB *VAN* yaani *Outside Broadcasting Van* kwa ajili ya matangazo ya nje ya Radio na Televisheni ikiwemo mikutano ya Bunge na matukio ya kitaifa;

(ii) Kujenga vituo vya *FM* na kuongeza usikivu wa matangazo ya *TBC* katika Mikoa mipya ya Simiyu, Njombe na Geita, pamoja na Zanzibar;

(iii) Kuendesha mafunzo ya Stashahada kwa washiriki 150 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 200 walio kazini;

(iv) Kujenga jengo la utawala katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamayo (TaSuBa) na kukamilisha mitaala ya shahada ya kwanza ya sanaa za maonesho na za ufundi ili kuwasilisha *NACTE* kwa ajili ya kupewa ithibati;

(v) Baraza la Sanaa la Taifa litaendesha mafunzo ya Ukufunzi (TOT) kwa wasanii 20 kutoka Mikoa 10 kuhusu utengenezaji wa batiki, uchapaji na nguo za mafundo;

(vi) Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya "Lugha ya Taifa," vipindi 52 vya "Kumepambazuka" katika redio na vipindi 52 vya "Ulimwengu wa Kiswahili" katika televisheni;

(vii) Kuandaa na kuendesha semina ya matumizi ya Kiswahili Sanifu katika mabango, matangazo na lebo;

(viii) Kuchunguza maneno ya lugha za makabila na lahaja za Kiswahili yanayoweza kusanifiwa katika Mikoa ya Kanda ya Mashariki, Magharibi, Kusini na Kati;

(ix) Kukamilisha mchakato wa urasimishaji wa tasnia ya filamu, kusimamia ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na tasnia hii na kuhakikisha filamu zinazotengenezwa zinazingatia maadili ya Kitanzania na kuzingatia Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya Mwaka 1976 na Kanuni zake;

(x) Kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa Walimu wa Michezo wapatao 3000 nchini kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Manispaa; na;

(xi) Kuimarisha ushiriki wa Wanawake katika michezo na uongozi wa michezo kwa ushirikiano na *UK Sport International* kupitia mradi wa *International Inspiration*.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013. Ili Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iweze kutekeleza kikamilifu majukumu iliyojipangia kwa mwaka wa Fedha 2012/2013, inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 19.3. Ingawa kiasi hiki cha fedha kimeongezeka ikilinganishwa na shilingi bilioni 18.5 zilizoidhinishwa katika bajeti ya mwaka jana, bado bajeti hii ni finyu. Kamati inaishauri Serikali iangalie namna ya kuongeza fedha za bajeti ya Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake hasa kwa kuzingatia kwamba inashughulika na vijana ambao ni wengi na wanakabiliwa na changamoto nyingi ukiwemo ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2012/2013. Kamati inaipongeza Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* kwa namna ilivyotekeleza majukumu yake ikizingatia malengo iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2011/2012. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kununua na kufunga *saver* na *Deck* za *TV*, vifaa vya mfumo wa *Digital Intercom*, kifaa cha *satellite*, Jenereta tatu katika vituo vya Arusha, Mwanza na Mbeya na vifaa vya mfumo wa Dijitali kwa ajili ya kudhibiti matangazo *(remote monitoring).*

Mheshimiwa Spika, pia Shirika limeweza kukamilisha kazi ya kuunganisha mfumo wa *TV* na Radio kwenye Mkongo wa Taifa pamoja na kuweka mfumo mzuri wa kudhibiti matangazo *(TV & Radio Monitoring System of Airtime, Sales and Billing and SMS project)* kwa lengo la kuzuia wizi na kuboresha utendaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Shirika la Utangazaji Tanzania linakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Kuendelea kupungua kwa fedha inayotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Shirika limetengewa shilingi milioni 300, hii ikiwa ni wastani wa shilingi milioni 25 kwa mwezi. Fedha hizi ni pungufu kwa asilimia 75 ikilinganishwa na wastani wa milioni 100 kwa mwezi zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Hali hii inaathiri utendaji wa jumla wa shirika ikitiliwa maanani kuwa shirika linalipia umeme si chini ya milioni moja kwa mwezi, hivyo kiasi hiki kilichotengwa kinaweza kulipia umeme kwa miezi mitatu tu;

(ii) Uchakavu wa mitambo na uhaba wa majengo kwa ajili ya mitambo na ofisi;

(iii) Uchache na uchakavu wa vitendea kazi kwa upande wa Radio na Televisheni;

(iv) Ufinyu wa bajeti iliyodumaa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Shirika. Katika mwaka huu wa fedha *TBC* imetengewa shilingi milioni 500 kwa shughuli za maedeleo, kiasi ambacho ni sawa na kile kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Fedha hizi ni kidogo sana ikilinganishwa na hitaji la Shirika lisilopungua shilingi bilioni 12 kwa mwezi. Hata hivyo, licha ya kiwango hicho kuwa kidogo ikilinganishwa na mahitaji, bado fedha zimekuwa hazitolewi kwa wakati. Hali hii inalikwamisha Shirika kutekeleza shughuli za maendeleo na miradi mbalimbali;

(v) Utata katika utekelezaji wa Mkataba baina ya *TBC* na *Star Media (Tanzania) Limited* ambapo kuna madai kwamba, mkataba huo unainufaisha *Star Media (Tanzania) Limited* na kuinyonya *TBC* ambayo haina mwakilishi katika Menejementi ya Kampuni hiyo licha ya mkataba kuelekeza hivyo;

(vi) Kutotekelezwa kwa Mkataba wa Utendaji wa mradi wa dijitali ambao unasubiri dhamana ya Serikali kwa mkopo unaotarajiwa kutolewa na Benki ya Maendeleo ya China *(China Development Bank)*;

(vii) Ukarabati wa vifaa vya kurushia matangazo *(OB VAN equipment)* vya televisheni bado haujafanyika kutokana na ukosefu wa fedha;

(viii) Shirika lina upungufu wa watumishi 33 pamoja na vitendea kazi kwa ajili ya vituo vipya vya *FM* vilivyoanzishwa na vinavyotarajiwa kuanzishwa katika Mikoa mipya;

(ix) Bado Wizara na Idara nyingi za Serikali zinadaiwa na *TBC* madeni ya muda mrefu na ya karibuni kutokana na huduma za vipindi mbalimbali vilivyotangazwa. Hali hii inaiathiri *TBC* katika mwenendo wa kifedha na hivyo kukwamisha utendaji; na

(x) Hatua ya kutegemea Tume ya Ajira kupata wafanyakazi wapya, kunaiathiri *TBC*, kwani mbali na kuchelewesha utaratibu, bado shirika linaweza kukosa watu wenye sifa za ziada zinazohitajika katika utangazaji wa Televisheni na Radio kama vile mwonekano wa sura na sauti.

Mheshimiwa Spika, ili kuisaidia *TBC* iweze kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali itambue kwamba *TBC* ndicho chombo cha pekee cha utangazaji cha umma hivyo kinahitaji kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na pia maendeleo.

Aidha, fedha hizo zitolewe kwa wakati ili *TBC* iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati muafaka, hasa kwa kuzingatia kuwa mwaka huu nchi inakabiliwa na Sensa ya Taifa pamoja na mchakato wa kukusanya maoni kwa ajili ya mabadiliko ya Katiba na *TBC* kama chombo cha habari cha Umma ndicho chenye jukumu la kuwaelimisha Watanzania;

(ii) Ili kufikia lengo kabla ya ukomo wa matumizi ya mitambo ya kurushia matangazo katika mfumo wa analojia kwa nchi za Afrika Mashariki, ifikapo Desemba 31, mwaka huu, kampuni ya *Star Media (Tanzania) Limited* ambayo ni mbia mwenza wa *TBC* inatekeleza mradi wa televisheni kuhamia kwenye mfumo wa kurusha matangazo wa dijitali. Utekelezaji wa mradi huo umekuwa ukisuasua kutokana na Serikali kutotekeleza baadhi ya vipengele vya mkataba wa utendaji kikiwemo kile cha udhamini wa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya China *(China Development Bank)* ambao utagharamia ujenzi wa mitambo hiyo ya dijitali kwa nchi nzima. Hadi sasa ikiwa imesalia miezi mitano (5) kabla ya ukomo uliowekwa na mamlaka za mawasiliano kwa nchi za Afrika Mashariki katika matumizi ya mfumo wa analojia, ujenzi umekamilika katika Mikoa saba (7) tu.

Kamati inaisisitizia Serikali juu ya umuhimu wa kutoa udhamini wa mkopo huo haraka iwezekanavyo ili kuiepusha nchi na athari ambazo zitajitokeza iwapo muda wa ukomo utafika kabla ya mradi huo haujakamilika. Serikali ni vyema ikazingatia kwamba, ni *TBC* pekee ndiyo imeanza utekelezaji wa ujenzi wa mitambo ya dijitali;

(iii) Aidha, Kamati inashauri kuwa Serikali za nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zibadilishe tarehe ya mwisho ya kutumika kwa mitambo ya analojia yaani Desemba 31 mwaka huu na kuisogeza mbele, kwani Kamati inaamini hiki ni kipindi kifupi mno na hata nchi zilizoendelea zimeweka ukomo kwa matumizi ya mitambo hiyo ya analojia kuwa Desemba 31 mwaka 2015.

Kwa upande mwingine, Kamati inahoji kuwa ikiwa mataifa yaliyoendelea katika nyanja zote ikiwemo ya teknolojia ya mawasiliano na habari yametenga muda wa kutosha kujiandaa kabla ya kuachana na mfumo wa matangazo wa analojia na kuhamia mfumo wa dijitali, kwa nini nchi ambazo bado ziko nyuma kimaendeleo na hasa kiteknolojia zinataka kutekeleza mabadiliko hayo ya mfumo wa matangazo kutoka analojia kwenda dijitali kwa haraka kiasi hicho?

(iv) Ni aibu kwa chombo cha habari cha Umma kama *TBC* kuendelea kuwa katika majengo ya ofisi ambayo ni chakavu. Kamati inaishauri Serikali itoe dhamana ya asilimia 100 ili Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* ambao uko tayari kukamilisha ujenzi wa jengo hilo uweze kuanza utekelezaji. Kukamilika kwa jengo hilo ambalo msingi wake uliwekwa zaidi ya miaka 10 iliyopita, kutaiwezesha *TBC* kuhamia Mikocheni na hivyo kutoa nafasi kwa ofisi zake za *Nyerere Road* kutumiwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kama ofisi na hivyo kuokoa fedha nyingi zinazotumiwa na Wizara kwa ajili ya kodi ya pango;

(v) Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zilipe madeni ambayo zinadiwa na *TBC* kama malipo ya vipindi vya Televisheni na Radio ili kuiwezesha *TBC* kugharamia utekelezaji wa baadhi ya huduma hasa pale ambapo ruzuku ya Serikali imechelewa au haitoshi;

(vi) Serikali iiwezeshe *TBC* kukarabati au kununua vifaa vya kurushia matangazo *(OB VAN equipment)* vya televisheni vipya ili iweze kurusha matangazo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, mfano michezo ya mpira wa miguu inayochezwa hapa nchini na nje ya nchi, michezo ya olimpiki na ile ya Jumuia ya Madola. Mara kadhaa *TBC* imeshindwa kufanya hivyo kwa kuwa vifaa vilivyopo havikidhi haja. Mfano, kifaa cha sasa ambacho kina uwezo wa kuwa na kamera 6 hadi 8 hakina hata kamera moja na kimechakaa; na

(vii) Kwa kutambua ufinyu wa bajeti hii inayotengwa kwa ajili ya *TBC*, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha kodi ya televisheni yaani *TV license* ili sehemu ya fedha hizo iweze kutumika kimarisha *TBC* kama ilivyo katika nchi za Ghana, Uingereza, Japan na nyingine nyingi ambazo zinakusanya kodi hiyo kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa mashirika ya utangazaji ya umma. Kamati inaamini kwamba, iwapo jambo hili litafanyika, litapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya kuliendesha shirika hili.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Haki ya Kupata HabarI na Muswada wa Huduma za Vyombo vya Habari. Ni muda mrefu umepita tangu Serikali ilipouondoa Muswada wa Habari kwa lengo la kuuboresha kabla ya kuuwasilisha tena Bungeni. Kuendelea kuchelewa kwa Muswada huo kumekuwa kukiibua manung'uniko miongoni mwa wadau wa habari nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wake, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali juu ya kuharakisha mchakato wa maandalizi ya Muswada wa Haki ya Kupata Habari na ule wa Huduma za Vyombo vya Habari. Kukamilika kwa Miswada hii, kutawezesha kupatikana kwa Sheria zitakazosimamia tasnia ya habari nchini na kuifanya iendeshwe kwa kuzingatia taaluma, weledi, miiko na maadili pamoja na kutoa fursa kwa umma kupata taarifa, jambo ambalo ni haki ya msingi kama inavyotamkwa na katika Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati jamii ikisubiri kwa hamu Serikali kutekeleza ahadi ya kuuwasilisha Muswada huo Bungeni mwaka huu, ni imani ya Kamati kuwa Serikali itatekeleza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri Serikali iendelee kushirikiana na Baraza la Habari Tanzania *(MCT)*, Jukwaa la Wahariri *(TEF)*, Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari *(MOAT)*, Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika *(MISA)* pamoja na Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania *(TMF)* ili kuhakikisha wadau wakuu wa habari (waandishi wa habari, wamiliki wa vyombo

vya habari na vyombo vya habari) wanatimiza wajibu wao kwa kuzingatia taaluma, weledi na maadili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa kupata habari ni haki ya Kikatiba ya kila mwananchi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inawawezesha Watanzania kupata haki hiyo muhimu. Sote tunatambua kuwa pale wananchi watakapowezeshwa kupata taarifa muhimu zinazowahusu ndipo wataweza kufanya maamuzi sahihi juu ya jambo lolote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ule msemo wa Kiingereza kwamba, *'information is power'*, Kamati inadhani ni muhimu wananchi wakawezeshwa kisheria kupata taarifa sahihi na kwa muda muafaka kwa lengo la kuwapa uwezo wa kupambanua masuala mbalimbali yanayohusu maisha yao na mustakabali wa Taifa lao. Kutungwa na kutekelezwa kikamilifu kwa Sheria ya Haki ya Kupata Habari, kutachagiza ukuaji wa demokrasia na kustawisha uwazi na uwajibikaji katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA). Lugha yetu ya Kiswahili inazidi kupata mashiko na kukua kwa kasi duniani ambapo sasa inakadiriwa kuwa na wazungumzaji zaidi ya milioni 500. Lugha hii adhimu inatambulika na kutumika katika majukwaa ya kimataifa kama vile vyombo vya uwakilishi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika. Hata hivyo, ni jambo la kusikitisha kwamba, Tanzania ambayo ni kitovu cha lugha hii imekuwa haichukui nafasi yake kikamilifu katika kukitangaza Kiswahili kwenye medani ya kimataifa na badala yake nchi jirani ndizo zimekuwa mstari wa mbele katika kukieneza na kukitumia katika majukwaa hayo. Kwa kuzingatia umuhimu huo wa lugha ya Kiswahili, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iiwezeshe BAKITA katika azma yake ya uchunguzi wa maneno ya lugha za makabila na lahaja za Kiswahili ambayo yanaweza kusanifiwa katika maeneo mbalimbali nchini;

(ii) Serikali iendelee kusisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mikutano, semina, warsha, mabango ya matangazo barabarani, matangazo ya biashara pamoja na maelekezo yaliyo katika bidhaa zinazotengenezwa nchini. Serikali pia iwe makini na kauli zake kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli rasmi za Serikali kwani suala hilo limekuwa likileta mkanganyiko;

(iii) Serikali iangalie umuhimu wa kulishirikisha Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) katika kuandaa vitabu vya Bajeti za Serikali kwa miaka ijayo kwa Lugha ya Kiswahili ili kuwapa wananchi fursa ya kuelewa na kufuatilia kikamilifu hali ya kiuchumi, mapato ya Serikali pamoja na utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele; na

(iv) Serikali kwa kutumia Balozi zetu iandae mazingira yatakayoiwezesha lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa nje ya nchi kwa kutafuta fursa za kufundisha lugha hiyo katika vituo vya lugha na Vyuo Vikuu vya nchi husika. Utafiti unaonesha kuwa yapo mahitaji ya raia wa mataifa mengine kutaka kujifunza lugha hii. Mfano, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wapo raia wa mataifa mbalimbali ambao wanajifunza Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Tasnia ya sanaa ni moja ya maeneo ambayo yakitazamwa vizuri na kuboreshwa yataweza kuvutia vijana wengi wasio na ajira. Tasnia hii pia inaweza kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi na hivyo kukuza pato la Taifa. Kutokana na usimamizi hafifu wa kazi za sanaa ya muziki, mapato yanayopatikana ni asilimia 12 tu ya kiwango ambacho kingepaswa kukusanywa kutoka katika sekta hii. Usimamizi hafifu huo wa kazi za Wasanii na mapato yake haujitokezi katika tasnia ya muziki pekee, bali hata katika maeneo mengine kama vile sanaa za michezo ya kuigiza, filamu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa, udhaifu huo wa usimamizi ambao umetoa mwanya kwa maharamia wa kazi za wasanii kuendelea kujinufaisha isivyo halali, unachangiwa na mapungufu yaliyomo kwenye Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 pamoja na usimamizi hafifu wa utekelezaji wa sheria hiyo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuitikia wito uliotolewa na Kamati wa kutaka sheria hiyo ifanyiwe marekebisho ambapo mchakato umeshaanza na sasa Waraka wa Mawaziri umeshawasilishwa katika Sekretarieti ya Baraza la

Mawaziri. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali iharakishe ukamilishwaji wa mchakato huo ili kuwakomboa Wasanii dhidi ya uharamia unaofanywa katika kazi zao na watu wachache ambao wananufaika kupitia migongo ya Wasanii.

Mheshimiwa Spika, iwapo sheria hiyo itafanyiwa marekebisho na utekelezaji wake ukasimamiwa kikamilifu, faida zifuatazo zinatarajiwa kupatikana:-

(i) Ongezeko la mapato yatokanayo na kazi za sanaa kwa wadau wote wa tasnia ya sanaa pamoja na Serikali ambayo itaweza kuongeza wigo wake wa kodi;

(ii) Mazingira ya kazi za sanaa yataboreshwa na kipato cha wasanii kitaongezeka na tasnia hii itaweza kuvutia vijana wengi wasio na kazi na hivyo kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira nchini; na

(iii) Tasnia ya sanaa itaonekana ni ajira ya kudumu na hivyo kuwafanya watu wajikite huko muda mwingi tofauti na sasa ambapo wengi hujihusisha na sanaa kama kazi ya kujipatia kipato cha ziada na hutenga muda mchache wa kujihusisha nayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inatambua na kupongeza hatua ambazo zimechukuliwa hadi sasa na Serikali katika kulinda Hakimili na Hakishiriki za kazi za wasanii. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Makubaliano ya *TRA* kutoa stika kwa ajili ya kazi za filamu na muziki, yaliyofikiwa baina ya Wizara za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fedha, Viwanda na Biashara. Stika hizo zitasaidia kurasimisha kazi za wasanii na hivyo kurahisisha ufuatiliaji wa kina katika kazi hizo tangu hatua ya maandalizi hadi usambazaji wake; na

(ii) Mpango wa kuanzisha mtandao wa kielektroniki *(electronic network system)* ambao utaunganisha wadau, Wizara na taasisi zinazosimamia tasnia ya filamu na muziki ili kuharakisha taratibu za kuingiza kazi za wasanii sokoni.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha mafanikio endelevu yanapatikana katika juhudi hizo ambazo zinafanywa na Serikali kulinda Hakimiliki na Hakishiriki za kazi za wasanii nchini Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Vyombo vya kusimamia utekelezaji wa sheria vishirikiane na *COSOTA* na viongeze juhudi za kukabiliana na uharamia wa kazi za sanaa;

(ii) Baraza la Sanaa kwa kushirikiana na Bodi ya Filamu Tanzania, liongeze juhudi katika kudhibiti uingiaji holela wa filamu za nje zenye maudhui inayopingana na maadili ya Taifa letu; na

(iii) Ili kuhakikisha inaibua na kukuza vipaji katika tasnia ya sanaa, Serikali iboreshe vyuo vya sanaa vinavyotoa mafunzo ya ukufunzi *(TOT)* na ishirikiane na BASATA kufuatilia wahitimu na kuwafanyia tathmini ili kujua iwapo ujuzi wanaoupata ni endelevu na unanufaisha wengine au la.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Baraza la Michezo Tanzania ndicho chombo chenye dhamana kisheria kuhamasisha wananchi wa ngazi zote wapende na kujihusisha na michezo. Chombo hiki pia kinapaswa kuendeleza na kusimamia vyama vya aina zote za michezo ya ridhaa. Kamati inapenda kutumia fursa hii kuupongeza uongozi wa chombo hiki chini ya Mwenyekiti wake Dionizi Malinzi kwa namna ambavyo umekuwa ukijitahidi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi tangu uliposhika hatamu licha ya ufinyu wa bajeti ambao unalikabili baraza. Tunawaahidi viongozi hao ushirikiano wa kutosha katika juhudi za kusimamia na kuinua ari ya michezo nchini kwani sote tu wadau wa michezo, michezo ni afya na michezo huleta furaha.

Mheshimiwa Spika, licha ya majukumu mazito ambayo yanakikabili chombo hiki, bado kimekuwa kikitengewa bajeti finyu sana ambayo inakifanya kiiendelee kukabiliwa na changamoto kadhaa miongoni mwa hizo zikiwa zifuatazo:-

(i) Ukosefu wa ofisi zinazoendana na hadhi ya chombo hiki. Kwa sasa ofisi za Baraza ziko katika majengo ya siku nyingi ambayo ni mabovu; na

(ii) Ukosefu wa fedha kwa ajili ya maandalizi ya timu zinazopata fursa ya kuiwakilisha nchi katika mashindano ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Baraza la Michezo Tanzania kukabiliana na changamoto hizi, Kamati inatoa ushauri ufuato:-

(i) Serikali iongeze bajeti inayotengwa kwa ajili ya Baraza na pia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo, ambalo litakapokamilika litawezesha Baraza la Michezo kupata ofisi za kisasa. Kabla kazi hiyo haijakamilika, Kamati inashauri Baraza la michezo lihamishie ofisi zake katika uwanja mkuu wa Taifa kwa sasa kwani ofisi zilizopo ziko katika hali mbaya;

(ii) Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuhudumia timu za Taifa za michezo mbalimbali zinapopata fursa ya kuiwakilisha nchi katika michezo ya kimataifa;

(iii) Wizara itafakari uwepo wa Baraza la Michezo na Kurugenzi ya Michezo katika Wizara kama havileti mgongano katika utekelezaji wa majukumu yao;

(iv) Kamati inaamini kwamba kuwepo kwa michezo ya ligi kuu ya soka ya muungano kutainua kiwango cha soka kama ilivyo kuwa hapo nyuma hivyo inashauri Baraza la Michezo la Taifa BMT na lile la Zanzibar BMZ kukaa na TFF na ZFA ili kuirejesha ligi kuu ya soka ya Muungano kuanzia mwakani;

(v) Kuwe na utaratibu utakaowawezesha wataalamu wa michezo wa nje wanaokuja kufundisha michezo, kuwarithisha ujuzi wataalamu wa ndani *(succession plan)* ili wanapoondoka, Taifa liweze kubakiwa na ujuzi huo; na

(vi) Serikali ihakikishe maafisa wanaoteuliwa kusimamia michezo katika ngazi za Mikoa na Wilaya wanatengewa fedha ili waweze kuhamasisha maendeleo ya michezo katika maeneo yao kuliko ilivyo sasa ambapo wanategemea hisani ya Maafisa Tawala wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Vijana. Vijana ndiyo nguzo na nguvu ya Taifa lolote duniani. Dhana hiyo inatokana na ukweli kwamba, vijana ndiyo kundi kubwa katika jamii. Takribani nusu ya Watanzania ni vijana, lakini sehemu kubwa ya vijana hao hawana ajira. Wengi wa vijana hao wako katika kipindi cha mpito *(transition period)* baada ya kuhitimu masomo katika ngazi mbalimbali za elimu na wako mtaani, hawajui waelekee wapi.

Mheshimiwa Spika, ni ukosefu wa ajira kwa vijana ndiyo unaifanya Dunia kuingiwa na hofu kwamba huenda hili bomu linalosubiri muda ufike ili liweze kulipuka *(timed bomb).* Kamati isingependa kuona Taifa letu nalo linaingia katika mkumbo huo wa hofu na badala yake inashauri hatua za makusudi kuchukuliwa na Serikali ili kuboresha Sekta ya Maendeleo ya Vijana kwa kukabili changamoto zinazowakabili vijana na kutatua tatizo la ajira ambalo ndilo kubwa.

Mheshimiwa Spika, ingawa Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuwaendeleza vijana, bado ingependa kutilia mkazo maeneo yafuatayo:-

(i) Wizara iharakishe mchakato wa kusajili vituo vinavyotoa mafunzo ya vijana katika Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* ili vipatiwe ithibati ambayo itawezesha mafunzo kutolewa katika ngazi zote za elimu ya juu;

(ii) Serikali iongeze bajeti ili kuwezesha vijana wengi kupata mafunzo ya programu ya ujasiriamali kwa vijana ambayo yanalenga kuwawezesha kujiajiri kwa kubuni na kuanzisha miradi ya uzalishaji mali;

(iii) Serikali iongeze fedha za kutekeleza programu ya Stadi za maisha kwa vijana walio nje ya shule. Programu itaanza kwa kuwapata waelimishaji rika kitaifa ambao wataandaa waelimishaji rika katika ngazi ya Kata. Lengo la programu ni kuwaelimisha vijana kuhusu uzazi, athari za mimba za utotoni na namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU; na

(iv) Serikali iuongezee fedha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana nchini *(YDF)* ili kuwezesha vijana wengi zaidi kupata mikopo ambayo itawawezesha kujiajiri na hivyo kuondokana na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla. Pamoja na maoni yote hayo. Kamati inatoa ushauri wa jumla wa kisekta kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ikamilishe uanzishwaji wa Mfuko wa Vijana ili kuwawezesha vijana kupata mitaji ya kuanzisha miradi ambayo itawawezesha kujikwamua kiuchumi;

(ii) Ili kusaidia kundi kubwa la vijana ambalo liko katika kipindi cha mpito *(transition period)* baada ya kuhitimu elimu katika ngazi mbalimbali na sasa liko mtaani, Kamati inashauri, Serikali ianzishe kituo cha kutambua vijana hao na ujuzi walionao, kuwapatia stadi zitakazosaidia kuwabadilisha mtazamo wao *(mind set)* na kuwa Serikali pekee ndiyo itakayowakwamua kimaisha na kuwawezesha kwa kuwapatia vitendea kazi na mitaji. Hilo linawezekana na mfano mzuri ni katika Mkoa wa Pwani ambako Mkuu wa Mkoa - Mwantumu Mahiza amewezesha vijana zaidi ya 100 kujitambua, kupatiwa stadi za kazi na kisha kujiajiri katika uzalishaji;

(iii) Serikali iangalie namna nzuri ya kuwashirikisha vijana katika mpango wa Kilimo Kwanza kwa kuwatambua na kuwatenga katika kanda na kisha kuwawezesha kuendesha kilimo cha kisasa cha mazao ambayo yanalimwa kwa wingi katika kanda hizo. Mfano ni Kanda ya Kusini (Korosho), Kanda ya Kaskazini (Maua na Kahawa), Kanda ya Ziwa (Pamba) na Kanda ya Kati (Alizeti) na kadhalika;

(iv) Serikali ichukue juhudi za makusudi kulisaidia Shirika la Utangazaji Tanzania *TBC* kifedha, kwani lina hali mbaya kwelikweli na huenda ikafikia wakati likafunga matangazo yake. Hatua hiyo italisaidia Shirika hilo kutimiza wajibu wake kikamilifu hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa linajiandaa kwa ajili ya sensa ya watu na makazi na pia mchakato wa kukusanya maoni kwa ajili ya mabadiliko ya Katiba;

(v) Serikali itazame upya na kuuboresha mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya *Star Media (Tanzania) Limited* na *TBC* unaohusu kubadili mfumo wa matangazo kutoka analojia kwenda dijitali. Mapungufu yaliyo katika mkataba huo yanaiathiri zaidi *TBC* na pia mkataba huo unahusu *TV* peke yake na kuiacha Radio kitu ambacho si kizuri;

(vi) Serikali iisaidie *TBC* kupata hati za kumiliki maeneo ya ardhi waliyo nayo katika Mikoa ya Dar Es Salaam, Mwanza na kwingineko ili waweze kuingia ubia na makampni mbalimbali yenye nia ya kuwekeza na hivyo kuipunguzia ukata;

(vii) Fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo ni chache sana, jambo ambalo litachelewesha kukamilika kwa mradi huu. Serikali iongeze fedha ili mradi huu uweze kukamilika haraka ambapo miongoni mwa mambo mengine utawezesha Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Baraza la Michezo kupata ofisi zenye hadhi;

(viii) Serikali ianze utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya programu za timu za Taifa badala ya mzigo huo kuachwa kwa vyama vya michezo husika pamoja na wadhamini. Kamati haioni mantiki ya kutenga fedha kwa ajili ya kuwalipa walimu Walimu wa timu za Taifa wakati hakuna fedha inayotengwa kwa ajili kuhudumia timu hizo;

(ix) Serikali ibuni utaratibu wa kusimamia na kuendesha Uwanja wa Taifa kwa tija zaidi. Kamati inashauri atafutwe Meneja Binafsi *(Private Manager)* au kampuni ili kutekeleza jukumu hilo. Utaratibu huo utasaidia kupunguza utitiri wa mgawanyo wa mapato, utaongezea

mapato ya Serikali na vilabu na wachezaji watanufaika zaidi kuliko ilivyo sasa ambapo wanavuja jasho lakini hawafaidi matunda yake; na

(x) Serikali iharakishe mchakato wa kutunga sheria ambazo zitawezesha kutekelezwa kwa Mikataba na Maazimio ya Kimataifa ambayo yameridhiwa na nchi yetu ili kuliwezesha Taifa kunafaika nayo.

Mheshimiwa Spika, shukrani. Nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Kwa niaba ya Kamati, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara (Mb) - Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Naibu Waziri - Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla (Mb); Katibu Mkuu - Ndugu Sethi Kamuhanda; Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Sihaba Nkinga na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa waliotuonesha wakati tunatekeleza shughuli za Kamati. Ninawashukuru na kuwatakia mafanikio zaidi katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mhe. Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti na Mheshimiwa Juma Nkamia Suleiman, Makamu Mwenyekiti. (Makofi)

Wengine ni Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Donald Kevin Max, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa Asha Mohamed Omar, Mheshimiwa Ramadhan Haji Salehe, Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo na Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah akisaidiwa na Makatibu wa Kamati, Ndugu Chacha Nyakega na Ndugu Hosiana John, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru Wanambeya wenzangu kwa imani na ushirikiano wao kwangu kwani ndiyo vitu vinavyonisukuma kuwatumikia na ninapenda kuwahakikishia kuwa tulivyoanza ndio tutakavyoamaliza kwa nguvu ya umma.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa heshima kama nitashindwa kutambua msaada na mchango wa CHADEMA Makao Makuu na Mkoa wa Mbeya katika kuhakikisha Mbeya tunakwenda sawa na nguvu ya umma inaendelea kushinda. Sambamba na hilo, ni kumshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mb), kwa imani yake kwangu hivyo

kuniteua tena kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii. Natoa ahadi kwake na kwa Kambi nzima kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kutimiza yale yote ninayotakiwa kuyafanya. Mwisho lakini kwa umuhimu, niishukuru pia familia yangu na marafiki zangu, naomba tuzidi kuombeana Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Habari. Sheria ya Vyombo vya Habari. Kwa muda mrefu sasa wanahabari pamoja na wadau wengine wa tasnia hii wamekuwa wakiitaka Serikali kuleta Muswada wa Sheria Mpya ya Habari ili kuweza kuwa na sheria inayokidhi matakwa ya uhuru wa vyombo vya habari nchini lakini Serikali imekuwa ikitoa ahadi ambayo haijatekelezwa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, kukamilisha kutunga sheria kuhusu vyombo vya habari ni jambo ambalo litafanya Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 kufutwa. Pamoja na Serikali kutoa kauli kuwa kuna uhuru mpana wa vyombo vya habari nchini bado mfumo wa kisheria ni kandamizi, jambo ambalo linaleta mashaka makubwa kuhusu uhuru wa vyombo vya habari ambapo uhuru huo utakuwa unatolewa kama zawadi kulingana na aliyepo madarakani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tunahoji; kwa nini utekelezaji wa suala hili umechukua muda mrefu na kila mwaka Serikali imekuwa ikija hapa Bungeni na kutoa ahadi? Kudhihirisha hilo, naomba kunukuu Hotuba ya Waziri wa Habari ya mwaka wa fedha 2010/2011, ukurasa 61 kama ifuatavyo:-

*"Kufuta sheria za vyombo vya habari zilizopitwa na wakati na ambazo zinalalamikiwa na wadau".*

Mheshimiwa katika hotuba ya Waziri kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ukurasa wa 5 ahadi ziliendelea kutolewa kama ifuatayo:-

*"Hivi sasa Wizara inaendelea na mchakato wa kukamilisha Sera Mpya ya Habari na Ukamilishaji wa Rasimu ya Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari".*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali iache kutoa ahadi zisizotekelezwa kila mwaka ambapo na mwaka huu pia Serikali hii hii inakuja na ahadi nyingine tena kwa mwaka huu wa fedha kama inavyoonekana katika randama ya Wizara ukurasa wa 9:-

*"Kukamilisha Mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari hivi sasa ipo katika ngazi ya maamuzi".*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Baraza la Umoja wa Mataifa ya tarehe 12/03/2012 kuhusu mapitio ya masuala ya haki za binadamu, Serikali ilitoa taarifa, naomba kunukuu (taarifa ya lugha ya Kiingereza):-

"Serikali imejipanga kupitia upya sheria zinazohusiana na uhuru wa habari. Miswada ya Sheria ya Magazeti na Vyombo vya Habari kwa Tanzania Bara zipo katika hatua ya mwisho kwenye Baraza la Mawaziri. Kwa Tanzania Zanzibar mchakato upo katika hatua za awali". (Tafsiri yangu).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuungwa mkono kwa kauli hii ya Serikali na Baraza la Umoja wa Mataifa, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kutoa kauli rasmi kwa Bunge hili Tukufu kuwa ni lini sheria hizo zitaletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uhuru wa Habari/Maoni. Uhuru wa vyombo vya habari hauwezi ukahuishwa na kuwa uhuru wa mtu kupokea na kutoa habari/maoni. Kwa mwaka uliopita tulihoji pamoja na kusisitiza kutungwa kwa sheria inayotoa uhuru wa vyombo vya habari na uwepo na mchakato wa kutunga sheria ya uhuru wa habari/mawazo.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa mbalimbali kama ambavyo zimekuwa zikitolewa na vyombo vya habari kuwa wapo wananchi katika baadhi ya maeneo nchini ambao wamekuwa

wakikamatwa au kutishwa mara kwa mara kwa kuwahoji viongozi kwenye mikutano ya hadhara jambo ambalo ni kinyume na Katiba.

Mheshimiwa Spika, matatizo haya yanatokana na kutokuwepo kwa sheria inayotoa uhuru wa kutoa na kupokea maoni kwa kila Mtanzania kuliko msimamo wa Serikali wa sasa wa kubaki na Ibara ya 18 pekee ya Katiba yetu bila kuwa na sheria ya kutekeleza Ibara hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kuwapo kwa uhuru huo uliotajwa katika Katiba, tumeshuhudia Serikali ikikandamiza uhuru huu. Serikali imekuwa ikivinyanyasa baadhi ya vyombo vya habari kwa kisingizio cha kuandika habari za uchochezi. Imekuwa ikivinyima matangazo baadhi ya vyombo vya habari na hasa magazeti ambayo yanachapisha nakala nyingi na badala yake imekua ikitoa matangazo hayo kwa magazeti madogo, machanga na yale yanayochapisha nakala chache. Mfano hai, ni gazeti la Uhuru na Habari Leo yanayochapisha nakala zisizozidi 7,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni babu hivyo lazima ikubali kujenga utamaduni wa kuvumilia na kukubali kukosolewa. Katika nchi nyingi zilizoendelea duniani, maendeleo yamepatikana kutokana na Serikali kuvitumia vyombo vya habari kujitazama na kuwasilisha ujumbe wake mbele ya wananchi. Tabia ya Serikali ya kuminya vyombo vya habari hasa vyombo vya habari huru, haiwezi kukubalika. Sisi kambi ya Upinzani tunapinga kwa nguvu zote ujima huu.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Baraza la Umoja wa Mataifa kama nilivyonukuu hapo juu inaonyesha kuwa Serikali haijaungwa mkono katika msimamo wake kuwa uhuru wa kutoa na kupokea maoni upo kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kauli ya Serikali kuhusu mchakato wa uwepo sheria hiyo ili kutoa nafasi kwa wananchi kutoa na kupokea maoni kuliko ilivyo sasa kwa Serikali kujinasibu kuwa kuna uhuru wa vyombo vya habari kwa kigezo cha uwepo idadi kubwa ya magazeti, vituo vya redio na televisheni.

Mheshimiwa Spika, Uhuru kwa Wahariri wa Vyombo vya Umma. Uhuru wa tahariri kwa vyombo vinavyomilikiwa na Serikali kama vile Magazeti ya *Daily News* na Habari Leo pamoja na Television ya Taifa na Radio zinazomilikiwa na Serikali, ni jambo la umuhimu mkubwa sana kwani hivi ni vyombo vya umma na vinajiendesha kwa kutumia kodi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, mbali na ukweli kwamba bodi ya uendeshaji wa vyombo hivyo ni huru kimuundo, lakini hakuna uhakika wa uhuru wa vyombo hivyo katika uandishi wa tahariri kwa vyombo hivyo bali tahariri inashawishiwa kwa kiasi kikubwa na mamlaka za uteuzi wa watendaji wakuu wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanzisha mchakato wa kuanzisha sheria ambayo italinda uhuru wa tahariri kama zitakavyokuwa zinatolewa na Wahariri Wakuu wa vyombo husika. Hii inatokana na ukweli kuwa mfumo wa siasa za vyama vingi unahitaji usawia katika uandishi wa tahariri bila kupendelea upande wowote au upotoshaji kwa lengo la kulinda wale waliowateua. Kambi ya upinzani tunataka kupata majibu ni lini Serikali italeta sheria hiyo hapa Bungeni ili kuviepusha vyombo vya umma kuendeshwa kwa matakwa ya Serikali bila kuzingatia uhalisia uliopo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kulinda Chanzo cha Habari. Taarifa muhimu ambazo kwa kiasi kikubwa zinahusu mustakabali wa matumizi ya rasilimali za nchi yetu kwa kiasi kikubwa zinakuwa za siri na hivyo kuzifanya zisiwe wazi kwa wananchi. Kitendo cha kuzifanya taarifa au nyaraka hizo kuwa siri hupelekea raia wema wanaozitoa kwa umma kupoteza ajira zao au kufunguliwa mashtaka kwa kutoa siri. Hii inatokana na ukweli kwamba waandishi wa habari hawana sheria inayowalinda katika utendaji kazi wao wa kuipatia jamii kile inachotakiwa kukielewa.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya vyombo vya habari ambavyo kwa umahiri wao wa kutafuta na kuhabarisha jamii walipata nyaraka hizo zenye mihuri ya “za siri” na kuziandika kwenye

magazeti yao. Kwa masikitiko makubwa ni kuwa walipata msukosuko mkubwa kutoka kwenye vyombo vya dola na pia kuwalazimisha kueleza chanzo cha habari hizo au kuwakataza kuendelea kuandika habari husika.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili hutumika sana Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970 *(The National Security Act)* kama ilivyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, Na.133, kifungu cha 2(1) ambapo kinaeleza kuwa mambo ya siri ni pamoja na nyaraka zote za Serikali zenye muhuri wa neno siri na hakuna utaratibu unaoeleweka kuwa ni nyaraka ipi inakuwa siri na ni wakati gani kwani mara nyingine zipo barua zinapigwa mihuri hiyo lakini hazina usiri wowote kwenye maudhui ya barua husika.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kilitumika kulifungia gazeti la Kulikoni mwaka 2009 kwa siku 90 na magazeti ya Mwanahalisi na Mwananchi kupewa barua za onyo kuhusiana na habari ambazo walizichapisha. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka kifungu cha kulinda waandishi kutokueleza chanzo cha habari kama itatokea kuwa habari hiyo inahusu maslahi mapana ya nchi na kama wakitakiwa kufanya hivyo basi iwe ni Mahakamani na sio kwenye Serikali hiyohiyo ambayo inakuwa ni mtuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya michezo ni eneo ambalo kama likiwekezwa vyema inaweza kuwa nimojawapo ya vyanzo vikuu vya mapato na kuchangia katika pato la Taifa. Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo wananchi wake wengi ni wapenzi wa michezo mpira wa miguu, pete, kikapu, masumbwi, riadha, bao na kadhalika. Hili linajidhihirisha kutokana na uchangiaji wa hiari kwa ujenzi wa viwanja vya michezo, uchangiaji wa timu mbalimbali za michezo zinapokuwa zikijiandaa katika mashindano mbalimbali katika ngazi ya Taifa hadi Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na matukio mengi ya michezo yanayohusu kuuza na kununua wachezaji kwa timu za ndani na nje, lakini kwa masikitiko makubwa Serikali haina takwimu za kifedha ni kiasi gani cha fedha Serikali imepata kama stahiki yake ya kodi. Aidha, sambamba na hilo baada ya kupitia kitabu cha hali ya uchumi hakuna sehemu inayoonyesha kuwa Serikalini kuna chochote kinapatikana kutoka sekta ya michezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uwekezaji wowote unaofanyika lengo kuu ni kupata faida, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni kiasi gani kinatarajiwa kupatikana na baada ya muda gani kutokana na uwekezaji wa shilingi bilioni 56.4 uliofanywa na Serikali kwenye uwanja wa michezo wa Taifa?

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Serikali imeshindwa kutumia fursa hii ya kuwekeza vilivyo katika sekta ya michezo, michezo kama michezo ni fursa pekee ya kuitangaza nchi yetu katika medani za kimataifa. Kenya imetumia vyema fursa hiyo, kwani wao wamejikita katika riadha na imewalipa, dunia inaelewa wanariadha mahiri wa mbio ndefu duniani ni kutoka Kenya na Ethiopia na sasa Jamaica kwa mbio fupi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa kila mara ikipendekeza na kuishauri Serikali kuanzisha uwekezaji mkubwa katika sekta ya michezo kwa ujumla lakini mapendekezo na ushauri huo umeshindwa kuchukuliwa kwa umakini. Tunaamini kabisa kuwa mazingira ya wanakotoka wanariadha maarufu nchini Kenya na Ethiopia ni sawasawa kabisa na mazingira yaliyopo Tanzania, tatizo ni umakini wa mipango yetu na ufisadi katika vyama vyetu vya michezo na wale wote waliopewa dhamana ya kusimamia michezo.

Mheshimiwa Spika, malipo kwa Makocha Wazalendo. Yapo malalamiko ya muda mrefu ya Makocha Wazalendo wanaofundisha timu zetu ambapo wamekuwa wakipata malipo kidogo sana ukilinganisha na makocha kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka 2011/2012, tulihoji suala hili na Naibu Waziri wakati akichangia katika hoja ya Waziri katika Wizara hii alisema yafuatayo na naomba kunukuu:-

*"…Hoja ya malipo kwa Makocha Wazalendo, Mheshimiwa amezungumzia malipo kwa Makocha Wazalendo kwamba Makocha Wazalendo malipo yao ni tofauti na wale wa nje. Katika enzi napenda kusema tu kwamba Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) lipo katika mchakato wa kuandaa mikataba kwa makocha wazalendo wanaofundisha timu za Taifa. (Makofi)"*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu kuhusu hatua iliyofikiwa kuhusiana na maandalizi ya mikataba kwa Makocha Wazalendo. Hii ni kwa sababu katika randama iliyotolewa na Wizara kuhusu Fungu 96, ukurasa wa 27, Serikali imetenga shilingi milioni 400 kwa ajili ya makocha wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Makocha Wazalendo wanalipwa vizuri na pia uwepo mkakati maalumu kwa ajili kuwaendeleza na kuwafundisha wengine kuliko kutegemea kila wakati makocha wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili la Kambi ya Upinzani kuhusu kuwaendeleza Makocha Wazalendo na kuwafundisha wengine wapya linatakiwa kwenda sambasamba na kuanzisha shule za michezo *"sports academy"* ambazo zitakuwa chachu katika ukuaji wa michezo nchini kwa sababu michezo ni ajira.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Timu za Taifa. Maendeleo ya michezo nchini hasa mpira wa miguu na pete bado yanasuasua na hii inatokana na kutokuwa na bajeti rasmi ya timu zetu za Taifa. Ukata wa fedha katika timu zetu za Taifa unajitokeza mara kwa mara timu zetu zinapokuwa na mashindano ya kimataifa na kupelekea kutafuta michango kutoka kwa wananchi na wahisani mbalimbali. Kambi ya Upinzani haioni tatizo la wananchi na wadau mbalimbali kuchangia timu zetu za Taifa. Tatizo lililopo ni kuwa Serikali haitengi bajeti ya mwaka kwa ajili ya timu zetu na kufikia hatua kumfanya hata mke wa Waziri Mkuu hivi karibuni kuonekana kwenye vyombo vya habari akitembeza bakuli kwa wahisani kuomba fedha kwa ajili ya chama cha Netiboli Tanzania, wakati bajeti iliyokuwa inahitajika ni shilingi milioni 100 tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya timu zetu zote zinazoshiriki mashindano ya kimataifa ili kuweka dhamira ya dhati kuendeleza michezo nchini kwani tusitegemee kuvuna wakati hatujapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Viwanja. Sambamba na kuwa na bajeti ya timu zetu za Taifa kama tulivyopendekeza, ni vizuri pia kukawa na mpango mkakati wa kuboresha/kujenga viwanja vya michezo ili kuweza kuandaa mashindano ya Kimataifa na hivyo kuliingizia taifa fedha za kigeni na kuboresha sekta ya utalii kuliko ilivyo sasa, kwa sababu kiwanja kilicho na ubora wa kimataifa ni kimoja tu.

Mheshimiwa Spika, tulitoa mapendekezo yetu mwaka uliopita kuwa viwanja vyote vilivyochukuliwa na CCM baada ya kuwa na mfumo wa vyama vingi virudishwe Serikalini. Hii ni kwa sababu pamoja na kuwa viwanja hivyo vilichangiwa na wananchi wote bila kujali itikadi zao, baada ya mfumo wa vyama vingi CCM wameendelea kumiliki viwanja hivyo hata baada ya Tume ya Jaji Nyalali kupendekeza kuwa viwanja hivyo virudishwe Serikalini ili kutumiwa na wananchi wote bila kujali itikadi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na viwanja vingi chini ya CCM kutoendelezwa na kupelekea kutokuwa na hadhi yenye viwango vya kutumika kuandaa mashindano ya Kimataifa, Kambi ya Upinzani tunarejea pendekezo letu kwa mwaka uliopita kuwa Serikali ianzishe Mamlaka ya Michezo nchini ili kuweza kuweka mikakati ya kuendeleza michezo ikiwa ni pamoja na kujenga/kuboresha viwanja na kuwa na hadhi ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kukubali pendekezo letu kwa mwaka wa fedha 2011/2012, waliahidi kuwa wataanzisha Wakala wa Michezo badala ya Mamlaka ya Michezo kama ambavyo tulipendekeza.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kambi ya Upinzani tunahoji hatua zilizofikiwa kutekeleza ahadi hiyo ya Serikali kwa kuwa wakati akihitimisha hoja yake Naibu Waziri wakati huo alisema yafuatayo na naomba kunukuu:-

*"...Hoja ya kuanzishwa Mamlaka ya Viwanja vya Michezo, nieleze kuwa mchakato wa kuunda Wakala wa Kuendesha Viwanja tayari unaandaliwa na utakamilika mwaka huu..."*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunahoji hatua zilizofikiwa katika kuunda Wakala wa Michezo huku tukizidi kusisitiza kuwa ni muhimu kuwa na mamlaka kamili ambayo pia itashughulikia na kuratibu mapato yanayopatikana kwenye michezo mathalani malalamiko ya timu zinazoshiriki katika ligi kuu Tanzania Bara kuhusu mapato ya viingilio katika viwanja mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo na Utamaduni. Nafasi ya utamaduni katika nchi imekuwa haipewi umuhimu na kutambuliwa kikamilifu katika mipango ya maendeleo. Mipango mingi ya maendeleo imekuwa ikibuniwa na kutekelezwa bila ya kujali utamaduni wa wananchi katika maeneo husika. Jambo hili kwa kiasi kikubwa limesababisha mipango mingi kushindwa kutekelezeka. Tanzania ilitunga Sera ya Utamaduni mwaka 1997 lakini kwa masikitiko makubwa hadi muda huu sera hiyo haijawahi kutungiwa Sheria na Kanuni za utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliona jambo hili kuwa ni kitendo cha Serikali kutokuichukulia sekta hii ya utamaduni kuwa ni nyenzo muhimu katika kuifikishia jamii maendeleo yanayohitaji. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaitaka Serikali kulieleza Bunge ni lini sheria itatungwa ili yale yaliyomo katika sera hiyo yaweze kutekelezwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, Mbio za Mwenge. Tangu uhuru kumekuwa na zoezi la kukimbiza mwenge nchi nzima kila mwaka na hufanywa na vijana ambao wanateuliwa na Wizara hii. Pamoja na ukweli kuwa hakuna uwazi katika uteuzi wa vijana hao na zipo tuhuma kuwa suala la uteuzi linafanywa kisiasa zaidi na ndio maana kila mwaka wanateuliwa vijana kutoka jumuiya ya CCM kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kuhusiana na zoezi hili kwani wafanyakazi wa Serikali na hasa Walimu wamekuwa wakilazimishwa kuchanga fedha kwa ajili ya mbio za mwenge na mfano ni kwa mwaka huu ambapo Walimu wa shule za msingi nchini kwenye maeneo mbalimbali kama vile Wilaya ya Kondoa wametakiwa kutoa shilingi 2,000 kila mmoja, kwa ajili ya ujio wa mwenge na hili tamko lilitolewa kwenye kikao kilichofanyika tarehe 16/07/2012 kwa ajili ya mwenge kwenda Mrijo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, tunataka kupata majibu ni kwa nini Walimu pekee ndio ambao wanatakiwa kuchangia mwenge? Wizara haina bajeti kwa ajili hiyo na kama ipo fedha hizo zipo fungu gani? Kuna tija gani imepatikana mpaka sasa kwenye kukimbiza mwenge kwa ajili ya kwenda kuzindua miradi ya watu binafsi?

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utamaduni. Katika majadiliano ya hoja iliyowasilishwa hapa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wabunge kadhaa walitoa maoni yao dhidi ya kipindi cha *Big Brother Africa* kuwa hakiendani na tamaduni na mila za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kwenye majumuisho ya hoja hiyo Serikali kupitia Waziri wa Habari alitoa msimamo wa Tanzania kuwa Serikali haiungi mkono kipindi hicho na pia hata wanaoshiriki hawana baraka za Serikali. Naomba kunukuu maelezo ya Waziri kama ifuatavyo:-

*"... malalamiko kuhusu Big Brother Africa. Nataka nikubaliane na wote waliolalamika kwamba kile kipindi ni kero! Kile kipindi ni kero! Tunataka Watanzania wanaotusikiliza wajue kwamba Serikali haikiungi mkono, wala Bunge halikiungi mkono! Kinaonesha mambo ya fedheha waziwazi, hatujui kinataka kufundisha nini watoto wetu. Ni bahati mbaya tu kwamba utaratibu wa kualikana unafanywa kwa njia ya internet, si utaratibu unaopitia Serikalini. Lakini tunataka Watanzania wanaotaka kwenda kule wajue kwamba, hawana baraka za Serikali. Hatuwashabikii! Hatuwaungi mkono na ndiyo maana hatujawahi kwenda kuwapokea. Kwa hiyo, wazazi wajitahidi*

*kushauri watoto, kipindi kile hakina maana yoyote, kinamharibu anayekwenda na kinaharibu ndugu zake waliobaki nyumbani ".*

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo ni kuwa kwa mwaka huu Tanzania iliwakilishwa na washiriki wawili ambao walishatolewa mapema katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa na msimamo unaoeleweka kuhusu jambo hilo kwa sababu pamoja na kutoa kauli hiyo hapa Bungeni imedhihirika kuwa bado Tanzania inashiriki mashindano hayo na kipindi hicho bado kinaendelea kutazamwa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa la Taifa. Pamoja na uwapo wa BASATA (Baraza la Sanaa Tanzania) na *COSOTA* (Chama cha Haki Miliki), bado vyombo hivyo vimeshindwa kuwaletea mafanikio wasanii. Sanaa ya muziki pia ikitumika vizuri, ni tija kwa Taifa kwa vile itasaidia Serikali kupata kodi itakayotumika kwa maendeleo ya nchi kwa jumla. Kinachodaiwa hapa ni haki na usawa katika sanaa na malipo sahihi kama wanavyolipwa wanamuziki wengine wakija nchini kufanya maonyesho. Sanaa na michezo ni fursa pekee ya kumfanya mtoto wa masikini kujikomboa kupitia ajira binafsi.

Mheshimiwa Spika, sanaa hapa nchini inatakiwa kuwa kama soka nchini Brazil ilivyowanyanyua vijana wengi, sambamba na kuliingizia Taifa hilo mapato mengi.

Mheshimiwa Spika, Kazi za Wasanii. Kambi ya Upinzani katika hotuba yetu ya mwaka wa fedha 2011/2012 katika Wizara hii tulieleza kwa undani juu ya namna wasanii wanavyonyonywa na kuibiwa kazi zao na kuwafanya kupata mafanikio yasiyolingana na kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuhoji utekelezaji wa ahadi ya Rais kwa wasanii ya kuunda Kikosi Kazi (Task Force) kufanya kazi ya kutafiti namna ya kulinda haki za wasanii nchini, Kambi ya Upinzani tulipendekeza kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ili kuunda Mamlaka ya Haki Miliki nchini kwa maana ya kuipa mamlaka zaidi *COSOTA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali wakati wa kuhitimisha hoja, Waziri alikubalina na maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu suala hilo na naomba kununukuu kauli yake kutoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge:-

*"Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kutaka COSOTA iwe Mamlaka, nayo ni wazo la maana, tutalifikisha Wizara ya Viwanda na Biashara ili ione maana hoja yenyewe ya msingi anayotaka kujenga Ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ni hoja ya COSOTA kuwa na nguvu zaidi, iwe na meno ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi kuliko inavyofanya sasa. Kwa hiyo, hii ni hoja ambayo Waziri mwendawazimu tu anaweza akaikataa. (Makofi)" mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na kutambua Wizara kupokea mapendekezo yetu, ni wakati sasa wa kuhoji utekelezaji wa ahadi hii kwa kuwa hakuna taarifa rasmi zinazoonyesha utekelezaji wa jambo hili muhimu na hivyo kuendelea kuwa na chombo ambacho hakina nguvu za kutosha kwa ajili ya kulinda kazi za wasanii nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu na uzito wa mapendekezo hayo ya Kambi ya Upinzani, Waziri aliahidi kutekeleza azma hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na naomba kununukuu sehemu ya ahadi hiyo:-

*"Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria Namba Saba ya mwaka 1999 kuhusu hakimiliki. Niwahikikishie kama ambavyo siku ya bajeti ya Wizara ya Viwanda, Mawaziri wake walilihakikishia Bunge kwamba, jambo hilo litashughulikiwa kwa karibu sana. Naomba niwahakikishie kwamba nitaendelea kuwa karibu sana na Wizara hiyo ili kuona kwamba jambo hili linashughulikiwa". Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Wizara kusimamia na kutekeleza ahadi hii ambayo ilitolewa wakati Waziri wa sasa akiwa Naibu Waziri na kwa kuwa sasa ni Waziri kamili, ni

vema akalichukulia suala hili kwa uzito ili sheria hiyo ifanyiwe marekebisho na kuipa meno *COSOTA* kuweza kusimamia maslahi ya wasanii na hivyo kukuza uchumi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya *Stickers* Maalumu. Katika kulinda kazi za wasanii nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani tuliitaka Serikali kuanzisha utaratibu wa kuwa na *Stickers* Maalumu kwenye kazi za wasanii ili kurahisisha utozaji wa kodi lakini pia kudhibiti wizi wa kazi za wasanii.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hilo, Serikali kupitia Waziri wa Fedha katika hotuba yake ya Bajeti aliahidi Serikali kuanzisha utaratibu huo Januari mwaka 2013, naomba kunukuu ukurasa wa 65 wa hotuba kama ifuatayo:-

*"kutoza ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za muziki na filamu (mfano DVD, VCD, CD na mikanda ya video) hatua hii inalenga katika kurasimisha biashara ya bidhaa hizo na kuhakikisha kwamba uasili wake unatambulika na hivyo kuzuia kurudufu kazi za sanaa (piracy of artist work) hali ambayo inadumaza ukuaji wa sanaa na vipaji hapa nchini…Mamlaka ya Mapato Tanzania itaweka stampu kwenye bidhaa hizo…"*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunatambua Serikali kutekeleza pendekezo letu ambapo kwa mwaka uliopita kupitia pia Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo aliahidi kulifanyia kazi kama ambavyo aliahidi hapa Bungeni, naomba kunukuu;:-

*"...mradi wa Stickers kwa kazi za wasanii, jambo hili pia tumewahi kuzungumza na Ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na tumelizungumza sana Kiserikali na kwenye Kamati nililitolea taarifa kwamba, tumeanza kutafakari baada ya kupata maoni ya kutosha kutoka kwa wasanii wenyewe… Mimi binafsi nauamini utaratibu ule kuwa utafaa…." Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na kutambua kuwa Serikali imeanza kutekeleza pendekezo hili ambalo lilianza muda mrefu sana tangu mwaka 1996 kwa Mzee John Kitime alipoanza kulifanyia kazi suala hili na kulipigania, tunapenda pia kuutambua mchango wa Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi aliyekuwa Waziri wa Wizara hii, 'mnyonge, mnyongeni haki yake mpeni' kwani alilichukua wazo hili na kulifanyia kazi mpaka kulifikisha hapo lilipofikia leo na wasanii wameanza kuona nuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kwa namna ya kipekee kumshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa kulipokea hili baada ya mimi kuliwasilisha kwenye Kamati na hatimaye Kamati kuisimamia Serikali kuhakikisha kuwa utekelezaji wake unaanza kwa manufaa ya wasanii wote nchini. Kambi ya Upinzani tunasubiri utekelezaji wa suala hili kama ambavyo lilitolewa ahadi na Waziri wa Fedha na tutaendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha kuwa suala hili linafanikiwa kwa manufaa ya wasanii wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Mchakato wa Vazi la Taifa. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inatumia fedha za walipa kodi kuendesha mchakato wa kutafuta vazi la Taifa. Tunashauri wanaoendesha mchakato huu kuzingatia kuwa Tanzania ni Taifa kubwa lenye mchanganyiko wa watu wa makabila, tamaduni na mienendo ya aina mbalimbali. Kadhalika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa Tanzania ni nchi yenye makabila zaidi 120, kwa hiyo kupendekezwe mavazi matatu ya Taifa kwa wanaume na pia kwa wanawake. Watu wapewe uhuru wa chaguo katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, mavazi ya nchi hii yanafahamika, kama khanga, kitenge, lubega, kaniki, kibwebwe na mengineyo mengi. Tunaitaka Serikali mitindo hii izingatiwe katika uteuzi wa mavazi ya Taifa. Aidha, tunaitaka Serikali kutoa taarifa ni shilingi ngapi zimetumika mpaka sasa katika kutafuta hilo vazi la taifa?

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Vijana. Changamoto zinazowakabilii vijana siku hizi zote zinaonekana dhahiri. Kuongezeka kwa idadi ya mimba za ujana, kuacha shule, ukosefu wa ajira, kutumia dawa za kulevya, matatizo ya kijamii, kujamiana na afya ya uzazi kama vile kubakwa kwa miadi, maambukizo ya magonjwa ya kujamiiana *(STIs),* ikiwa ni pamoja na Virusi Vya

Ukimwi (VVU) na Ukosefu wa Kinga Mwilini (UKIMWI). Vyote hivi ni viashiria ambavyo inaonekana vijana wengi wanashindwa kuvimudu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia changamoto hizo, hatuna budi kama Taifa kujiweka sawa kuhakikisha kwamba kweli tuliyoyapanga yanatekelezwa. Suala kubwa ni kuhakikisha kuwa vijana wetu wanapata fursa ya elimu, si tu ya awali, bali sekondari na vyuo vya ufundi na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa (AU) kwa ajili ya maendeleo ya vijana uliopitishwa mwaka 2006 na kuridhiwa na nchi 18 za Afrika kufikia mwaka 2009, Tanzania ikiwemo ni mwanzo wa msukumo kwa nchi za Afrika kuanza kuchukua hatua zinazopimika kuinua hali ya vijana. Mkataba huo una malengo makuu sita: kuimarisha ushiriki wa vijana katika maendeleo; kuimarisha uwezo; na kuongeza utashi wa mataifa katika kutekeleza sera za vijana, kuratibu, kuongoza na kusimamia utekelezaji wa sera, programu na miongozo yenye lengo la kuinua vijana kimaisha; kuwezesha vijana kisiasa, kiuchumi na kijamii; kupanua na kuboresha sera mbalimbali zinazohusu ustawi wa vijana; kuimarisha bajeti kwa ajili ya shughuli za vijana na kuimarisha miundombinu ya kusimamia, kutathmini, kufuatilia na kuripoti masuala ya shughuli za vijana.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya mkataba huo wa vijana wa Afrika kama ulivyopitishwa mwaka 2006 ambao maudhui yake ni kuinua maisha ya vijana kimaisha ni lazima kuwe na chombo cha kuwaunganisha vijana wote bila kuangalia itikadi au dini zao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kupata majibu ya kina juu ya uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa programu hiyo imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, Ajira kwa Vijana. Kwa mujibu wa Taarifa Rasmi za Bunge, Mkutano wa Kumi na Mbili, Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 27 Juni, 2003. Wakati Serikali ikijibu swali Na. 123 lililohusu tatizo la ajira kwa vijana ilisema kuwa, nanukuu:-

*"…Serikali imekwishachukua hatua mbalimbali ambazo zitasaidia kupanua ajira kwa vijana ili hatimaye waondokane na uzururaji…Serikali itakuwa karibu na Halmashauri, Manispaa na Jiji ili kuhakikisha kuwa sehemu ya mapato yanatumika katika kutunisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kuanzisha rasmi Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (Youth Development Revolving Fund)." Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, aidha, sasa imetimia takribani miaka minane, tangu swali namba 123 liulizwe hapa Bungeni mwaka 2003, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge Mfuko huo wa Maendeleo ya Vijana unaochangiwa na kuendelezwa kwa ngazi za Halmashauri, Manispaa na Majiji umekwishawezesha makundi mangapi ya vijana katika ngazi za Vitongoji, Vijiji, Kata na Wilaya? Mfuko huo unaendeshwa kwa utaratibu gani katika kuwawezesha vijana?

Mheshimiwa Spika, tathmini zinaonyesha kuwa mikakati na shughuli zinazotekelezwa na Serikali kwa ajili ya kutengeneza ajira kwa vijana, bado haijaweza kuondoa vikwazo vya kimsingi vinavyosababisha vijana washindwe kujiajiri. Aidha, fursa za ajira zinazotengenezwa zimekuwa ni chache mno kuliko kasi ya ongezeko la vijana wanaohitaji ajira kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, akielezea utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya vijana kupitia hotuba ya bajeti ya Serikali ya Wizara hii mwaka 2010/2011, Mheshimiwa Waziri, pamoja na mambo mengine alisema, nanukuu:-

*"Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umeendelea kuimarishwa ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo kwa vijana kupitia SACCOS. Mpaka kufikia mwezi Juni 2011, jumla ya SACCOS 242 zilikopeshwa shilingi 1,210,000,000" mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, ukweli huu unaonyesha kuwa Serikali inashughulikia tatizo la ajira kwa kasi ndogo sana. Wakati vijana ni takribani asilimia 40 ya watu wote takriban milioni 43 waliopo nchini hivi sasa, uwezo wa Serikali kutoa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo uliweza kukidhi

mahitaji ya *SACCOS* za vijana 242 tu nchini katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 na kiasi cha fedha zilizokopeshwa ni shilingi 1,210,000,000 pekee.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliahidi kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Vijana ili iweze kutoa mikopo yenye masharti nafuu na kuchochea ajira kwa vijana. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze imefikia wapi katika kutekeleza ahadi hii na imeweka malengo gani ya kuzalisha ajira kwa vijana na je, utekelezaji malengo hayo utalichukua Taifa hili miaka mingapi kuweza kukidhi mahitaji ya vijana wenye shida ya ajira nchini?

Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili. Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) ni moja ya taasisi muhimu sana katika nchi yetu kwa ajili ya kukuza na kuindeleza lugha yetu adhimu ya Kiswahili. Kadhalika ni chombo kinachotakiwa kutoa miongozo mbalimbali kuhusu matumizi ya Kiswahili sanifu pamoja na kuratibu masuala ya kukuza misamiati ya lugha hiyo ili kuendana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea nchini na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa uwepo wa taasisi hii, bado Serikali haijaonyesha nia thabiti ya kuliboresha Baraza ili kutekeleza majukumu yake na kuna ahadi ambazo zimetolewa katika Bunge hili Tukufu ambazo hadi leo zinabaki kuwa ahadi hewa.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri kwa mwaka wa fedha 2010/2011, ukurasa wa 68 kuhusu kuboresha majengo ambayo Baraza linatakiwa kuhamia, Waziri alitoa kauli ifuatayo, naomba kunukuu:-

*"Kukarabati na kuboresha baadhi ya majengo yaliyonunuliwa ili yaweze kukidhi mahitaji ya kiofisi hatimaye BAKITA ihamie katika majengo hayo na kuyatumia kama ofisi zake mpya".*

Mheshimiwa Spika, kuonyesha kuwa kauli zilezile zinajirudia kwa mwaka 2011/2012, Serikali iliahidi kukarabati majengo kuliwezesha Baraza kuhamia katika majengo hayo, lakini katika randama ya Wizara ukurasa wa 21, malengo ya mwaka 2011/2012 yalikuwa yaleyale yaliyoahidiwa kwa mwaka uliotangalia na naomba kunukuu:-

*"Kukarabati na kuboresha baadhi ya majengo yaliyonunuliwa ili yaweze kukidhi mahitaji ya kiofisi ili BAKITA lihamie katika majengo hayo na kuyatumia kama ofisi zake mpya".*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya utekelezaji ya Wizara kuhusu ahadi hiyo ukurasa wa 22 wa randama 2012/2013, yanasomeka ifuatavyo:-

*"Baraza limewasiliana na Wakala wa Majengo Tanzania ili kupata ushauri wa kitaalamu wa kukarabati majengo yake yaliyonunuliwa kutoka Shirika la Bima la Taifa".*

Mheshimiwa Spika, kuonyesha kuwa bado wimbo uleule unaendelea kwa ubeti uleule katika malengo ya mwaka 2012/2013 ya Wizara ukurasa wa 22 yanasomeka maneno yafuatayo, naomba kunukuu:-

*"Kukarabati na kuboresha baadhi ya majengo yaliyonunuliwa kutoka Shirika la Bima la Taifa ili yaweze kukidhi mahitaji ya kiofisi kwa ajili ya matumizi ya BAKITA".*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Serikali inalihadaa Bunge kwa ujumla kwa kutoa ahadi ambazo zimekuwa zikijirudia mara kwa mara bila kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa kauli za mara kwa mara kuhusu kulitumia Baraza kwa ajili ya maandalizi ya Hotuba za Bajeti pamoja na Miswada ya Sheria ambayo kwa sasa inatumia lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka uliopita Serikali katika kujibu hoja za Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na maoni ya mtaalamu na mdau wa Kiswahili Prof. Kulikoyela Kanalandwa Kahigi, iliahidi Wizara kutumia Baraza katika maandalizi ya bajeti na Miswada na Waziri wakati anahitimisha hoja yake hapa Bungeni aliahidi utekelezaji wa jambo hilo na naomba kunukuu:-

*"…Kamati ilitoa maelekezo ambayo ni muhimu kwamba BAKITA ishirikishwe katika kuandaa vitabu vya bajeti katika Wizara mbalimbali ili kupata usanifu wa Kiswahili. Sisi Kama Wizara hatuna pingamizi na jambo hili, wakati wowote ambapo Wizara mbalimbali zikihitaji usaidizi wa BAKITA basi BAKITA ipo na ina uwezo wa kufanya kazi hiyo…"*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kutekeleza ahadi zake kwa vitendo na sio maneno yanayojirudia mwaka hadi mwaka bila utekelezaji. Lazima kama Taifa tuwe na mkakati wa kuitumia lugha yetu kwa ajili ya maendeleo yetu. Ni vema Serikali ikatekeleza ahadi zake ili kuboresha utendaji wa Baraza na kulifanya liwe na tija kwa taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokubaliana, hii ni Wizara itajadiliwa siku moja. Kwa hiyo, tutakuwa na wachangiaji wachache. Kwanza, nitamwita Mheshimiwa Idd Azzan ingawa yuko kundi la pili, kwa kuwa atafikiwa isipokuwa ana matatizo, amefiwa na mlezi wake, inabidi aondoke sasa hivi kwenda kushiriki mazishi Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Idd Azzan.

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza, na kama ulivyoeleza sababu ambayo imenikabili ya msiba, ambaye amefariki ni Bwana Azzan Mangushi, ni Mwana michezo, ni mshabiki mkubwa wa *Coast Union* na ni mshabiki mkubwa sana wa *Simba Sport Club*. Kwa ujumla ni mwana michezo. Kwangu mimi ni mlezi wangu. Kwa hiyo, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niwahi mazishi.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, naomba nichukue nafasi hii kwanza kutamka wazi kwamba siungi mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri na siungi mkono kwa sababu ambazo nitazieleza. Lakini kama ingekuwa inawezekana, nafikiri Wizara hii hakuna haja ya kuwepo, ni bora ianzishwe hata Kurugenzi kwenye eneo lingine kuliko Wizara hii kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hayo kwa masikitiko makubwa sana. Mwaka 2006 tulizungumza kwenye Wizara hii kuhusu kuhuisha Sheria ambazo zimepitwa na wakati. Leo tunakwenda kwenye michezo ya kulipwa, sisi bado tuko tu kwenye sheria ambazo wakati huo zilikuwa ni za chama kimoja, lakini zimeendelea kuwepo. Nilisema, mwaka 2006 nimeendelea kuelezea mwaka 2007 na kila mwaka majibu yanakuwa ni hayo hayo kama ambayo yametolewa leo asubuhi kwenye majibu ya Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwamba Wizara hii ambayo ina watendaji ambao wameaminika na ambayo inapewa kila mwaka siyo chini ya Shilingi bilioni 13 kwa ajili ya matumizi yao tu, ukiachilia mbali zile hela kidogo za maendeleo; fedha hizi ni kwa ajili ya mishahara na mambo mengine, wanakula zaidi ya Shilingi bilioni 12 kwa mwaka, lakini hakuna kazi ya maana ambayo wanaifanya. Inanisikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, niende kwenye vitabu vya hotuba vya mwaka 2010, naomba tu nisome baadhi ya maneno katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2010/2011. Katika maelezo yao mengi kwenye Sekta ya Michezo, walieleza ni jinsi gani wanakamilisha Sera ya Michezo pamoja na Sheria ya Baraza la Michezo na wamesema, naomba ninukuu: "Kukamilisha marekebisho ya Sera ya Michezo." Kukamilisha hiyo ni mwaka 2010, wanakamilisha. Lakini majibu ya Waziri leo hapa bado mchakato unaendelea.

Mheshimiwa Spika, hii michakato inachukua muda gani kwa ajili ya kurekebisha tu sera ambayo ipo na imepitwa na wakati? Ni kuzirekebisha, lakini imeanza tangu mwaka 2006 hadi leo tunazungumza hivyo hivyo. Lakini hotuba yao pia ya mwaka uliofuata waliendelea kuja na hadithi zao hizo hizo. Kwenye Hotuba ya Waziri ya Bajeti ya mwaka 2011/2012, anaendelea kusema kwamba: "Kukamilisha marekebisho ya Sheria Na. 12 ya Baraza ya mwaka 1967." Hii ni bajeti iliyopita. Lakini mpaka leo hadithi zinakuja hivyo hivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaniwia vigumu sana, ningewashawishi hata Wabunge wenzangu tuache kuiunga mkono Wizara hii ili fedha hizi Shilingi bilioni 12 kwa ajili ya mishahara na mambo mengine zikafanye kazi nyingine kuliko kwenda kuliwa bila faida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuje sasa kwenye suala la michezo. Tunayo matatizo makubwa sana kwenye maendeleo ya michezo hapa kwetu. Tumesema tumerudisha michezo mashuleni, lakini wanaambiwa watu wa Wizara ni kazi gani waliyoifanya kuhakikisha kwamba michezo hiyo iko mashuleni, inachezwa na nini wamekisaidia? Hakuna. Lakini tuje kwenye timu zetu zinazowakilisha nchi, na kwa taarifa niliyonayo, hivi sasa timu yetu ya *Olympic* ambayo iko *London,* leo ni siku ya 10 hawajapata posho yao. Kwa taarifa nilizonazo, sijui kama Wizara wanajua hilo. Ni aibu! Fedha zinaletwa na Kamati na *Olympic* ya Dunia, zinakuja kwenye Kamati ya *Olympic* ya Tanzania lakini leo siku ya 10 wachezaji wetu wa *Olympic* hawajapata posho yao. Kuja na medali ni miujiza ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia maendeleo ya michezo pamoja na mambo mengine, tunazungumzia pia na viwanja vya michezo. Tunavyo viwanja ambavyo vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi na mimi nakipongeza sana Chama cha Mapinduzi kwa kumiliki viwanja hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Chama cha Mapinduzi kwenye viwanja vile hakifanyi biashara, kinatoa huduma. Kuna mechi zinachezwa, hela inayolipwa ni ndogo, na mimi juzi nilikuwa na *final* tu, hapa nimecheza kwenye uwanja wa CCM bila kulipa chochote kwa ajili ya kuwasaidia vijana wetu. Sasa ninyi Serikali/Wizara/Chama cha Mpira ambacho ndio kinatumia viwanja hivi, kiangalie ni jinsi gani sasa wanasaidia Chama cha Mapinduzi kuboresha viwanja hivyo. *(Makofi)*

Kwa kuanzia, mngeanza na Kiwanja hiki cha Makao Makuu ya CCM, lakini Makao Makuu ya Serikali pia. Kuna uwanja mbovu tu pale wa Jamhuri. Jukwaa ni zuri, lakini mngeweza hata kusaidia pakawekwa nyasi bandia, tungekuwa na uwanja mzuri sana ambapo mashindano ya Kagame yanayofanyika Dar es Salaam mchana na jioni yangeweza kuja kufanyika hata kwenye Mikoa mingine. Lakini hilo bado mmelala usingizi, hakuna mnachokifanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwaombe sana, pamoja na kwamba viwanja vinamilikiwa na CCM, CCM haifanyi biashara kwenye viwanja hivyo, na ninyi ndio mnavitumia. Kwa hiyo, mhakikishe mnawasaidia ili waweze kuvijenga viwanja hivyo. *(Makofi)*

Tuje sasa kwenye suala ambalo tulilizungumza na mkasema mmechukua hatua. Aibu ambayo Taifa letu limepata kwenye Uwanja wa Taifa kuzimika taa kwenye *Finally* ya Kagame lakini na kutokupigwa nyimbo za Taifa wakati Mheshimiwa Rais akiwepo na mkasema mmechukua hatua. *TFF* wamemwondoa Kaijage aliyekuwa Afisa Uhusiano wao, ninyi mkasema mtamwondoa Meneja, lakini Meneja mpaka leo yuko kazini, hakuna hatua mliyochukua, mmemsimamisha kwa mwezi mmoja tu. Kwa hiyo, inasikitisha sana kwamba yale ambayo yanatia aibu kwenye nchi hii ninyi mnaendelea kuyafumbia macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije sasa kwenye riadha. Tunayo matatizo makubwa sana kwenye Chama cha Riadha Tanzania. Matatizo hayo watu wa Wizara mnayajua, lakini mmekuwa mkiyafumbia macho, na kwa bahati mbaya sana kwenye uchaguzi ambao umefanyika Morogoro hivi karibuni, ninyi watu wa Wizara badala ya kutumia sheria iliyotungwa na Bunge, ninyi mkapeleka waraka wenu ndiyo utumike kwenye uchaguzi huo. Hiyo ni kuidharau Bunge kwa sababu huwezi kutengua sheria iliyotungwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna ujenzi wa Kituo cha *Olympic* ambapo ilikuwa tuwe tumejenga Kituo hiki, lakini kumekuwa na tatizo kwenye ujenzi huu. Watu wanajiuliza, ama ni kwa sababu Filbert Bayi ambaye ndio Kiongozi wa *TOC* hataki uwanja huo ujengwe kwa sababu timu zetu za Taifa zinaweka kambi kwenye shule yake?

Kwa hiyo, ni maswali ambayo na ninyi mnatakiwa mtujibu. Lakini upo urasimu ama wizi wa fedha ambazo zinaletwa kwa ajili ya kusaidia *TOC,* fedha zile haziwafikii wanariadha, fedha zile haziwasaidii wanariadha na mwisho wana riadha wetu wanakuwa hawafanyi vizuri kwa sababu

ya fedha kuliwa na wachache. Tunataka uchunguzi wa kina na Wizara ije itueleze hapa kwamba kwanza wanariadha waliokatwa fedha zao mwaka 2008 ni lini watarudishiwa fedha zao? Fedha zao za posho zilikatwa ili kumlipia Afisa wa *TOC* apate nauli, wakakatwa wao. Tunataka kujua, lini hela hizo zitarudishwa kwao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara ilieleze Bunge pia, ni kwa nini Mkataba wa *PUMA* na *LINING* haukuingiwa, uliishia wapi na mkataba ambao ulikuwa una manufaa makubwa sana kwa nchi yetu? Lakini tunataka kujua pia, uchaguzi wa *RTC* uliofanyika Morogoro, ni kwa nini mlitumia waraka wenu badala ya kutumia sheria iliyotungwa na Bunge? Tunataka kufahamu kuhusu kituo ambacho nimeshakizungumzia cha *Olympic,* ujenzi umefikia wapi? Nao tunataka tupate majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nitazungumzia ni suala la filamu. Ipo Bodi ya Filamu, mwaka 2011 wakati nachangia, nilisema wamelala usingizi, na leo narudia tena kwamba bado wameendelea kulala usingizi. Filamu zipo Tanzania, zinatengenezwa na Watanzania, na wao wanazipitia, wanaruhusu kuingia sokoni. Lakini ziko filamu zinazotoka nje, zinaingia Tanzania na nyingine ni chafu.

Bahati mbaya sana kwenye filamu chafu hizo, picha ya mbele inayoonekana, ni msanifu wa filamu wa Tanzania, ndio waliocheza picha hiyo. Sasa sijui kama ukiingia ndani kama ni yeye ameshiriki ama picha yake tu ndiyo imetumika. Ni sinema za X ambazo zimetapakaa Mitaani. Nataka maelezo ya kina kwenu kama ni kweli Watanzania ama wasanii wetu wamecheza picha hizo za uchi na ziko Mitaani zinauzwa, ama picha zao zimetumika tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya.

Mheshimiwa Spika, katika kuichangia hoja hii ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, nianze na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa Taifa letu la Tanzania, leo tunamesheherekea miaka 48 ya Muungano, miaka 50 ya Uhuru, tumeshindwa kubuni vazi la Taifa. Tanzania ni moja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna Uganda, Kenya na Burundi. Burundi wana vazi lao la Taifa, Uganda wana vazi lao la Taifa. Kwa nini Tanzania mpaka leo tuna kigugumizi cha vazi la Taifa? Kwa nini vazi hili la Taifa wasipewe Waheshimiwa Wabunge wanawake kwa sababu Wabunge wanawake wao wanawakilisha Mikoa yote? Wafanyiwe mashindano, wananchi wao ndio watakaochagua vazi gani linafaa kuwa vazi la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake aniambie vazi la Taifa litapatikana lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija katika sanaa zetu za filamu, filamu zetu za Kitanzania zimekosa maadili. Asilimia kubwa ya Watanzania wa leo tunaangalia kanda, *Bongo Movie.* Unashindwa kuangalia filamu na watoto wako kwa sababu filamu zimekosa maadili. Lakini Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema kwamba filamu moja tu ndiyo imekosa maadili, ndio imetolewa katika tasnia ya filamu. Lakini kuna filamu zinaashiria ushoga, kuna filamu zinaashiria usagaji, hizo zote hajazisema. Mheshimiwa Waziri nataka atakapokuja kufanya hitimisho aniambie ni filamu ngapi zinaashiria ushoga, zinazoashiria usagaji, aniambie ni ngapi amezifungia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku hizi kuna muziki wa dansi wa kanga moja, wanasema kanga moko. Haufai katika maadili yetu ya Kitanzania! Unapotosha, na muziki huo unaangaliwa na watu wenye fedha, watu wenye heshima zao, watu wenye familia zao. Ni aibu kwa Tanzania. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya hitimisho, aniambie mchezo wa kanga moja ameufungia au anatarajia kuufungia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nataka kuwatetea vijana kidogo. Nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa ufafanuzi anijibu: Je, ameweka mikakati gani ya vijana? Kwa sababu, vijana ndio Taifa la leo, tutasema ndio Taifa la kesho. Sasa ana mikakati gani aliowapangia vijana kutokana na changamoto za sasa hivi zinazoendelea katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, siungi mkono hoja. Nitaunga mkono nitakapopata majibu. *(Makofi)*

**MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza kuwaombea dua ndugu zetu waliopatwa na ajali ya meli iliyotokea kule Zanzibar. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ya pekee, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa fursa aliyotupa vijana wa UVCCM Baraza Kuu. Tunamshukuru kwa nafasi alizotupa za U-*DC* na nafasi ya Naibu Waziri kupitia Mjumbe wa Baraza Mheshimiwa Masele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaheshimu nafasi aliyotupa Mheshimiwa Rais. Nasema kwamba nafasi alizotupa tutazitumia kama alivyokusudia na hatutamwangusha. Kati yao hakuna kijana aliyekosea kumteua. Wote wana uwezo na wote wana uwezo wa kufanya kazi ambazo yeye kazikusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye suala zima la kuchangia hoja hii. Kuna mambo manne katika hoja hii. Kuna suala zima la habari, kuna suala zima la vijana pamoja na utamaduni na michezo. Lakini nianze kwenye vijana ili nisije nikagongewa kengele, lengo langu likawa halijatimia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekuwa na jitihada kubwa ya kuleta maendeleo pamoja na Mawaziri na Manaibu Waziri wote waliokuwemo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ila tatizo la uzoroteshaji wa maendeleo na uzoroteshaji wa kazi zinazokusudiwa na Serikali, linafanywa kwa makusudi. Sisi kama vijana, linatutia uchungu tena linatutia uchungu kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la vijana, tatizo kubwa lililopo nchini ni suala ajira. Leo kila anayesimama kijana anazungumzia suala zima la ajira. Hakuna kiongozi atakayepewa kuongoza nchi hii akasema ana uwezo wa kuwapa ajira vijana wote Tanzania. Hilo halipo. Hiyo ni sawa sawa na kulala una njaa ukaamka umeota unakula, ukapiga miayo halafu ukaomba maji ya kunywa kwa sababu uliota kwamba unakula chakula. Kinachowezekana kifanyike na kupunguza kero kwa sisi vijana. Wengi tuna imani na Serikali ndiyo maana kila siku tunaipa kura kwa sababu tuna imani na tunaona jitihada zao za makusudi za kutatua matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala zima la vijana linalotukera. Sisi kama vijana, suala linalotukera ni ajira kurudi miongoni mwa wastaafu. Hili suala limekuwa ndani ya vijana, ni kero Tanzania, tunaambiwa uzoefu haupo. Vijana wengi wanamaliza shule, wana vyeti vizuri vya kufanya kazi, leo unaambiwa uwe na uzoefu.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama kupita kuanza kuhangaika kuanza kutafuta kazi, hiyo ni suala la yeye kupata uzoefu. Hili twende vizuri, sambamba. Naomba sana unipe fursa ya kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba suala hili kwetu ni kero. Tunajua matatizo yaliyokuwepo nchini mwetu, jitihada za Serikali yetu, ila tunaomba sana wastaafu wasirudishwe makazini, nafasi zirudi kwa walengwa ambao wanamaliza shule, wapewe nafasi hizo kwa ajili ya kupatiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala zima linaloendelea kukera, wale Wakurugenzi au Watendaji wanaozorotesha jitihada za Serikali pale zinapotolewa fedha ili Serikali itoe mikopo kwa vijana, badala yake watumia matumizi wanayoyataka na kuwapa wale ambao wao wanaona kwao ni vyema. Lakini tunasema, vijana tunaelewa kwamba zile fedha zinatolewa na Serikali kwa vijana wote wa Tanzania. Tunataka fedha hizo zifikishwe kwa vijana, na siyo kama hivi zinavyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niende kwa haraka kwa sababu ya muda wako. Nije kwenye suala zima la habari. Suala la habari tunashukuru kwamba Tanzania tumepiga hatua, tunaona maendeleo yanayobadilisha kila siku Tanzania yetu. Asiyeona, tutamwambia atufuate ili tumwonyeshe hatua gani zinazopigwa. Lakini katika suala zima la habari, pamoja na uhuru wanaopewa Vyombo vya Habari, bado tuna wakati wa kusema kasoro zilizokuweko. Mimi nasema kuiga jambo zuri siyo vibaya. Nichukulie mfano, *TV* ya Zanzibar, habari zinakwenda kwa Itifaki. Naomba Mheshimiwa Waziri alishukue hili, chombo chochote hasa chombo chetu cha Serikali, tunataka habari ziende kwa Itifaki. Lazima aanze Mheshimiwa Rais. Sisi tunatarajia kujua Kiongozi wa nchi kazungumza nini, kafanya nini, zile habari tunazitaka zitangulie kuliko habari nyingine zozote, na kama kuna za Waziri Mkuu, Mawaziri baadaye zije za mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhuru usiokuwa na mipaka siyo uhuru. Uhuru unatakiwa uwe na mipaka. Hili ninaliomba sana tena sana. Utakuta katika Vyombo vya Habari naweza nikasema namtolea mfano dada yangu Mheshimiwa Maida, yeye kwa kuwa ni Mbunge, anachukua zaidi ya dakika 20 au 30 kwenye habari. Mheshimiwa Rais anapewa dakika 10 au dakika tano. Siyo utaratibu mzuri hata kidogo! *(Makofi)*

Sisi tunataka kusikia Viongozi wa nchi wanasema nini, wanataka iweje, nini kimetokea, sasa unakuta kwenye Vyombo vya Habari sasa hivi inatolewa habari ya muziki, linatolewa tangazo, yaani hakuna utaratibu mzuri. Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa, ili niunge mkono hoja yako, naomba haya uyatolee majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nije kwenye suala zima la utamaduni. Hili suala la utamaduni nadhani sisi Viongozi tunapozungumza tamaduni tunawalenga watu wengine, kwamba hao ndiyo wanapaswa kuwa na utamaduni. Utamaduni mzuri tuuanze sisi wenyewe. Sisi viongozi ndiyo tuuanze huo utamaduni tunaoutaka, wao watu-*copy* sisi kwamba, utamaduni ndani ya nchi yetu uwe wa aina gani? Sio sisi kama tu viongozi, na familia zetu! Mwenye Mke, Mume, watoto, huo utamaduni uwe mfano, halafu tuzungumze huo utamaduni tunaoutaka, wengine waufuate.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwa haraka kwa sababu ya muda. Tuje kwenye suala zima la wasanii. Mheshimiwa Waziri ufahamu na uelewe kwamba pamoja na tatizo la ajira lililokuwepo nchini, suala la wasanii ni ajira kwao. Kila siku tumekaa tunapiga kelele, tunataka haki za wasanii zilindwe, tunataka Mheshimiwa Waziri ukija hapa, ulitolee majibu. Leo unakuta, yaani nizungumze hili linanitia simanzi kweli!

Mheshimiwa Spika, leo unamkuta msanii anaumwa, nitoe mfano wa msanii aliyefariki, au mama yangu Khadija Kopa anakaa kwenye *TV,* kuangalia *ITV* au TIV nyingine yoyote, samahani kwa kutoa mfano huo, *TV* nyingine yoyote anamkuta Marehemu Omari Kopa anawekwa, anatoa tangazo, maana inapigwa nyimbo aliyoimba, ananufaika nini? Nini kinachomnufaisha? Tumchukulie sasa hivi Marehemu Kanumba, amefariki, lakini bado matangazo *television* zinaonyesha. Mzee wake hili linamuumiza moyo pale anapomwangalia mtoto wake. Anathaminiwa nini? Anapewa pale haki gani kama Mzee? Tuyaangalie haya mambo, tusiwe watu ambao kila siku tunapanga mipango ya kukurupuka. Tena Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Wizara yako uliyopewa tunasikitika sana, maana sisi tutakuwa na wewe tu, Wizara hii tunataka tuone kazi jinsi gani zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nije kwenye suala zima la michezo. Tanzania imekuwa inajitangaza kwenye suala la michezo. Suala la michezo sisi kama Watanzania lazima tujue michezo hii ni moja kati ya kujitangaza kama Watanzania. Leo tuna timu zetu Simba na Yanga, upinzani wao siyo upinzani wa vita, na siyo upinzani mbaya. Ni upinzani wa kuleta upendo ndani ya nchi yetu pamoja na ushirikiano. Lakini leo hao hao utamkuta Simba au Yanga katoka nje ya

Tanzania kaenda kucheza, utashanga Mtanzania, mshabiki wa Simba au Yanga kafungwa, anafurahia kufungwa ile timu. Hivi huo ni utamaduni? Siyo utamaduni mzuri! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachojifunza ni kwamba, bado utumwa unaendelea ndani ya Tanzania. Leo utamkuta hata mwanaume anatoka ndani ya nyumba yake anakwenda kufurahia *Manchester* kwenye *Bar*, anamwacha mke wake ndani. Anakwenda kufurahia *Liverpool* kwenye *bar!* Huu siyo utaratibu. Tuwe wenye tamaduni zetu, wenye kujipenda. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli nalizungumza kwa uchungu! Ukienda nchi za wenzetu, kwa mfano *South Africa,* unakuta timu yao imetoka nje ya nchi yao imekwenda kucheza, utakuta wote wameamka wamevaa bendera kama nguo. Tanzania haipo hiyo!

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu katika nchi yetu. Lakini kabla ya yote nichukue nafasi hii kuipongeza timu ya Yanga kwa kuweza kuingia nusu fainali na tunaiombea kila la kheri waweze kutetea kombe hili la Kagame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, napenda sasa nianze na viwanja vya michezo na nitaanza kuvisemea viwanja ambavyo vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi. Nimefarijika kumsikia Mheshimiwa Iddi Azzan, Mbunge wa Chama cha Mapinduzi amekiri na ameeleza hapa jinsi viwanja hivyo vilivyo vibovu. Mimi ni mmoja wa wale Wabunge, huwa tunakwenda kufanya mazoezi kwenye Uwanja wa Jamhuri ambao uko Makao Mkuu ya nchi na Makao Makuu ya Chama cha Mapinduzi ambao ndiyo wanamiliki viwanja hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanja vile viko kwenye hali mbaya, nyasi hazinyeshewi, kule wanakokimbilia wanamichezo kumebomoka, na nilishangaa juzi wanajaza mchanga na vumbi na kumwagia maji. Sasa kwa kweli hapa Chama cha Mapinduzi imefika wakati mmrejeshe vianja hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule wanakokalia watazamaji walikojengea kwa *cement* vimevunjika, hali ni mbaya sana, hata ukiangalia wachezaji wa Bunge kwenye magoti wanachubuka, Mheshimiwa Msigwa ameumia mguu kwenye uwanja ule ule. Kama matengenezo ya haraka hayatafanyika, hata timu zako za Bunge tunaweza kuzuia kucheza katika uwanja ule. Mimi nakishauri Chama cha Mapinduzi kwa nia njema kabisa, vile viwanja wameshindwa kuvisimamia. Ifike wakati sasa wavirejeshe viwanja hivi Serikalini ili itengwe bajeti kwa ajili ya kuvitengeneza. Ninaamini vitaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa la nchi yetu na hata timu kutoka nje wanaweza kuja kuvitumia viwanja hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili wameweza kufanya wenzao wa Jumuiya ya Wazazi, waliweza kurejesha Shule za Sekondari chini ya Wizara ya Elimu. Ni kwa nini sasa Serikali hiyo hiyo moja ya Chama hicho hicho upande wa kwenye viwanja wanashindwa kuvirudisha viwanja hivi Serikalini kama Jumuiya ya Wazazi ilivyoweza kurudisha Shule zile baada ya kuona wameshindwa kuzisimamia? Nafikiri umefika wakati muafaka sasa ndugu zangu wa Chama cha Mapinduzi kwa nia njema kabisa mvirejeshe viwanja hivyo, kwa sababu kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani, vilijengwa wakati wa mfumo wa chama kimoja na wananchi walikuwa hawana chama kingine na wote walichangia ujenzi wa viwanja hivi. Kwa hiyo, ufike wakati muafaka sasa mvirejeshe viwanja hivyo, na nina amani vitu vinavyoweza kuchangia michezo yetu kukua, ni pamoja na viwanja. Kwa kuwa viwanja hivyo mmevishikilia kwa muda mrefu, vimekuwa magofu, hakuna chochote kinachopatikana kutoka kwenye vile viwanja, nimetolea mfano kiwanja hiki kilichopo Dodoma na ninahisi hata maji yamekatwa kwa sababu nyasi zimenyauka. Zamani ule uwanja ulikuwa unanyeshewa, lakini sasa hivi hakuna chochote kinachoendelea kwenye viwanja hivi. Huo ndiyo ushauri wangu wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nije pia kwenye timu ya Taifa ya wanawake *(Twiga Stars).* Kwanza, nawapongeza wachezaji wa timu ile kwamba pamoja matatizo waliyonayo, lakini wameweza kuonyesha kwamba akina mama wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Ofisi yako kwa kuweza kuichangia timu yetu ya *Twiga Stars* Shilingi milioni 15 ambapo walikuja kwako Mheshimiwa Ummi Mwalimu na Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* – Mheshimiwa Iddi Azzan na uliweza kuchangia timu hiyo. Lakini pia niwapongeze wale wapenzi wa *Twiga Stars,* Wabunge walioweza kuchangia *Twiga Stars,* tunawashukuru sana na tuendelee na moyo huo huo*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini timu hii imekuwa na matatizo mengi sana na wachezaji wamekuwa wakitupigia na wakaomba Wizara hii itakapokuja, tuweze kusema matatizo ambayo wanayo. Wanasema kwamba maandilizi yao yanakuwa ni ya muda mfupi sana na hii inasababisha timu hii kushindwa kufanya vizuri. Lakini pia wanasema kambi wanazopelekwa mara ya mwisho walikuwa kambi ya Jeshi Ruvu, wanadai mazingira ya kambi hiyo siyo mazuri, hata mahali pa kulala penyewe ni tatizo. Wanakwambia ukilala, ukiamka asubuhi mbavu zote zinauma. Sasa wachezaji tunajua wanahitaji sehemu nzuri za kupumzika, wanahitajika kupata chakula kizuri na wapate muda wa kutosha wa kupumzika. Lakini timu hii wanalalamika kwamba hawapati.

Mheshimiwa Spika, kingine, wanadai kwamba timu ya Taifa ya wanaume, wamekatiwa Bima. Lakini timu hii ya wanawake hawana Bima na hii inawasababishia kwamba wanacheza kwa tahadhari kubwa, wanaogopa wakiumia watatibiwaje? Hii sitaki kuonekana kwamba nina ubaguzi, lakini napenda kuisemea hii timu ya wanawake kwa sababu kama timu ya Taifa ya wanaume wameweza kukatiwa Bima, ni kwa nini timu hii ya wanawake ambayo inaiwakilisha Taifa nje ya nchi na imeweza kuonyesha michezo mizuri, nao wasikatiwe Bima ili wanapocheza basi angalau wajue wanacheza, hata wakiumia wanaweza kupata matibabu?

Mheshimiwa Spika, kingine wanadai kwamba wana matatizo katika timu yao, kwamba Uongozi wa *Twiga Stars* wakikuona wewe ni msemaji sana, wanakuondoa kwenye timu. Sasa hii inawasababisha watoto hawa kukata tama, kwa sababu tunajua kabisa mpira ndiyo ajira yao na ni watoto wa kike, tunatakiwa tuwasikilize matatizo yao na tuweze kuwasaidia. Ninaamini Twiga ni timu nzuri na kama tutawasaidia na kuacha hii biashara ya kupitapita kuomba, itakuwa ni timu nzuri.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Juma Nkamia - Mbunge wa Kondoa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, aliuliza swali hapa, na wakadai kwamba kuna fedha zinazotoka *FIFA* kwa ajili ya *Twiga Stars*. Tungependa kujua ni kiasi gani kinatengwa kwa ajili ya timu hii ili tuweze kuijenga timu yetu vizuri na ninaamini inaweza kuiletea heshima nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine la mwisho, nizungumzie Kiswahili. Kiswahili ni lugha ya Taifa ya nchi yetu, lakini Tanzania tumekuwa hatujisikii fahari kukitumia Kiswahili chetu. Tunakuwa na semina mbalimbali, makongamano mbalimbali, lakini cha kushangaza unakuta kinatumika Kiingereza wakati washiriki wengi ndani ya semina hizo ni Waswahili, Watanzania. Wageni unaweza kukuta ni wawili, watatu lakini kinatumika Kiingereza, tunakiacha Kiswahili chetu. Ifike wakati sasa sisi kama Watanzania tukiheshimu Kiswahili chetu na tujisikie fahari kukitumia popote pale tunapokuwa.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazotungwa hapa Bungeni zinatungwa kwa Kiingerza, wapiga kura wetu, Watanzania wengi ni wangapi wanaojua Kiingereza? Sheria hizi zinatumika Mahakamani, wapiga kura wetu wanalalamika, hawaelewi! Kwa hiyo, naomba sana Kiswahili kipewe nafasi yake ili kiweze kutumika maeneo yote na Watanzania waelewe ni kitu gani kinazungumzwa, kwa sababu hata kama tunapata ufadhili kutoka nje, isiwe kigezo cha kutunyima sisi kukitumia Kiswahili chetu. Kiswahili ni lugha ya Taifa, lazima tuienzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo machache niliyokuwa nayo. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini kwanza, nilikuwa naomba niungane na Watanzania wenzangu kwa kutoa pole kwa maafa yaliyotokea Zanzibar. ungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi. Kwa wale ambao wamepata majeraha, basi Mungu awape unafuu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuishukuru familia yangu nikianzia na mume wangu mpenzi Hamid Ahmed Hamid, mtoto wangu Asha Hamid na wadogo zangu George na Monica kwa uvumilivu wao kipindi ninapokuwa natekeleza kazi za Taifa. Napenda pia kuwatakia Mfungo mwema Waislamu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuchangia hotuba yangu na nitagusa katika masuala ya michezo, habari, nitazungumzia pia na vijana.

Mheshimiwa Spika, sitasita kuanza kwa kuipongeza Serikali yangu kwa kuhakikisha kwamba mashirikisho yameundwa. Lakini pamoja na pongezo hizo, bado naikumbusha Serikali yangu kwamba tatizo la hati miliki kwa wasanii bado ni tatizo kubwa. Japokuwa kwamba Serikali imeanza kurasirimisha kazi za wasanii kwa kuweka *bar code* na stempu katika kazi zao, lakini bado tatizo hili ni kubwa. Hivyo, naomba Serikali izidi kuliangalia kwa macho mawili kwa sababu waathirika wengi katika sanaa ni vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishauri Serikali kutokana na tatizo kubwa la usambazaji wa kazi za wasanii. Kazi za wasanii zinazosambazwa, haziwanufaishi wasanii, kwa sababu katika kila video moja, msanii anapata Sh. 300/= tu na katika *CD* za muziki wanapata Sh. 250/= mpaka Sh. 200/=. Suala hili tumelizungumzia mara kwa mara katika Bunge hili lako Tukufu, lakini bado hatujaona kwamba hatima ya tatizo hili inafikia. Hivyo basi, naikumbusha Serikali yangu iweze kufuatilia kwa ukaribu tatizo hili ikiwa ni pamoja na Serikali kuweza kuchukua jukumu hili la kusambaza hizi kazi yenyewe ili kuweza kuwapa manufaa wasanii hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sasa niende kuzungumzia suala la habari. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, naomba anieleze katika Tanzania kuna magazeti mangapi? Ili niweze kuyatambua. Lakini pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, kila mara Mawaziri wa Wizara hii ya Habari, Michezo, Utamaduni na Vijana wanapenda kuzungumzia kuwa Waandishi wa Habari wawe wanaandika habari ambazo zina ukweli na zinaelimisha jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Kuna baadhi ya Waandishi wa Habari ambao wanaandika habari siyo za kweli na pia zinaleta uchochezi katika jamii. Kwa mfano, sisi Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji, tulikwenda Misenyi kuangalia matatizo kati ya wafugaji na wakulima. Tulivyofika kule, tulitizama matatizo haya ya wafugaji na wakulima na mimi ndiyo niliyekuwa nikiongoza Kamati. Baada ya kurudi tu Dar es Salaam, tukakuta kwenye magazeti habari imeandikwa *DC* Misenyi awekwa kitimoto, kitu ambacho hata katika ratiba yetu ile hakukuwa na sehemu ambayo tulimhoji *DC* huyo. Hivyo basi rai yangu kwa Waandishi, tuwe makini katika kuandika habari za ukweli na habari ambazo zitaisadia jamii na siyo kupotosha jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Museveni alisema, kutokana na *Makanjanja* katika utoaji wa habari, aliamua kuweka Sheria ya kwamba, kila Mwandishi wa Habari awe na Digrii ili kuleta weledi katika taaluma hii ambayo ni muhimu sana katika jamii. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri: Je, kwa upande wetu sisi Watanzania, tunalichukuliaje suala hili? Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kwa Waandishi wa Habari ambao wanatoa habari ambazo siyo za ukweli na zenye kupotosha jamii?

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la *TBC.* Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na pongezi zake nyingi sana alizozitoa kwa *TBC,* lakini bado kuna matatizo madogo madogo ambayo yanatokea *TBC.* Tatizo mojawapo ni kukwama kwa habari mara kwa mara. Utakuta mtu umekaa unatazama Taarifa ya Habari, mara habari imekwama. Naomba Mheshimiwa Waziri, anapokuja kufanya majumuisho aniambie, kuna matatizo gani katika mitambo hii au mashine hizi zinazotoa habari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nigusie suala la *blog.* Tumeweza kupata habari mbalimbali kutokana na *blog,* nyingine zinaelimisha, nyingine zinabomoa, nyingine zinadhalilisha watu, nyingine zinawapendezesha watu. Lakini, nataka leo Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho aniambie, ni maadili gani yanayotawala habari zinazotokea kwenye *blog?*

Wasiwasi wangu ni kwamba, zisije kuhataraisha maslahi na amani ya nchi yetu, pia heshima binafsi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie suala la Vijana. Naishukuru Serikali kwa kuweka mchakato mzuri wa kuweza kutambua vijana walipo na wanafanya kitu gani, lakini pia, kuwatayarisha, ili waweze kuajirika na kuweza kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha Serikali, katika Halmashauri, kuna asilimia kumi ya mapato ambayo, 5% inakwenda kwa vijana na 5% ya mapato inakwenda kwa wanawake. Lakini nahisi katika Halmashauri zetu kwamba, zile 5% za mapato ambayo yanatakiwa yaende yakatumike kwa vijana, hayatumiki ipasavyo. Hivyo basi, naishauri Serikali, na kuikumbusha tena kwamba, hizi pesa 5% za mapato katika kila Halmsahauri, zitumike kwa kadiri ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nizungumzie suala la Mfuko wa Vijana. Kwa kweli, mimi nasikitishwa sana, katika Watanzania asilimiwa 68 ni vijana, lakini leo kweli, ukija kwenye Mfuko wetu sisi Vijana, unatengewa Shilingi milioni 100. Hii siyo haki na hii inazorotesha maendeleo ya vijana kwa sababu, Mfuko huu, utatumika katika kukopesha *SACCOS* za vijana. Sasa leo mnavyotuwekea Shilingi milioni 100 tu, na sisi tuko karibia 68% ya Watanzania, hivi kweli vijana tuna nia ya kukombolewa kiuchumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako vijana ambao wanaamua kujiajiri wenyewe kwenye kilimo. Ukienda pale Ruaha Mbuyuni, utakuta vijana wanafanya kazi, wamejiunga kikundi, wanalima vitunguu, wengine wanalima hoho. Ukienda kule Ilula, utakuta vijana ambao wanalima nyanya, ukienda kule Kalenga, utakuta vijana ambao wanalima mahindi mabichi maarufu kama gobo.

Mheshimiwa Spika, pia kule Njombe, kuna vijana ambao wamejiunga wanalima viazi na wanalima chai na mboga mboga. Vijana hawa, wote, tunategemea mfuko huo huo wa vijana, ili tuweze kukopesheka kwa sababu, sehemu nyingine wanazokwenda kukopa wanakuta masharti magumu, ikiwa ni pamoja na kuweka Hati za Nyumba, na mtu kama kijana hajakuwa na nyumba, ndiyo kwanza anaanza maisha, ameamua kujishughulisha na shughuli hizi za kilimo, lakini hawezi kukopesheka.

Hivyo basi, tulikuwa tunaiomba Serikali, iwaandalie mazingira rahisi ya kukopesheka, ikiwa ni pamoja na kuongeza pesa katika Mfuko huu wa Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, pembejeo kwa vijana wale ambao wamejikita katika kilimo ni tatizo, kwa sababu hazifiki kwa wakati. Hata kama zikifika, bado zinakuwa ziko chache.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ni kengele ya pili Mheshimiwa.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, ashirikiane na Wizara nyingine katika kuhakikisha vijana hawa wana…

**SPIKA:** Ahsante, kengele ni ya pili.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi pia, niweze kuchangia katika Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Kwanza kabisa, napenda kusema kwamba, siungi mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa sababu nimeona kwamba, mambo yale ya msingi kabisa katika Wizara yake bado hayajapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, Wizara hii iliomba kutengewa Shilingi bilioni 18.5 na ukiangalia fedha ambayo Wizara hii imeomba kutengewa kwa mwaka huu wa fedha, Shilingi bilioni 19.3 inaweza kuonekana kwamba ni nyingi. Lakini kimsingi, fedha hii haitoshi

hata kidogo. Kwanza kabisa, kwa sababu suala zima la vijana linahitaji kutengewa fedha za kutosha, kwa sababu imekuwa kama wimbo katika Bunge lako hili Tukufu, kwamba vijana watengewe fedha, vijana watengewe fedha. Tumeambiwa itaanzishwa benki kwa ajili ya vijana, lakini mpaka sasa hakuna kitu chcochote ambacho kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia kuhusu utamaduni. Nchi yoyote duniani inakuwa na utamaduni wake. Tanzania imebahatika kuwa na makabila mbalimbali. Katika Makabila hayo, makabila mengi yana tamaduni zake. Wizara kama hii ambayo inashughulikia tamaduni, sijaona kwamba imetenga fedha za kutosha kushughulikia utamaduni wa nchi yetu. Bado vijana na hata watu wazima, wanaishi kwa kuigaiga tamaduni za nchi mbalimbali, kwa sababu tunashindwa kutumia vyombo vya habari ipasavyo kuwaelimisha Watanzania umuhimu wa kudumisha utamaduni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utamaduni uko wa aina mbalimbali. Kuna muziki wetu, ngoma zetu za kienyeji, kuna vyombo vya asili, vijiko, vikombe, sahani, kuna mavazi na lugha. Ni hivi karibuni nimeona katika Vyombo vya Habari, Mtaalamu kutoka Japan, akionyesha utamaduni wa Japan, katika maonesho yaliyokuwa yamefayika Dar es Salaam. Lakini ni mara ngapi sisi Watanzania, tumeweza kuwa na maonyesho ya tamaduni ya mambo yetu, ya vifaa vyetu vya kale, kuvidumisha kwa vizazi vyetu, ili vijana wetu na watoto wetu wanapokua waweze kuheshimu utamaduni wetu? Waweze kuuenzi na kuupenda na kujua kwamba, huu ni utamaduni ambao ni mzuri na siyo lazima kuchanganywa na utandawazi na kubabaishwa na kuendelea kuiga utamaduni wa nchi nyingine? Ni kweli, inafaa kuiga utamaduni wa nchi nyingine, lakini utamaduni wetu ni vizuri tukaudumisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee Kiswahili. Kiswahili ni lugha ambayo inakua kwa kasi sana. Sasa hivi tumeambiwa kwamba, zaidi ya wazungumzaji milioni 500 wanazungumza Kiswahili. Lakini tunaambiwa, katika Vyuo vingi vya nje, Walimu, Watafsiri, wanaotumika ni Wakenya. Wanatumia Kiswahili kilichoharibika, kilichovunjwavunjwa na sisi Watanzania, hatutaki kuchangamkia fursa hizo. Tumeendelea kukaa tu na kuwaachia Wakenya, wanaendelea kukitumia Kiswahili na sisi tumekaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako watu katika Karne ya 19, kwa mfano, mtaalamu mmoja, Tonsen Cameroon, ambaye aliona umuhimu mkubwa wa kufanya utafiti wa lugha ndogo ndogo za duniani na kuziweka katika kuandika. Nimeshangaa hapa Dodoma Shirika hilo lipo, *SIL Tanzania.* Linahusika kufanya utafiti wa makabila madogo madogo na kuandika. Lakini Tanzania, Wizara, siyo ajabu hata haina habari kwamba hapa Dodoma kuna Shirika kama hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeishauri Wizara iweze kufuatilia na kujua kwamba, hawa *SIL Tanzania* wanafanya nini? Kwa sababu, duniani, wanaitwa *SIL,* lakini kwa hapa Tanzania, wanatumia *SIL Tanzania.* Wizara ingefuatilia ikajua hili Shirika linafanya nini? Kwa sababu, ni muhimu tusizipoteze lugha zetu. Zile lugha za makabila zinapotea, Wasegeju kwa mfano, lugha ile haiko, haijaandikwa; Kisandawe, nasikia pia hakijaandikwa na kama kimeandikwa ni kwa kiwango kidogo, lakini tunahitaji kuona kwamba, lugha za makabila mbalimbali zinahifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia sasa kuhusu mavazi. Kwa kweli, sielewi ule mpango wa Vazi la Taifa umefikia wapi. Labda inakuwa ni vigumu kwa sababu katika makabila hayo zaidi ya 120 pengine Wizara inashindwa kujua sasa ichukue vazi gani.

Mheshimiwa Spika, nataka niwapongeze sana Wamasai kwa sababu, kwa kiwango fulani Wamasai, wameweza kuuenzi utamaduni wao na vazi lao. Hata hivi karibuni, naona sasa hivi wameboresha, badala ya kukaa tu nusu uchi, wameweza kuweka nguo ya ndani, lakini ule utamaduni unabaki. Ni utamaduni ambao ni kweli, wageni pia wameupenda na ni utamaduni ambao hata Mataifa ya Nje yanapokuja yanapenda kuvaa viatu vya Kimasai, kuvaa nguo ile ya Kimasai. Sisi tunahitaji kuwa na Vazi la Taifa ambalo litakuwa ndiyo sura ya Tanzania na ndiyo utambulisho wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda kwa haraka pia, niongelee kuhusu habari, nikijua kwamba, vyombo vya habari vina nguvu sana. Kama tukivitumia vyombo vya habari vibaya, vitafanya

vibaya, mambo mabaya yataendelea. Lakini tukitumia vyombo vya habari vizuri, vina nguvu na watu wanaweza kuelimishwa kuhusu masuala mbalimbali hata ya Kilimo Kwanza na masuala mbalimbali yanayohusu Utamaduni, Michezo na Maendeleo mbalimbali kwa wananchi, kwa kutumia vyombo vya habari. Lakini, labda nizungumzie kwamba, Waandishi wa Habari wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Pengine ni kwa sababu hakuna Sheria ambayo inawalinda na hivyo wanapotaka kupata habari, inakuwa ni vigumu sana wao kupata ile habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hivi majuzi Mwandishi mmoja wa *Channel ten* ametishiwa kuuawa na Kiongozi mmoja wa Serikali wa ngazi ya juu Mkoani Pwani, kwa jina huyu Mwandishi anaitwa Marieta. Alipokuwa kazini, akitafuta habari kuhusu Afisa huyu wa ngazi ya juu wa Serikali, ambaye ametumia njia za panya kuunganisha umeme katika nyumba yake na hivyo, jamaa zake na huyu Afisa, wamemtishia huyu binti kwamba, wangechota mchanga wa nyayo zake na kwenda kumloga ili ashindwe kufanya kazi. Huyu ni Mwandishi mmoja ambaye tumepata taarifa yake. Lakini kuna Waandishi wengi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu, liwepo jua, iwepo mvua, masaa mengi bila kupata mlo na wakati mwingine kulipwa mshahara kidogo au kukopwa mshahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Dkt. Reginald Mengi kwamba, hivi karibuni ameweza kutangaza kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wake. Hivyo, ningetoa wito kwamba na wamiliki wengine wa vyombo vya habari wazingatie maslahi ya waandishi. Pia, Wizara mbalimbali za Serikali, zitoe ushirikiano kwa Waandishi wa Habari. Sikatai kwamba kuna Waandishi wengine ambao hawafuati Maadili ya Uandishi, wapo. Wengine hawaandiki katika viwango vinavyokubalika, huo ni ukweli, sipingi. Lakini wako wengine ambao wanafanya vizuri. Hivyo, basi, ninaomba Wizara, iharakishe kutengenezwa kwa Sheria hii ya Habari, ili Tasnia hii ya Habari, iweze kufanya kazi katika taaluma na katika weledi na miiko ipasayo katika habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa kufikia hapo, naomba kumaliza, lakini kwa kusema kwamba, suingi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Namshukuru Mungu pia kwa kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya habari.

Mheshimkiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza watendaji wa Wizara hii, nikianzia Mheshimiwa Waziri, nikianzia Naibu wake na Watendaji wote kwa bajeti nzuri na kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu ya muda, ningeomba tu nijikite moja kwa moja kwenye kuchangia hoja katika kushauri. Kwanza nianze na mavazi ya vijana.

Mheshimiwa Spika, kuna mavazi ya *skin tight,* kuna mavazi ya vi-*top* tumbo wazi, haya mavazi yanavaliwa mpaka sehemu za *public* kama Mahospitali, Posta, yaani ni kama yamehalalishwa. Wakati mavazi haya kwa kweli, yanakera, mavazi haya yanatia aibu, hata kama ni vijana, basi mjue na mahali penu pa kuvaa mavazi kama haya. Lakini sio mahali ambapo watu wazima tunawaona, maumbile wengine ni maumbile makubwa, halafu unaacha tumbo wazi kwa kweli, jamani Wizara, iangalieni kama mtatunga Sheria. Kwa kweli, kuna uhuru wa kuvaa, lakini sasa vaa mavazi ambayo yanastaha. Lakini kama hayana staha, uhuru wa mavazi ni kama vile hatuutendei haki. Kwa hiyo, naomba vijana wetu muangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wa kiume nao wanaendelea kuvaa suruali chini ya makalio. Eeh! Jamani, kweli, ni mavazi ya vijana, lakini mtafute mahali pazuri pa kuvaa, siyo mbele ya wazazi wenu. Kuna wazazi wengine wanasema, nimemnunulia mwenyewe. Unatetea kweli, jamani, mtoto wako akitembea nusu uchi! Si aibu! Hata kama tumesoma, hata kama tumekaa Ulaya miaka mingi, sasa si tumerudi Tanzania kwenye utamaduni wa Kitanzania? Sasa tukiwafundisha watoto wetu mambo haya yaendelee, ambayo mlikuwa labda mkifanya kule Ulaya, kwa sababu watu wote wanafanya hivyo, siyo vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mzazi, naomba wazazi wote wa Tanzania, tuangalie watoto wetu wanapotoka nyumbani wanakwenda wapi? Baadaye, tunalalamika amebakwa, kwa sababu ya mavazi, yanavutia watu, eeh! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba tena niongelee jambo moja la Ngoma ya Kanga Moja. Hii kanga moja, mwenzangu ameongea kidogo, lakini hakufikia maana yake ni nini au wanavaaje. Hiyo nguo ya kanga moja, tena inalowanishwa maji, ikishalowanishwa maji, binti anaivaa hiyo, halafu anafanya mnenguo. Sasa niambie, kila kitu kinaonekana! Tuseme ni kama hakuvaa nguo. Sasa hapo niambie, mtu mwenye umbile kubwa, acheze bila nguo mbele za watu, inakuwaje? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni mchezo unachezwa kweli, siyo mchezo! Tena wazi na watu wanafurahia wanakwenda. Jamani tuangalie vitu vingine jamani! Hata kama haujawa mtu wa dini sana, lakini si kuna maadili? Eeh, tushikilie maadili yetu, yanamomonyoka, tunayamomonyoa wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu naomba pia nichangie kuhusu vipindi vya *TV* na vya Redio. Kuna vipindi, vyote vimejikita kwenye muziki, vimejikita kwenye tamthilia, vimejikita kwenye michezo ya mapenzi, lakini mafundisho ni machache sana. Mimi nilikuwa naomba, jamani, mbona tuna Wataalamu wengi? Tuna Madaktari, wanaweza kutufundisha, kuna watu ambao wamestaafu, wana nafasi zao, wana uwezo, wana ujuzi mwingi, wangeweza kutumiwa kufundisha kilimo, kufundisha Sheria, kufundisha mambo mbalimbali; tutumie muda mwingi kufundisha. Kwa sababu, kwa asilia tunajulikana kwamba, Watanzania, ni wavivu wa kusoma, tunapenda tu kusikia. Sasa kama tunapenda tu kusikia na kuona, basi tuone mafundisho ambayo, yanaweza kutusaidia, kwa maana hatuna muda wa kusoma vitabu. Kwa hiyo, *chance* tuliyonayo ni kuangalia *TV,* kuliko kila saa kuangalia tamthilia, nini.

Mheshimiwa Spika, halafu naomba pia niongelee habari ya taarifa za habari kwenye vyombo vyetu vya habari, zinakuwa fupi mno. Leo ukiangalia kama *East Africa* unaonyeshwa tu, kweli ni habari za Afrika Mashariki, habari za Kenya, lakini unaonyesha tu pyaa, inapita sekunde moja nyingine inapita pyaa, nyingine inapita; jamani, mbona nzuri habari hizo! Tungependa kuzijua kwa undani, mbona muda mnao? Mbona tamthilia mnaipa lisaa lizima? Kwanini taarifa muhimu hamzipi muda wa kutosha? Jamani tungetoa pia muda wa kutosha kwenye kipindi kile cha taarifa ya habari ikiwezekana irudiwe kama *CNN* na *BBC.* Mara nyingi wanarudia, unakaa tena baada ya masaa fulani wanarudia, baadaye wanarudia. Kwa hiyo, wataalam wanasema kwa mtu kuelewa jambo ni mpaka asikie mara 16. Sasa sisi tunasikia mara moja tu, tena kwa kiduchu. Kwa kweli ni kama watu hawapati habari za uhakika. Nilikuwa naomba wenye vyombo vya habari wazingatie taarifa ya habari. Ni muhimu sana, ni kipindi kinachoelewesha, kinachofundisha na ni vizuri kweli! Tupatiwe muda wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia tena jambo lingine kuhusu utabiri wa hali ya hewa. Utabiri wa hali ya hewa unatolewa, yaani kijanja kijanja, ooh itakuwa hapa pande hizo kushoto na za kulia itanyesha mvua, kutakuwa na manyunyu ya hapa na pale! Watuambie vizuri tuelewe, kwa sababu udhibiti wa hali ya hewa unasaidia. Kwa mfano kwenye hii ajali, kama tungekuwa na wale watu wanaotupa hali ya hewa wangesema hii meli isiondoke, kuna mawimbi makubwa, kuna nini, kuna upepo mkali. Watu wasingeondoa meli, kwa sababu kweli siku ile miti iling'oka, upepo mkali, asubuhi kulikuwa na upepo mkali sana kule Dar es Salaam. Kwa hiyo, nyumba mbovu mbovu zilizokaa karibu na ufukwe na nyingine zimeng'oka kwa sababu kwa kweli ilikuwa ni upepo mkali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama na hawa watu wa utabiri wa hali ya hewa, watutabirie vizuri, tena wachukue muda, watangaze. Kama siku moja walikuwa wametangaza kwamba kuna Tsunami, kwa hiyo, watu wanaokaa pembezoni mwa bahari mjihadhari. Watu wakaondoka, wengine wakaenda Kibaha, watu walikimbia, wengine walikuja Morogoro, lakini haikutokea. Tunashukuru Mungu, lakini *message was sent* na tulifurahi. *(Makofi)*

Sasa mimi nilikuwa nasema hivi, jamani zile habari zitolewe kwa makini na zikitolewa kwa makini watu watakuwa na tahadhari kwa maana hakuna mjinga anayesikia hatari halafu

ajipeleke huko kwenye hatari. Halafu kitu kingine cha mwisho, nilikuwa nasema, jengo la *TBC, TBC* wanasema Desemba tunakwenda kwenye *digital*, wanatoka kwenye *analogue* lakini kwa kweli majengo yao hayafananii na *digital.* Inatakiwa na majengo tuyakarabati, au tumalize lile jengo ambalo ni nusu, liweze kulingana na hali halisi ya mabadiliko ya ulimwengu *digital,* twende ki-*digital.* Kwa hiyo, jamani *TBC* mjitahidi na Wizara tunaomba muisaide *TBC* yenyewe pia iweze kwenda *digital* kama tunavyotarajia kubadilika. *(Makofi)*

Mwisho, vazi la Taifa. Muda bado unaniruhusu, niongelee vazi la Taifa. Kwa kweli mtupe watu tunaovaa mavazi ya staha. Kwa kweli tunaweza kabisa, kwa sababu sasa unamwambia mtu achore mchoro, tunachojua ni nini? Wote tunajua vazi letu la kitaifa ni khanga, ni kitenge, kitu muhimu ni mshono tu. Mimi sioni namna ya kuchora, kupanga kufanya nini michoro ya kisasa, wengine hatutaivaa, wekeni vazi *decent* kwa kitenge au kwa khanga kwa maana wote tunajua hizi ndiyo nguo muhimu Tanzania zinavaliwa au Afrika Mashariki ndiyo zinavaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana Utamaduni na Michezo pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kuchangia michezo. Mwaka 2005, Mheshimiwa Rais alipokuwa akizindua Bunge, alivitaja vipaumbele 10 ikiwa ni pamoja na michezo. Wakati ametoa vipaumbele 10 hivyo, michezo ikiwa ni kimojawapo, Mheshimiwa Rais alipomaliza tu alimteua Kocha wa michezo Ndugu Maximo enzi hizo, akaja Tanzania, akafundisha timu ya *Taifa Star* na walipokwenda kucheza na Burkina Faso, *Taifa Star* walifunga 2-1 kutokana na juhudi alizokuwa amezionyesha Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuja kuwafundisha vijana wetu. *(Makofi)*

Vijana wale waliposhinda Watanzania tulifurahi sana na kwa mara ya kwanza walikuja humu Bungeni tukawapongeza. Kwa kweli walilileteа Taifa letu heshima kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu sasa sisi viongozi kufuata nyayo za Mheshimiwa Rais wetu, alionyesha mfano, kwa hiyo, sisi tunatakiwa kuiga jinsi alivyotufundisha. Vijana wengi katika Halmashauri zetu na katika vijiji vyetu wamekuwa na hamasa kubwa ya kutaka kucheza mchezo wa mpira, lakini kutokana na hali duni, wakati mwingine wanaishia vijijini na kwenye Halmashauri zetu vipaumbele vinabaki huko huko kwa sababu ya ukosefu wa pesa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Michezo kwa kushirikiana na Waziri wa TAMISEMI waweze basi kurejesha ile asilimia tano ipelekwe kwenye Halmashauri zetu, ikiwezekana pesa hiyo ikipatikana vijana waweze kupata pesa hiyo, wapewe waende kujiendeleza katika vipaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi midogo midogo ili wanapotaka kuanzisha michezo yao, wachukue pesa ile ambayo wamepewa kusudi waendeleze juhudi zao walizokwishajiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Diwani kwa mujibu wa sheria, kwamba kila Mbunge wa Viti Maalum au Mbunge yeyote hata akiwa wa Jimbo katika Halmashauri ni Diwani. Sioni kama Halmashauri zetu zinatilia maanani kuhakikisha michezo inapewa kipaumbele. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe anawasiliana na Waziri wa TAMISEMI kuagiza Wakurugenzi wote suala la michezo katika Halmashauri lipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maafisa Utamaduni walioko kwenye Halmashauri zetu na wao pia wanahangaika, hawana mashiko kwa sababu hawana vitendea kazi. Naomba nao waongezewe pesa ili waweze kuzuka kila sehemu kwenda kuhamasisha suala la michezo. Michezo ni afya, michezo ni ajira, michezo inaongeza ajira nyingi kwa sababu vijana wakiwa imara watakuwa ni wepesi hata kwa kufanya kazi za maendeleo. Kwa hiyo, naomba, tunajua kabisa kwamba Wizara yako haina pesa, naomba Serikali waweze kuwaongezea pesa ili muweze kusaidia na Halmashauri zetu kuweza kuhakikisha mnaongeza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo tutawezaje kuinua vipaji vingi kwa vijana wetu? Vijana wanapenda sana kucheza na hata wakati mwingine kwa kupitia Bunge lako Tukufu, nawaomba Watanzania na hasa kule ninakoishi, Kasulu, mara nyingine wanaposikia kwamba vijana wanataka kujitokeza kuanzisha ligi katika vijiji vyetu, katika Tarafa zetu, katika Wilaya zetu, wanapotaka michango, tujitolee kuwachangia, kwa sababu hata harusi tunazichangia, *kitchen party* tunazichangia. Sioni sababu kutokuwachangia vijana wetu kwa ajili ya kuanzisha michezo katika Halmashauri zetu katika vijiji vyetu na katika Tarafa zetu. Kwa hiyo, nawaomba Watanzania mjitolee kuwachangia vijana wetu ili kuendeleza michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Tauhida, mchezo wa mpira unachezwa, unapendwa, na mara nyingi timu hizo za nje ikianza ligi, hakuna mtu anayebaki ndani. Kila mmoja anataka kwenda kuangalia kwenye kumbi za mchezo.

**MBUNGE FULANI:** Simba!

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE**: Siyo Simba, Yanga bwana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kila mmoja anapenda kwenda kuangalia michezo, sioni sababu tusijitolee kuchangia timu zetu katika Halmashauri zetu, katika vijiji vyetu ili michezo iweze kusonga mbele. Mimi binafsi napenda mpira wa miguu, lakini na *netball* naipenda. Nawaomba Watanzania tujitolee kuwachangia vijana wetu waweze kuendeleza michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya kwangu yalikuwa ni hayo, nawaomba vijana wote nchini wasikate tama, sisi Wabunge tutaendelea kuwatia moyo ili waweze kuanzisha timu zao za michezo, nami kuna timu ambazo nimeshaahidi kuziunga mkono, siku moja Mheshimiwa Waziri nitakuita uje uzizindue, nakukaribisha Kasulu. Lakini naipongeza timu ya Yanga kwa kuingia nusu fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** iko tofauti kati ya kupenda na kucheza. Sasa Mheshimiwa Ngezabuke kama anaweza kucheza *football* sawa. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baadaye tukirudi mchana nitamwita Mheshimiwa Jasson Rweikiza atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad na Mheshimiwa Mkuchika ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mengine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.15 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilipokuwa nasitisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi nilisema nitamwita Mheshimiwa Jasson Rweikiza na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad na wengine nitawataja baadaye.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza!

**MBUNGE FULANI:** Mtera!

**SPIKA:** Siyo Mtera, yupo!

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kuhusu Wizara hii ambayo ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita kwenye eneo la habari, japokuwa hii Wizara ina vitengo vingi kama Vijana, Habari, Utamaduni na Michezo, lakini nitapenda nizungumzie habari na muda ukiruhusu, nizungumzie pia Vijana.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba vyombo vya habari vina jukumu kubwa katika jamii kama kuelimisha wananchi, kupasha habari, kuburudisha na kadhalika. Pia kutokana na sera nzuri ya CCM na Serikali yake, nchi hii ina vyombo vingi vya habari, ambavyo vinafanya kazi ya kupasha habari, kuelimisha na kuburudisha. Lakini baadhi ya vyombo hivi vimekuwa havifanyi vizuri ama havina uwezo wa kutosha kufanya kazi zake ama kwa makusudi vinapotosha. Kuna vyombo vya habari havina Waandishi wa Habari au vina Waandishi wa Habari ambao hawana taaluma ya Uandishi wa Habari, vinachukua vijana tu ambao hawakusomea habari, hawana ujuzi na Uandishi wa Habari, lakini wanasema ni Waandishi wa Habari. Hawajui miiko.

**SPIKA:** Naona mashine yako inakusumbua labda uhamie nyingine.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa hiyo, Waandishi wa Habari wanafanya kazi kwa kubahatishabaharisha, hawazingatii maadili ya Waandishi wa Habari, matokeo yake tunapata habari ambayo siyo sahihi kwenye vyombo hivi. Ama wana waandishi lakini hawawapi vitendea kazi vya kutosha.

Juzi nilikuwa naongea na mwandishi mmoja wa habari nikamwuliza, mbona hamwendi vijijini? Akasema hatuna uwezo wa kwenda vijijini, hatuna *camera*, hatuna magari na kadhalika. Lakini hata wenye uwezo huo, hiyo ndiyo muhimu zaidi. Wanafanya uandishi wa habari ama wanatoa habari ambayo siyo kwa maslahi ya Taifa, yaani hayazingatii sheria wala maadili ya uandishi wa habari. Utakuta wanafanya kazi kwa upendeleo mkubwa, hasa enzi hizi ambapo kuna Vyama vingi vya Siasa, Chama Tawala au Vyama vingine. Sasa mmiliki anaweza kuwa ni wa Chama kingine au ni wa Chama Fulani, hata kama ni Chama Tawala, anaandika habari kwa kuegemea upande mmoja, lakini mimi nasema hili siyo sawa! *(Makofi)*

Vyombo ni kwa manufaa ya umma kuzingatia sheria, kutoa habari…

**SPIKA:** Kuna *interruptions* sana katika *microphone* yako. Sijui uhamie mstari wa pili! Tutakurudishia *time* hiyo iliyopotea.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Hata hii ni hivyo hivyo, maana imeanza ku-*flash*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapata matatizo kwenye vyombo vya habari, hasa pale ambapo wamiliki na wengine kwenye vyombo hivyo wanakuwa na mwegemeo mmoja kwenye upande wa kisiasa. Kwa hiyo, lile lengo la kutoa habari sahihi kwa wananchi, kuelimisha na kuburudisha linakiukwa. Wananchi wanapewa habari za uongo, lakini tumesikia asubuhi Waziri amesema katika kipindi kilichopita cha mwaka mmoja, wametoa onyo kwa vyombo vitano vya habari. Sasa asubuhi ukisoma magazeti yanapouzwa, vichwa vya habari unakuta ni uchochezi, na uchochezi siyo makusudi ya kuunda vyombo hivi. Wanaingia kwenye mambo ya kisiasa. Sio wote, ni baadhi yao, tunawajua wamiliki wengine, tunajua mielekeo yao ya kisiasa, lakini tunawaomba wawe waadilifu, watoe habari kwa ukweli na kwa uhakika bila upendeleo wa kisiasa ili wananchi wanaowasikiliza au kuwasoma au kuwaona kwenye televisheni wasipotoshwe. Hili ni la muhimu sana kwa Wizara kulizingatia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutoa adhabu kwa vyombo vitano katika mwaka mzima haitoshi, lazima Wizara iwe macho sana, yaani iwe makini sana kuangalia vyombo ambavyo vinapotosha wananchi kwa kutoa habari potofu kwa lengo la kutoa upendeleo kwa upande mmoja. Hili lizingatiwe sana na lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana, Wizara hii ina wajibu mkubwa kwa nchi hii kuhusu vijana, maadili, malezi na mwenendo mzima wa makuzi ya vijana na hakuna chombo kingine chenye wajibu huo wa kuangalia vijana hawa wanafanya nini na wanakua vipi. Kwa hiyo, naiomba Wizara hii pia iweke msisitizo mkubwa upande wa vijana.

Mheshimiwa Spika, asubuhi tumepewa dodoso na tumelijaza kuhusu matatizo ya vijana kwenye Majimbo yetu. Tuna matatizo makubwa kama ukosefu wa elimu ambayo ni elimu ya ujasiriamali, ukosefu wa mitaji, lakini pia na tabia nyingine ambazo vijana wanajiingiza kutokana na ujana wao bila kujua madhara yake. Wengine wanakwenda kwenye kuvuta bangi na

wengine wanaiga tamaduni za nje bila kujua madhara yake, wanakuta wameingia kwenye mkumbo ambao siyo mzuri. Kwa hiyo, nchi hii haiwezi kuwa na mustakabali mzuri huko tunakokwenda bila kuwa na malezi mazuri kwa vijana, kwani hawa ndio raia wa kesho. Lakini wenyewe wanasema, raia wa leo. Lakini na kesho pia ndiyo watatakiwa washike madaraka. Sasa bila kuwa wamekaa vizuri na kuelimika vizuri na kulelewa vizuri, nchi haiwezi kuwa na viongozi wazuri baadaye wa kuongoza nchi hii na wananchi wa nchi hii. Kwa hiyo, Wizara iweke msisitizo wa makusudi katika malezi na makuzi ya vijana.

Bukoba Vijijini mwaka 2011 nilisema hatuna Chuo cha *VETA* cha ufundi kwa vijana. Sasa vijana wanajiingiza kwenye mambo ambayo siyo mazuri. Chuo hiki kingekuwepo, vijana wangejiunga, wangesoma ufundi stadi mbalimbali na wakajiajiri wenyewe au wakaajiriwa. Kwa Wizara hii na Wizara nyingine zinazohusika kama Wizara ya Ajira na Vijana, wangeshirikiana kwa umakini mkubwa kuboresha hasa Vyuo vya Vijana vya Stadi mbalimbali ili kujenga ustawi na mustakabali wa vijana. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumejenga mustakabali wa nchi hii kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na sasa nimwita Mheshimiwa Hamad Ali Hamad na baada ya hapo, nitamwita Mheshimiwa Mkuchika.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kupata nafasi hii, lakini awali kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na kunikutanisha tena na mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Niwaombee Waislamu wote Tanzania na duniani, funga njema na yenye baraka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar kwa maamuzi magumu aliyoyafanya kwa maslahi ya Zanzibar. Naomba uwe ni mfano kwa wengine katika Wizara mbalimbali za Bara na Zanzibar. Lakini pia niwapongeze timu ya Mafunzo ya Zanzibar kwa namna walivyotoa upinzani mkali kwenye mashindano ya Kagame yanayoendelea. Wametolewa, lakini wametolewa kishujaa, na katika ile hali ya kawaida tu ya kwamba wanaoshindana wawili ni lazima mmoja aibuke mshindi. Lakini Yanga watakumbuka na wataweka kwenye kumbukumbu zao kwamba jana ilikuwa siku moja nzito kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la habari. Katika suala la habari, nayo pia ni sehemu moja katika sehemu za ajira kwa vijana wetu. Katika suala la ajira, kila mmoja anapata ajira kwa namna ya uwezo na fani aliyonayo. Lakini tunajua kwamba kuna waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali ambao hawajaajiriwa, lakini wanasaidia Watanzania wengine kupata taarifa juu ya matokeo mbalimbali. Lakini mafao yao waandishi hawa ambao hawajaajiriwa yanategemeana na *story* ambazo wanapeleka katika vyombo mbalimbali. Kinachosikitisha pia ni kwamba baadhi ya wamiliki wa vyombo wanakuwa wakitumia kigezo cha kupima *story* zao kwa kutumia rula kama kigezo cha kwamba sasa wanaweza wakalipwa kwa kutumia kigezo hicho.

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi, waandishi wengi wanakuwa hawajaajiriwa kwa hiyo, uwezo wao pia wa kujiendeleza unakuwa mdogo. Ni vyema na ninaomba wamiliki wa vyombo hivi, lakini pia Serikali na Mheshimiwa Waziri naye atilie mkazo kuwataka wamiliki wa vyombo hivi wawasharikishe wenye vyombo hivi waweke mafungu maalum kwa ajili ya kuwaendeleza kimasomo waandishi ili waongeze uwezo wao wa kuandika taarifa zile ambazo tunazihitaji.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la *TBC. TBC* ndicho chombo chetu Tanzania cha Habari cha Taifa, lakini mazingira ya *TBC* yanasikitisha sana. Naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ambayo Wizara ya Habari ipo chini ya Kamati yetu. Lakini nadhani watu wa *TBC* katika kuonyesha mazingira magumu ya utendaji wa kazi katika maeneo yao, walitualika siku moja na tulibahatika nadhani ndiyo siku waliyochagua, tulikwenda siku ambayo mvua inanyesha.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni aibu kubwa kwa chombo cha Taifa kama hiki ambacho tunakitegemea, mle ndani katika maeneo ya vyumba vya kutangazia na vyumba vingine vya kuweka kumbukumbu tulivyoingia tulikuta mtangazaji amejifunika mwamvuli na tulidhani kwa haraka haraka kama vile ni wale vijana wanaouza *voucher* za *Tigo* na *line* za *Zantel* katika vijiwe vya huko Mitaani. Inatia aibu sana na inasikitisha! Lakini wafanyaje? Hii ndiyo hali yao na kwamba Serikali inatumia mara nyingi fedha nyingi kulipa pango kama tulivyosema kwenye Kamati yetu kwa ajili ya kukodisha Ofisi ambazo *TBC* wanafanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako, jengo ambalo lina sura ya gofu lililopo Mikocheni katika eneo la *TBC* pamoja na *NSSF,* sina uhakika kama wameshalipwa na deni lao lililotokana na ujenzi wa *UDOM,* lakini pia wapo tayari kuendelea kudhamini ujenzi wa jengo la *TBC* jambo ambalo lingeokoa pesa nyingi za Serikali ambazo zinalipwa kila mwezi, ama kila mwaka. Lakini kinachotakiwa na *NSSF* ni *guarantee* ya Serikali. Serikali imekuwa na kigugumizi katika kuchukua dhamana kwa *NSSF* kwamba wamalizie lile jengo bila kujali kwamba kufanya hivyo kutaokoa fedha nyingi ambazo zinalipwa kama kodi ya pango kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali sasa ione kwamba kuna wajibu wa kuchukua dhamana na kuwapa nafasi hiyo *NSSF* ili wamalizie lile jengo.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la michezo. Michezo ni ajira na tumekuwa tukishuhudia nchi nyingi na Mataifa mengi, wachezaji wenye vipaji na wanaoshiriki kwenye mashindano mbalimbali wakiwa wanapata kazi za maana na wana vipato vizuri kiasi kwamba vinaonewa choyo na watu wengine ambao hawajafikia viwango hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mataifa mbalimbali ambayo yapo na mfumo wa kimuungano kama ilivyo Tanzania yetu, timu zote ambazo zipo kwenye Mataifa hayo katika ile dhana ya kukuza viwango, kutoa ajira kwa vijana wao na kuinua vipaji wanatoa fursa kwa timu zote zile kuingia au kuwa wanachama wa *FIFA* ili kuongeza vipaji vya watu wao na kuinua vipato.

Mheshimiwa Spika, naomba niiulize Serikali, kuna kigugumizi gani kwa Tanzania kuiruhusu Zanzibar kuwa mwanachama wa *FIFA* kwa muda wote huo hasa tukijua kwamba ni fahari kwetu kuona kwamba kwenye mashindano yale tunakuwa na wawakilishi wawili katika Taifa moja?

Naomba sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, atuambie jambo hili litakwisha lini? Kero hii, usumbufu huu na mchakato huu usiokwisha, naomba sasa usiwe mchakato, lakini uwe mchakamchaka, maana mchakato unachelewesha kufika kwenye malengo. Uwe ni mchakamchaka ili twende kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la utamaduni, lakini kwenye jambo hili la utamaduni naomba nizungumzie utamaduni wa mavazi. Inasikitisha na hivi sasa nchi ya Tanzania tunaonekana kana kwamba tumepoteza mwelekeo katika ile dhana ya utamaduni wa kuheshimu na kuheshimiana hasa katika suala la mavazi.

Inatia aibu, leo imekuwa ni jambo la kawaida mama anavaa nguo za kubana ambazo hazimwekei heshima yake na anathubutu kwenda kwenye familia bila kujali kwamba kuna watoto wake wakubwa au kuna wazee wake, lakini hata kwenda kwenye jamii mbalimbali anathubutu kwenda na mavazi yake hayo na huku akijivuna kwamba amevaa mavazi yanayoridhisha. Ni aibu!

Mheshimiwa Spika, jambo hili naomba niseme kwamba, nchi za wenzetu kuna mavazi, ukivaa yanaashiria wewe uliyevaa mavazi haya ni mtu wa aina gani na inatia shaka kwamba hata ile hoja ya akina David Cameroon ya kwamba, Tanzania iingie katika mfumo wa ndoa za watu wa jinsia moja, pengine hawa walikuja kutembelea Tanzania na wakakuta kuna wanaume ambao wanatamani kuwa wanawake, lakini pia kuna wanawake ambao wanatamani kuwa wanaume. Ni aibu na ajabu, mtoto wa kiume unategemewa kwenu, unarudi nyumbani umevaa hereni…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ameir, ahsante.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Newala na mimi nichangie Wizara hii. Kabla sijaendelea nichukue nafasi kuipongeza klabu yangu ya Yanga kwa kufanya uchaguzi mzuri majuzi, jana wamefanikiwa kuingia *semi final*, mwaka jana walichukua kombe la *CECAFA* na maagizo ya wazee wao sisi kwa wachezaji ni kwamba, mwaka huu kombe walibakishe kama mwaka jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitangulie kusema, nimesimama hapa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wasemaji hapa nimewasikiliza kana kwamba miaka saba hii ya awamu ya nne hakuna tulichofanya katika Wizara hii. Nataka kukumbusha wenzangu mambo machache sana. Moja, nataka niipongeze kabisa *TFF*. Taasisi ile ilikuwa na migogoro huko nyuma, mara rufani za kesi na nini, sasa hivi wale wamejijengea utaratibu mzuri, Waziri hasikilizi rufaa za kesi, mambo yao wanamaliza wenyewe na viongozi wao wamechaguliwa kwenda katika Kamati mbalimbali za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimtoe mashaka mwenzangu wa Zanzibar aliyeongea sasa hivi, msimamo wa *TFF* na Tanzania Bara ni kutaka Zanzibar ipate uanachama wa *FIFA*. Ndiyo maana mara ya mwisho Mheshimiwa Shamuhuna, Waziri wa Michezo wa Zanzibar alipokwenda *FIFA* kuomba uanachama aliongozana na Joel Bendera, Naibu Waziri, Leodga Tenga *President* wa *TFF* kwenda kuomba uanachama wa Zanzibar. Kwa hiyo, naomba ieleweke kwamba kama tunanyimwa wanaotunyima ni *FIFA*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania Bara itafurahi sana Zanzibar kuwa mwanachama kwa sababu tutafaidika, ile misaada tutapata mara mbili kuliko tunavyopata sasa. Kwa hiyo, nataka kusema taasisi ya *TFF* imejijengea uhalali mzuri, sasa wafadhili wanajitokeza baada ya kuona chombo kile kinakwenda kwa *transparency*, kiutaalam, wana *president* mcheza mpira na msomi.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kusema tunakwenda vizuri na nitoe mifano ni kwa nini tunakwenda vizuri. Mara ya mwisho Tanzania wameshiriki kombe la *CHAN* mwaka 1980 kocha wa timu ya Taifa, Joel Bendera na kapteni Leodga Tenga. Tangu mwaka 1980 hatukurudi *CHAN* mpaka mwaka 2009 katika Serikali hii ya Awamu ya Nne, kuonesha kwamba tunafanya jitihada.

Mheshimiwa Spika, Twiga *Stars* wameingia *CHAN* wamekwenda Msumbiji mwaka 2011. *Copa Cocacola* vijana wetu hapa wamekwenda Brazil na kwa dunia nzima wameshika nafasi ya pili. Tuliwaleta hapa Bungeni wakaja kuonesha na kikombe. Sasa watu wanaposema kwamba hakuna kinachofanyika katika Wizara hii, nafikiri watu hao pengine wana macho lakini wana tatizo la kuona.

Mheshimiwa Spika, hata ukiwachukulia wale wapenzi wa mpira miaka ya nyuma sisi kucheza na Senegal ingekuwa goli 16 au sijui ngapi, lakini *Senegal* wamekuja hapa nchini, wamekwenda Mwanza pale tumetoka nao droo, Cameroon tumetoana nao 1-1, Ivory Coast walitufunga goli moja kwa tabu.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme lingine, ilipita hapa timu ya Brazil inakwenda *South Africa*. Nchi zote za Afrika walikopita hawakufungwa goli hata moja. Sisi pamoja na kwamba walitufunga matano (5) lakini kijana wetu wa Tanzania alimfunga goli moja goli kipa wa Brazil. Magazeti ya Brazil wakasema nchi zote walizopita golikipa wao hakuwahi kufungwa goli isipokuwa Tanzania. Haya mambo hamuyaoni? (*Makofi/Kicheko*)

Sasa mambo ya *CECAFA* ndiyo sitaki kusema maana tunashiriki kila mwaka. Mmeona sasa Tanzania inakuwa kama ni nyumbani kwao, kila siku wako hapa. Nchi zingine hawawezi kumudu haya mambo, sisi mambo yetu yako vizuri na ndiyo maana na vijana wetu sasa wamejijengea utaratibu wa kubakisha kombe kama wanavyofanya Yanga kila mwaka. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nimesoma kwenye magazeti juzi, yameandika hivi katika nchi za Afrika, Ligi Kuu ya Tanzania ni 16th, Kwa hiyo, tunapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine twende kwenye upande wa mpira wa wanawake. Wao pia wamefanikiwa wamekwenda *CHAN*, lakini juzi wamefungwa hilo goli moja na nilikuwepo, kwa sababu ya kukosa *stamina* tu. Ndiyo maana huko mbele ya safari lazima sasa tukazanie majeshi, wanajeshi wanapimwa kwa urefu, wanakula vizuri, wanafanya mazoezi asubuhi na jioni, ndiyo maana mnaona nchi nyingi jeshi ndiyo linakuwa na timu. Vijana wale wa Twiga wamejitahidi sana, lakini pengine shauri ya lishe, mazingira na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nipongeze pia mchezo wa *netball*. Kwa upande wa *netball* Tanzania ni ya pili kwa ubora katika Afrika. Tanzania ni ya 20 kwa ubora katika dunia nzima kwenye mchezo wa *netball*. Mmeona juzi hapa tumekwenda *all Africa games* kama siyo wale akinamama Tanzania tungerudi patupu bila medali. Wamerudi na medali, hamuoni hayo?

Mheshimiwa Spika, juzi tumeandaa mashindano hapa Dar es Salaam, timu yetu ikawa ya pili, ingawa msemaji mmoja alisema ooh, mke wa Waziri Mkuu amechangisha. Eeh, ukishakuwa kiongozi wewe na mkeo, mkeo akiwa na uchungu anaweza kuchangisha. Sasa walitaka milioni 100, mke wa Waziri Mkuu akachangisha zaidi ya milioni 100, Mungu atupe nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini mafanikio mengine ni kwamba, tumerejesha mashindano kwenye shule za sekondari, mmeona matokeo yake sasa kupitia *Copa Cocacola*, wanacheza mpaka michezo ya kulipwa. Kwa nini? Kutokana na Rais kuagiza kwamba sasa turudishe mashindano katika shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kuzungumzia kuhusu maendeleo ya shughuli za utamaduni na michezo huko vijijini katika Majimbo yetu. Nampongeza Waziri Mkuu mwaka 2008 alitoa maagizo kwamba, Halmashauri lazima zitenge fedha kwa shughuli za utamaduni na michezo. Halmashauri nyingi zimeanza kufanya hivyo, lakini pengine mafungu yanayotengwa hayajatosheleza bado kwa sababu Wilaya nyingi ukienda leo ukikuta kuna mashindano, ni kombe limetolewa na Mbunge. Kwa hiyo, nataka niwapongeze Wabunge wenzangu, katika Majimbo mengi mmetoa vikombe na jezi ili kuendesha mashindano haya. Naziomba sana Halmashauri nazo ziendeshe mashindano kama haya ili tuweze kuibua vipaji kule vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyofuatilia kwa umakini sana utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika masuala ya utamaduni. Kila mchezo Rais ameunga mkono, amewasaidia vijana wetu. Nakumbuka huko nyuma timu ya *netball* ilitakiwa kwenda kucheza *West Africa*, walikuwa hawana usafiri, akatoa ndege ya Rais ikawapeleka. Vijana wakaenda kule, wakacheza vizuri kwa kibri, wamepelekwa kwa ndege ya Rais, watu wa wapi hawa? Watu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimesema nimesimama kuunga mkono hoja, kwa kweli naamini kwamba, tunaendelea kufanya vizuri. Kama nilivyogusia miaka ya nyuma tulikuwa na mashindano makubwa sana ya majeshi, majeshi yote yalikuwa yanashindana yenyewe kwa yenyewe halafu kilele kilikuwa mashindano ya majeshi yote na pale ndiyo tulikuwa tunaibua vipaji. Zamani Jenerali Sarakikya alipokuwa Mkuu wa Majeshi, kulikuwa na Kombania ya Majeshi akasema kwamba, mtu wa kwanza kuleta ubingwa katika nchi hii atatokana na jeshi. Ndivyo ilivyotokea Filbert Bayi, alitokana na kombania ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kusisitiza kuwa kuna umuhimu wa Wizara kushirikiana na Wizara zinazohusika kurejesha mashindano yale kwa kasi kama ilivyokuwa zamani ili tuweze kuibua vipaji vipya kwa sababu naamini jeshini kuna watu wamepimwa wako *physically fit*, wanakula vizuri, wanafanya mazoezi kila siku na hivyo naamini wataweza kutusaidia kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie suala la lugha ya Kiswahili. Nawashukuru wale wenzangu mliozungumzia hili. Naomba sana Wizara pengine mbele ya safari itabidi tubadili sheria ili kulipa meno Baraza la Kiswahili la Taifa ili wakikemea mahali wasikilizwe, maana sasa hivi wanakemea watumiaji wabaya wa lugha lakini hawasikilizwi. Kuna kampuni moja ya simu inatoa matangazo kila siku mnasikia, wakisema masaa matano.

Mheshimiwa Spika, wameambiwa katika Kiswahili yale maneno tunayoyaazima hayana wingi. Chama cha Skauti wa kike, hakuna maskauti wa kike, baiskeli tumeiazima, baiskeli moja, zikiwa nyingi baiskeli mia mbili (200). Humu ndani wakati mwingine huwa tunateleza teleza, lisaa limoja, hakuna lugha hiyo ya lisaa. Masaa matano hakuna *plural* ya saa, unasema muda wa saa moja, ndege yetu itaruka kutoka hapa kwenda Nairobi kwa muda wa saa mbili. Kwa kuwa vijana wetu wanatusikiliza, jamani kuanzia leo tuachane na kusema, masaa, masaa, masaa. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa saa imetosha, ni kengele ya pili.

**MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, aah, sikusikia kengele! Naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kupongeza uongozi wa Wizara hii hususani Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Hata hivyo, naomba kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijana wanaunda asilimia kubwa sana ya watu hapa Tanzania. Hata hivyo, ingawa ndio nguvu kazi ya Taifa hili, vijana wameendelea kuteseka kutokana na ukosefu wa ajira na hivyo kupelekea kujiingiza katika vitendo viovu. Vijana wameendelea kuteseka kutokana na maambukizi ya maradhi hususani UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwe mratibu wa kuhakikisha bajeti za Wizara nyingine zinaoanisha mipango yao na *'issues'* za vijana kama vile ajira, kujikinga na maambukizo ya virusi vya UKIMWI, utamaduni na kadhalika. Aidha, Wizara iwe inatoa *reports* za kila mwaka kuhusu masuala ya vijana kupitia vipindi vya Television, Radio na Magazeti. Kazi hii imekuwa ikifanywa sana na *NGO's* na hivyo Wizara inaonekana kama vile haina '*active role'* katika ushajiishaji wa vijana.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea sana kujitangaza kupitia michezo mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa. Hata hivyo, ushiriki wa upande mmoja wa Muungano kwenye michezo inaleta sana manung'uniko upande mwingine wa Muungano (Zanzibar). Kwa kipindi kirefu miaka iliyopita timu za Taifa zimeendelea kuwa *dominated* na wachezaji kutoka Tanzania Bara pekee. Waziri alielezee hili kwa kina sana ili ieleweke taratibu za uteuzi wa wachezaji wa Timu ya Taifa. Timu zetu zinaposhiriki kwenye michezo hazileti sura za Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi zinazochukuliwa na Wizara kuhakiki filamu nyingi Tanzania. Hata hivyo filamu nyingi bado zimeendelea kuwa chafu sana kulinganana na tamaduni za Tanzania. Wizara iangalie jinsi hizo *categories* za filamu za Tanzania tokea mavazi, lugha na matendo hayaendani na maadili ya kitanzania. Filamu hizo zipo sokoni na zinaendelea kuuzwa. Aidha, kuwe na usimamizi pamoja na kutoa *categories* za filamu za hapa kwetu kama zile za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina kazi kubwa ya kuendeleza vijana. Serikali inaweza kutengeneza ajira kwa vijana kupitia michezo kama wanavyofanya nchi za Brazil. Serikali ijenge Chuo cha *Physical Education* na *emphasis* ya michezo kama *football, basketball, tennis* na kadhalika. Serikali ijifunze kutoka kwa wenzetu nchi za nje, Ulaya, America, Afrika Magharibi wao wanafanyaje vijana wao wanapata ajira kwenye timu za nje ya nchi na wanalipwa vizuri?

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe na *serious commitment* na hili mfano *Olympics* zinazofanyika London 2012, Kenya wamepeleka wanamichezo 143, Uganda 16, Afganistani sita (6) na Tanzania sita (6). Tanzania ambayo haikuwa vitani inapeleka vijana 6 *in comparison to a country* ambayo imekuwa na vita muda wote! Tunaitangaza vipi Tanzania katika dunia ya nje?

Mheshimiwa Spika, Serikali iwape vijana elimu ya ujasiriamali, elimu ya mkopo, elimu ya *marketing* baadaye wafundishwe kuandika *business proposal* na waombe mikopo kutoka asasi za fedha ili wajitegemee.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianzishe viwanda vidogovidogo katika maeneo yote nchini kwa mtindo wa *PPP*. Halmashauri zinawezaingia ubia na *private sector* ili kupata ajira ya vijana (Baraza la Mawaziri li-*discuss* hili). Mfano eneo linalolimwa mahindi kianzishwe kiwanda cha kukoboa mahindi, kusaga na ku-*pack*. Eneo lenye mpunga hivyohivyo. Mahindi yatawekewa *value addition* hata bei itakuwa nzuri. Soko la Afrika Mashariki ni kubwa badala ya kununua mahindi wanunue unga, mchele uliokuwa *graded and packed* na kadhalika. *SIDO* inaweza kutengeneza mashine za viwanda hivi vidogovidogo. Wachumi wa nchini hapa wafanye utafiti wajue ni mazao gani yawe *processed* eneo gani, watafiti kuhusu masoko, naishauri Serikali ianzishe viwanda hivi kwa ubia na *private sector.* Serikali ikifanya hili, Waziri wa Habari na Vijana atapata amani.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa habari ni mkubwa na *it seems as if there is no rule of law*. Wanahabari wanaandika kumkashifu kiongozi mkubwa wa Taifa na hakuna hatua inayochukuliwa. Magazeti-Wahariri wanaacha *profession* zao wanaandika kuhusu *personal issues* za wanasiasa. Serikali iingilie kati kujua *profession* za Wahariri wa magazeti yote ili kutoruhusu habari za kuuza tu magazeti.

Mheshimiwa Spika, ziko Redio zinatangaza habari kilugha. Hii ni hatari! mfano Redio Kwizera Kigoma wakati mwingine wanaweza kutangaza mambo yatakayowezaanzisha uvunjifu wa amani. Serikali ihakikishe Redio zote zinatangaza Kiswahili tu au na Kingereza.

Mheshimiwa Spika, sanaa iko ya aina nyingi, nyimbo za injili zimeleta na kugundua vipaji vingi. Vipindi kama *Bongo Star Search* navyo vinaibua vipaji. Michezo ya kuigiza aina ya filamu, nayo inaibua vipaji. Makundi haya yapewe *support,* wajiendeleze ili watoe pato kubwa kwa Serikali lakini pia ajira kwa vijana, Serikali iwasaidie pia kutangaza nje ya nchi. Ni vema pia waimbe kwa lugha zaidi ya moja ili waweze kuuza kazi zao nje ya Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba kumpongeza Waziri Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Amos Makalla, kwa kuteuliwa na Rais kuiongoza Wizara hii. Ni imani yangu, kazi hii wataifanya kwa ujasiri na kuweka mwongozo ambao utatutoa tulipo na kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia zaidi kuhusu habari. Upande huu hasa ni muhimu kwa wananchi hapa kwetu na hata nje ya nchi lakini bado kuna wanahabari wengi hupotosha habari ama kwa maslahi ya chama fulani au mtu fulani na kuipotosha kabisa habari, huu ni mchezo mchafu na pia ni kuwaaminisha Watanzania ndivyo sivyo. Kama Serikali ni wakati muafaka kuleta Sheria ya Habari na ndani yake kuwe na kipengele cha adhabu ya wapotoshaji habari, hii itasaidia nidhamu kwa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa Wizara kuwa na wakalimani wa lugha ya alama kwani watu wenye ulemavu wa kutosikia nao wanahitaji kujua habari za nchi hii. Ni wakati muafaka sasa kwa kuwa kila Mtanzania anayo haki ya kupata habari.

Mheshimiwa Spika, pia ni vema Wizara ya Habari na Wizara ya Elimu zikashirikiana kwa pamoja na kuendelea kukagua mara kwa mara shule za walemavu hawa wasioona na kiasi kikubwa kwa wasiosikia kwani hali huko sio nzuri sana jinsi ambavyo wanavyopata elimu zao. Ni muhimu sana hata *Television* kuwa na wakalimani wa lugha ya ishara katika vipindi vyake (yaani wataalam).

Mheshimiwa Spika, sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kutumia juhudi zote za ziada kutoa asilimia fulani katika vifaa vya michezo viingiavyo nchini na kuipa *BMT* ili nayo iweze kujiendesha. Kwani vifaa vya michezo ushuru wake ni mkubwa lakini *BMT* hawanufaiki na ushuru huo, sasa ni bora nao kama Baraza la Michezo linufaike na ushuru huo japo kwa 3%. Kupitia kwako nashauri atoe mapendekezo kwa Baraza la Mawaziri ili liridhie hilo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa utamaduni wa Mtanzania unaendelea kupotea kwa vijana wetu kuvaa nguo zinazokinzana kabisa na utamaduni wetu. Wengi wanaiga mavazi ya watu wa Magharibi na vijana wa kiume kuvaa suruali maarufu kama K-K. Haipendezi! Sijui Wizara ina mipango gani ya kuwaelimisha vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, hata vijana wa kike hupandisha matiti na kuyaacha nje na wengine kuwa hata kwenye matangazo ya biashara hali wakiwa uchi kifuani. Mfano tangazo la magodoro ya Dodoma, dada yule yuko uchi kabisa, matiti yako nje tena hapendezi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa kuwahamasisha wenye biashara hakuna haja ya kuleta matangazo ya biashara kutumia wasichana waliovaa uchi. Matangazo ambayo hutolewa na kama baba na mtoto mnaangalia *Television* ni lazima mmoja aondoke wakati wa matangazo ya biashara hizo.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri anapokuja kufanya majumuisho, naomba atoe kauli kwa wafanyabiashara kuacha kutumia watu kutangaza matangazo ya biashara wakiwa wamevaa nguo za kuacha maungo yao uchi kama tangazo la magodoro ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchangia upande wa mechi, ni bora makocha kutoka nje ya nchi wakahamasishwa kuwashirikisha makocha wazalendo ili baada ya muda tutumie makocha kutoka ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii pamoja na Watendaji wote waliofanikisha kuleta hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu ili nasi Waheshimiwa Wabunge tupate kutoa maoni yetu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya habari na haki ya kupata habari, napenda kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni kwa jinsi gani Wizara inajipanga kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wa kusikia nao wanapata habari kama watu wengine? Mfano, kuwepo na wataalamu wa lugha za alama wakati wa kipindi cha Bunge kinaporushwa ili walemavu wasiosikia nao waweze kufuatilia mijadala ya Waheshmiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge inavyoendelea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, vijana na michezo, sote tunatambua kuwa vijana wengi kwa sasa wapo kwenye wimbi kubwa la ukosefu wa ajira. Je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kuwa vijana wetu wanawakilisha vizuri katika michezo mbalimbali ili wasiendelee kuingia kwenye matumizi ya madawa ya kulevya kama ilivyo sasa?

Mheshimiwa Spika, natambua Serikali imerudisha michezo mashuleni, je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kuwa michezo katika shule zetu inatekelezeka kivitendo na sio

kinadharia? Kwa mfano kuhakikisha kuwa vifaa vya michezo vinapatikana mashuleni kama vile mipira ya kutosha, jezi, nyavu na vifaaa vinginevyo?

Mheshimiwa Spika, utamaduni, kumekuwepo na changamoto kubwa sana katika upande au sekta hii ya utamaduni hususani katika kipindi hiki cha utandawazi. Mfano mavazi yasiyo na heshima kwa vijana wetu kama vile wasichana kuvaa nguo za kubana sana kama *skintight* wakati wa mchana na blauzi fupi ambazo zinaacha maumbile yao wazi. Je, Serikali imejipanga vipi kutoa elimu kwa vijana kuhusu umuhimu wa kuvaa vizuri na hasa kuvaa mavazi ambayo yanaendana na tamaduni zetu?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha mashirikisho yameundwa lakini bado tatizo la hati miliki kwa wasanii lipo. Najua Serikali imeweza kurasimisha kazi za wasanii kwa kuweka bakodi na stempu. Naiomba Serikali kuhakikisha *program* hii inafika mwisho.

Mheshimiwa Spika, tatizo la usambazaji wa kazi za wasanii nalo pia bado ni tatizo kweli. Video moja, msanii bado analipwa shilingi mia tatu na ya *CD* ya muziki mia mbili hamsini hadi mia mbili. Tatizo hili linawarudisha nyuma wasanii.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwasaidie wasanii hawa ambao wengi wao ni vijana wanaotafuta maisha ili kujikwamua na utegemezi. Serikali iwawekee mpango maalum, Serikali ichukue fursa ya kusambaza kazi za wasanii kwa kuweka vituo kila kona ya nchi ili nao wapate kufaidika na kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wasanii, nawaomba kwa kupitia mashirika yao waunde *association* moja ambayo itawapa nguvu kubwa katika kutetea haki za kazi zao na masoko kwa ujumla kwani umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri magazeti yapo mangapi? Napenda kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hii mara kwa mara huwasisitiza waandishi wa habari kuandika habari za ukweli na zinazoelimisha jamii. Nami naungana nao kuwapongeza waandishi hawa ambao wanaandika habari za ukweli na kuelimisha jamii lakini bado kuna waandishi wachache ambao wanatoa habari si za ukweli na zenye uchochezi kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Museveni alisema kwa sababu ya makanjanja katika vyombo vya habari, aliamua kuanzisha Sheria kwamba mwandishi wa habari lazima awe na *degree* ili kuleta weledi katika taaluma hii ambayo ni muhimu sana katika jamii. Naomba ufafanuzi kwa Waziri, hatua gani inachukuliwa kwa baadhi ya waandishi ambao wanaandika habari ambazo si za ukweli na zenye kupotosha jamii?

Mheshimiwa Spika, *Blogs,* naomba kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri anieleze maadili gani yanatawala habari zinazotokea katika ma-*blog* ili zisihatarishe maslahi na amani ya nchi na heshima binafsi za wananchi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi nyingi alizozitoa Mheshimiwa Waziri dhidi ya *TBC* lakini bado kuna changamoto ya kukatikakatika kwa habari, mara nyingi habari zinakwama, hizo mashine zina nini? Kuna matatizo gani?

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira bado ni kubwa, naiomba Serikali iliangalie tatizo hili kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Vijana nao utengewe fedha za kutosha. Vijana ni takribani asilimia 68 ya Watanzania wote wanaungalia mfuko huu.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuchangia kwa maandishi. Pia sina budi kumshukuru Mheshimiwa

Waziri kwa hotuba yake. Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Wizara hii juu ya kuboresha shughuli zake, napenda kuishauri Serikali kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, udhibiti na usimamizi wa *DVDs, CDs* na kanda nyinginezo. Ni jambo lisilopingika kwamba utoaji au uuzaji wa *DVDs, CDs* kwa vijana wetu uko huru sana. Nasema hivi kwa sababu watoto wadogo wananunua *DVDs* na *CDs* na kwenda kuangalia zikiwa hazina maadili na hivyo kupotosha vijana. Napendekeza Serikali iweke utaratibu mzuri wa upatikanaji wa *CDs* na *DVDs* kwa vijana wadogo ili kudumisha mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Spika, wasanii (mavazi), sote tunaona kuwa baadhi ya wasanii wetu wanaonyesha sanaa zao wakiwa na mavazi yao hayalingani na utamaduni wa Mtanzania. Wasanii wetu hasa wanawake wanaonyesha sanaa zao wakiwa uchi, hii ni kinyume na utamaduni wa Mtanzania. Naomba Wizara hii kukemea na kuzuia mavazi yanayokwenda kinyume na utamaduni wa Mtanzania. Pia vijana wanaona ili wapate umaarufu lazima waige utamaduni wa nje. Ni vyema tuangalie utamaduni wa nje usiathiri utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, waandishi wa habari ni muhimu sana kwa Taifa lolote lakini hapa Tanzania inaonekana waandishi wanatoa habari bila ya kufanya utafiti na hivyo kuandika habari zisizo na ukweli na hivyo kuhatarisha amani nchini. Ili taaluma ya habari iwe bora Tanzania, Wizara hii lazima ihakikishe wanahabari wote wana uzalendo na Taifa lao katika uandishi wa habari, hii itasaidia kudumisha amani nchini.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato, Tanzania kupitia Wizara hii ina nafasi kubwa ya kuchangia mapato ya Serikali, hii inatokana na udhibiti na usimamizi wa sanaa na kanda za nyimbo, miziki na maonyesho mbalimbali. Ni vyema Wizara ijipange vizuri ili kutoa ufanisi mzuri juu ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kunyanyua viwango vya michezo ya aina zote, Tanzania ina rasilimali kubwa ya vijana ambao wanajishughulisha na mchezo. Ni vyema kabisa Serikali ikajipanga upya kunyanyua viwango vya michezo ili kuliletea heshima Taifa letu katika medali ya michezo. Serikali kama itafanya hivi basi pato la Tanzania litaongezeka na kujengea heshima Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, naomba kuwasilisha.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam kwa kuandaa hotuba nzuri. Hotuba imebainisha yale yaliyotekelezwa kwa kipindi kilichopita na mipango itakayotekelezwa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara ikamilishe mapitio ya Muswada wa Habari, Tanzania na kuurejesha Bungeni ili kupitishwa na uanze kutumika kusimamia na kudhibiti vyombo vya habari Tanzania.

Mheshimiwa Spika, M*edia Council of Tanzania* iandae *code of conduct* itakayosainiwa na vyombo vyote vya habari na kutumia kuboresha weledi, maadili na *credibility* katika kutafuta ku-*report* na kutangaza taarifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara ikusanye tunu bora kutoka kwenye kila utamaduni. Tunu hizi ziwekwe pamoja na kuchapishwa katika kitabu/vitabu na kutumika katika shule zetu za msingi, sekondari na vyuo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifungue vituo Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Morogoro, Tanga, Arusha na Iringa, vituo hivi visaidie kuwaandaa vijana kuingia kwenye soko la ajira. Vituo hivi viwaelekeze vijana juu ya mwenendo wa masoko ya ajira, uandaaji wa *CVs,* kushiriki katika *interviews* na kuji-*market.* Katika shughuli hii, Wizara ishirikiane na Wizara ya Kazi na Ajira.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, tasnia ya filamu, wasanii wengi takribani wote katika filamu zao ama kazi zao huiga zaidi tamaduni na hata namna wanavyoishi katika mila na desturi za kigeni. Kama msanii, ni vizuri kuelimisha jamii kwa kuwa na taswira au kuvaa sura tofautitofauti katika kazi yake kwa lengo la kuelimisha, kuburudisha na kuliwaza pamoja na kufundisha kama kazi ya sanaa inavyotaka lakini kwa sasa, wasanii wengi wanajikita katika kufuata zaidi tamaduni za kigeni na kuacha kabisa kupeleka ujumbe kwa Watanzania kuhusiana na tamaduni zao hasa kwa kizazi kipya, watoto wengi wa siku hizi hawajui tamaduni, mila wala desturi zao na pia nao kuiga tamaduni za kigeni ambazo wengi wao haona na kuiga wasanii.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, suala hili linatufanya Watanzania kuwa watumwa kwa kukumbatia zaidi tamaduni za kigeni na kuacha zetu. Pamoja na hayo, ndio yanayochangia Watanzania wengi kutojua tamaduni zao na wasanii wetu kushindwa kufikisha ujumbe ipasavyo katika jamii husika. Sababu ya yote hayo ni kutokana na Serikali kutokuwa na usimamizi mzuri wa kazi za sanaa na badala yake usimamizi huu kuwa mikononi mwa watu binafsi na kutokuwa chini ya usimamizi wa vyombo vilivyopo kisheria mfano BASATA, TASUBA.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu na ushauri wangu katika suala hili ni kwamba kazi zote za sanaa ziwe chini ya usimamizi wa vyombo vilivyopo kisheria. Vilevile kupelekea hata kuzalisha filamu zenye staha na heshima ambazo hazitaleta picha mbaya akiwa mzazi na watoto wanaangalia kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, *copyright* na faini yake, wasanii wengi wananyanyaswa katika suala zima la uuzaji na kutoa nakala nyingi kinyume na sheria ambapo hupelekea msanii husika kutokufaidika na kazi yake na hata kukata tamaa mapema. Pamoja na sheria zilizopo na faini zilizowekwa kutokana na kukopi kazi ya msanii kinyume na sheria bado tunaona haitendi haki kwani katika suala la faini kiwango kikubwa ni milioni kumi yaani *maximum* ya faini ni milioni kumi wakati hakuna kipengele kinachoonesha kiwango cha chini cha faini anayotakiwa kutoa mtu na badala yake kuonesha kiwango cha juu pekee, hivyo basi kupelekea na kuwapa mwanya zaidi wahalifu kuendelea na kutoa nakala za wasanii kinyume cha sheria na kudumaza na hata kunyonya wasanii kutofaidika na kazi zao.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo, ni vyema katika faini kuhusiana na *copyright* pia kuwe na maelezo au kipengele maalum kinachoelezea na kutaja kiwango maalum cha chini (*minimum*) ili kuzuia wahalifu wanaopata faida kubwa na kutozwa faini ndogo. Pia faini ilingane na faida au kiwango ambacho wahalifu wamekipata kinyume na sheria. Naamini kufanya hivyo kutapelekea wasanii wengi kufaidika na kazi zao na hata kupunguza uhalifu wa kukopi kazi za wasanii kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya *TBC Radio* kwani kuna malalamiko mengi ambayo hupelekea Watanzania waliopo vijijini na wasio na *television* kushindwa kufuatilia kipindi cha Bunge na hata kutojua ni nini kinaendelea kwa Wabunge wao wakiwa Bungeni na mambo mbalimbali pia kutotambua. Maoni na ushauri wangu katika suala hili ni kuangalia utaratibu ambao utawezesha Watanzania wasio na *television* nao kusikiliza kipindi cha mjadala wa Wabunge wakiwa Bungeni kama ambavyo Television ya TBC inavyofanya.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara na Waziri mliangalie suala hili kwa umuhimu wake na kuwawezesha wananchi wengi wenye redio nao wafuatilie mjadala wa Wabunge wakiwa Bungeni.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanywa. Naomba kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha mtandao wa michezo vijijini ili kuweza kuibua vipaji vya vijana;

(ii) Kusimamia vyema kazi za sanaa ili kulinda haki za wasanii;

(iii) Kusimamia vyema vyombo vya habari ili kulinda heshima na maadili ya nchi yetu;

(iv) Kuimarisha *TBC* ili iweze kutoa huduma inayokidhi haja ya Watanzania; na

(v) Kwa muda mrefu vijana wamekosa fursa ya haraka ya upatikanaji wa mikopo. Naiomba Serikali ianzishe Benki Maalum ya Vijana ili vijana waweze kupata mikopo kwa ajili ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuimarisha mtandao wa kutoa habari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

(i) Kuisimamia vyema timu yetu ya wanawake yaani *Twiga Star* kwani imekuwa ikifanya vyema katika mazingira magumu. Naiomba Serikali iipatie kipaumbele timu hii kama inavyopewa timu ya *Taifa Star*;

(ii) Naomba Serikali isimamie vyema suala zima la udhibiti wa madawa ya kulevya kwani madawa ya kulevya yameendelea kuangamiza vijana wengi hapa nchini;

(iii) Naomba Serikali ilete Muswada wa Sheria ya Habari; na

(iv) Naiomba Serikali ianzishe Benki ya Vijana ili vijana waweze kupata fursa ya upatikanaji wa mikopo bila kikwazo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PUDENCIANA KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni juu ya vyombo vya habari nchini. Mara nyingi vimekuwa vikitoa habari ambazo si sahihi hasa zinazohusiana na wananchi. Jambo hili si zuri na mara nyingi limekuwa likipotosha jamii. Naishauri Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari iharakishwe kuundwa ili vyombo vya habari viweze kufanya kazi kwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara bado haijajielekeza vizuri kuhusiana na masuala yanayowahusu vijana katika kuwawezesha kujiajiri na kujitegemea ili waweze kujikwamua kutoka katika umasikini.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wizara bado haijaweza kuvisimamia vizuri vyombo vya habari kwa upande wa matangazo mbalimbali ambayo hayana maudhui kwa jamii. Kwa mfano matangazo mengi yanayotolewa na makampuni ya simu na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali na Wizara iangalie namna ya kuwekeza katika aina moja au mbili ya michezo kwa mfano kama ilivyo kwa Marekani (*basketball).*

Mheshimiwa Spika, tano, uwekezaji katika *TBC*. Uwekezaji uliopo kati ya *TBC* na *Star Media* haueleweki vizuri mara *TBC, Star Media* au *Star Times.* Wananchi wamekuwa wakihoji na kutaka kujua hali ikoje katika uwekezaji huo na hisa zake zikoje?

Mheshimiwa Spika, sita, je, Wizara imetoa maelekezo na elimu kuhusiana na mfumo wa digitali unaotaka kuanza kutumika hasa kwa wananchi wengi waliopo vijijini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la ukosefu wa ajira kwa vijana si la Tanzania pekee bali nchi yetu inatakiwa kulipa kipaumbele kwani muda wa ujana ndio muda mrefu kwa binadamu yeyote kujitengenezea maisha yake na kujiwekea misingi mizuri ambayo itamsaidia pindi atakapozeeka na kukosa nguvu ya kufanya kazi. Hivyo basi, naomba Serikali iliangalie hili kwa ukaribu zaidi na ikizingatiwa tatizo hili linakadiriwa kuwa 11.8% kwa vijana wenye umri kati ya miaka 25-35 hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili hupelekea baadhi yao kujiunga na makundi maovu mfano uvutaji bangi, utumiaji wa madawa ya kulevya, ujambazi pamoja na vijana na wasichana kujiuza miili na vijana wanaobakia wanajishughulisha na shughuli za ujasiriamali mfano uchimbaji madini, kilimo, uvuvi, ufundi, biashara, ufugaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo hili napendekeza kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendelee kutoa semina za kutosha na elimu kwa vijana kuhusu kujikinga na maambukizi ya *HIV* pamoja na athari za mimba za utotoni.

(ii) Wizara kuandaa *program* ya kuwaelimisha vijana jinsi ambavyo wataweza kujiajiri wenyewe na kuachana na makundi yasiyofaa pamoja na kushinda vijiweni.

(iii) Serikali iache kutumia kigezo cha *experience* ya kazi ya muda mrefu ambacho mara nyingi kimekuwa kikiwanyima vijana fursa za kupata ajira mara moja mara tu watokapo masomoni.

(iv) Kuanzisha/kujenga vyuo vya ufundi katika Wilaya zote nchini ili kuwasaidia vijana kupata elimu ya ufundi ambayo itawasaidia katika kujiajiri.

(v) Mwisho Wizara na Serikali ioneshe uharaka na dhamira na umuhimu wa kushugulikia tatizo hili la ukosefu wa ajira kwa vijana na pia kutoa habari zinazohusu program mbalimbali kwa wahusika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, michezo kwa walemavu, kama tulivyosikia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuwa michezo ina faida kubwa ya kurefusha maisha kwa hiyo basi sio vyema michezo ikasisitizwa tu kwa makundi fulani pekee ila Wizara iangalie uwezekano wa kuhamasisha michezo kwa jamii yote ya kitanzania yaani wazee, vijana, watoto, watu wazima, wake kwa waume na sehemu zote ikiwemo mijini na vijijini na zaidi kwa walemavu ambao ndio nitawazungumzia zaidi leo katika maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwaangalie walemavu kipekee zaidi kwani kihalisia nao ndio wanaohitaji michezo zaidi ili kuwasaidia katika viungo vyao ambavyo vimepata ulemavu na kama inavyojulikana michezo au mazoezi ni afya. Tumeshaona katika michezo ya Ulaya walemavu wakishirikishwa katika michezo kwa kiwango kikubwa sana na hata imekuwa ni sehemu ya ajira kwao kwani huwapatia kipato na kuwawezesha kujihudumia na kuhudumia familia zao bila kutegemea misaada na kukomesha tabia ya kuombaomba barabarani.

Mheshimiwa Spika, pia kuondoa dhana ya kuwa kila mlemavu anapaswa kukaa barabarani na kuomba misaada kama inavyofanyika katika miji mikubwa kama Arusha, Mwanza, Dar es Salaam na kadhalika. Mfano walemavu wa miguu (wanaotambaa) wanaweza kucheza vizuri sana muziki na tumeona hata mwanamuziki Rose Mhando amekuwa akiwatumia sana na hasa katika wimbo wake wa “Nibebe” na hivyo kuwapatia ajira.

Mheshimiwa Spika, vilevile wananchi wa vijijini wasisahaulike katika michezo kwani michezo sio mipira tu bali kuna kuruka kamba, kurusha tufe, kukimbia ambavyo vinaweza kufanyika sehemu yoyote ile nchini ambako kuna uwazi wa kutosha na hivyo kuondoa dhana ya Wizara kuwajali wananchi wa mijini kwa kuwa kuna viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Spika, katika hili la michezo kwa walemavu, napenda kulishukuru Bunge la Tanzania na Idara inayohusika na michezo Bungeni kwa kuonesha mfano mzuri wa kuwashirikisha walemavu katika michezo mfano *week* iliyopita tu timu ya Bunge ya *football* ilicheza na timu ya walemavu wa ngozi ambao walialikwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, vipaji vya kipekee, hakuna ufuatiliaji ili kuwasaidia watoto, vijana, wazee wenye vipaji maalum katika nyanja ya michezo mfano kumekuwa na watoto ambao wanaonekana kupenda na kuweza kufanya michezo fulani kwa kiwango kikubwa hata kuliko watu wazima mfano kuimba, kukimbia, kucheza tenisi lakini wamekuwa hawasaidiwi *either* na wazazi au Wizara na hata wakati mwingine ambao ndio wamekuwa wakikaa nao kwa muda mwingi na hasa wakati wakiwa shuleni.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kuipongeza Wizara na Serikali kwa kuanzisha kikundi cha kuwawezesha vijana wenye kipaji cha kuimba kiitwacho *THT* kwani kimewapa ajira vijana wengi hapa Tanzania na kuweza kujikwamua katika maisha tegemezi. Mfano wa wanamuziki hao ni Lina, Mwasiti na kadhalika ambao wamekuwa wakifanya vizuri katika fani hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naiomba Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuzidi kuiinua sekta ya michezo nchini, kuongeza ajira kwa vijana na semina ambazo zitawasaidia vijana wengi kuweza kufanya kazi za ujasiriamali zaidi kuliko kukaa mitaani bila kazi na matokeo yake kujikuta wanaingia katika makundi ya matendo maovu eti kwa kuwa tu Serikali haina ajira za kutosha.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Waziri pamoja na Naibu Waziri lakini pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa vizuri kabisa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe masikitiko yangu makubwa sana kwa Serikali kuhusu wimbi la vijana wanavyokosa ajira na kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu kama kuvuta bangi na kutumia madawa. Nashauri kwamba ni muda mwafaka sasa Serikali iweze kuona ni namna gani itawasaidia hawa vijana baada ya kuhitimu masomo yao ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na nchi yetu kukosa ajira, vijana wapewe mikopo ili waweze kujiajiri wenyewe. Aidha, Serikali ingefufua viwanda vyetu pia ili vijana wengi waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja. Katika mchango wangu naomba kujadili suala la vijana na ajira. Naomba Serikali ije na mkakati unaobainisha wazi namna inavyojikita kuelimisha vijana kuzitambua na kuzitumia fursa zinazoweza kutoa ajira za uhakika, lakini vijana hawazioni, kama kilimo. Nikiwa Mbunge kutoka Nkasi Kusini ambako kilimo ni mwajiri wa vijana kwa asilimia 80 kwa maeneo ya vijijini, ninashuhudia mabadiliko makubwa yanayoletwa na vijana wanaojihusisha na kilimo. Kilimo sio kama zamani, lazima vijana waione fursa hii.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ianzishe makazi mapya ya vijana waliosomea Kilimo, itoe mikopo ya matrekta, pembejeo na mtaji kwa vijana watakaopenda kuendeleza taaluma zao katika kuendeleza maisha yao. Hawa wanaweza kutoa ajira kwa vijana wenzao kwa kuwa karibu kila Mkoa una mabonde. Mabonde mazuri yaimarishwe na yaanze kuandaliwa kwa uzalishaji huu ambao pia utakuwa ni shule kwa wakulima wa maeneo ya karibu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni vijana na ajira. Nashauri Vyuo vya Ufundi (*VETA)* vijengwe kila Wilaya viweze kuwajengea uwezo wa kujiajiri kwa taaluma za ufundi ambazo zinatolewa na Vyuo

hivi muhimu. Wilaya ya Nkasi iwe miongoni mwa Wilaya za kwanza, kwani hakuna chuo chochote cha utoa ujuzi wa ufundi.

Mheshimiwa Spika, janga la Ukimwi limeliandama sana kundi hili la vijana. Kwa namna yoyote lazima elimu iendelee kutolewa bila kukoma, kwani wanakabiliwa na changamoto nyingi katika suala hili. Vijana wa kike wako hatarini zaidi na wengi wanapoteza fursa za kusoma kwa kupata ujauzito. Ninaishauri Serikali kumwezesha binti aliyepata ujauzito kurejea masomoni ili lizingatiwe suala la kuleta usawa wa kielimu miongoni mwa vijana wa kike na wa kiume.

Mheshimiwa Spika, vijana walemavu hawaendelezwi. Walemavu hawa Wamebaki hawana chombo cha kuwaendeleza kwa kazi za ujuzi au elimu ambazo wangeweza kujikita wangefanikiwa sana. Naishauri Wizara ije na mkakati kutambua njia na walemavu na kuanzisha namna ya kuwasaidia ili kupunguza pia unyanyapaa ambao umekuwa kikwazo kwa maendeleo ya jamii ya walemavu nchini kwa kutambua kuwa kila jamii ina walemavu.

Mheshimiwa Spika, nashauri hata kwenye ngazi ya Halmashauri, pawepo Madiwani Wawakilishi wa kundi hili linaloongezeka kwa kasi kutokana na ajali nyingi hasa za pikipiki maarufu kama bodaboda.

Mheshimiwa Spika, habari kama haki ya Watanzania wote, ni muhimu ipatikane kote kupitia Redio ya Taifa. Maeneo ya Jimbo la Nkasi Kusini, kandokando ya Ziwa Tanganyika, hakuna mawasiliano ya kufikika kwa utulivu Redio Tanzania. Wizara ifanye jitihada kuangalia usikivu wa Redio Tanzania Kata za Ninde, Kala na Wampembe.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya, michezo ni burudani, michezo inajenga kufahamiana, michezo ni ajira. Naomba mkazo uliopo sasa katika michezo, hasa wakati wa Serikali ya Mheshimiwa Kikwete, uendelezwe ili kunufaika na mambo yaliyotajwa hapo juu, yaani afya, ajira, burudani na kufahamiana *(interraction)*.

Mheshimiwa Spika, nchi isiyolinda desturi na tamaduni zake ni mfu, au nchi ya kitumwa. Naomba tuendeleze utamaduni kwa kukutanisha Mikoa mbalimbali kila baada ya miaka mitatu au minne kuishindanisha na kutoa zawadi kitaifa. Hii inaendeleza utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, hakuna vazi la heshima la Taifa pamoja na kupigiwa chapio muda mrefu. Kwa sasa hakuna linaloendelea. Wasanii nao waendelezwe hapa, kwani kwa sasa wanaendeleza tamaduni zetu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi sipingi Sera ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, lakini magazeti yamekuwa utitiri na mengi yamekuwa yakipotosha ukweli na chonganishi sana kwa Serikali na wananchi wake na sijaona hata mara moja Serikali ikichukua hatua yoyote kuthibiti hali hii, Serikali ina maana gani? Ni kwamba upotoshaji na uchonganishi ambao unailazimu Serikali wakati mwingine kukanusha inaridhika nao?

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu wengi wanaamini vyombo vya habari, kuendelea kuacha upotoshaji unaoendelea na wenye mamlaka hawachukui hatua ni kutaka kutuletea shida baadaye. Sisi bado tuna imani na Serikali kama kuna mtu ana dhamana ya kuyawekea utaratibu wa kufanya kazi kwa maadili lakini hafanyi, hivyo ajiuzulu asitoe mwanya kwa watu kupata viongozi au watawala wapotoshaji na itakuwa mwisho wa utulivu nchini, chondechonde. Nataka kusikia mikakati ya Wizara ikoje katika jambo hili.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, vyombo vingi vya habari hasa kwa upande wa *TV* hujikita zaidi kwenye mambo ya muziki, tamthilia ambazo hazina mafunzo kwa jamii. Kuna wakati kunajitokeza matokeo makubwa ya muhimu lakini *TV* huendesha programu zake nyingine. Mfano badala ya kuonyesha vipindi vya kuhamasisha wananchi kujiepusha na majanga, kupinga vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake, watoto, vikongwe, albino na kadhalika na au kuonyesha tamaduni za Mwafrika na hasa Mtanzania na kadhalika, vyombo hivyo hujikita katika kuonyesha katuni, muziki tena wa nje na mambo yasiyo na asili na Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, lugha zinazotumika katika vyombo hivyo hawana maadili mema kwa Watanzania na haifundishi mafunzo mazuri vijana wadogo ambao hufuatilia sana vipindi vya *TV*. Lakini pia wakati *TV* inachukua muda mrefu kuonyesha vipindi vyake kama Bunge na kadhalika lakini redio zake kama TBC Taifa, FM na Redio nyingine zinaendelea na program nyingine wakati kuna wananchi wengi vijijini hawasikii matangazo ya *TV*.

Mheshimiwa Spika, bajeti ndogo kwa vyombo vya habari vya Serikali kama vile *TBC, TBC-Taifa, TBC-FM*. Hilo linafanyika huku Serikali ikitambua kuwa vifaa na mitambo pamoja na majengo yamechakaa na yamezeeka. Mfano mzuri ni kituo cha *TBC,* Kanda ya Kusini ambacho Makao Makuu yake yapo Lindi. Kila mara kumekosekana umeme kwa kuwa jenereta ni mbovu. Mitambo ya kurusha matangazo huzimika kila wakati. Serikali ieleze ni lini itaboresha sekta hii kwa upatikanaji wa habari wa uhakika?

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu wadau wa tasnia hii ya habari wanaisubiri Sheria ya Haki ya Kupata Habari na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari, lakini bado Serikali inasuasua katika kuleta Muswada wa Sheria hii Bungeni. Ni vyema Serikali ikaharakisha mchakato huu haraka. Haijulikani hofu gani Serikali inayo juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, Wizara ni vyema ikakamilisha majengo yake ambayo bado ni ya muda mrefu katika barabara ya Nyerere Dar es salaam. Ushindani wa sasa ni mkubwa kwa vyombo vya habari. Ni vyema kama *TBC Radio* na *TBC Television* navyo vikaboreshwa vikaingia katika ushindani wa kweli, kwani vyombo binafsi ndivyo vinavyotoa huduma bora zaidi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, Serikali haioneshi ni ya kuwakwamua vijana kutoka kwenye lindi la umaskini kwa kukosa ajira rasmi. Lakini hata pale wanapoonesha juhudi za kujikwamua kwa kujitafutia riziki kwa kufanya biashara ndogondogo, Mamlaka za Miji, Manispaa, Majiji na Vijiji husumbua vijana kwa kuwapora mali zao na kuwafikisha Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, vitendo hivyo hurudisha nyuma jitihada za vijana na nguvu kazi ya Taifa na hivyo kuwafanya kuendelea kuwa maskini. Kumbe Tanzania badala ya kuwa na Sera ya kuutokomeza umaskini ina Sera ya kuwatokomeza maskini. Matendo haya yanafanyika wakati Wizara yenye dhamana ya vijana iko kimya.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana ni tatizo kubwa katika Taifa hili. Naomba Wizara itoe tafsiri sahihi katika maana ya maneno haya mawili kazi/ajira. Kazi ni shughuli yoyote ambayo inaweza kumpatia kijana kipato chake na kumudu maisha na mazingira yanayomkabili na kuyamudu. Mifano ya kazi ni kama kilimo, uvuvi, ufugaji na kadhalika. Zaidi ya vijana 70% wanaishi Vijijini wanajihusisha na shughuli hizo. Ni vyema Wizara ikajishughulisha zaidi na vijana hao huko Vijijini ambako ndiko waliko wengi kwa kuwapatia mikopo, taaluma na kutoa elimu ya ujasiriamali kwao. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kupunguza umasikini kwa vijana wetu ambao ni nguvu kazi katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, ajira ni shughuli yoyote kijana ambayo anaweza kuajiriwa aidha kwa mkataba kupitia asasi binafsi, au Serikali. Sasa hivi kuna mahitaji makubwa ya wanaohitaji kuajiriwa, lakini nafasi za kuajiri ni finyu sana. Ushauri wangu ni kuitaka Serikali ijitahidi kusimamia eneo la kazi bila kusahau eneo la ajira ya vijana na nguvu kazi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeonyesha udhaifu mkubwa katika kusimamia michezo, jambo ambalo hufanya michezo mingi kuzorota. Michezo kama *netball, basketball, football* kila mwaka tumekuwa vichwa vya mwendawazimu. Leo tunaambiwa timu ya mpira wa miguu ya wanawake badala ya kuonyesha kile kilichowapeleka kushiriki mashindano na kuliwakilisha Taifa wamejikita katika vitendo vya kusagana. Serikali ina taarifa juu ya hili na inatoa tamko gani?

Mheshimiwa Spika, mchezo kama *volleyball, rugby*, mashindano ya pikipiki, baiskeli na kadhalika haijapewa vipaumbele kabisa. Kwa nini Serikali ikiona imeshindwa mashindano ya vilabu vya mpira isijikite katika michezo ambayo inawezekana hata kama ngoma zetu za asili na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, timu za *Academy* hazisimamiwi vyema kwa lengo la kunua michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo limebaki kupokea ruzuku na mapato ya mlangoni ya mechi za mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, viwanja vingi vya michezo vilivyopo vimeuzwa na kumilikiwa na taasisi binafsi na Vyama vya Siasa. Pia maeneo mengi ya viwanja vya wazi yamebadilishwa matumizi yake na kufanywa maeneo haya kujenga majengo yasiyohusiana na makusudio ya kuwepo maeneo hayo. Kwa mfano, nje ya uwanja wa Ilulu Stadium huko Lindi yamejengwa magereji badala ya vijana kutumia viwanja hivyo kwa mazoezi kama mpira wa miguu, netiboli, gofu, *table tennis, basket ball* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshindwa kulinda maadili ya Taifa letu na kusababisha tamaduni zetu kupotea na kuifanya jamii kuiga tamaduni za nje mfano *Big Brother, Miss Tanzania* na kadhalika. Serikali ina mpango gani wa kufufua tamaduni za Mwafrika na kuacha zile za nje?

Mheshimiwa Spika, utamaduni ni kielelezo cha Taifa kama utambulisho wa Taifa hili. Utamaduni wetu kwa sasa ni uigizaji wa tamaduni za nje na kuharibu tamaduni zetu hapa nchini. Je, Serikali ina mkakati gani ambao unaweza kudhibiti uendelezaji mila na desturi za kigeni na kufanya nchi yetu kuwa jalala la tamaduni za nje?

Mheshimiwa Spika, Serikali italitangaza rasmi vazi la Taifa lini?

Mheshimiwa Spika, lini Serikali itaandaa vituo mahususi vya kuwatunza walioathirika na madawa ya kulevya sambamba na kuwawezesha walioamua kuachana na madawa hayo kwa hiyari?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mawaziri Dkt. F. Mukangara na Mheshimiwa Amos Makalla, kwa kuteuliwa kwao kuongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, *issue* yangu ni moja kubwa, kutosikika kwa Radio ya Taifa *(TBC)*, Jimbo la Manyoni Magharibi kilomita za mraba 18,000 kutoka Kamenyanga, Njirii, Gurungu, Sanjaranda, Aghondi, Mabondeni, Idodyandole, Mbughani, Doroto, Itigi, Damweru, Ipande Lulanga, Itagata, Kayui, Makale, Mtakuja, Mitundu, Kalangali, Mwamagembe, Kintanula mpaka Rungwa mpakani na Chunya na mpaka Chaya mpakani na Igalula Tabora. Kata zote 11 hazipati Radio hii. Maeneo kadhaa tunategemea Redio Mwangaza na muziki wake wa injili tu. Chondechonde kulikoni Singida? Naomba jibu la uhakika, nini kinafanyika yarabi?

Mheshimiwa Spika, aidha, naunga mkono hoja kwa sababu ya imani kwa Mawaziri hawa, nawasilisha.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii iliyowasilishwa mbele yetu. Naomba nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari hasa taarifa ya habari zinazotolewa na vyombo mbalimbali havina mfumo unaolingana na muda haulingani. Je, ni Sera ya habari? Nilitaka kujua.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vimekuwa vikiwahoji watu walewale bila kupata fursa ya watu wengine.

Mheshimiwa Spika, matangazo yamezidi ndani ya habari, yafanyike baada ya habari.

Mheshimiwa Spika, magazeti yawe na ukurasa wa kuandika habari za kweli na za uchochezi/kubuni ili tuelewe.

Mheshimiwa Spika, Wizara imewatenga sana vijana hapa Tanzania kwa sababu zifuatazo:-.

(i) Hakuna mikutano ya vijana inayofanyika ndani ya nchi hii, mashuleni, vyuoni na hata nje ya mfumo wa shule. Hakuna ushauri unaotolewa na Wizara. Mfumo wa kuwafikia vijana ni mbovu sana.

(ii) Mipango ya maendeleo ya vijana haipo Tanzania, vikundi vya vijana hakuna na hakuna malezi na maelekezo toka Wizarani kwa vijana. Naomba Wizara ijiangalie haifanyi vizuri.

(iii) Mikopo, mitaji, vyuo vya kuendeleza vijana hakuna. Je, nini ufanisi wa Wizara?

(iv) Vijana, machinga Wizara imewatenga na haiwaendelezi kwa mawazo na kufanya mipango mizuri kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, utamaduni, toeni umuhimu kwa ofisi za utamaduni kwa kuwapatia *budget* ya kutosha kwani ofisi zote zina hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, ngoma za asili zinazidi kupotea na ni wito wangu kwamba Wizara iweke msukumo wa kutunza na kuenzi ngoma za asili. Wizara imelala sana.

Mheshimiwa Spika, bendi za muziki zinapoburudisha, zinadhalilisha utamaduni; pia *uniform* hazitumiki wakati wa burudani kwenye *stages.*

Mheshimiwa Spika, mafundisho ya *kitchen party* yafundishwe mashuleni kwa kina dada ili wawe wazazi safi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, mipira, jezi ni tatizo mashuleni, Wizara ijiandae. Aidha, bajeti za michezo kwenye Halmashauri hakuna tunaomba mkazo ufanyike haraka na Baraza la Michezo liwajibike pale ambapo hatufanyi vizuri kwenye michezo.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, kwa nini vyombo vya habari nchi hii hususani *TV* hazitumii lugha za *sign language* ili kuwawezesha watu wasiosikia pia kupata taarifa kwenye *TV* kama taarifa ya habari? Je, Serikali inasemaje kuhusu hili?

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA**: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja ya makadirio ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari wamekuwa wanafanyakazi kubwa ya kutoa habari za kusaidia nchi hii. Wanahabari hawa hufanya kazi kubwa kutafuta habari za kiuchunguzi na nyingine zinazohatarisha maisha yao. Wanaandika kuhusu matendo ndani ya jamii yanayohatarisha maisha ya wanawake na watoto kama ubakaji, ukeketwaji, uharamia na kadhalika lakini pia huonyesha ufisadi katika matumizi mabaya ya Serikali, Mashirika ya Umma, Vyama vya Ushirika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninachopenda kujua Serikali ina mahusiano gani na wanahabari na hasa wanapochunguza na kutoa habari zinazoonyesha hujuma, Serikali inachukua hatua gani? Mara nyingi taarifa zinazotolewa na waandishi wa habari huonekana kama porojo na wengine hudiriki kusema “haya ni mambo ya magazeti” kuna kitengo katika Serikali kinachofuatilia taarifa hizo na kuzichunguza na kuzifanyia kazi kwa maslahi ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano Meli ya MV Skagit iliyozama na kuua watu katika bahari ya Hindi majuzi, inaponunuliwa kutoka Marekani, Magazeti ya Marekani yaliandika na kutoa taarifa kuwa meli hiyo ambayo ilikuwa iharibiwe huko imenunuliwa na nchi maskini kwa bei ya kutupwa. Je, Serikali iliposoma habari hizo ilichukua hatua gani? Mimi naishauri Serikali iwe na kitengo cha kusoma habari na kuchukua zenye umuhimu kwa Taifa, kufanya uchunguzi na kuzifanyika kazi kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko kuhusu mchakato wa kupata wimbo wa Afrika Mashariki. Wimbo huu ameanza kuimbwa wale waliohusika kuutunga na hata wale walioingia katika mchakato hadi hatua fulani wanapata maslahi yapi?

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, hongera kwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi wanazofanya, nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji vijana wanaojua pia kutumia vyombo vya muziki kuliko kutegemea sauti zilizoandaliwa tu, wajue pia gitaa, vinanda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mashindano ya kwaya yahimizwe.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayofanya na ni nzuri sana. Nawapongeza pia watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya kuandaa bajeti pamoja na ufinyu wa fedha. Mchango wangu utakuwa juu ya mapato na matunzo ya uwanja wa Taifa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, imekuwa hadithi kwa mapato ya uwanja kwenda Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Gawio la asilimia mbili (2%) ya mapato ya uwanja yanatakiwa yaende Temeke lakini hakuna gawio linaloenda mpaka sasa. Wizara ikiulizwa inasema *TFF* hawa *TFF* ni nani na wako juu ya Wizara?

Mheshimiwa Spika, uwanja ule unawaathiri sana wananchi walio jirani na uwanja, kama kawaida kila jambo lina changamoto zake. Naomba sasa Wizara iniambie lini wataleta gawio la asilimia mbili (2%) kwa Manispaa ya Temeke?

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nataka kujua hatma ya uwanja wa Karume. Uwanja wa Karume ni uwanja mzuri ulio katikati ya mji, ungeweza kupromotiwa vizuri ukatumika kwa ligi mbalimbali ungesaidia Serikali kuingiza mapato na Halmashauri ya Wilaya ya Ilala ingepata gawio la asilimia mbili (2%) lingesaidia kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara iwe na ubunifu wa kutafuta eneo la uwanja katika Manispaa ya Kinondoni. Tunaona Halmashauri inagawa viwanja vya ujenzi lakini hatuoni ombi la Wizara kutaka kupata eneo la kujenga uwanja wa michezo Kinondoni. Kwa idadi ya watu iliyopo Dar es Salaam kuna ulazima wa kupata uwanja wa michezo katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa ya Serikali na imesaidia sana katika ukusanyaji wa mapato lakini bado jitihada ziongezeke.

Mheshimiwa Spika, mawakala wa ukatishaji wa tiketi wanachaguliwa au kuteuliwa kwa kutumia vigezo gani?

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie suala la vijana na maendeleo yao, Wizara inatoa mchango gani kwa vijana katika suala la ajira, kuajiriwa na kuajiri, inawasaidiaje vijana?

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda nichangie tena katika sekta ya habari. *TBC* ni *television* ya Taifa lakini bado haijawa na hadhi ya Kitaifa, hatujui tatizo ni nini? Uendeshwaji wake na vipindi vyake ni vilevile, wafanyakazi wanashindwa kumudu ushindani kwa ukosefu wa fedha. Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi ifanye mpango mkakati wa makusudi kuisaidia *TBC* kupata chanzo kizuri cha mapato nayo iweze kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, *TBC* inapewa kazi ya Kitaifa ya kuonyesha Bunge kwa muda wote. Je, Serikali inalipia huduma hii? Kama huduma ya kuonyesha Bunge saa zote ni bure basi Kampuni hii itashindwa kujiendesha kwa faida, ni lazima ipate hasara.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali yangu sikivu waandae wataalam wabunifu, wabuni mbinu za kuipeleka *TBC* kifaida kwa kuandaa program mbalimbali zenye kuleta tija kwa Taifa na Shirika letu lizidi kuendelea. Redio Tanzania haina mawasiliano, utakapotoka kilometa 20 toka Dar

es salaam unakuta redio haiongei tena, redio yetu inatakiwa isikike pande zote nchini Tanzania. Pamoja na ufinyu wa bajeti, tuangalie jinsi ya kusaidia chombo chetu hiki cha Kifaita.

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze upande wa magazeti, magazeti yamekuwa mengi sana na vyombo vingine vya habari vinafanya kazi vizuri sana na hasa kipindi hiki Wizara mmesimamia vizuri endeleeni hivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja bajeti ipitishwe, ushauri wangu uzingatiwe.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya hotuba ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza bajeti ya Wizara hii kila mwaka ni ndogo sana kiasi kwamba inakuwa vigumu kwa Wizara hii kutekeleza mipango ya maendeleo na kusababisha kiwango cha michezo kushuka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi wa michezo, kumekuwepo migogoro kila mwaka katika vyama vyenye dhamana ya kusimamia michezo hapa nchini. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutunga sheria kali zitakazowabana waanzishaji wa migogoro hiyo?

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari, baadhi vinatumia lugha chafu hasa magazeti, yapo magazeti kazi yake kuandika matusi na kashfa kwa viongozi, nini msimamo wa Serikali? Yapo vilevile magazeti yanayoitwa ya “Udaku” ambayo mengi ya hayo huandikwa habari na kutoa picha chafu ambazo hukiuka maadili na hasa watoto huyasoma na kuyashabikia, Wizara ina mpango gani wa kunusuru hilo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni, naomba Waziri atufahamishe ni kwa namna gani Wizara hii imesimamia utamaduni na manufaa yake ni nini kwa Watanzania na nchi inapata kipato gani kutokana na utamaduni wetu?

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuishauri Serikali, ni kweli kabisa michezo ni burudani na ni ajira. Jimboni kwangu kuna vikundi vingi sana ambavyo vikiwezeshwa kwa kupewa ushauri wa kitaalamu na nyenzo za kisasa kama vifaa vya kurekodia *CD, DVD* na kuziuza kwa gharama nafuu, tutakuwa tumewawezesha na kuuenzi utamaduni wetu wa asili na kupunguza wimbi la vijana kuwa wazururaji na wavuta bangi mitaani. Naomba sana ushauri huu ufanyiwe kazi.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, kutokana na muda naomba, nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kuhusu habari, Serikai imeachia huru sana vyombo vya habari, magazeti kutumia lugha na maudhi kinyume cha maadili ya Kitanzania *(against acceptable values and norms of Tanzania).* Nashauri Baraza la Magazeti (*Media Council*) liagizwe kutazama jambo hili. Aidha, Serikali kwa haraka iweke kanuni ya kudhibiti sinema na *film* zinazoonyeshwa kwenye runinga zetu, matusi na vitendo vichafu vinaigwa na watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala zima la vijana wa Kitanzania hawana elimu stadi kwa ajili hiyo wanakosa sifa ya kuajiriwa kwenye viwanda au kujitegemea wenyewe. Nashauri shule za Kata zibadilishwe kuwa shule za *VETA* ili vijana wapate elimu ya ustadi na baadaye elimu ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kuhusu Utamaduni na michezo, kwa kuwa uzoefu umeonyesha kuwa timu za Tanzania za michezo ya mpira, riadha na michezo mingine hazishindi katika mashindano ya Kimataifa kwa sababu ya matayarisho mabaya kwa ajili ya bajeti finyu, naishauri Serikali itafute wawekezaji wa ndani na nje ili michezo iendelezwe. Aidha, ni lini Serikali itawekeza katika kuwalea vijana wenye vipaji vya mchezo wa riadha hasa mbio za masafa

marefu (*long distance running*) kama vile Mbulu na Hanang katika Mkoa wa Manyara vijana hawa wameiletea Tanzania sifa lukuki Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ili kupata washindani wa kiwango cha juu, Serikali ianzishe michezo ya kulipwa (*professional*) hasa riadha, *boxing na football*. Michezo ya hiari (*amateur*) haina mshiko wowote.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, umefika wakati ambapo kilio cha kuletwa Bungeni Muswada wa Habari kingesikilizwa. Sheria mpya ya habari itatupatia kama Taifa nafasi ya kuijenga kwa manufaa ya nchi Tasnia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, sheria itaondoa upungufu uliopo hivi sasa ambao tunafikiri kwamba inatoa uhuru, lakini ukweli ni kwamba inadhalilisha uhuru wenyewe. Kuwepo kwa vyombo vingi vya habari hakumaanishi kwamba kuna uhuru wa vyombo vya habari. Hivi sasa tunashuhudia magazeti, redio na *TV* vimeanzishwa kwa ajili tu ya wanasiasa kuchafuana au kujibizana.

Mheshimiwa Spika, vilevile baadhi ya vijana bila utaalam na baada ya kukosa ajira kushika kalamu na kutunga habari za kudhalilisha viongozi au wabaya wao, Sheria ya Habari bila shaka itatatua matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya michezo ni ndogo sana, michezo ingeweza kwa kiasi kikubwa kutangaza nchi yetu na kutengeneza ajira kwa vijana wetu. Kwa kuwa fedha ni kidogo, ni jambo la muhimu walau kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya timu za Taifa kama *Taifa Stars*, *Serengeti Boys* na Twiga.

Mheshimiwa Spika, hali inayojionyesha hivi sasa kuhusu utamaduni inaelekea kwamba jukumu la kusimamia sanaa ya utamaduni limeachwa kwa watu binafsi badala ya vyombo ambavyo vimeundwa kisheria kama BASATA na TASUBA ya Bagamoyo. Hali hii imesababisha ngoma zetu za asili za makabila mbalimbali kuanza kupotea.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba ngoma za asili zinatumika sio kama starehe peke yake bali zimebeba elimu katika mambo mbalimbali yanayoihusu jamii na hutumika katika hamasa za matukio mengi ya kijamii. Ni makosa makubwa kama jamii kuacha ngoma zetu zipotee huku jitihada zikielezwa kwenye Bongo fleva, dansi, filamu na mambo mengine ambayo hata hivyo mengi yanaharibu vijana wetu ukilinganisha na ngoma zetu za asili.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Wizara. Pia ninapenda kumpongeza Dkt. Fenella Mukangara, Waziri wa Wizara hii pia Naibu wake Mheshimiwa Amos Makalla kwa kupewa kusimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inabeba jukumu kubwa sana kwa Taifa hili hasa katika rika la vijana. Pia ni tegemeo kubwa kwa vijana wa nchi hii ambao ndio rasimaliwatu tegemewa kwa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, vyama vya siasa vinazo jumuiya zao za vijana kiitikadi. Lakini pia bado nchi haijaonesha nia thabiti ya kuwakusanya vijana wote, wa dini zote na itikadi zote tayari kwa kuanzisha Baraza la Vijana la Taifa lililo thabiti. Nalisema hili makusudi kwa kuwa kuna mgawanyiko mkubwa sana kwa vijana hasa kwa itikadi za vyama, hii ni hatari sana kwa Taifa na lazima kuwe na juhudi thabiti za kuliondoa wingu la mgawanyiko baina ya vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuwepo na Baraza la Vijana la Taifa ambalo litawakusanya vijana wote walio tayari kulitumikia Taifa na kuanza kuwapa mafunzo ya JKT, pia kuwatumia wakufunzi Maafisa Ugani na kuwapa ardhi yenye hati ambayo ni rahisi kukopea pembejeo kutoka katika taasisi za fedha ili wazalishe mazao ya biashara na chakula ambapo ziada itauzwa.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara kupitia *SIDO* iwasaidie vijana walio ndani ya Baraza kupata viwanda vidogovidogo na vikubwa kwa ajili ya kusindika vyakula na mazao mengine ili kuwapatia ajira vijana waliopo ndani ya Baraza la Vijana la Taifa kulingana na maeneo waliyopo vijana (hii itawavuta vijana wengi) waliokata tamaa kujiunga na Baraza kwa ajili ya mustakabali wao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia ikumbukwe tunao wataalam wengi sana wanaozalishwa na vyuo vikuu ambao ni vizuri kama wataajiriwa na Baraza kwa ajili ya kutoa msaada na ushauri wa kitaalam kwa vijana wa Baraza. Pia itatoa ajira rasmi na zisizo rasmi kwa vijana ikiwemo umoja wa vijana Kitaifa na pia itaweza kupunguza uhasama wa kiitikadi na kuleta mafanikio. Pia Baraza hili lijihusishe na michezo na hasa muziki wa kizazi kipya na pia Baraza lianze ngazi za Mitaa, Kata hadi Taifa. Hii ndiyo njia pekee ya kuleta umoja wa Kitaifa kwa nchi huru inayojitawala.

Mheshimiwa Spika, nategemea katika majumuisho ya Waziri atatueleza juu ya Baraza la Vijana la Kitaifa. Nashukuru sana kwa kupata nafasi hii.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nachangia katika suala la mapato ya uwanja wa Taifa kuja Manispaa ya Temeke. Mapato hayo bado hayajaletwa Temeke na badala yake Serikali ikatoa *Parking* za magari ambazo zimechukuliwa na Halmashauri ya Jiji. Temeke hatutaki maneno, tunataka asilimia mbili ya viingilio ya kwetu na ni haki yetu kama wale wa migodini wanavyodai asilimia yao.

Mheshimiwa Spika, ushauri, kama Wizara inashindwa kusimamia basi tushirikiane na Halmashauri na *TFF* kukusanya mapato tujue nini kinapatikana. Kwa kipindi kirefu tumezungumzia na kuomba fedha zetu kwa nini hamleti?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Tunataka majibu yenye faida kwa wananchi wa Temeke.

Mheshimiwa Spika, pia naomba ufafanuzi kwa masuala yangu mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni lini Wizara yako itatenga fedha kwa ajili ya Vyama vya Michezo kama *TFF*, CHANETA, Chama cha Mpira wa Vikapu, Chama cha Kuogelea, Chama cha Tenis, Chama cha Mpira wa Miguu Wanawake, Chama cha Mieleka na vinginevyo. Kwa sababu kila kunapokuwa na mashindano yanayohusu kati ya vyama hivyo kumekuwa na desturi ya kuomba omba (kutembeza bakuli) kwa hali hii michezo haiwezi kendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mashindano ya ligi kuu (*Premium*) na ligi daraja la kwanza, mpira wa miguu timu inapoingia uwanjani bila ya kuwa na vitambulisho vya wachezaji vya kuwatambulisha kama hawa ni wachezaji halali waliosajiliwa, je. timu hiyo inakuwa ni halali kushiriki katika mashindano hayo?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kuunga mkono hoja ya bajeti asilimia mia moja. Pia nawapongeza viongozi wote wa Wizara na hasa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wamejitahidi kufanya kazi nzuri ya kudumisha michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni juu ya upotevu wa fedha za viingilio kuingia mifukoni mwa wajanja. Mara nyingi utaona idadi ya watu wanaoingia uwanjani ni kubwa lakini fedha zinazokuja kutangazwa za mapato hayo ni kidogo.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, tangu Tanzania ianze kushiriki michuano ya Olimpiki mwaka 1964, Tanzania imepata medali mbili tu katika michezo hiyo. Medali hizo zimepatikana mwaka 1980 wakati Filbert Bayi alipopata medali ya fedha mbio za mita 3,000 na Sukiman Nyambui alipopata pia medali ya fedha katika mbio za mita 5,000.

Mheshimiwa Spika, mwezi ujazo Tanzania itakuwa ni miongoni mwa nchi zitakazoshiriki katika mashindano ya michezo ya Olimpiki itakayofanyika jijini London, Uingereza kuanzia Julai 27 hadi Agosti, 2012. Tegemeo letu katika michezo hiyo liko kwa Suleiman Kidunda na mwanariadha Samson Ramadhani na Zakhia Mrisho ambao wamefikia viwango vya kushiriki michezo hiyo ya Olimpiki huku kukiwa na nafasi mbili za upendeleo katika michezo wa kuogelea na Paralimpiki. Idadi hii ni ndogo licha ya Kamati ya Olimpiki kutenga bajeti ya shilingi 156 millioni kwa ajili ya maandalizi ya wanamichezo wetu mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Kenya wana wanamichezo wengi hasa kwenye riadha (zaidi ya 20) ambao tayari wanavyo vigezo vya kushiriki michezo ya Olimpiki, ambapo unachagua wale walio bora zaidi kwa kuhakikisha wanarudi na medali za dhahabu badala ya kuwania kushiriki tu kama ilivyo kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, licha ya kutengwa bajeti ya shilingi milioni 156 na hata ikitengwa kubwa zaidi ya hapo bado Tanzania itaendelea kubaki kuwa wasindikizaji katika michezo hiyo na mashindano mengine ya Kimataifa endapo hatutabadilisha mfumo wa maandalizi ya wanamichezo wetu katika michezo yote sambamba na viongozi kuwa wawazi katika fedha za misaada. Mfano angalau Shirikisho la Soka Tanzania *(TFF)* kidogo lipo wazi na matumizi ya fedha inazopata kutoka Shirikisho la Soka Duniani *(FIFA)*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Pamekuwepo na malalamiko mengi kuhusu haki, maslahi ya waandishi wa habari na mchakato wa Muswada wa Habari ulikuwa umefikia hatua za mwisho, je, nini kinachozuia au kuzorotesha kutoletwa Muswada huo Bungeni?

Mheshimiwa Spika, matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kiswahili ni kati ya lugha rasmi inayotumika hapa nchini na kwa sasa hivi nchi nyingi zinajifunza kiswahili lakini cha kusikitisha mpaka sasa hivi bado sheria zinazoletwa Bungeni zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza iwapo ni (*Official*) lugha kutumika hapa nchini lakini tukumbuke siyo Watanzania wote wanaoweza kutumia lugha hii. Hii ni pamoja na hukumu zinazotolewa Mahakamani hutolewa kwa Kiingereza. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuhakikisha lugha ya Kiswahili inatafsiriwa kwenye sheria zetu ili kila Mtanzania aweze kuelewa.

Mheshimiwa Spika, haki ya walemavu kupata habari. Vyombo vyetu karibia vyote havina mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu kupata habari. Kwa kuanzia, je, vyombo vya habari vya Taifa ni kwa nini kuanzia na Television ya Taifa *(TBC)* waweke Mkalimani kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa kusikia?

Mheshimiwa Spika, suala la utamaduni, kutokana na utandawazi kwa sasa hivi hapa nchini utamaduni wetu hupotea kila kukicha kwa mfano lugha zetu za asili kwa kizazi cha sasa hazipo kwa asilimia kubwa. Wengi wao hawawezi kuongea lugha za kikabila lakini tukumbuke maadili yalikuwa mazuri na hata ujumbe wa kukanywa uliweza kuwaingia kwa hisia walengwa. Kwa mfano, kule Kagera walipoanza kutoa elimu kuhusu suala zima la ugonjwa wa Ukimwi, ilibidi watafsiri kwa lugha ya Kihaya ili watu wengi waweze kuelewa zaidi. Kwa kiasi kikubwa maadili mengi yanapotea hata kwenye mavazi, vijana wanavaa suruali chini ya makalio, vijana wa kiume wanatoboa masikio, yote haya ni kusahau mila na desturi zetu na kuiga za kigeni.

Mheshimiwa Spika, je, mpaka sasa hivi mchakato wa vazi la Taifa umefikia wapi?.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki za wasanii. Naipongeza Serikali kwa kujitahidi kulinda haki za wasanii lakini miaka kumi na tano iliyopita kuna Wamarekani waliochukua michoro ya wasaniii ( Sanaa) Tingatinga (Dar es salaam Mwenge) na kwenda kuitumia Marekani, palikuwepo na ufuatiliaji wa haki yao, je, suala hili limefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, kama tujuavyo michezo ni sehemu ya wanadamu kuwa na afya nzuri na kuondokana na maradhi na kuleta furaha. Ni wakati muafaka Serikali kuwa na ushirikiano na Wizara nyingine kama Ardhi, ili kuhakikisha viwanja vyote vya wazi virudishwe

ambavyo vingi ni kwa ajili ya watoto kuchezea na kuhakikisha viwanja ambavyo vimekufa vifufuliwe mfano Moshi Mjini pale *KDC* karibu na Ikulu kuna uwanja wa mpira na *netbal* lakini umekuwa ni wa kufugia ng'ombe, hii ni aibu?

Mheshimiwa Spika, uwanja wa King *Memorial* uliopo Moshi, ni uwanja unaoweza kutumika kwa michezo ya Kimataifa kwa bahati mbaya sana siasa zinaingilia uwanja huu na sasa unatumika kama soko. Mwaka 2006, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ilikuwa inaongozwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa bahati mbaya na ya kusikitisha walipitisha maambukizi ya kufanya kiwanja kile kuwa soko la kuuzia mitumba. Nashauri Serikali iangalie ni kwa jinsi gani inaweza kuurejesha uwanja ule ili utumike kikamilifu ukizingatia kila mwaka mwezi Februari kuna Kilimanjaro Marathon ambako hutumia uwanja wa Chuo cha Ushirika ambao ni wa binafsi wakati huu wa Serikali ungeweza kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya vijana, kama tujuavyo vijana ndio Taifa la leo na ndio nguvu na nyenzo kubwa ya Taifa lakini sehemu kubwa ya vijana hawana ajira na hii ni hatari kwa usalama wa nchi sababu vijana wakiwa hawana kazi wanaweza kujiingiza kwenye biashara haramu kama kuuza madawa ya kulevya, ujambazi na kadhalika. Hivyo kuna haja ya Serikali kuiongezea bajeti Wizara hii ili vijana wengi waende au wawezeshwe kusoma ujasiliamali.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana *(YDF)* uongezewe bajeti ili uweze kukopesha vijana waweze kujiajiri. Mwisho, Serikali ijitahidi kukamilisha uanzishaji wa Mfuko wa Vijana ili waweze kujikwamua kutokana na umaskini na kupata mitaji.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, haki ya kupata habari ni haki ya kila Mtanzania. Napenda kufahamu kwa nini kuna ubaguzi katika kupata habari kati ya maskini na wenye kipato? Matangazo ya *TBC* yanayorushwa toka hapa Bungeni Dodoma ni ya ubaguzi, wale wenye kipato na kumiliki luninga *TV* wanapata matangazo yote ya kutoka Bungeni kikamilifu. Wananchi maskini wasiomiliki *TV* na kutegemea redio zao wanapata matangazo hayo hadi mwisho wa kipindi cha maswali na majadiliano yanaendelea baada ya maswali hayarushwi na redio na yanaendelea kurushwa katika luninga tu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanalalamikia hali hiyo na kwa mujibu wa Katiba yetu wanayo haki ya kupata habari na kwa kipekee habari toka Bungeni. Je, ni kwa nini hali hii inaendelea na lini dosari hii itarekebishwa na kuanza kupata majadiliano hayo kwenye redio ili wananchi wajue nini kinaendelea katika nchi yao kupitia mijadala ya Bunge? Nitafurahi sana kama matangazo hayo yataanza hivi sasa wakati Bunge hili la Bajeti likiendelea.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote kwa kuandaa bajeti nzuri yenye kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Wizara kwa kurejesha mashindano ya michezo kwa Shule za msingi (UMISHUMTA), Shule za Sekondari (UMISETA) na kwa Vyuo kwa kuwa ni kutokana na mashindano haya wanamichezo mahiri hupatikana ambao huwakilisha nchi yetu katika mashindano ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mashindano haya ya shule na vyuo kuwa na manufaa makubwa sana, dhana na ukweli huu hautimii kutokana na kutokuwa na matayarisho ya kutosha ikiwa ni pamoja na mazoezi ya muda mrefu yenye tija. Kukosekana kwa mazoezi husababisha Taifa kuwa na washiriki dhaifu ambao hatupati wanamichezo wakakamavu na mahiri. Aidha, katika mashindano haya, hukosa motisha na uhamasishaji ambavyo ni muhimu sana katika kupata wanamichezo wazuri. Mfano mzuri ni wakati wa mashindano hayo huwa taarifa haitolewi mapema ili wananchi waweze kushiriki kuwapa moyo na '*morale*'.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta maana na kupata wanamichezo ambao watailetea heshima nchi yetu, ni muhimu Serikali ijiandae vizuri kabla ya kuendesha mashindano ya shule na vyuo,

tofauti na ilivyo sasa. Aidha, ni muhimu kualika viongozi wa Kitaifa wakati wa mashindano ili kuongeza hamasa. Ni muhimu pia waasisi wa mashindano haya waalikwe ili kuthamini mchango wao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, sina budi kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri na Naibu wake kwa namna wanavyofanya kazi zao kwa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika utamaduni wa Mtanzania umeendelea kupotea kutokana na mageuzi makubwa ya kimawasiliano na kisayansi duniani ambapo malezi/makuzi ya watoto wetu yanaingia katika mitihani mizito. Ni jukumu la Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha wanadhibiti baadhi ya matangazo katika redio, magazeti, majarida na luninga ambayo kwa njia moja ama nyingine huchangia sana upotoshaji na ukiukwaji wa maadili ya Mtanzania. Niiombe Wizara kukiimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Habari na kushirikiana kwa karibu sana na wahariri wetu wa Serikali na wale wa vyombo binafsi kuhakikisha utamaduni wa Mtanzania unalindwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya habari, wakati Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete anatoa tuzo mwaka huu aliwaomba wamiliki wa vyombo vya habari nchini kuangalia upya utendaji wa shughuli zao kwani vyombo hivi ni moja kati ya vyombo ambavyo vinaleta amani katika nchi yetu. Namwomba Mheshimiwa Waziri atafakari upya muundo wa vyombo vyetu vya habari vya Serikali kwani ni aibu hivi sasa *TBC* ukiangalia majengo yanayotumiwa na chombo hicho cha Serikali ni vyema Serikali kuwekeza fedha zaidi kwa kuinusuru *TBC* ambayo haisikiki Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara isimamie upatikanaji wa mikataba baina ya waandishi na wamiliki wa vyombo vya habari hususan vyombo binafsi. Hivi sasa waandishi wengi wa vyombo binafsi hawapati stahili zao sawasawa kwa hivyo ni vyema Wizara kusimama kidete kuona kunakuwa na mikataba mizuri baina ya Waandishi, Wahariri na wamiliki wa vyombo vya habari. Namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili ni lini mikataba hiyo itakuwa tayari?

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, nchi za wenzetu na baadhi ya nchi jirani zinapiga hatua katika michezo kwa kuamini 'Michezo ni ajira' bali kinachoonekana Tanzania ni *vise versa*. Serikali bado haijaona umuhimu wa michezo kwa kuiacha sekta hii ikiwa inaelea kama vile watoto ombaomba. Kwa mfano, Serikali hadi sasa imeshindwa kusaidia Timu zetu za Taifa za Mpira wa Miguu na kuiachia *TFF* pekee.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri atapowasilisha maelezo yake, anipe jibu la ni kiasi gani Wizara imewekeza kwa timu zetu za Taifa hadi sasa? Nina mfano wa Timu ya Taifa ya Zambia, ilifanikiwa kupata Kombe la Afrika kwa sababu Serikali ya Zambia iliigharamia asilimia mia timu ile kwa nini Tanzania tushindwe?

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara kwa hotuba nzuri, hongereni kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kama bajeti ilivyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia na napenda nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mavazi ya skintight na blauzi za tumbo wazi zisitumike kwenye sehemu za *public places*, kama hospitali, mashuleni na kadhalika. Vitopu na suruali za chini ya makalio zipigwe marufuku, zinaudhi na zinaleta aibu. Kweli kuna uhuru wa mavazi ila hayo mavazi niliyoyataja hapo juu hayafai.

Mheshimiwa Spika, suala la ngoma ya kanga moja, naomba ipigwe marufuku. Ni ngoma inayodhalilisha wanawake, wanacheza na kanga moja iliyolowa maji, hivyo maumbile yote yanaonekana, shanga zinaonekana ili mradi ni kama uchi.

Mheshimiwa Spika, pia kuna vipindi katika redio na *TV* zetu, vingi sana vimejikita kwenye burudani na tamthilia (muziki/sinema) na masomo machache sana. Kuna wataalamu wengi kama Madaktari, Wanasheria wenye mengi ya kufundisha, kwa nini wasitumike kufundisha jamii?

Mheshimiwa Spika, vilevile Taarifa za habari ni fupi sana, hazipewi kipaumbele kama muziki na (tamthilia), habari za Afrika ni fupi sana, taarifa ya habari zingerudiarudia. Vilevile utabiri wa hali ya hewa nao pia ni mfupi sana, kama ungetolewa mara kwa mara meli isingezama ingeonywa na watabiri kuwa bahari ni chafu wasingeruhusu kusafiri.

Mheshimiwa Spika, mwisho jengo la *TBC* halina hadhi, *NSSF* wangemalizia kujenga jengo hilo, Desemba, 2012 tunatoka kwenye *analogy* kwenda *digitali*, tunaomba na jengo hilo na Ofisi za *TBC* ziende kwenye digitali.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumpongeza Mheshimwa Waziri Dkt. Fenella na Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Amos Makalla, kwa kazi zao nzuri katika kuiongoza Wizara hii, napenda kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja katika eneo la utamaduni/sanaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utamaduni ni kielelezo cha nchi husika, kwa kuwa utamaduni wetu Tanzania unaendana na makabila mbalimbali na kuweza kutofautisha kabila moja na jingine, kinachosikitisha sasa utamaduni wetu Tanzania umeingiliwa sana na tamaduni za kigeni, kitu ambacho kimeleta athari mbaya sana katika mavazi na malezi ya watoto wetu. Hizi ngoma za kigeni sasa zinaharibu maadili yetu kama kukaa nusu uchi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mfano kuna ngoma inayoitwa Ngoma ya Kanga Moja, wanenguaji wa kike huvaa kanga moja ambayo imeloweshwa maji, kitendo ambacho kinaonesha maumbile yote ya wanenguaji hao wanawake. Huku ni kukosa maadili kwa hiyo naishauri Serikali isitishe uchezaji wa ngoma hii maana ni ya hatari sana na inadhalilisha wanawake.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifanye utafiti na kuona madhara yatokanayo na ngoma hii ya kanga moja na ikomeshwe kabisa ngoma hii ambayo ni kinyume na maadili hayo ya Kitanzania. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati atakapokuja kujibu, anijibu kwa manufaa ya Watanzania maana ngoma hii inaleta athari mbaya kuliko ngoma zote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza naunga mkono hoja ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na naomba nichangie katika meneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu soka, kuna matatizo mengi sana kwenye soka, inaelekea Wizara bado haijaelewa ya kuwa soka ni siasa na ndio maana hata katika bajeti hakuna fungu lolote lililotengwa kwa ajili ya *Taifa Stars* na vilabu vinavyowakilisha Taifa.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya michezo bado tunalalamika ushuru wake ni mkubwa sana. Tunaomba Serikali isaidie ili angalau mipira na jezi kodi ipungue.

Mheshimiwa Spika, kuhusu riadha, Serikali itoe msukumo wa pekee kwani riadha imekufa sana. Iko haja ya kushirikiana na Ofisi za TAMISEMI ili kuendelea kuboresha michezo hasa mashuleni.

Mheshimiwa Spika, iko haja Halmashauri zikabanwa ili ile asilimia tano kwa ajili ya vijana itolewe ili vijana waweze kufanikiwa kwani vijana hawapati msaada wowote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni, tunapenda kuomba Wizara ianzishe mashindano ya Kitaifa hasa katika shughuli za utamaduni kama vile ngoma za asili, muziki wa dansi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari, Wizara katika sekta hii imelala kwani vyombo vya habari hasa magazeti mengi hayafuati weledi.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni ya muhimu sana kwa vijana wetu hata kwa jamii nzima. Tanzania haifanyi vizuri katika michezo sababu kubwa hatuna vifaa vya kutosha kwa michezo pia ufinyu wa bajeti ya Wizara. Vijijini vijana wanapenda sana michezo lakini hakuna Walimu wa Michezo, hakuna viwanja, hakuna mipira ya *football* na *netball,* ni tatizo kubwa kwa vijana wa vijijini na ushauri ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuwasomesha/kuwapeleka vyuoni Walimu wa Michezo ili tupate Walimu wa michezo wa kutosha;

(ii) Kuwa na bajeti ya kutosha kwa Wizara hii ya Habari na Utamaduni;

(iii) Kupeleka vifaa vya michezo katika kila Wilaya ili kuimarisha michezo kwa shule za misingi na kwa vikundi vya vijana Wilayani;

(iv) Michezo iimarishwe kuanzia Vijiji, Kata, Tarafa hadi Wilaya. Pia kupata makocha wa michezo ya mpira kwa kila Kata/Tarafa; na

(v) Elimu ya michezo itolewe mashuleni kama somo darasani ili kupata wataalam wengi vijijini.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara sasa ishuke mpaka vijijini ili kuimarisha michezo siyo kuangalia mijini.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichangie katika sekta ya habari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Watanzania wana haki ya kupata habari ya mambo/masuala mbalimbai ya Serikali yao na nchi yao kupitia vyombo mbalimbali vya habari na magazeti. Usikivu wa Tanzania *Broadcast Corporation (TBC)* ni mgumu sana na badala yake wananchi wa Ngorongoro wanasikiliza na kupata habari kutoka *KBC* ambayo usikivu wake ni mzuri sana. Naomba *TBC* iweke mitambo yake Loliondo mpakani na Kenya ili kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kwa vijana, hili ni tatizo kubwa sana kwa nchi yetu kwa sasa. Ukosefu wa ajira uliangusha Serikali kadhaa duniani. Lazima Serikali yetu kwa kushirikiana na sekta binafsi itafute ufumbuzi kwa tatizo hili kabla halijafikia kiwango kibaya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utamaduni (Vazi la Taifa), naomba kufahamu mpango wa kupata au kuwa na vazi rasmi la Taifa umefikia wapi na ni lini tutegemee vazi hilo lianze kutumika rasmi nchini Tanzania. Taifa lolote duniani linatambuliwa kwa mila zake, desturi zake, utamaduni wake, vyakula vyake, mavazi yake na kadhalika. Wamasai kwa mfano wamefanikiwa kuendeleza utamaduni wao kwa miaka mingi licha ya wimbi kubwa la tamaduni za Ulaya na Marekani.

**MHE. OMARI R. NUNDU**, Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, vijana wengi hawana ajira jambo linalowafanya wajiingize katika ujambazi na matumizi ya dawa za kulevya. Hata hivyo, michezo ni ajira na mingi yao ni ajira zinazolipa sana kama mpira wa miguu, hata hivyo uendelezaji wa vijana kwenye michezo hiyo inafanywa na vyama au jitihada za vijana wenyewe. Hii ni dhahiri kuwa uwezo na msukumo wao peke yao hautoshi kuweza kupatikana vijana wengi wa kuweza kupata ajira katika nafasi ya Kimataifa. Je, Serikali ina mipango gani ya kulivalia njuga suala hili kwa kulibeba

kikamilifu na pia ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa vipaji vya vijana wote vinakuzwa kikamilifu? Kwa nini Serikali isianzishe vituo vya mendeleo ya vijana?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Pamoja na pongezi hizi bado ninayo machache ya kuchangia ili kuboresha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, suala la vijana, nasikitika kusema kuwa Wizara hii haijawajali vijana kote nchini hasa kuwaendeleza kiuchumi. Umekuwepo Mfuko wa Vijana (mikopo) katika Halmashauri lakini fedha hii ilikuwa ni kidogo sana ukilinganisha na idadi ya vijana waliopo.

Mheshimiwa Spika, hitaji kubwa la vijana ni elimu ya ujasiriamali na mtaji wa uhakika kuanzisha biashara, huduma hii ni muhimu sana ishuke iwafuate vijana mahali walipo yaani vijijini na ngazi ya Kata. Mkakati wa makusudi ufanyike wa kutoa elimu endelevu kwa vijana wote katika vijiji vyetu vyote, pia Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya kutoa mikopo (mitaji) na mikopo hii iwe ni ya kutosheleza kuanzisha biashara zao iwe ya vikundi au hata mmoja mmoja na utaratibu wa urejeshaji mikopo hiyo uwekwe vizuri kwa maana ya kuajiri Maafisa Mikopo ya vijana wa Wizara watakaokaa kwenye kila Kata.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwe *serious* na suala la vijana kwani kuwasaidia vijana ndiyo njia pekee ya kuinua uchumi wa Taifa letu na kupunguza tatizo la ajira. Miradi ya vijana ni pamoja na uvuvi, kilimo, mifugo, useremala, ususi, bidhaa za vyakula, duka na kadhalika. Hivyo fursa ni nyingi sana kwa vijana wetu wa jinsia zote.

Mheshimiwa Spika, suala la michezo ni muhimu kwa Taifa lolote duniani, michezo ni afya, burudani, furaha na uchumi. Katika miaka ya hivi karibuni, michezo imeendelea kudorora katika nchi yetu. Michezo ya ngazi zote inashuka hata mpira wa miguu ambao unapendwa sana duniani. Tanzania inashika nafasi ya mia moja na kwenda juu duniani wakati nchi ya Uganda iko kwenye nafasi kati ya hamsini na sitini. Hivyo bado Tanzania tuko chini katika upande wa soka katika Afrika Mashariki. Ushauri wangu katika soka ni kwamba tuwekeze zaidi katika vijana wetu wa shule za msingi na sekondari kwa kujenga viwanja vizuri, vifaa vya michezo na Walimu wa michezo waliobobea.

Mheshimiwa Spika, pia ligi yetu ya Vodacom iongeze timu za kushiriki mara mbili kuliko ilivyo sasa ili kupanua wigo wa timu shiriki katika ligi ya Vodacom. Pia kombe la Taifa lililokuwa linashirikisha Mikoa yote liimarishwe zaidi ili kupata wachezaji wazuri wenye vipaji. Pia *TFF* na Wizara ijitahidi kupeleka vijana wadogo nje ya nchi kwenye shule za michezo ili wajifunze soka wakiwa bado wadogo. Vilevile mashindano ya shule, vyuo na taasisi mbalimbali yapewe uzito wa aina yake.

Mheshimiwa Spika, michezo si soka peke yake bali ni pamoja na riadha, ngumi, mieleka, *darts*, *chess*, bao na kadhalika. Hivyo, Serikali iweke mkazo katika michezo yote ikiwemo mpira wavu, pete na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Habari, ni lini Muswada wa Habari utaletwa hapa Bungeni ili Sheria ya Habari iweze kutungwa na kuondoa tatizo la makanjanja na matatizo mbalimbali yanayoikumba sekta hii ya habari na kuifanya iende na wakati?

Mheshimiwa Spika, kuhusu vazi la Taifa, tuambiwe ni lini vazi la Taifa litapatikana kwani limechukua muda mrefu. Sambamba na hili nauliza salaam ya Taifa ni ipi? Wengine wanaanza kwa kusema ‘Salaam Aleikhum au Tumsifu Yesu Kristo au Bwana asifiwe’. Tunataka tupate salaam moja ya Kitaifa. Wilaya yetu ya Karagwe tuna salaamu ya Wilaya isemayo, ‘Kiongozi Karagwe’ wananchi wanaitikia ‘Amani na maendeleo’. Je, salamu ya Taifa ni ipi? kama hatuna basi tutumie ya wananchi wa Karagwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake ya wataalam kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuzungumzia suala zima la michezo. Bado Wizara haijafanya kazi kubwa ya kuwaandaa vijana katika shule za msingi kwenye michezo ya riadha na mpira ili Tanzania iweze kupata vijana wazuri wa kushindana katika michezo ya Kimataifa kama michezo ya *Olympics*.

Mheshimiwa Spika, suala la utamaduni bado tuna changamoto ya kuimarisha utamaduni wetu kuliko vijana wetu kuendelea kuiga utamaduni wa Kimarekani. Sasa hivi Marekani inapata fedha nyingi sana kwa kuuza filamu za *Hollywood.* Vijana wa Kitanzania wameharibika sana kwa sababu ya filamu hizo za *Hollywood.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la habari, *it is light time* kwa Wizara kudhibiti vyombo vya habari ambavyo vinatoa taarifa za ajabu bila *ethics* zozote. Wanahabari wanatakiwa kujiendeleza katika tasnia ya habari ili wafikie viwango vya kimataifa. Wanatakiwa kusoma masomo ya uchumi, sayansi ya siasa na masomo mengine yatakayowawezesha kutoa ripoti za kitaalam.

Mheshimiwa Spika, suala la vijana, Wizara hii inatakiwa kushirikiana na Wizara ya Kazi katika kuwatafutia vijana ajira ili vijana waweze kujiajiri na waache kukaa kijiweni. Vijana wanahitaji kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali na kupatiwa elimu ya ujasiriamali pamoja na mikopo yenye riba nafuu. Vijana wasipokuwa *busy* ndipo wanajiingiza katika madawa ya kulevya.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuchangia eneo ambalo sijaona kama Serikali inalifuatilia. Wasanii wengi nchini ama kwa makusudi ama kwa kutokujua wamekuwa wakiiga mitindo ya wasanii wa Marekani ambao kwa bahati mbaya mitindo hiyo haikubaliki kwenye jamii nchini Marekani. Ombi langu kwa Serikali ni kutoa elimu kwa wasanii ambao wanaiga chochote kutoka Marekani hata kama hakifai kwa Wamerekani wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, katika dunia ya leo michezo sio tu ni ya kujenga afya na burudani bali ni *industry* ambayo inaongeza ajira, kujulikana kwa Taifa na pia kuongeza mapato ya Taifa husika. Hivyo nashauri kuwa wakati sera inatayarishwa ni vyema ikaangaliwa kidogo na sanaa kama *industry* inayoweza kuchangia pato la Taifa na kuinua vipaji vya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, michezo kuwa ya mfumo wa kikampuni, ili michezo iwe kama viwanda, ni vyema taaluma ya kuvifanya vilabu vikapenda kuwa Kampuni ikatumika, hii inaongeza nidhamu ndani ya vilabu, upatikanaji wa mapato ya uhakika na pia wachezaji kujua wajibu na haki zao, lakini zaidi kuipatia nchi mapato yatokanayo ya kodi mbalimbali kama ya kulipia mifuko ya jamii na kadhalika. Utaratibu huu utasaidia pia Mifuko ya Jamii kupata mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la kutambua vipaji, upo umuhimu wa kutambua vipaji mbalimbali katika ngazi ya *primary school* ili vipaji vya aina moja vipatiwe fursa za kuwa katika shule za aina moja. Utaratibu huu ni mzuri siyo tu tutatambua vipaji bali tutaamsha ari ya ushindani miongoni mwa vijana wetu, hivyo kujenga kiwanda cha vipaji vya aina mbalimbali kwa kuanzia shule za vipaji zikiwemo katika kila Mkoa husika, wataamua ni wapi shule ya vipaji yenye huduma zote za kimichezo zinaanzishwa. Ili kufanikisha lengo hili suala la kuandaa vijana wenye vipaji ni lazima maandalizi ya wakufunzi na wakaguzi yaandaliwe kwa umakini sana ili kusiwe na upendeleo wa uteuzi.

Mheshimiwa Spika, suala la habari, Taifa letu limepiga hatua kubwa kwa kuwa na vyombo vingi vya habari ni vyema sheria inayotawala vyombo hivi sasa ikawasilishwa Bungeni na pia

Taasisi zilizoundwa na Mabaraza ya Habari, wamiliki wa vyombo vikatambuliwa kisheria. Lakini nachukua fursa hii kuvipongeza vyombo vya habari kwa kazi nzuri wanayoifanya, waendelee kuwapa habari za uhakika na zisizo za upendeleo ama kwa vyama, mtu au kampuni fulani.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, natanguliza masikitiko yangu kwa vyombo vya habari vya Taifa, TV na Redio kutokana na kusababisha vifo vya Watanzania zaidi ya 120 na kwamba vyombo hivi vya Taifa vya habari, kama vile hapakutokea chochote, hawakuwa wakionesha matokeo ya ajali ile kwa siku mbili, ila pia walikuwa wakionesha vipindi vya ngoma kama vile hapakuwa na msiba wa Kitaifa, inasikitisha na tunajiuliza mengi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la habari la *TBC* linasikitisha pia kwamba linapata shida kubwa ya kukodisha Ofisi kwa ajili ya kufanya shughuli zao lakini pia kuna Wizara na Idara mbalimbali za Serikali zinadaiwa madeni makubwa na Shirika hili la *TBC* jambo ambalo linazidi kudhoofisha maendeleo katika shirika hili, naomba wadaiwa sugu hao wote walipe madeni yao.

Mheshimiwa Spika, majengo ya *TBC*, jengo la *TBC* pale Mikocheni, ilianzisha jengo kubwa la kisasa lililowekewa jiwe la msingi na mstaafu Mzee Mwinyi miaka 10 iliyopita na hadi leo imebaki katika hali ya gofu bila kumalizwa na huku *TBC* wakikosa eneo la kufanyika kazi. *NSSF* wako tayari kumalizia jengo hili ila wanahitaji tu garantii ya Serikali iil waweze kumalizia jengo hili, ukweli ni aibu kwani kwa nyakati za mvua Ofisi zinavuja na wanalazimika kujifunika miamvuli kama vile wanauza vocha za tigo katika vijiwe ni aibu kwa chombo cha Taifa kama *TBC*.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya digitali, nchi yetu ifikapo tarehe 31 Desemba, 2012 imeamua kuondokana na matumizi ya sasa ya analojia na kuingia katika digitali, si jambo baya lakini kwa sisi ni mapema sana na tumekurupuka hata kama huu ni msimamo wa Umoja wa nchi za Afrika Mashariki lakini jambo hili litawasononesha sana Watanzania kwani hata Mataifa makubwa duniani yaliyoendelea wao wamekubaliana mtindo huu uanze rasmi katika nchi zao ifikapo tarehe 31 Desemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, Watanzania ni maskini na wengi wamenunua vitivii vyao angalau wajiliwaze na kwamba miezi michache uwaambie basi, ni tatizo. Nauliza swali je, Tanzania imeshajiandaa kwa kiasi gani kuhusu suala la uharibifu wa mazingira utakaotokana na *TV* zenye mgongo ambazo zinaonekana hazitotumika tena kwa mtindo huo wa digitali?

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni, naomba niishauri Serikali sasa kwamba ichukue hatua za makusudi za kudhibiti utamaduni wa mavazi katika nchi yetu kwani jambo hili linaonekana kwamba hivi sasa hakuna tena nidhamu katika kuvaa, wanawake wanavaa mavazi ambayo hayaleti heshima kwa jamii kwani nguo wanazovaa ni za nusu uchi, zinabana sana, fupi zisizoficha maungo yao, wanawake kuvaa nguo za kiume, wanawake na mavazi katika ngoma mbalimbali lakini hata wanaume nao wanatutia aibu kwani wanathubutu kuvaa vidani shingoni, hereni lakini uvaaji wa suruali nusu tako, kusuka nywele na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inatembelewa na wageni mbalimbali na inatia shaka kwamba hata ile hoja ya ndoa ya watu wa jinsia moja iliyoletwa na David Cameroon, ilitokana na namna ambavyo alikuja kuitembelea Tanzania na akaona kuna mambo hayo ambayo yanaashiria kwamba wapo wanawake wanatamani wafanane na wanaume, lakini pia kuna wanaume wanatamani wafanane na wanawake.

Mheshimiwa Spika, suala la mavazi yasiyo ya heshima hivi sasa inaonekana ni jambo la kawaida hasa kwa wanawake, lakini na hata Serikali inaonekana kuridhia jambo hili na kuthubutu kumpokea na kumuonesha kama burudani kiongozi mwenye heshima katika nchi kama Rais wasichana waliovaa nguo za kubana na nyingine zinaficha tu matiti na zile sehemu za siri na huku tunashangilia, jambo ambalo linahamasisha ngono na kupelekea kuenea kwa Ukimwi na magonjwa mengine yatokanayo na zinaa. Serikali ikiamua, jambo hili litakoma kama ambavyo siku za nyuma tulipiga marufuku uvaaji wa suruali pana (Buga) na viatu vya raizoni na likawezekana na hili lipigwe marufuku na watakaovaa hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii kwanza kwa kuanza kuwapa changamoto Serikali, kwa kuwa idadi ya vijana kwa uwiano na watu kwenye nchi yetu ni kubwa (*populations*), vijana ni zaidi ya asilimia hamsini na vijana hawa ni zaidi ya asilimia sitini ya watu wote wasiokuwa na ajira Tanzania, licha ya takwimu hizi ambazo ni tishio kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu pamoja na ukuaji wa uchumi kwani kwa miaka mitano ijayo itakuwa ni nchi/Taifa la ombaomba.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara hii ambayo si tu muhimu katika kuendeleza tamaduni zetu, bali ichukue hatua kwa kushirikiana na Wizara nyingine zenye kuhusika na uwezeshaji wananchi (vijana) *in particulary* ili waweze kwanza kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana wote mijini na vijijini ili baada ya kutoa elimu vijana hawa wapatiwe mitaji ambayo itawawezesha kujishughulisha na shughuli za maendeleo, hii itapunguza wimbi la vijana wanaokaa vijiweni na hata wengine kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeshuhudia Taifa letu likiwa nyuma katika kujishughulisha na michezo ya aina mbalimbali, Tanzania tumekuwa tukijishughulisha na michezo ya mpira wa miguu na wa pete kwa kiwango kidogo na riadha pamoja na bondia tu, lakini tumekuwa hatushindi kwa maana ya kutoleta nishani yoyote ile, hii ni mbaya sana. Hii inatokana na kuwepo uhamasishaji duni wa watoto na vijana kujishughulisha na michezo kuanzia shule za sekondari hadi ngazi za juu na michezo ni mingi sana ambayo ingeendelezwa ingeleta tija kubwa kwa kutoa ajira kwa vijana wengi na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muhimu sasa kwa Serikali kuwekeza katika michezo mbalimbali kama tunavyoona Mataifa mbalimbali duniani yakifanya. Michezo ni moja ya sekta ambayo ajira yake inaleta kipato kikubwa sana kuliko fani na sekta nyingine nyingi na pia michezo ni afya kwani huimarisha mwili na kujikinga na magonjwa. Hivyo naomba Serikali itilie mkazo na kuchukua michezo kama chanzo kizuri cha kipato.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni kwa nini Wizara haiipi uzito wa kutosha *Twiga Stars* kama wanavyofanya kwa *Taifa Stars* kwani vijana hawa wa *Twiga Stars* wamekuwa wakifanya vizuri sana, lakini cha kusikitisha hawana hata Bima ya Maisha yaani leo wakipata ajali kama kuvunjika viungo inakula kwao. Pia hata wakiugua hujihudumia wenyewe, hii si haki kabisa, inabidi *Twiga Stars* wawe na bajeti yao na sio kuwa ombaomba mara watakiwapo kuwa kambini.

Mheshimiwa Spika, vilevile mkazo utiliwe na haki sawa kwa maana ya fungu liwepo katika CHANETA maana nao tumeshuhudia wakihangaika mara watakiwapo kuwa kambini, licha ya kuwa na ushindani mzuri ambao unalipa sifa Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilitaka kujua pato ambalo Wizara hii katika Idara zake mbalimbali imechangia katika pato la Taifa na limekuwa likipanda na kushuka kwa miaka mitatu (3) iliyopita. Je, nini vyanzo vikubwa vya pato hilo?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya hoja zangu, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja asilimia zote. Pili, napenda kufahamu ni hatua zipi Wizara inachukua kuhusu baadhi ya vyombo vya habari vyenye kuchochea na hivyo kueneza chuki katika jamii?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kila dalili ya mporomoko wa maadili katika jamii, je, Idara ya Utamaduni ina mkakati gani kukemea baadhi ya vijana wetu wanaodiriki wengine wakiwa viongozi kutoa lugha ya matusi kwa viongozi wetu? Huu utamaduni tunaiga kutoka wapi, hatuna tija asilani na chokochoko hizo zinakera wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la vazi la Taifa tumefikia wapi? Tunahitaji utambuzi wa Kitaifa kupitia viazi hili, ni utamaduni mzuri kuwa na vazi la Taifa na ni soko hata kwa watalii ili wajapo nchini wangependa kufanana nasi kupitia vazi, itakuwa biashara nzuri ndani na nje ya nchi. Vazi liharakishe ili nasi tujinafasi.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Baraza la Vijana, Azimio la Kitaifa lilikuwa mwaka 2006, hapa Bungeni tuliridhia mwaka 2011, je, utekelezaji wake umefikia wapi na mfumo wake utatufikia mpaka Igalula ili vijana wa Jimbo hili wafaidike pia?

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igalula ni kubwa kieneo, *TBC* ni chombo cha umma chenye manufaa makubwa katika nyanja za kilimo, afya, biashara na kadhalika. Nini mikakati ya Kitaifa ili *TBC* isikike nchi nzima?

Mheshimiwa Spika, nina vijana wengi wenye kipaji cha kucheza mpira wa miguu, nimebaini vipaji 20 kutoka Kata kumi Jimboni Igalula na kila wawili kwa kila Kata. Hii ni baada ya kushiriki *Mfutakamba Igalula Super League Cup* mwaka jana 2011. Naiomba Wizara itusaidie ili hawa vijana waje kufanyiwa majaribio timu B za *Yanga Sport Club, Simba Sport Club, Azam Sport Clup, Mtibwa Football Club na Ruvu Shooting Stars Football Club*.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni na Michezo, ni kioo cha jamii yoyote ulimwenguni. Katika ulimwengu wa sasa sekta hizi zimekuwa na mchango mkubwa katika ukuzaji wa uchumi na kuwa chanzo cha ajira hivyo ni muhimu Serikali ikatilia mkazo sekta hizi muhimu kwa kutenga kiwango kikubwa cha fedha ili kufanikisha malengo yake. Sote ni mashahidi jinsi watu wanavyopenda michezo ulimwenguni na hata hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sanaa pamoja na sekta zingine kwenye Wizara hii ni chanzo kikubwa cha ajira. Habari ni sehemu ya jamii na inayo mambo ya msingi ikiwemo kutoa burudani, kuelimisha na kuburudisha.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ya msingi na changamoto mbalimbali zinazotukabili sisi kama Taifa kuzitafutia ufumbuzi, ikiwa ni pamoja na uhaba wa ajira, mmomonyoko wa maadili miongoni mwa makundi ya kijamii. Ni kupitia Wizara hii nchi yetu inapata fursa ya kuyabaini na kisha kuyapatia ufumbuzi mambo mbalimbali ya msingi ikiwemo kuunda Wizara mahsusi kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa namna inavyojishughulisha na kuzisimamia Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara. Naipongeza Wizara pia kwa namna inavyosimamia maadili katika vyombo vya habari. Basi changamoto hizi ni vema na muhimu kuendelea na shughuli hii muhimu sana katika kuharakisha mustakabali na usalama na kujenga Taifa lenye misingi ya umoja na usalama.

Mheshimiwa Spika, ipo haja kwa Wizara kuhakikisha kuwa vyombo vya utangazaji hasa televisheni *TBC*, redio na magazeti yaweze kuwa kioo katika Tasnia ya Habari. Ni Wizara hii inayopaswa kuwa sekta kiongozi katika kuweka mambo sawa na kuliwezesha Taifa kuwa na sekta ya utangazaji utakaowafanya Watanzania kuwa wamoja zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nizungumzie juu ya uteuzi wa wachezaji wa Timu yetu ya Taifa. Uteuzi wa wachezaji wa mpira wa Timu ya Taifa *(Taifa Stars)* bado ni mbovu, tumelalamika katika *budget* iliyopita, tulisema hayohayo kuwa timu ya Zanzibar yaani wachezaji wa mpira hawateuliwi kuchezea *Taifa Stars*. Mwaka jana Waziri alisema jambo hili atalipatia ufumbuzi, je, kwa nini mpaka leo hii Mheshimiwa Waziri hajalipatia ufumbuzi? Je, wachezaji wa timu za Zanzibar hawana sifa za kuchezea timu ya Taifa? Naomba Mheshimiwa Waziri unipatie majibu ya kuniridhisha utakapokuja kufanya majumuisho.

Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha za *FIFA*, siku nyingi tunalalamika kuhusu fedha ambazo tunapewa Tanzania lakini pesa zote huchukua *TFF* na *ZFA* hawapewi na hizi pesa zinakuja kwa Tanzania na kila siku tunalalamikia lakini Waziri alisema atalipatia ufumbuzi. Hivi karibuni nilisikia

kwenye vyombo vya habari tayari hizo pesa kwa mwaka huu wameshapewa, je, ufumbuzi umeshapatikana na je, wamepata kiasi gani na *TFF* wamepata ngapi na *ZFA* wamepata ngapi?

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko makubwa na Wizara ya Michezo wakati Taifa limepata msiba mkubwa na Taifa limetoa siku tatu za maombolezo lakini bado Wizara ya Michezo imeshindwa kuahirisha mpira wa kombe la Kagema (Kagame *Cup*). Je, huu msiba nyinyi Wizara ya Michezo haukuwagusa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanja vya michezo, kule Zanzibar tunacho kiwanja cha kuchezea mpira wa miguu na kiwanja chenyewe ni kikubwa sana tu (Amani) lakini mpaka leo hii sijaona kuchezewa na Timu ya Taifa *(Taifa Stars)* wanapocheza na Timu za nje na hii Wazanzibar wanakosa fursa ya kuona michezo hiyo. Nakuomba Mheshimiwa Waziri ulione hili na ulipatie ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, suala la habari, vyombo vya habari vimekuwa na uhuru mkubwa si vibaya lakini vimekuwa na upotoshaji mkubwa, baadhi ya vyombo vya habari havifanyi utafiti kabla hawajatoa habari na hii inapelekea kutoa habari za uongo. Lengo la Serikali kuwapa uhuru vyombo vya habari sio kutoa taarifa za uongo na za uchochezi, je, Serikali iko wapi? Naomba Serikali ifuatilie hivi vyombo vya habari na pia magazeti ambayo hayana maadili yafungiwe haraka bila kujali ni ya nani.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukipongeza chombo cha Serikali cha *TBC* ambacho kimekuwa makini wakati wa kutoa habari.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru Mungu kwa kuniwezesha kuiona siku hii ya leo ambayo Wizara hii inapowasilisha bajeti yake nami niweze kutoa mchango wangu kidogo ili kuboresha Wizara hii muhimu ambayo inaweza kupunguza kwa sehemu tatizo la ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la bajeti ndogo ya Wizara hii. Kama nilivyoanza kusema kwamba hii ni Wizara muhimu sana, nina imani kubwa Wizara hii ikipewa bajeti ya kutosha na ikatumika kama ilivyopangwa, tutaweza kuondoa tatizo kubwa la ajira kwa vijana kwa sababu kuna sekta nyingi ziko chini ya Wizara hii mfano, michezo, utamaduni na nyingine nyingi ambazo vijana wanaweza kushiriki kwa wingi na kuondoa tatizo hili la ajira.

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo kwenye sekta ya habari, ni muda mrefu sana umepita toka Serikali iseme italeta Muswada wa Habari hapa Bungeni. Napenda kujua sasa ni lini suala hili litafikishwa hapa Bungeni? MUswada huu naamini utapunguza matatizo mengi yanayojitokeza kwa sasa kwa upande wa vyombo vya habari, wamiliki wa vyombo vya habari na wanahabari wenyewe.

Mheshimiwa Spika, yapo mawazo ya wadau wanaopendekeza kuwe na sheria mbili tofauti yaani Sheria ya Haki ya Kupata Habari na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari. Je, Serikali inasema nini juu ya mapendekezo hayo ya wadau wa habari? Naamini sheria hizi zikiwepo zitasaidia sana kuvisimamia vyombo hivyo, waandishi na hata wale ambao wanatakiwa kutoa habari, pia itawasaidia waandishi wetu kuweza kulipwa vizuri kuliko ilivyo sasa wanalipwa fedha kidogo sana na kusababisha taaluma hii kupoteza hadhi yake na kufanya watu wenye fedha na wanasiasa wachache kutumia vyombo hivi vibaya.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia suala la vazi la Taifa. Ni miaka 50 sasa toka nchi yetu ipate uhuru hatuna vazi la Taifa hili. Jambo hili halipendezi kwa Taifa letu. Suala hili limechukua muda mrefu sana, sasa lifikie mwisho kwa sababu ni aibu kuvaa mavazi ya watu wengine hasa katika sherehe zetu za Kitaifa na hata siku hii ambayo Wizara hii inawasilisha bajeti yake leo hapa Bungeni kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 21 ameelezea mchakato wa kupata kitambaa umekamilika, tunaomba sasa utaratibu huo ambao uko kwenye hatua za mwisho uwe mwisho kweli ili tuweze kuwa na vazi letu la Taifa.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo suala la utamaduni wa Mtanzania, jinsi siku zinavyozidi kwenda utamaduni wetu unazidi kupotea, vijana wetu ndiyo kabisa badala ya kukuza utamaduni wetu wao wamekuwa wakiiga utamaduni toka nje na hii inachangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa maadili ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, Sekta hii bado ina kazi sana ya kutoa elimu si tu kwenye vipindi vya redio na *TV* tu kuna kila sababu kwenda zaidi ya hapo kwenye mashule, vyuo na kwenye makundi ya vijana na hata wazazi ikibidi maana hali kwa sasa ni mbaya.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na viongozi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ilete Sera ya Michezo haraka ili vijana wetu wajihusishe zaidi kwenye michezo kama ajira na afya kwani kwa kukosa hilo, tutapoteza nguvukazi kwa vile watajihusisha na ulevi na uzinzi na hivyo kupata maradhi kama Ukimwi. Halmashauri za Wilaya ziweke bajeti ya michezo na kila Kata ipate mgao kwa ajili ya kuendeleza michezo.

Mheshimiwa Spika, magazeti ya siku hizi mengi yamepoteza kazi ya msingi ya kuhabarisha na badala yake wako kibiashara zaidi na kuwadhalilisha watu wengine ili waweze kuuza magazeti. iletwe sheria kali na Wizara iwasimamie ikiwa ni pamoja na kuwafungia waandishi wanaokosa maadili na vyombo vinavyochapisha magazeti yasiyofaa kwa umma.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji hasa Redio haisikiki nchi nzima hasa Mikoa ya Iringa na Njombe. Wizara ifanye kila linalowezekana ili redio ya Taifa isikike nchi nzima ikiwa ni pamoja na televisheni.

Mheshimiwa Spika, suala la wasanii na utamaduni lisichakachuliwe ni kuiga tamaduni za kigeni. Pia wasanii kama *Comedy* kwa wanaume kubadili mambo na kuigiza kama wanawake hii si sawa, kuwe na namna ya kuwakagua (*regulate*) kabla ya *public performance*.

Mheshimiwa Spika, bado sijaona Wizara hii kama ina mipango yoyote ya kuendeleza vijana, tunahitaji kuwa na bajeti yao na ifike kila Kijiji au Kata ambako vijana wako na shughuli zinapangwa kufanywa na Wizara kwa maendeleo ya vijana iwe wazi (*transparent*) na sisi Wabunge tuelezwe ili tukirudi majumbani tukawaeleze kwani hayo huwa ni maswali yao kila tunapofanya ziara.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya kusimamia sekta hii. Pamoja na pongezi, nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya vijana, moja ya changamoto kubwa Kitaifa ni ukosefu wa ajira kwa vijana. Tatizo hili haliwezi kutatuliwa na Wizara pekee, ni suala/tatizo mtambuka. Vijana sharti wawekewe programu maalum ya kuwawezesha kujiajiri/kuajiriwa. Wizara ishirikishe *VETA*, Wizara ya Uwezeshaji, Kilimo, Biashara na TAMISEMI ili kwa pamoja kuweka utekelezaji wa programu ya kupanua ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanja vya michezo, viwanja vingi vya michezo vinamilikiwa na CCM, kutokana na historia ya nchi yetu, hili sio kosa kama baadhi ya watu wanavyohoji. Historia ni historia, sio rahisi kuifuta! Hapa Wizara itakapounda Wakala wa kusimamia viwanja vya michezo ufanyike utaratibu wa wakala kuingia ubia na wamiliki wa viwanja (kama CCM) ili washirikiane kuviendesha na kuvikarabati.

Mheshimiwa Spika, aidha wafadhili wa michezo (*sponsors*), hivi sasa wafadhili wao unaishia kutoa vifaa vya michezo na posho za wachezaji na viongozi wao. Ni vema waelekezwe ili sehemu ya fedha hizo zielekezwe kukarabati viwanja kwani viwanja ni sehemu muhimu ya maendeleo ya michezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo mashuleni, Serikali imechukua hatua sahihi kurejesha michezo hiyo mashuleni na mashindano ya UMISHUMTA/UMISETA kwani mchezo ni sehemu muhimu ya malezi ya watoto na ni maandalizi ya kupata vipaji vya kukuza mchezo nchini. Tatizo lililopo ni kwamba mashindano hayo yamerejeshwa bila bajeti. Wizara iratibu suala hili ili ishirikiane na Wizara ya Elimu, TAMISEMI na sekta binafsi kuhakikisha fedha zinapatikana kuendesha mashindano mashuleni. Michezo inaleta heshima ya Taifa, inakuza mapato ya Taifa na pia ni ajira ya uhakika ya vijana, kwa hiyo ni vema tuwekeze.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH**: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi nami kuchangia hoja ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri, Naibu Wazri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara hii ni makubwa na muhimu kwa vile yanagusa wananchi wote wa Tanzania. Ninasema wote kwa sababu Watanzania wote tuna tamaduni zetu, wote tunaongea Kiswahili, vijana ni asilimia kubwa ya Watanzania na watoto na vijana wengi na hata wazee wanashiriki katika michezo. Kazi ya kuhabarisha jamii ni jambo moja muhimu katika kukuza uelewa wa watu kuhusu mambo mbalimbali yanayotokea nchini na duniani kote. La kushangaza ingawa Wizara hii ina majukumu hayo makubwa lakini bajeti yake ni finyu. Ninaiomba Serikali katika mwaka ujao bajeti ya Wizara hii iongezwe na iendelee kuongezwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lugha ya Kiswahili, Watanzania tunajivunia kuwa tunayo lugha inayo tuunganisha sote, ni lugha inayounganisha Watanzania kama watu wa Taifa moja. Lugha yetu ni lazima iendelezwe na ipanuliwe na tuimiliki sisi wenyewe Watanzania kwa sababu zimejitokeza nchi zinazojifanya kuwa ndio wamiliki wa lugha ya Kiswahili na hata kutoa Walimu wengi wa kufundisha katika taasisi za nje. Serikali ijipange vizuri kutayarisha Walimu wa Kiswahili ili Tanzania ndio iongoze katika kutoa Walimu kufundisha nchi za nje na hata kutoa Wakalimani na si nchi nyingine zozote.

Mheshimiwa Spika, michezo ya asilia ifufuliwe, kama ile michezo ya bao, mbio za magunia, mashindano ya kukuna nazi kwa yale maeneo yanayotumia nazi zaidi mfano Zanzibar na Dar es Salaam, Mkoa wa Pwani na kadhalika. Michezo hii sasa imeanza kusahaulika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana na ajira. Vijana wengi wamelundikana mijini na vijijini bila ya kujishughulisha na kazi za kujipatia kipato. Vijana walio wengi wanaendelea kuwa tegemezi kwa wazazi wao ingawa wazee wenyewe nao hawana uwezo kifedha na wengine wana umri mkubwa. Vijana wa aina hii ni rahisi kurubuniwa na watu wabaya kufanya vitendo viovu visivyokubalika Kitaifa na kijamii. Mfano kusafirisha na kuuza madawa ya kulevya, kufanya vurugu mbalimbali zinazohatarisha amani ya nchi yetu, wizi na mambo mengi maovu.

Mheshimiwa Spika, vijana wanapokuwa wamekata tamaa ni hatari. Hivyo Serikali isimamie na kutekeleza mikakati ya ajira kwa vijana kama ilivyopangwa. Ianze kwa kuwatambua vijana maeneo waliko na idadi yao. Mitaala ya elimu ya ujasiriamali iandaliwe kulinga na maeneo (mazingira ya maeneo mbalimbali) mafunzo ya wakufunzi *(TOT)* yatolewe katika maeneo husika ili iwe rahisi kwa vijana kufikiwa (ni vema ikawa katika ngazi ya vijiji au mitaa).

Mheshimiwa Spika, kwa vile kuna tatizo la kuibua miradi (*business creation*) katika eneo moja utakuta kuna miradi inayofanana maana yake miradi ya kukopiana ambayo haina tija kubwa kwa maana wenye miradi ile wanagawana wateja walewale wa maeneo yaleyale. Hivyo wasaidiwe kuibua miradi tofauti ambayo ina soko katika maeneo yao. Aidha, michanganuo ya miradi hiyo iandaliwe na vikundi tofauti viamue ni mradi upi wangependa kuuendesha.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kuwaelimisha vijana wa vijijini kushiriki katika kilimo. Sio vijana wote wanachukia kilimo kwa madhumuni ya kuchukia tu, bali wanakichukia kutokana na

ugumu wa kazi hiyo, hakuna kijana ambaye atakuwa tayari kulima kwa jembe la mkono, bila ya pembejeo na hatimaye asipate mavuno yoyote iwe nguvu zake zimepotea bure.

Mheshimiwa Spika, mikakati madhubuti iandaliwe ya kuwawezesha vijana kushiriki na kupenda kazi za kilimo kama:-

(i) Vijana katika maeneo yao wapimiwe maeneo ya kilimo na wapewe hatimiliki;

(ii) Wapatiwe matrekta hata kama ya mikopo (kupitia vikundi vyao);

(iii) Wakopeshwe pembejeo (ikiwemo mbolea, mbegu bora na kadhalika);

(iv) Utaalam wa kilimo bora (kupitia Maafisa Ugani waliomo katika maeneo husika);

(v) Miundombinu ya umwagiliaji (hata kama ni *scheme* ndogondogo za kumwagilia kutokana na vianzio vya maji vilivyomo katika maeneo hayo); na

(vi) Miradi ya kuanza nayo ni ile inayoleta mrejesho wa mapato harakaharaka, yenye soko kubwa, mfano, mbogamboga, matunda, maua, ufugaji wa kuku wa kienyeji na mengine kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwapatia taarifa ya masoko vijana kwa ajili ya miradi yao ipewe kipaumbele ili waondokane na kulundika bidhaa zao bila ya kuuzwa jambo ambao linavunja moyo na kuondoa ile morali ya kuendeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifuko ya uwezeshaji kwa ajili ya vijana, ninaipongeza Serikali kwa azma yake nzuri ya kusaidia na kuendeleza vijana kwa kuanzisha mifuko mbalimbali ya kuwapatia mitaji vijana. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa mifuko hiyo haijawanufaisha walengwa ambao ni vijana. Vijana walio wengi wanalalamika kushindwa kujiajiri wenyewe kwa kuanzisha miradi kwa kutokuwa na mitaji. Hivyo Serikali ipitie upya taratibu zake za kutoa mkopo kwa vijana kutoka mifuko hii. Aidha, iharakishe uanzishaji wa Benki ya Vijana ambayo itatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana ili vijana wengi wanufaike.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI**: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa Waganga Tiba Asili, Tiba Mbadala hawa wanapitia Wizara ya Afya lakini katika Mikoa mingi huwa Afisa Utamaduni wanawalipisha hati za kuwatambua wakati Wizara ya Afya inawasajili na kuwapa cheti cha kuwatambua. Sasa naomba Wizara itamke kuwa wao wanawajibika wapi?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na usumbufu sana kwa Waganga wa Tiba Asili, kila kukitokea mauaji wanahusishwa Waganga wa Tiba Asili. Serikali ina mpango gani wa kufuta kauli potofu wanazopewa Waganga hawa ili wapewe heshima kama waganga wengine wenye fani zao?

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itamke rasmi kwamba tiba asilia wapo Wizara ya Afya na Afisa Utamaduni wasiwasumbue waganga walioko vijijini ila waelekezwe Wizara ya Afya.

**MHE. NAOMI A.M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema hadi kuweza kuchangia kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kidogo tu lakini muhimu sana. Nasikitishwa sana na tafsiri finyu ya utamaduni. Utamaduni unamaanisha jumla ya maisha ya mtu. Ni muhimu kabisa unapozungumzia utamaduni, moyo wake ni uhai wa Taifa, maana yake anavyoishi, anavyoweza kuendesha maisha yake, je, huyu binadamu anakula vipi, anajipatiaje chakula, mavazi, *shelter* (malazi) na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, katika kuzungumzia utamaduni, ingefaa tuzame zaidi katika maisha halisi ya vijana. Tujiulize utamaduni wa vijana kutopenda kufanya kazi, vijana kupenda maisha rahisi ya kukaa vijiweni na kusindikiza jua hadi linazama. Utamaduni wa kupendelea kazi za kuajiriwa tu au kuombaomba je, tunazalisha kizazi cha aina gani? Hivi kweli tunajenga kizazi cha aina gani?

Mheshimiwa Spika, pia elimu ndiyo nyenzo kuu ya kujenga utamaduni wa Taifa. Jambo hili hufanikiwa kupitia vitabu vinavyosomwa na vijana ambavyo vingi vyake vinakuwa kwenye mitaala, lakini vitabu hivi mfano "*Things Fall Apart, The Centre Cannot Hold by* Chinuo Achebe na kadhalika vilikuwa na mafundisho mazuri ya ujasiri, kuthamini kufanya kazi kwa bidii na kadhalika. Siku hizi vitabu hivi havitiliwi mkazo. Ingekuwa vizuri kuvirudia na kuvipa umuhimu katika kukazia tabia njema ya vijana katika ujenzi wa Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, mwisho napendekeza tuache mzaha na suala la utamaduni yale yote niliyoyaulizia hapo juu tuyafanyie tafakari na kurekebisha popote pale tunapolegea, wakati ni huu.

Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo napendekeza yafuatayo:-

(i) Wizara iimarishe Baraza la Kiswahili Tanzania;

(ii) Jitihada zifanyike za kuimarisha michezo katika Majimbo kwa kuwahimiza Wabunge wachangie michezo;

(iii) Halmashauri za Serikali za Mitaa, Manispaa na Majaji wachangie mifuko ya michezo; na

(iv) Wizara ihimize kufundisha wazalendo.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari kwa asilimia 90 hufanya kazi maeneo ya mijini. Kwa takribani miaka yote tangu tupate uhuru, vyombo mbalimbali vya habari hususan televisheni, redio na magazeti vimekuwa vikiripotiwa taarifa mbalimbali za habari kwenye maeneo ya mijini hususan majiji makubwa kama vile Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Tanga na kadhalika hali ambayo inaonyesha kuwatenga sana wananchi wa vijiji ambako kuna matatizo makubwa sana kuliko mjini kama vile mauaji ya vikongwe na Albino, manyanyaso ya wanawake, yatima, njaa, magonjwa, umaskini uliokithiri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivyo kwa kuendelea kufanya hivyo kunapelekea nchi yetu kuendelea kushindwa kuyapatia ufumbuzi wa kudumu matatizo haya kwa kuwa yamekuwa hayapatiwi uzito wa kutosha kama inavyofanyika kwa matatizo ya mjini. Hivyo basi, tunaomba kufahamu mkakati wa kudumu wa Wizara utakaohamasisha vyombo vya habari kwenda maeneo ya vijijini kubainisha changamoto mbalimbali na kuzipa uzito kama inavyofanyika katika maeneo ya mijini.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, utamaduni ni utambulisho wa Taifa lolote duniani. Kwa muda sasa kumekuwepo na mchakato na harakati ya wadau mbalimbali kupiga vita kile kiitwacho mila potofu. Hili ni jambo jema na linapaswa kuwa endelevu kwani bila kufanya hivi maendeleo ya kweli hayatafikiwa na pia baadhi ya ndugu zetu wataumia mfano *Albino*. Juhudi hizi za kutokomeza mila potofu hapa nchini kwetu ziende sambamba na juhudi za kupiga marufuku mila na tamaduni za kigeni zilizo mbaya.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na kasumba mbaya miongoni mwa Watanzania walio wengi kuwa mila zetu ni potofu wakati huo huo wakishabikia tena kichwa kichwa mila potofu za kigeni, mfano wanaume kuvaa hereni na kadhalika. Ni lazima kujitambua kama Taifa ili tusije kupoteza mila zetu zote na kupokea za kigeni bila utaratibu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Kiswahili ni utambulisho halisi wa Tanzania, kuna maeneo hatufanyi vizuri na kupelekea Taifa kama Kenya kufanya vizuri kuliko sisi. Eneo mojawapo ni la uchapishaji hasa suala zima la urasimu. Jambo hili limesababisha waandishi wengi wa Kiswahili kukwama. Serikali ifuatilie hili na kuamuru vyombo husika kuondoa urasimu wa uchapishaji ili kuhamasisha waandishi wengi kuchapisha makala za Kiswahili, Kenya wameweza, kwa nini sisi tushindwe?

Mheshimiwa Spika, mpira wa miguu hapa Tanzania umekumbwa na kasumba hasi ya kuabudu makocha toka nje na kuwadharau wazalendo. Jambo hili halileti afya na ni lazima tujiulize ni wapi wamejikwaa au mdudu gani anatutafuna kufikia hatua hii ya kujidharau. Wizara ifanye utafiti na kuweka wazi matokeo, ili sisi kama Taifa tujifahamu udhaifu wetu wa kuwainua wageni huku tukijikandamiza.

Mheshimiwa Spika, ili vijana wahamasike kimichezo ni lazima maeneo ya wazi yatengwe kwa kiasi cha kutosha ili watoto wadogo waanze kutumia maeneo hayo kimichezo. Kwa hakika samaki mkunje angalli mbichi, vijana wetu wakipewa fursa hii ya maeneo ya wazi toka wakiwa wadogo watajijenga kimwili na kisaikolojia, kimichezo na baadaye kupata wachezaji wazuri. Tatizo lililopo sasa ni kutokuwa na maeneo ya wazi na wahujumu wakishirikiana na watumishi wasio waaminifu. Napendekeza Wizara ipewe maeneo ya wazi iweze kuzitunza na kuendeleza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilileta Bungeni Muswada wa Sheria ya Vyombo vya Habari kwenye Bunge la Tisa, Muswada ulirudi Serikalini ili ufanyiwe kazi zaidi. Sasa hivi ni karibu miaka minne imepita na Muswada bado haujaletwa Bungeni. Naiomba Serikali iharakishe kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, miaka ya sitini na sabini Tanzania ilikuwa inang'ara sana kwenye medani ya michezo katika ukanda huu. Ni katika michezo yote, sababu kubwa ni kuwekeza kwenye michezo tangu shule za msingi mpaka juu kwa sababu ambazo hazieleweki Serikali imeacha kuwekeza kwenye michezo kuanzia kwenye shule za msingi. Naiomba sana Serikali irudishe haraka uwekezaji kwenye shule za msingi na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu ilifanya vizuri sana kujenga uwanja wa michezo mkubwa na mzuri sana pale Dar es Salaam. Uwanja huu pia utasaidia kuboresha michezo nchini hasa kutokana na mapato yatokanayo na viingilio kwenye uwanja huo. Bahati mbaya sana mpaka sasa uwanja hauna mashine za kuhesabu na kukagua tiketi! Bei ya mashine hii haizidi dola 30,000 kwa nini mashine hiyo hainunuliwi? Au kwa nini Serikali kupitia *TFF* haiweki Wakala wa kujitegemea wa kudhibti mapato ya viingilio.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote na Wizara kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana katika kuinua vipaji vya watoto, kujenga uwezo wa watoto kitaaluma, kielimu na kimichezo. Wizara hii pia inaweza kusaidia vijana wengi sana kwa ajira katika fani mbalimbali kama sanaa na muziki.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini bado Wizara hii haijaweza kufanya kazi kwa ufanisi na hivyo kusaidia vijana wengi kuwa na uhakika wa ajira za kudumu kupitia michezo sanaa na muziki. Vijana wengi waliojiajiri kwenye fani hizo wana hali ngumu ya maisha kwa sababu kipato ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma Serikali ilidhamiria sana kulipa uzito suala la michezo mashuleni kuanzia *primary school,* shule zote zilikuwa na vifaa vya kutosha vya michezo yote na hata kwenye mitaala na ratiba za masomo michezo ilipewa nafasi. Hili lilisaidia sana watoto kuimarika kitaaluma, nidhamu na kiakili pia.

Mheshimiwa Spika, japokuwa sasa Serikali imeona umuhimu wa kurudisha michezo mashuleni, suala la uwezeshaji wa fedha bado halijatekelezwa na hivyo kubakia kuwa kwa nadharia zaidi kuliko matendo. Serikali ilieleze Bunge ni kiasi gani cha fungu la pesa limetolewa kwa kila shule, hapa nchini kwa lengo la kuendeleza michezo ya watoto mashuleni.

Mheshimiwa Spika, wapo wanamuziki ambao uvaaji wao unakiuka maadili ya Taifa letu, pia wanatoa picha mbaya kwa watoto na jamii kwa ujumla. Serikali ieleze Bunge ni mikakati gani imeandaliwa kwa wanamuziki hasa wa kike waheshimu maadili ya Taifa letu na kulinda heshima ya wanawake wa Taifa hili. Ni adhabu gani inatolewa kwa wanamuziki wanaovaa kinyume na maadili ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iandae *programme* maalum wa kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana vijijini na mijini na wakishapata elimu wawezeshwe mitaji ya kuanzisha miradi ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifuatilie mashamba yaliyotelekezwa na wawekezaji katika maeneo mbalimbali yarejeshwa Serikalini, vijana waunganishwe waanzishe vikundi vya kilimo cha kisasa kwenye mashamba hayo. Vijana wetu wanazurura mitaani wanajiingiza kwenye makundi ya ulevi na uvutaji madawa ya kulevya kwa sababu ya kukosa ajira rasmi.

Mheshimiwa Spika, masomo ya sanaa za mkono yarudishwe mashuleni kama ilivyokuwa mwanzoni mwa miaka ya themanini, somo la sanaa liliwezesha watoto kufikiria kuwa watafiti na hivyo kuinua na kujenga vipaji vyao.

Mheshimiwa Spika, viwanja vya michezo kwenye makazi ya wananchi vimevamiwa vyote na matokeo yake watoto wanachezea mipira barabarani. Kwanza hii ni hatari kwa maisha yao kwani wanagongwa kila leo na baadhi yao kuuawa. Lakini pia kitendo cha kubadili matumizi ya viwanja vya michezo ni kuwanyima watoto haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kushindwa kuwezesha timu yetu ya wanawake ya Twiga *Stars* kikamilifu na hivyo kusababisha Mama Tunu Pinda kuomba misaada kwenye vyombo vya habari, hii ni aibu kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, tunawakatisha tamaa wanawake hawa waliojitoa kupeperusha bendera yetu ya Taifa, iweje Serikali tuweze kuleta makocha kutoka nje na kulipwa vizuri *then* tushindwe kuwezesha timu moja ya wanawake kuweza kufanikisha mipango yao na hivyo kusonga mbele.

**MHE. ABDUL J. MAROBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. Pamoja na kuunga mkono bado kuna changamoto nyingi ambazo Wizara inatakiwa izitafutie ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo inayowahusu vijana ambao ni zaidi ya asilimia 50 ya idadi yote ya Watanzania, mpaka sasa Wizara haijaweza kuweka *programu* za namna ya kuwakusanya na kuwaunganisha vijana katika ngazi mbalimbali. Shughuli hizi kwa kiasi kikubwa zinafanywa na Vyama vya Siasa badala ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna mtumishi maalum (*specific)* anayeshughulikia kuratibu mipango ya vijana na badala yake katika Halmashauri zetu vijana hawa wanasimamiwa na Afisa Utamaduni ambaye hana fungu lolote la kumwezesha kufanya kazi hiyo kubwa. Pamoja na kutokuwa na Afisa Vijana Wilaya, pia katika ngazi zote za utawala kwa maana ya Kata na Vijijini hakuna afisa yoyote anayeratibu shughuli za vijana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na pengo hilo ni vizuri Serikali kukaa na kuona umuhimu wa kuwa na Afisa Vijana badala ya Afisa Utamaduni, ambaye kazi yake kubwa ni kuratibu mambo yanayohusu vijana. Kwa kufanya hivyo, vijana watakuwa na kila sababu ya kuipenda nchi yao

kwani watakuwa kitu kimoja. Kwa sasa vijana wamegawanyika kutokana na itikadi zao za Kivyama.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili ni suala zima la michezo. Kwa miaka mingi nchi yetu inaonekana haileti ushindani katika mashindano mengi ya Kimataifa, badala yake tunakwenda kushiriki tu. Hali hii si nzuri haya yote ni matunda ya kuacha mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA kwa kuwa UMITASHUMTA na UMISETA imeanza, ni vizuri Wizara hii ishirikiane bega kwa bega na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na TAMISEMI ili kuyaendeleza mashindano hayo ambayo ndio msingi wa vipaji vya wanamichezo wote.

Mheshimiwa Spika, pia kupitia mashindano hayo, vijana watakaoonesha vipaji Serikali kupitia Wizara hii iwachukue kwa kuanzisha *Academic* ili kukuza vipaji vyao na baadaye waweze kuwa wachezaji wazuri watakaowakilisha nchi yetu *academy* hizi zinatakiwa ziwe katika michezo yote na si mpira wa miguu pekee kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, naishukuru tena *TFF* kwa kukubali kuandaa kwa mara ya tatu mfulullizo mashindano ya klabu Bingwa, Afrika Mashariki na Kati pamoja na kuwa na timu nyingi kushiriki hasa za Tanzania na mara nyingi timu zetu zinachukua ubingwa huo, lakini timu hizo hazioneshi viwango vizuri vya kukua kwa mpira wa miguu na badala yake kubebwa na watazamaji tu kwa maana ya washabiki.

Mheshimiwa Spika, hebu tujiulize tangu mashindano hayo yaanze ni mara ngapi timu zetu za Tanzania zimechukua ubingwa nje ya Tanzania? Ni vizuri kwa hali tuliyokuwa nayo sasa mashindano hayo yafanyike nje ya Tanzania ili tuweze kujipima viwango vyetu tukiwa hatuna mashabiki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa Taifa letu la Tanzania, kwa kuwa Wizara hii ina nafasi kubwa ya kuwaandaa vema vijana wetu kwa kuwaandalia mipango mizuri ya michezo mbalimbali kuanzia shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, kuwaanda vijana mashuleni kutasaidia sana kuwafanya vijana wasipate nafasi ya kuzurura na kujifunza mienendo mibaya iliyoko mitaani.

Mheshimiwa Spika, napenda Wizara itoe uwezeshaji wa fedha na vifaa vya michezo kwa shule mbalimbali hususan katika Mikoa ambayo inaongoza kwa michezo.

Mheshimiwa Spika, tunayo historia ya wachezaji wa mpira wazuri kutoka Mkoa wa Kigoma, hivyo ni wakati muafaka kuwekeza huko na kuwaandaa vijana wa Mkoa wa Kigoma walioko mashuleni kwa lengo la kupata wachezaji wazuri wa baadaye kama akina Kaseja mdakaji anayetegemewa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni vema kwa sasa Serikali itoe agizo kwa kila Halmashauri kujenga viwanja vya michezo ili kuwaunganisha vijana kutoka katika vijiji mbalimbali na kutambua vipaji na wachezaji wazuri na kuwapandisha hadhi katika mazoezi.

Mheshimiwa Spika, Wizara iziwezeshe Idara ya Utamaduni katika Halmashauri ikiwa ni pamoja na kuwapatia vitendea kazi kama vile pikipiki, gari na kadhalika ili idara iweze kupanga ratiba ya kuzunguka vijijini na kutoa miongozo mbalimbali juu ya kukuza michezo na tamaduni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa fursa kuchangia leo hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza Wizara hii muhimu na kiunganishi cha wananchi wenye vitengo muhimu kabisa kama Habari, Utamaduni, Michezo na Vijana. Naomba sasa nichangie kwa kila sekta:-

Mheshimiwa Spika, habari ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi yetu, sekta hii inakabiliwa na changamoto nyingi, pamoja na uhuru mkubwa wa kuandika na kutoa maoni, nashauri elimu zaidi itolewe na sheria juu ya uhuru huu kuendelea kutolewa kwa waandishi wa habari, wenye kumiliki vyombo vya habari na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni wanahabari wengi zaidi ya asilimia 70 wako mijini na kutangaza au kutoa habari za mijini tu wakati kuna habari nyingi na matukio mengi vijijini. Pia habari za vijijini zikitolewa zinakuwa zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa wanahabari kwenda katika matukio mbalimbali ni mdogo na hutegemea wahisani, kama watakuwa wanalipwa gharama, basi hawataweza kuandika au kutoa habari tofauti na wale wanaowafadhili. Sehemu nyingi nchini hakuna mtandao wa mawasiliano, hivyo kusababisha habari muhimu kutotolewa kwa wakati.

Pia vifaa au vitendea kazi ni tatizo kubwa kwa wanahabari wengi, wamiliki wa vyombo vya habari wangekuwa wanatoa vitendea kazi kama *voice recorders,* kamera, *computer* na *moderm* ili waweze kutuma habari kwa urahisi. Lingine muhimu ni ajira kwa Waandishi wa Habari (*Journalists)* wengi wanakuwa na hali mbaya kimaisha na kutegemea kulipwa na wanaotaka habari zao ziandikwe.

Mheshimiwa Spika, hata kama mwandishi anataka kufanya utafiti na kuandika habari kwa manufaa wa umma wanashindwa kufanya kazi hiyo na ndiyo maana habari nyingi ni za wanasiasa, watu mashuhuri na matukio ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, tunashauri sheria zilizopitwa na wakati zibadilishwe mapema ili sekta ya habari kwa ujumla iwe katika moja ya nguzo ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie namna ya kuboresha huduma ya kupatikana na utoaji habari nchini, pia pawe na (*sensorship*) ukaguzi wa baadhi ya habari kulinda maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ihakikishe vyombo vyote vya sasa vinavyoletwa nchini vya mawasiliano kwa ajili ya habari iwe ya *Digital* tu. Tusiwe (*dumping ground*) sehemu ya kupata bidhaa zisizotakiwa kokote.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iangalie mitaala ya vyuo vya uandishi wa habari. Wengi wanapohitimu hawana ujuzi wa vitendo na pia hawajui sheria. Pia wanaokwenda katika vyuo hivyo ni wengi sana. Watakuja kukosa ajira ikawa lawama kwa Serikali, Serikali ingeangalia mitaala ili wapate mafunzo sambamba na uandishi wa habari kufanya kazi nyingine pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie namna ya kuboresha sekta hizi ngazi zote. Leo hii utamaduni wetu unapotea taratibu na tunaiga utamaduni wa nchi za Magharibi. Ni muhimu tuhifadhi na kutunza na kuendeleza utamaduni wetu na historia yetu ifundishwe kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, katika michezo tunashukuru Serikali kutoa vipaumbele katika michezo, bado tunahitaji kwa sehemu kubwa michezo iboreshwe kutoka shule za awali, pia michezo sio mpira wa miguu na vikapu tu. Kuna aina nyingi za michezo, yote ipewe umuhimu wake, utafanya vijana wengi watoke katika kutumia madawa ya kulevya na uvutaji wa sigara na unywaji wa pombe, pamoja na kukaa vijiweni na kutofanya kazi. Pia watu wenye umri mkubwa au si vijana wawe na hamasa ya michezo wapate mazoezi na pia ni njia ya kuunganisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, viwanja vya michezo vilivyovamiwa virejeshwe katika hali ya kawaida. Waliovamia wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya michezo visambazwe kote nchini kwa shule zetu za awali, msingi na sekondari zote. Pia mitaala katika vyuo vya ualimu ibadilishwe na walimu wote wawe na mafunzo ya michezo.

Mheshimiwa Spika, kama tunaweza kuchangia sherehe na masuala ya burudani, basi pia tuchangie sehemu kubwa katika michezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwapongeze na kuwatambua wote wanaochangia michezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie sekta hii muhimu, leo vijana ndiyo waliokuwa wengi nchini kwa hesabu ya wananchi. Leo hii wengi wao hawana ajira na taaluma mbalimbali ya kuwawezesha kuishi na kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, tunaomba elimu zaidi itolewe kwa vijana na pia kwa wazazi wao ili tuwe na nchi yenye vijana wenye nidhamu na watakaofuata utamaduni wetu. Serikali iangalie namna ya kuboresha Mfuko wa Vijana ili uweze kuwasaidia kujikomboa kiuchumi. Halmashauri zetu zitenge fedha kwa ajili ya bajeti ya kusaidia vijana.

Mheshimiwa Spika, leo hii vijana hasa wa kike wanapata shida sana, hawapati fursa nyingi zilizopo na hasa kule vijijini wao ndio wanabaki kuhudumia familia na kufanya kazi za nyumbani, hata wanaosoma wanapata shida hiyo hiyo. Wengi wanaosoma wanajikuta wanatembea na vijana wenzao na watu waliowazidi umri kimapenzi ili kupata mahitaji yao muhimu na si mahitaji ya anasa.

Mheshimiwa Spika, elimu ingetolewa kwa vijana hawa wote ili tuwe na Taifa lenye maadili, utamaduni na uzalendo. Suala la vijana lisiachiwe Wizara hii tu, Serikali kwa ujumla pamoja na wananchi wote tushirikiane tuangalie namna ya kuboresha maslahi ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kuwateua Waziri na Naibu Waziri katika Wizara hii ambao naamini wataweza kuleta mazingira bora zaidi katika sekta hii.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote na taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jamii yetu ya Kitanzania tunao utajiri mkubwa sana wa lugha yetu ya Kiswahili ambayo imechochea kwa kiasi kikubwa umoja wa Taifa letu. Ni vema Serikali ikatoa tamko rasmi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli zote na hasa zile za Serikali hasa makongamano, warsha, semina, midahalo na kadhalika kwamba ni lazima na vitendo vioneshe hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kiswahili ni mtoto wa Tanzania ni vema mtoto huyu alelewe vizuri, nchi za jirani wameanza kwa vitendo kukitumia Kiswahili katika wavuti, mfano *Microsoft* – Kiswahili. Tukitumia lugha yetu vizuri pamoja na kukuza uchumi wa Taifa letu pia itawezesha kuunganisha Bara la Afrika kwani Afrika hatuna lugha nyingine inayokuwa kwa kasi kama Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Habari la Umma *(TBC)* fedha zilizotengwa wastani wa shilingi milioni 300 ni kidogo mno, kinadhalilisha na kinatishia uhai wa shirika hili muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Kwa kuwa shirika hili kuanzia mwaka 2006 lilianza kwa kazi nzuri na ikaonekana kwa vitendo ni vema mwendelezo huu ukaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipatie dhamana Shirika hili ili liweze kukopa katika taasisi za fedha au za hifadhi ya jamii kwa haraka sana ndani ya siku 60 kabla Watanzania hawajakata tamaa na shirika hili la umma. Ukizingatia ushindani mkubwa uliopo katika tasnia ya habari. Angalizo, kwenye tamthilia na filamu zinazokiuka mila, utamaduni na desturi ya Mtanzania (maadili) zisipewe nafasi yoyote katika vyombo vyetu vya habari na hasa vile vya umma.

Mheshimiwa Spika, mifumo yetu ya elimu iangalie upya na hasa ile isiyozingatia utu wa Mtanzania. Mifumo ya elimu inayozingatia utu itamwandaa mtoto au kijana wa Kitanzania awe na upeo mpana wa kujitambua hasa kujiandaa kwa ubunifu wa kujiajiri wenyewe pindi wanapohitimu masomo yao.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu ya michezo lipewe nafasi katika mifumo yetu ya elimu. Suala la michezo liwe endelevu na siyo kwa utashi wa Waziri mwenye dhamana kwa wakati husika. Vyama vya michezo vijitahidi kuondokana na dhana ya utegemezi. Usimamizi, uhuru, uendeshaji endelevu na wenye tija.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni kati ya nchi yenye jina zuri na inayoheshimika sana katika Bara letu la Afrika. Ni vema vazi la Taifa likaharakishwa mchakato wake ili tuwe na utambulisho rasmi ndani na nje ya Taifa letu. Hasa kwenye majumuiko mbalimbali ya Kitaifa tuweze kuonesha umoja na udugu wetu wa Kitaifa.

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mungu kwa yote ya kheri na neema aliyotujalia, sasa nakushukuru kwa kuturuhusu kutoa michango ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa tatu (3) wa hotuba ya Waziri na Wizara hii kifungu cha tano (5), Waziri anawapongeza Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, CHADEMA na NCCR – Mageuzi kwa kuteuliwa na kuchaguliwa na hatimaye kujiunga na Bunge lako Tukufu amefanya jambo zuri, lakini naomba tumkumbushe kuwa na The *Civic united Front* (CUF), Chama cha Wananachi ni chama chenye Wabunge wengi humu Bungeni kuliko hata baadhi ya vyama anavyovitaja na kuvitukuza kwa ubaguzi! CCM haikupata hata Mbunge mmoja wa kuchaguliwa Kisiwani Pemba. CHADEMA haina hata Mbunge mmoja Unguja na Pemba. Hivi sio vyama vya Kitaifa, ukizingatia mgawanyo wa Wabunge kwa sehemu za Taifa letu; Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, *CUF* ni chama pekee cha Kitaifa kwa mtazamo huo, *CUF* inao Wabunge Pemba, Unguja na Tanzania Bara. Huu ni ubaguzi wa Wizara hii dhidi ya *CUF*. Hivyo, siungi mkono hoja hii kwa ubaguzi huu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 22 wa kitabu cha hotuba hii unataja kazi zilizotekelezwa. Ni nyingi kiasi na mafanikio yaliyopatikana ni jambo la kupongeza. Nawapongeza BAKITA kwa jitihada yao ya kutunza na kuendeleza lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, bado kuna kazi nyingine BAKITA inahitajika kuifanya, kuna matumizi mabaya ya maeneo ya Kiswahili. Mfano neno *sihi*, neno hili linatumiwa visivyo katika vyombo vya habari Radio na *TV,* mara kadhaa neno hili badala ya kuonya na kukataza, waandishi wengine hulitumia kwa maana ya kuhimiza! Nashauri idara zinazohusika kwenye vyombo vya habari wasimamie utoaji wa habari, maeneo na maana yake na uhalisia ili lugha ibakie kuwa ni nzuri na isipoteze maana.

Mheshimiwa Spika, neno habari na neno bora sio vitendo. Vyombo vya habari huyatumia vibaya mfano “kuhabarisha” au “kuboresha” kitendo kula kinaweza kutumika “kulisha” lakini kumpa mtu habari au kutoa habari ndio matumizi ya neno habari na sio kuhabarisha. Vyombo vya habari vinayatumia na jamii inafuata na inapotea katika utamaduni katika lugha ya Kiswahili. Neno likishatumika katika vyombo vya habari linaingia katika lugha moja kwa moja, hii ni hatari kwa lugha yetu. Vyombo vya habari visimamiwe vyema katika matumizi ya lugha yetu.

Mheshimiwa Spika, vipaji vya Watanzania katika michezo sio rahisi kupatikana. Uchaguzi wa wachezaji wa “Timu ya Taifa” mara nyingi hulalamikiwa kuwa unatumia udugu, ubaguzi na kujuana, ndio maana timu zetu hazikui. Ni lazima Wizara isimamie vema uteuzi wa timu zetu katika mpira wa miguu, riadha na michezo mingine.

Mheshimiwa Spika, kuna mchezo wa kanga ndembendembe. Kanga ndembendembe ni mchezo wa uchi na hauna maana hata kidogo hapa Tanzania, tunamwomba Waziri aufungie mchezo huo ili aiokoe jamii ya Tanzania kimaadili, kiutamaduni na kisilka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii, siungi mkono hoja.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Daktari Fenella E. Mukangara, kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina aliyoitoa asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, kipekee na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu, naomba nimpe pole sana Waziri pamoja na wafanyakazi wenzake wawili ambao walipata ajali mbaya ya gari iliyotokea Mkoani Tabora. Mungu ni mwema, tunamshukuru sana kwa kuwanusuru na ajali hiyo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Amos Makalla Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme waziwazi kwamba, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, naomba nikumbushie ombi la Halmashauri ya Wilaya yangu ya Siha la kusaidiwa kujenga viwanja vya michezo mbalimbali katika eneo yalipo Makao Makuu ya Wilaya eneo ambalo sisi wote tunajua ni jipya kutokana na upya wa Wilaya yenyewe. Ombi hili tumekuwa tukilikumbushia mara kwa mara bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, mwisho tunaomba kusaidiwa vifaa vya michezo ikiwemo mipira ili kuimarisha michezo katika Wilaya yangu.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema kwamba, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba nitoe pole kwa Watanzania kwa ujumla waliopoteza ndugu zao kutokana na ajili ya meli *MV. Skagit* iliyotokea juzi karibu na Kisiwa cha Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa hotuba nzuri iliyolenga jamii kwa ujumla kama bajeti ingetosha na kutekeleza ipasavyo malalamiko kwa vijana kwa ujumla yangepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia Wizara kwa makadirio ya makusanyo 714,209, 000/= kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Wizara pamoja na mapato iliyoainisha kuyatumia vyema mapato hayo kama yaliyokusudiwa ili kuondosha malalamiko kwa wananchi. Tegemeo langu na kama makadirio hayo yamevuka kiwango na kuongezeka, taarifa za ongezeko zitaainishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa vijana, sote tunafahamu kwamba vijana walio wengi wamekosa ajira nchini na kukosa tamaa ya maisha na kujiunga na vitendo visivyofaa. Ushauri, Tanzania tumesifika kwa kiasi fulani kwa kuandaa mikakati mbalimbali ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Spika, pia vijana walio wengi wamekosa ajira na kujishirikisha na vikundi vya madawa ya kulevya, wizi, ubakaji na mengineyo ni jukumu la Serikali sasa kuongeza bajeti ya kutoka katika fungu linalohusiana na vijana kwa kuwapatia mikopo kwa wingi ili kujiendeleza kichumi na kuondokana na dhana hizo potofu na kupunguza maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taasisi ya maji Muhimbili. Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imeanzisha *NGO* inayojulikana kwa jina la *MAT* na inajishughulisa na kuwapa dawa walioathirika na madawa ya kulevya aina ya *Heroin*. Baada ya kupatiwa dawa hiyo wengi wa vijana wameacha kabisa dawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, lakini vijana wale walio wengi wamekosa ajira ya kufanya kama hawakuangaliwa vizuri wanaweza wakarudia tena. Changamoto iliyopo kwa vijana wale, wengi wanapenda kuhudhuria kila siku kwenda kupata dawa kwa ajili ya matibabu hayo, lakini uwezo wa nauli kwao umekuwa ni kikwazo kwani wengi wao ni vijana kutoka maeneo ya mbali sana.

Mheshimiwa Spika, wengi wa vijana hao wametengwa na jamaa zao hivyo familia hawaamini kwamba kuna kitengo kinachoweza kuwatibu vijana hao.

Mheshimiwa Spika, Madaktari wanaowahudumia vijana hao wana kazi ngumu sana ya kuwaelimisha vijana hao na kukabiliana nao kwa nguvu zote hivyo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwatambue Madaktari wale na kuwapatia motisha ya aina yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, kuzitaka Halmashauri zote nchini kuainisha vijana waliopata matatizo kama hayo na kutenga fedha ndani ya fedha za UKIMWI kuwasafirisha na kuwapeleka Muhimbili (Taasisi ya *MAT*) kupatiwa matibabu hayo. Vijana waliotibika kuwaajiri hapo katika kazi za kufanya usafi ndani ya Halmashauri husika ili kuondoa wimbi kubwa la vijana kuwa waharibifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha zinazotengwa kwa ajili ya mikopo, sote tunafahamu kwamba vijana walio wengi wanakosa fursa za mikopo inayotolewa na Serikali kinachofanyika ni urasimu, ubinafsi na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa inalo jukumu la kuwapatia mikopo vijana wote waliohamasishwa nchini kujiunga na vikundi vya ujasiriamali na hawakurudi nyuma, wakaitikia wito wa viongozi wao, matokeo yaoneshe mikopo iliyotengwa na Serikali imewafikia walengwa na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, vijana wa nchi ndio tegemeo nchini tukiwadharau watakosa imani na nchi yao au na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Fenella E. Mukangara, Naibu Waziri Amos G. Makala, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete alipokuwa akizindua Bunge, Michezo ilikuwa kati ya vipaumbele kumi. Muda mfupi tuliona alivyomtafuta kocha wa mpira wa miguu Ndugu Maximo aliwafundisha vijana wa Taifa *Stars* wakaweza kushinda na kuja Bungeni kupongezwa na wakati huo wananchi wote tulifurahi. Hivyo, naomba na viongozi wote tuoneshe nia ya kuungana na Mheshimiwa Rais wetu katika kukuza michezo yetu. Naomba michezo iendelee kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwenye Halmashauri zetu suala la michezo halipewi kipaumbele. Naomba Waziri awasiliane na Waziri wa TAMISEMI ili aziagize Halmashauri zote nchini kutenga pesa kwa ajili ya Michezo.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Utamaduni wapo tu lakini hawana vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Vijana katika sera yetu hutakiwa kupewa asilimia 5%, je, ni Halmashauri ngapi ambazo katika mwaka wa fedha 2011 – 2012 zilitenga asilimia 5% kwa ajili ya Mfuko wa Vijana.

Mheshimiwa Spika, waandishi wa habari waweze kuandika habari za kuendelea kudumisha Muungano wetu, amani na utulivu waepuke kuandika habari za upotoshaji wakiendelea na tabia hii ya kupotosha ipo siku moja watasababisha kupoteza amani kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wanahabari kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutoa habari lakini nawaomba wale wanahabari ambao ni wachonganishi waache tabia ya kupotosha, waige wenzao ambao wana maadili ya uandishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Daktari Fenella E. Mukangara, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Mheshimiwa Amos Makalla, Naibu Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu sana kwa ustawi na maendeleo ya wananchi wetu. Vile vile nampongeza Ndugu Seth Kamuhanda, Katibu Mkuu na Bibi Sihaba Nkinga, Naibu Katibu Mkuu kwa kusimamia vema utekelezaji wa sera na sheria za sekta hii mtambuka. Nawatakiwa wote kheri na fanaka katika utekelezaji wa majukumu waliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, natamka kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia mjadala wa hotuba ya Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maadili ya Vyombo vya Habari:-

(a) Kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikihimizwa kuwa ikamilishe utungaji wa Sheria ya Habari ili pamoja na mambo mengine kuhakikisha kuwa watumishi wa tasnia ya Habari ni wataalam waliosomea fani hiyo badala ya utaratibu wa sasa ambapo wamiliki wa vyombo vya habari huwatumia vijana waliomaliza Kidato cha nne kwa kuwapa kibarua *(correspondent basis*) na kuwalipa fedha kidogo sana ambazo hulipwa baada ya muda mrefu sana wa mawasiliano mengi.

(b) Kutokana na udhaifu wa Sheria ya Habari iliyopo sasa maadili ya vyombo vya habari imeporomoka sana. Kwa maoni yangu moja ya sababu ni chombo kinachosimamia maadili hayo yaani Baraza la Habari Tanzania kuendekeza vyombo hivyo vinapokiuka maadili. Mara nyingi tuzo wanazopewa wahanga vyombo hivyo ni ndogo sana ikilinganishwa na hasara (*damage*) waliopata wahanga hao. Ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka, nashauri kuwa Serikali ianzishe Mdhibiti wa Magazeti, chombo kitakachohakikisha kuwa wamiliki wa vyombo vya habari wanawajibika kwa maudhui ya vyombo na wahanga wa maudhui hayo wanatunzwa ipasavyo.

(c) Mdhibiti aliyetajwa kwenye kipengele (b) hapo juu awe na jukumu la kuhakikisha kuwa mmiliki mmoja haruhusiwi kumiliki gazeti zaidi ya moja (*media unbundling*). Hii itapunguza matumizi mabaya ya vyombo hivyo ambavyo vyao kulinda maslahi yao na kuhujumu wengine.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Shirika la Habari Tanzania, nawapongeza viongozi na watumishi wa Shirika la Habari Tanzania *(TBC)* kwa utendaji wao ambao umefanya usikivu na uonekano wa matangazo yao kuwafikia Watanzania walio wengi. Pongezi zangu ni mahsusi kwa namna wanavyodumisha maadili na kuwa mfano wa kuigwa na wengine. Ili kuboresha huduma za Shirika hili na kuwawezesha kurusha matangazo yao hadi maeneo yote vijijini, nashauri kuwa shirika liongezewe fedha za maendeleo na wawezeshwe kutoa motisha kwa watumishi wake ambao wamekuwa wakijituma vilivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko ya mfumo wa utangazaji toka Analojia kwenda Digitali. Naipongeza sana Wizara pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) kwa kusimamia kwa uthabiti mpango wa mabadiliko ya mfumo wa utangazaji toka Analojia kwenda dijitali. Kwa kuwa Serikali imeamua kuwa mwisho wa kutangaza kwa Analojia ni Desemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri mamlaka kwa kushirikiana na wadau wote kutumia muda uliobaki kuwekeza katika elimu kwa umma kwani kwa maoni yangu wananchi wengi bado hawana taarifa ya mabadiliko yanayokuja, wataendelea kudanganywa na wafanyabiashara wenye tamaa kwa kuwauzia vifaa (*terminal equipment*) vilivyopitwa na wakati na hivyo kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa Waheshimiwa Wabunge wapewe elimu hiyo na wawezeshwe kwenda kuendesha semina kwa Mabaraza ya Madiwani na viongozi wengine walio karibu sana na wananchi. Aidha kwa kuzingatia kwamba muda uliobaki ni mfupi sana kwa wananchi hasa walio vijijini kujiandaa na kuhama toka Analojia kwenda Dijitali nashauri kuwa mashauriano yafanyike baina ya nchi za *SADC* na *EAC* ili kusogeza mbele muda kwenda Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa maudhui, nawapongeza sana mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya kupitia kwa Kamati ya Maudhui kuhakikisha kuwa matangazo yatolewayo na vyombo vyetu vya elektroniki yanazingatia maadili ya Taifa letu. Hata kwa kuzingatia ufuatiliaji niliokuwa naufanya kwa vyombo mbalimbali nashauri kuwa mamlaka iwe na mitambo yenye nguvu zaidi itakayowezesha kuzuia (*automatic suppression of content*) matangazo yanayorushwa toka nje na ndani ya nchi yanayokiuka maadili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji vijana. Hali ya vijana walio wengi nchini bado ni duni sana, hasa kwa sababu wengi hawana chanzo chochote cha kipato. Hali inakuwa mbaya zaidi kwa sababu Wilaya zilizo nyingi ikiwemo Wilaya yangu hazina Maafisa Vijana ambao wangefanya kazi ya uhamasishaji na ushauri kwa vijana kuwa wabunifu kwa kuanzisha miradi yao badala ya kusubiri Serikali iwapatie ajira. Nashauri kuwa Wizara hii iwezeshwe kifedha ili iweze kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuajiri Maafisa vijana na pia kutoa *seed money* kwa vikundi vya Vijana kwani tukitegemea Halmashauri za Wilaya lengo la kuwezesha vijana wajitegemee kamwe halitafikiwa.

Mheshimiwa Spika, ukusaji wa vipaji vya usanii, wako vijana wengi wenye vipaji mbalimbali nchini katika usanii. Kwa bahati mbaya, hata jitihada zao za kukuza vipaji hivyo zinarudishwa nyuma na wafanyabiashara wanaoiba kazi zao na kujinufaisha wao. Nashauri Serikali ipitie upya sheria inayosimamia usanii ili kulinda vipaji na kazi za vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na narudia kusema kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri kwa njia hii ya maandishi. Lakini pili, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake hapa Bungeni leo hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuuelekeza mchango wangu moja kwa moja katika kuviongolea vyombo vyetu vya habari kwa maana ya *radio, TV* pamoja na magazeti mbalimbali yanayochapishwa na kusambazwa kila siku hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya waandishi wa habari na vyombo vya habari wamekuwa wakichangia kwa kiasi kikubwa sana kuchochea vitendo vya uvunjifu wa amani hapa nchini kwa kuwa waandishi na vyombo vya habari hivyo wamekuwa wakiandika habari zilizobebwa na vichwa vya habari vikubwa na vya kutisha kuhusu migogoro ya watu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kasumba iliyojengwa na baadhi ya waandishi wa habari ya kuongeza chumvi na kukuza habari za matukio ya migogoro ya watu kupita kawaida, imechangia kwa kiasi kikubwa kuvuruga amani katika jamii yetu ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, waandishi wa habari wamekuwa ndio chanzo cha watu kuvurugana na kutishia amani hapa nchini kutokana na habari zao zenye vichwa vya habari vya kutisha. Wala sitoshangaa kuona baadhi ya watu wakishabikia kila jambo linalozungumzwa na kuandikwa na waandishi wa habari na hii inatokana na hisia na misimamo yao ya kisiasa waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kwa historia, uandishi wa habari ni miongoni mwa taaluma zinazothaminiwa na kuheshimiwa sana katika jamii duniani kote. Ni taaluma inayojulikana kama kioo cha jamii. Hata hivyo, katika hali ambayo haikutarajiwa, taaluma ya uandishi wa habari imeonekana kuweweseka kwa kiasi kikubwa kutokana na baadhi ya waandishi wa habari na vyombo vya habari kuingiliwa na chembe za siasa na fikra mbaya zenye kuambatana na chuki dhidi ya Serikali iliyopo madarakani.

Mheshimiwa Spika, misukumo ya hisia za kisiasa, chuki na ubinafsi miongoni mwa baadhi ya waandishi wa habari zimekuwa zikichangia kuporomoka kwa maadili ya uandishi wa habari na hivyo wakati mwingine kuinyima jamii habari za kweli, sahihi na zisizofanyiwa utafiti wa kina.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, niwapongeze Daktari Mukangara na Amos Makalla kwa kuteuliwa kwao kuongoza jahazi la Wizara hii adhimu. Vile vile niwapongeze kwa hotuba nzuri na *progress* ambayo imeanza kuonekana.

Mheshimiwa Spika, *issue* yangu kwa Wizara hii ni suala zima la michango ya Mwenge ambayo wananchi wanaendelea kutozwa tena kwa kulazimishwa badala ya kuwa iwe mchango wa hiari. Naomba kupata kauli rasmi ya Serikali kwani binafsi nimepata usumbufu mkubwa kutoka wa wananchi kwa sababu ya mkanganyiko uliopo kwenye suala hili. Je, wananchi wachangie elimu ya afya na miundombinu ya vijijini au sasa wachangie mwenge ambao kimsingi hauna tija na hauna *any diret impact* kwenye maisha ya wananchi. Namwomba Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri atupe kauli ya Serikali ili kuondoa sintofahamu hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nirudie tena kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri na niwatakie kila la kheri katika harakati za kufanya *information* na sio *transformation* kwenye Wizara hii inayogusa maisha ya vijana wa nchi hii.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa hotuba nzuri aliyowasilisha leo. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii inashughulikia masuala ya vijana ambao ni zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania wote, Wizara hii inayo majukumu makubwa sana kutokana na changamoto nyingi walizonazo vijana kote nchini. Napenda kukiri kabisa kwamba vijana wetu wanazo changamoto sana. Changamoto hizo ni pamoja na kukosa ujuzi na matokeo yake ni kukosa ajira. Ni wakati muafaka sasa Wizara ije na mikakati ya makusudi ya namna ya kuwawezesha vijana hawa wapate ujuzi wa kiufundi utakaowawezesha vijana hawa kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia katika Wilaya yangu ya Geita na Jimbo la Busanda naweza kusema kwamba hali ya vijana ni tete sana. Wilaya nzima na Mkoa mpya wa Geita hatuna Chuo cha Ufundi. Vijana wetu wanaomaliza masomo yao darasa la saba na *form four* ambao hawaendelei na masomo ya juu hawapati ujuzi wa aina yoyote. Nichukue fursa hii kuiomba Serikali ijenge Chuo cha Ufundi *VETA* ili kuwajengea uwezo vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utamaduni na michezo, Wizara inatakiwa itambue kuwa michezo na masuala ya utamaduni kwa sasa ni vyanzo vya ajira kwa wenye vipaji. Katika Jimbo la Busanda wapo vijana wengi wenye vipaji vya sanaa. Nifanyeje ili vijana hawa nao wapate nafasi ya kushiriki Kitaifa na hata Kimataifa. Wananchi wenye vipaji hasa walioko vijijini hawapati fursa ukilinganisha na wale walioko mjini.

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara ibuni njia ya utambuzi wa vipaji hivi kutoka mahali pote nchini yaani vijijini na mijini. Hili liende sambamba na kazi ya Baraza la Michezo la Taifa iliyoainishwa katika ukurasa wa 42 katika kitabu cha bajeti. Kazi ya kuimarisha ushiriki wa wanawake katika michezo na uongozi 2012/2013. Naomba ushiriki huu ushirikishe wanawake kutoka Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kupata ufafanuzi kuhusu sera ya michezo kuhusu ujenzi wa viwanja vya kisasa vya michezo hasa katika mikoa mipya ukiwemo Mkoa mpya wa Geita. Wananchi wa Geita ni wapenzi wa michezo sana, lakini hatuna viwanja vya michezo. Naomba wakati wa majumuisho nipate majibu kuhusu sera inasemaje.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nyeti na muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu ili jamii yetu iweze kutoa maamuzi sahihi katika changamoto mbalimbali zinazotukabili, ni vizuri Serikali ikahakikisha vyombo vya habari vinapata ujuzi na utaalam wa kutosha katika tasnia hii.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana vyombo vingi vya habari nchini havina ujuzi na utaalam wa kutosha. Wanahabari wengi wanapotosha umma kwa kuandika habari nyingi na maoni ambayo hayana utafiti wala uchunguzi wa kutosha, hatma yake badala ya kuboresha umma vinaingia kuipotosha jamii, jambo ambalo ni hatari sana kwa Taifa letu. Mfano mzuri ni *TBC1*, ambacho ni chombo cha Taifa, mara nyingi kimekuwa kikitoa habari za upendeleo na kuamua kukipendelea Chama cha Mapinduzi na imegeuka kuwa chombo cha propaganda badala ya kuelimisha umma na kueleza uhalisia wa hali ilivyo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika chombo hiki cha Taifa kina baadhi ya watangazaji ambao wana ulevi wa itikadi wa kisiasa, naomba Waziri katika majumuisho yake aniambie ni mikakati gani ya kuboresha shirika hili lisifanye kazi ya CCM.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa kuwasilisha bajeti yake kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iwekeze katika michezo kwa kuweka bajeti madhubuti hasa kwa wanamichezo wanaopata nafasi kwenda nje ya nchi kwa michezo ili kuweza kushiriki bila matatizo au kuvunja safari kwa kisingizio Serikali haina pesa. Tujue uwakilishi wao ni kuitangaza Tanzania kimichezo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iharakishe mchakato wa nchi kuwa na vazi la Taifa, hii ni muhimu kwani Tanzania tutaweza kuitangaza kwa vazi lake kama zilivyo nchi nyingine ikiwemo Indonesia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara hii isimamie vijana kwenye utumiaji wa madawa ya kulevya kwani imekuwa tatizo kubwa na vijana wengi wanaharibika, nguvu kazi inapotea na maadili ya nchi yanapotea kutokana na kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianzishe Benki ya Vijana kama ilivyo Benki ya Wanawake ili iweze kuwasaida kupata mikopo na kuweza kuwainua kimaisha kwani tumekuwa tukiona vijana wengi hawana uhitaji wala chombo madhubuti cha kuwasaidia kusabisha kujiingiza katika vitendo viovu na uzururaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke chombo cha kuratibu vijana chipukizi katika ngazi za Vijiji, Wilaya na Mkoa isiwe katika majiji tu ili tuweze kuibua wanamichezo, wanariadha na wanautamaduni wa kizazi kipya. Tumekuwa tukiona vipaji vingi vya wanamichezo vikitolewa mijini tu. Sasa wakati umefika wa kuhakikisha vijana wanatoka *from grassroot*. Pia vikundi hivi viwezeshwe na kupatiwa jezi, mipira na vifaa vingine vya michezo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ni moja ya Wizara ambayo ni tegemeo la Taifa katika kulifikisha kwenye maendeleo ya

kweli vinginevyo Wizara hii inaweza ikawa janga la Taifa endapo itaendesha mambo yake kiholela.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Habari, tasnia hii nchini inaweza ikawa kichocheo kikubwa cha maendeleo endapo itatumika vizuri mfano, Vyombo vya Habari vikiwemo Redio na Televisheni viwe vinatoa habari za kina na zisizochochea chuki na uadui miongoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi vinatakiwa vizingatie kwa ukaribu yale ambayo yalisababishwa na Redio Interahamwe ambayo yalichochea chuki na hatimaye kusababisha kutokea kwa mauaji ya kimbari jambo ambalo lilisababisha na chombo cha habari likapelekea kuingiza nchi katika janga la Taifa.

Mheshimiwa Spika, vile vile ni vema vyombo hivi vya habari vikatoa habari sahihi kwa wananchi na ambazo hazitozingatia upendeleo au makundi katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vyombo vya habari kama magazeti bado vinafanya kazi ya kusambaza habari kwa kuzingatia makundi, upendeleo na hata wakati mwingine kutoa taarifa za upotoshaji wa taarifa zao katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba nchi yetu imeelemewa na kuiga na pia kusambaza utamaduni ambao si urithi wa kizazi cha Watanzania. Vijana wetu wengi sasa wameiga utamaduni wa Kimagharibi ambao unakwenda kinyume na mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Spika, si utamaduni wa kijana wa kiume wa Tanzania kusuka nywele na kuweka rasta wala si miongoni mwa maendeleo kama wengine wanavyodai. Ikiwa kijana wa kiume atasuka nywele, atavaa bangili na ataweka hereni kwenye masikio yake mwanamke wa Tanzania afanye nini katika kuhakikisha kwamba yeye ndiye aliyewekwa na Mungu kama kitulizo cha mume.

Mheshimiwa Spika, vile vile utamaduni wa Watanzania haujatoa fursa kwa wanawake kuvaa mavazi ya kiume. Jambo hili ni kwenda kinyume na utamaduni wetu, lakini vile vile ni kwenda kinyume na dini zetu. Ni kweli kwamba Serikali haina dini lakini Watanzania wana dini zinazowaongoza, hivyo wasiafiki kauli ya kwamba Serikali haina dini wajiulize; je, wenye Serikali nao hawana dini zinazowaongoza?

Mheshimiwa Spika, kuhusu wasanii, katika utamaduni kuna utamaduni unaozingatia mambo mengi, moja ni suala zima la wasanii. Wasanii wapo ambao ni watungaji na waimbaji wa sanaa zao ambazo wanazifanya, lakini vile vile kuna wasanii ambao wanaandika riwaya, tamthilia na vitabu vya mashairi. Ni vema Serikali ikawaangalia kwa karibu zaidi wasanii ambao wamechipukia katika fani ya utunzi na uandishi wa vitabu jambo ambalo litaweza kuwasaidia wasanii hao katika kupata ajira lakini hata kulipatia sifa Taifa, lakini vile vile kuchangia pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya michezo, hii bado Tanzania tuko nyuma licha ya kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano ni mpenzi mkubwa wa michezo nchini. Moja kati ya mambo ambayo yameangusha sekta ya michezo Tanzania ni kutojali hali ya wachezaji wa Tanzania na hivyo kutoa fursa na ushawishi wa wageni kutoka nje kuwachukua wachezaji wa Tanzania kwenda kucheza soka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, bado Tanzania itaendelea kuwa kichwa cha mwendawazimu katika sekta ya michezo ukiwemo mchezo wa mpira wa miguu, pete (*netball*) na hata riadha. Hivyo ni wajibu wa Wizara kuhakikisha kwamba Watanzania tunashiriki na ushiriki wetu unazaa matunda ya ushiriki wetu. Kauli ya kwamba tumethubutu, tumeweza na tunazidi kusonga mbele iwe ya matendo, isiendelee kubakia kuwa ya maneno na maandishi yatakayobaki katika vitabu na makabati.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha vijana kuwa katika kiwango cha kuwa wanamichezo bora ni kuhakikisha kwamba wanashirikishwa na pia wanaepushwa kuingia katika ushawishi wa kimapenzi na pia kuepuka janga la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya, michezo hujenga Taifa imara, michezo hujenga umoja na michezo ni ajira kwa vijana wa jinsia zote kwa Taifa na dunia kwa ujumla.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu *(Subhanah Wataala)* kwa neema na rehema zake nyingi anazoendelea kunijaalia. Sina budi kusema *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina majukumu mazito na muhimu sana kwa Taifa letu. Vijana ndiyo afya ya Taifa lolote ulimwenguni ikiwemo Tanzania, vijana ndio nguvukazi na ndio fahari pia ya Taifa lolote ulimwenguni ikiwemo Tanzania. Kwa maudhui hayo, basi Wizara hii ina jukumu zito na muhimu kwa nchi yetu kama nilivyotangulia kusema hapo juu.

Mheshimiwa Spika, mtu huvuna alichopanda na hakuna mavuno bila kupanda, kupalilia, kutia mbolea, na pia kuyalinda mazao uliyopanda dhidi ya wanyama na wadudu waharibifu. Kwa mantiki hiyo ni lazima Wizara hii iwe na mipango yenye utekelezaji kwa ajili ya kuandaa vijana wetu ili tuweze kujivunia. Wizara iwe na utaratibu wa kuwajenga vijana katika umoja, upendo, uzalendo lakini pia tabia na silka nzuri zenye maadili mema. Vijana wajenge uwezo wa fikra ili wajione kuwa wao ni sehemu muhimu katika jamii yetu, badala ya ilivyo sasa, vijana kujiona wao ni mzigo na Taifa pia kuwaona vijana ni mzigo usiobebeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe wazi na iwe na usawa katika kuwaendeleza vijana pia katika ajira ili kujenga umoja na uzalendo kwa vijana wetu. Serikali pia iongeze juhudi katika kuwawezesha vijana kujiajiri, kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na mikopo kwa ajili ya mitaji. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunaienzi rasilimali watu tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ina jukumu la kusimamia utamaduni wa nchi yetu. Jambo hili sasa linaonekana kama wimbo tu, lakini Wizara imejisahau kutekeleza jukumu lake hilo. Utamaduni wa Mtanzania sehemu kubwa ni kuvaa nguo zenye kusitiri kiwiliwili cha mvaaji.

Mheshimiwa Spika, uvaaji wa nguo za stara hasa kwa vijana sasa imekuwa ni jambo la ajabu kwa mvaaji. Msichana anayevaa nguo za kujisitiri huitwa au kuonekana ni mshamba, hajasoma au hajakwenda Ulaya! Pia vijana wa kiume nao wameanzisha tabia chafu na ya “ubaradhuli” ya kuvaa suruali chini ya makalio na kuyaacha makalio yakiwa wazi au nguo yake ya ndani kuonekana wazi ikiwa nje juu ya suruali.

Mheshimiwa Spika, hii ni fedheha na ukosefu wa maadili kwa vijana hawa. Serikali ina wajibu wa kusimamia maadili kwa vijana. Suala la kusema ni utandawazi na ni utashi wa kijana mwenyewe haingii akilini, kwani tabia hii sasa imeenea mpaka mashuleni.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kudhibiti madawa ya kulevya kwa vijana na ulevi wa kupindukia, Serikali sasa ni lazima itoe maelekezo ya uvaaji wa nguo za nusu uchi hasa kwa vijana kama bado tunahitaji vijana wenye maadili. Je, Serikali haioni hili? Kama inaliona, nini kauli ya Serikali kwa tabia hii chafu?

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari ni muhimu sana katika kutoa habari zilizo sahihi na kwa wakati. Jambo la kusikitisha vyombo vingi vya habari hasa magazeti yanatoa habari kwa upendeleo au kutegemea kuhongwa! Magazeti mengi hasa ya binafsi yana tabia hii. Serikali lazima iangalie hili!

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuyapongeza magazeti ya *Daily News,* Nipashe na uhuru kwa kujitahidi kutoa habari kwa uwiano na bila kusubiri kupewa chochote ili waandike habari za siku husika.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizipongeze taasisi ambazo zimeanza kuchukua hatua kwa uvaaji usiostahili kwa wanafunzi wao. Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro na *College of Business Education* Dar es Salaam. Wakati sasa umefika Serikali kuweka kanuni za maadili katika vyuo vyote nchini ili kutoa vijana wazuri vyuoni.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Waziri wa Habari, Utamaduni na michezo pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maadili kwa vijana, napenda kusema kwamba vijana wetu wengi wanajiingiza katika mambo ambayo si mazuri kwa mfano ulevi, uvutaji bangi, madawa ya kulevya na mambo mengine ambayo hayafai kufanywa na vijana wetu. Wakati wa miaka ya nyuma ilikuwa kijana yeyote anapofanya makosa ilikuwa mzee yeyote anaweza kumwita na kumkanya au kumhukumu na mzee wa kijana hawezi kukasirika, lakini leo huwezi kumwona kijana kafanya makosa ukamhukumu. Mzee wake hakubali na anaweza kukupeleka Mahakamani wakati zamani hili halikuwepo na ndio maana hivi sasa vijana wengi wanaharibika. Vijana wengi hawana ajira na wanabakia vijiweni wanajiingiza katika mambo ambayo hayaridhishi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iache kuwaajiri watu wanapofikia muda wa kustaafu na badala yake wawaajiri vijana ambao tayari wamemaliza vyuo. Hii itapunguza vijana kukaa katika vijiwe na kujishirikisha na mambo ya wizi, madawa ya kulevya, uvutaji bangi na mambo mengine ambayo hayaridhishi kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, michezo ni ajira kubwa kwa vijana, ni uchumi na pia inakuza jina la nchi na pia inavutia utalii katika nchi na inapandisha heshima ya nchi Kimataifa. Napenda niishauri Serikali iwe na mikakati madhubuti ya kuinua na kukuza vipaji vya vijana katika michezo ili kuboresha ajira kwa vijana wetu. Ili kuinua uchumi wetu na pia kuipandisha heshima ya nchi yetu Kimataifa kupitia kada hii ya michezo.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie kuhusu utamaduni. Kwanza napenda niulize huu utamaduni wetu Watanzania hivi ni upi? Ni kwenda uchi? Vijana wengi unawakuta barabarani wamevaa nguo ambazo hata ukimwangalia basi unaona haya. Yuko uchi, vinguo havina mikono, maziwa yako nje, kitovu unakiona hata kutembea anashindwa hata kuinama kuokota kitu chini kinapoanguka kwa ufupi wa nguo aliyovaa. Hii sio mila au silka za Mtanzania, naomba Serikali isaidie kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari kwa sababu hali hii inachochea ongezeko la UKIMWI kwa kiasi kikubwa sana.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, changamoto kwa vijana; Vijana wengi hawa wanaomaliza shule za sekondari za Kata wameshindwa kujiajiri katika sekta hii ya michezo kwani hawakuandaliwa vizuri wakiwa mashuleni. Hivyo basi, naiomba Serikali itilie maanani zoezi la kurudisha michezo mashuleni, kuanzia shule za msingi na sekondari ili kuwajengea uwezo wa kimichezo vijana wengi. Hii itasaidia pia vijana wengi kuondokana na vitendo viovu vikiwemo madawa ya kulevya, uchangudoa na kuvuta bangi na matendo mengine maovu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbio za mwenge; binafsi naishauri Serikali kufutilia mbali zoezi hili, kwani hatuoni umuhimu wake ni uharibifu wa fedha za umma. Pia limekuwa likiambatana na vitendo vya dhuluma ikiwemo kuwachangisha walimu mashuleni.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione umuhimu wa kuwapa mitaji (mikopo) vijana yenye riba nafuu kama ilivyokuwa kwa akinamama wajasiriamali, hii itawajengea vijana uwezo wa kujitegemea kimaisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo kwa wanahabari, wamiliki wa vyombo vya habari, televisheni, Redio na magazeti wawaboreshee wanahabari wao mafao na mishahara yao ili kuondokana na utegemezi, ambapo wanahabari wamegeuka kuwa ombaomba.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kuwepo sisi Wabunge wa Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, pili nachukua fursa rasmi kukushuruku Mheshimiwa Spika kwa kuliendesha na kuliongoza Bunge lako kwa busara na hekima.

Mheshimiwa Spika, kwanza katika mchango wangu wa maandishi, nataka nianze mchango wangu kuhusu waandishi wa habari. Waandishi wa Habari naishauri Serikali wawe na mkataba na wamiliki wa vyombo vya habari kwani waandishi hawa lazima ieleweke kwamba kazi ya uandishi wa habari ni ngumu. Waandishi wa habari wanafanya kazi wakati mwingi katika mazingira hatarishi kwa sababu kazi hii inahitaji uchunguzi katika muda wote na mazingira yaliyo salama na hata yale yasiyo salama, kwa mfano kwenye machafuko au mapambano.

Mheshimiwa Spika, waandishi wa habari wana hali mbaya ya maisha, kwa hiyo kuna haja ya kuboreshwa kwa maslahi yao (mishahara) hasa waandishi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, waandishi watakapobakia katika hali hii duni kuna hatari ya kuweza kutumiwa na watu wengine kuvuruga maadili ya uandishi.

Mheshimiwa Spika, suala la utamaduni wa nchi yetu, maadili ya nchi yetu yameporomoka kwa asilimia 70 kwa kuacha kabisa utamaduni wetu na kufuata utamaduni wa nchi za magharibi.

Mheshimiwa Spika, nchi iliyopoteza utamaduni wake ni sawasawa na gari lililoacha njia kwenye mlima mkubwa na kuelekea bondeni. Watu wote waliomo kwenye gari hilo kuna uwezekano wa kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, Watanzania sasa hivi hasa vijana wetu wa kike wanatembea uchi, nguo zenye kubana na kuonesha miili yao kwenye sehemu za siri. Hii ni hatari vijana wengi wanavutika na kutumbukia katika zinaa jambo ambalo ndio chanzo kikuu cha maambukizo ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, shule zetu ni sehemu (mahali) pazuri pia kutoa mafunzo ya kuwaanda vijana na kupata wanamichezo wazuri katika Taifa letu, lakini jambo la kusikitisha hakuna sera yoyote ya Wizara inayoandaa vijana wetu shuleni kimichezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima yako na Bunge lako Tukufu mambo yafuatayo:-

(a) Serikali iandae sera rasmi juu ya maadili ya Mtanzania ikihusisha mavazi na muziki.

(b) Serikali irudishe michezo ya watoto mashuleni kama somo katika mitaala.

(c) Serikali iangalie upya malezi ya vijana wetu.

(d) Serikali iangalie suala la ajira kwa vijana kwani wengi wao hawana kazi.

**MHE. JUMA OTHMANI ALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu hili. Pia jinsi unavyoliendesha Bunge letu hili inatoa ile picha halisi ya kwamba, mwanamke akiwezeshwa anaweza kutekeleza ipasavyo majukumu yake aliyopangiwa. Lakini pia, napenda kumpongeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kuwasilisha vema hotuba yake hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkubwa upo kwenye vyombo vya habari. Itakumbukwa kwamba waandishi wa habari na vyombo vya habari ni mhimili wa nne wa dola usio rasmi wenye jukumu kuu la kuhabarisha, kuelimisha, kukemea, kukosoa na kuburudisha jamii, lakini kwa bahati mbaya mhimili huo unaotegemewa katika kutoa changamoto na kuhamasisha maendeleo katika jamii umeendelea kutiwa dosari na baadhi ya watendaji wake kinyume na maadili ya taaluma hiyo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya habari zilizoongezwa chumvi kupita kiasi zimekuwa chanzo cha baadhi ya watu kuchukiana, kujengeana uhasama na kuzusha migogoro isiyo ya lazima katika jamii. Kitendo cha kuandika habari za kupika zinazochonganisha na kuhamasisha watu kuchukiana ni cha hatari kwa kuwa kinashawishi vitendo vya uvunjifu wa amani katika jamii.

Mheshimiwa Spika, lazima watu wote tuitunze na kuikumbatia amani kwa gharama zote, mtu anayechezea amani yetu huyo si mwenzetu na wala hatufai katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari na vyombo vya habari haviwezi kujivua jukumu la kuchangia ujenzi wa amani kwa vile ndiyo vyenye nafasi ya kuipa habari jamii kuhusu matukio na masuala mbalimbali yanayojiri kila siku katika jamii yetu ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wasanii wa michezo (*Bongo Movie*), ni muda mrefu vijana wa nchi yetu wamekuwa na utaratibu wa kufanya michezo kwa gharama zao wenyewe, suala ambalo linaleta ajira na kujiajiri wenyewe. Hivyo naishauri Serikali kuweka utaratibu maalum wa kukinga kazi za wasanii ili wapate faida na kazi zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho namalizia kwa kusema naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ajira kwa vijana, wengi wamekuwa wakikimbilia mjini kutokana na Serikali kushindwa kuwawezesha huko walipo vijijini. Vijana hawa waapofika mjini kutokana na elimu yao kuwa ndogo wanashindwa kupata ajira na kujiingiza katika vitendo viovu kama vile wizi, madawa ya kulevya na kadhalika pamoja na hayo, miongoni mwa hao vijana kuna wengine wana vipaji, lakini Serikali imeshindwa kutambua vipaji vyao na kuwaendeleza vijana hawa. Je, Serikali ina mikakati gani kuwasaidia vijana waliopo vijijini kabla hawajafika mjini? Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuendeleza vijana ambao wana vipaji ili wapate kujiendeleza wenyewe?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu na kupelekea kujiingiza katika vitendo vya rushwa na kuandika habari ambazo hazina usahihi na waandishi wa habari wamekuwa wakinyanyaswa, wakivunjiwa kamera, kupigwa mabomu ya machozi. Kwa kuwa kuna sheria zinazowalinda, hata hivyo, baadhi ya waandishi wa habari wamekuwa hawawezi kutoa habari muhimu ambazo kwa kiasi kikubwa zinahusu rasilimali watu na wengine wakitoa inapelekea kufukuzwa kazi au kupoteza ajira. Je, ni lini Serikali itahakikisha kuwa kuna sheria ya kuwalinda Waandishi wa Habari?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Majengo ya *TBC*. *TBC* ni chombo cha habari cha Taifa, wanafanya kazi katika mazingira magumu. Majengo yao ni machakavu, vitendea kazi vyao ni chakavu. Havikidhi haja na Serikali itambue kwamba *TBC* ni chombo pekee cha umma cha Utangazaji, hivyo kinahitaji kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi ya kawaida pia maendeleo. Ni lini Serikali itamaliza majengo ya *TBC* na kupata vifaa vya kisasa vyenye kujitosheleza?

Mheshimiwa Spika, usanii ni kioo cha jamii. Wasanii hawa wanaiga utamaduni wa magharibi kiasi kwamba wanapotosha jamii na kufanya utamaduni wetu uzidi kupotea na wasanii hawa wamekuwa wakiipotosha jamii baada ya kuielimisha kutokana na michezo wanayoigiza na nyimbo wanazoimba. Zimekuwa hazina maadili ya Kitanzania na mavazi wanayovaa yamekuwa hayaelimishi jamii. Je, Serikali kupitia Wizara hii wamewahi kutoa semina elekezi, kama wamewahi ni mara ngapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu lugha ya Taifa, Tanzania ndio kitovu cha Kiswahili lakini tumekuwa tukisahau kwa kutumia lugha za kigeni na pengine kupenda kuchanganya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine. Ukitazama matangazo mengi badala ya kutumia lugha ya Kiswahili wanatumia lugha za kigeni na kuwafanya wananchi wengi washindwe kuelewa hasa wananchi

wengi waliopo pembezoni hawaelewi vizuri lugha za kigeni au kutoelewa kabisa. Nchi nyingine zilizoendelea wamekuwa wakitumia lugha zao kwa mfano Japan, Ujerumani, Ufaransa, Korea na kadhalika. Je, ni kwa nini Tanzania tumekuwa tukiibeza lugha yetu ya Taifa na kutotoa kipaumbele kwa lugha hii?

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa ufupi sana juu ya uhuru wa vyombo vya habari. Uhuru huu utaleta matatizo na balaa huko tuendako. Hakuna nchi yoyote inayoweza kuacha kila mtu kusema na kuandika lolote analowaza tena kwa kutukana na kukashifu. Mauaji ya Rwanda *Genocide* yaliyosababishwa na matokeo ya habari zilizoripotiwa vibaya.

Mheshimiwa Spika, leo hii magazeti yanaweza kuthubutu hata kuandika uwongo, taarifa za Naibu Waziri kuvamiwa. Baada ya kuthibitisha ukweli haupo na Naibu Waziri huyo alikuja humu ndani ya Bunge akathibitisha kuwa ni uwongo. Je, suala hili kwa nini Wizara husika isilifungie gazeti lililoandika habari hizi. Vyombo vya Habari havipo hapa kwa maslahi ya Watanzania bali kwa maslahi ya wamiliki wa vyombo vyao. Hivi hakuna Sheria ya Udhibiti habari zinazoleta uchochezi na upotoshaji?

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ichukue hatua za kisheria kuvifungia kabisa vyombo hivi ili nchi yetu isije ikaingia kwenye machafuko ya sisi kwa sisi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Daktari Fenella Mukangara, Waziri na Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Naibu Waziri kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitumikia Wizara hii. Ni mategemeo yangu kuwa watajitahidi kwa kadri ya uwezo wao kukabiliana na changamoto nyingi zilizopo chini ya Wizara hii. Nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, tunalo bado tatizo kubwa la usikivu wa mawasiliano ya Radio kwenye maeneo mengi nchini. Maeneo mengi redio ya Taifa *(TBC)* husikika usiku pekee huku mchana usikivu ukiwa adimu. Ni vyema nia ya dhati ya kuboresha tatizo hilo ikapewa kipaumbele. Kutenga Sh. 500,000,000 kwa ajili ya uboreshaji wa usikivu ni kama mzaha, kumbukeni kila Mtanzania ana haki ya kupata habari na redio na televisheni ni njia rahisi ya Watanzania kupata habari.

Mheshimiwa Spika, pili, Halmashauri za Wilaya nyingi zimeajiri Maafisa Utamaduni ambao hawana mafungu wala vitendea kazi. Ni kwa nini Wizara hii mama kwa Maafisa Utamaduni, Vijana na wanahabari haitoi msimamo wake wa namna ya kuwaunga mkono na msimamo kwa maafisa wao ni vema ikijulikana kuwa kukosa kwa maafisa hao kazi, mafungu na vitendea kazi huwafanya kuhamia kwenye kufanya siasa badala ya mambo ya msingi wanayopaswa.

Mheshimiwa Spika, tatu, maslahi duni ya wanahabari kutoka kwa wamiliki wa vyombo vya habari, binafsi wana habari wanaofanya kazi kwenye vyombo vya habari binafsi hulalamikiwa kwa kupokea kitu kidogo na pia vitendea kazi duni. Aidha, kuna tatizo la mikataba isiyozingatia Sheria za Kazi kama vile *confirmation* na kucheleweshewa malipo na waajiriwa wao.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali kama msimamizi wa tasnia hii kupitia Wizara hii isidhibiti hali hii na hivyo kujenga heshima na kupunguza rushwa au kitu kidogo kwa wanahabari.

Mheshimiwa Spika, nne, nchi yetu ina tatizo kubwa la miundombinu ya upatikanaji wa habari kwa kukosekana sheria ya kupata na kutoa habari *the right of information* na Sheria ya Habari inayokidhi hali ya sasa. Matokeo yake Watanzania wengi waishio vijijini pamoja na kuwa na taarifa na habari nyingi ambazo zingesaidia sana kuijenga nchi yetu, lakini imekuwa vigumu sana kwao na hivyo sekta ya habari kutosaidia kuleta haki, uchumi na maendeleo. Habari nyingi

ni za mijini tu, tena pengine hata zile za kiwango cha chini cha umuhimu na kuachwa habari za vijijini zenye tija.

Mheshimiwa Spika, vijijini habari zao hutoka kwenye vyombo vya habari pale kunapokuwa na semina na ziara za viongozi tu kama vile Rais, Waziri Mkuu, Mkuu wa Mkoa na Mbunge. Kwa nini miundombinu rahisi isiwekezwe ili habari iwe haki ya kila Mtanzania na hivyo upatikanaji wake uwe rahisi ili mradi tu sheria hazikiukwi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja huku nikiwatakia Waislamu wote mfungo mwema na pia nawaombea marehemu wetu wa meli ya *MV. Skagit,* pepo ya milele na nafuu ya haraka kwa majeruhi wote.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri Mukangara na Naibu Waziri Mheshimiwa Makalla, Katibu Mkuu wa Wizara, pamoja na viongozi wa taasisi au asasi zilizo chini ya Wizara hii kwa hotuba nzuri pamoja na kazi nzuri ya kusimamia Wizara hii na taasisi au asasi zake.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mdau mkubwa wa lugha ya Kiswahili na nchi nyingi duniani zinajua kuwa Tanzania ni waasisi wa wataalam wa lugha ya Kiswahili. Tuna nafasi kubwa duniani kueneza lugha ya Kiswahili, lakini fursa hii hatujaitumia sawasawa, tungeweza kuwapatia Watanzania ajira ya kufundisha lugha ya Kiswahili Afrika na duniani kote. Nashauri Serikali ione umuhimu wa kuitumia fursa kubwa tuliyonayo, Serikali pia itimize azma yake ya kuona kuwa Kiswahili kinatumika katika mikutano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, *TBC* inafanya kazi nzuri toka imeanzishwa lakini inakabiliwa na changamoto nyingi. Majengo yake ni mabovu, mitambo yake imechakaa na ina vitendea kazi duni, kiasi kwamba wakati wa matangazo ya kuunganisha na watangazaji walioko katika maeneo ya matukio huchukua muda mrefu na wakati mwingine hushindwa kuunganisha.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linatia fedheha kwa *TBC* na Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo, nashauri Serikali isaidie *TBC* kikamilifu na kuipatia bajeti ya kuridhisha itakayomudu kutatua matatizo yanayowakabili ikiwa ni pamoja na kuwapatia mitambo ya kisasa na kuwaendeleza watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilihoji suala la kusimamishwa uongozi kwa Katibu Mkuu wa CHANETA Bi. Anna Kibira kwa zaidi ya miaka miwili na nusu kwa tuhuma kuwa Bi Anna alishirikiana kwa karibu na Chama cha Netiboli, Zanzibar (CHANEZA) jambo ambalo linasaidia kuimarisha Muungano, lakini uongozi wa CHANETA ukaona hilo ni kosa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza Waziri aliahidi kulipatia ufumbuzi suala hilo, lakini hadi sasa bado suala hilo halijapatiwa ufumbuzi. Wengi wetu tunajiuliza kulikoni? Naomba kupata maelezo kwa nini suala hili halijamalizika.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza *TFF* kwa kazi nzuri wanayofanya ya kusimamia shughuli za mpira wa miguu. Nawapongeza kwa kuendelea kuwavutia wafadhili na kujenga uaminifu kwa wafadhili hao. Naomba waendeleze uaminifu huo ili kuweza kupata ufadhili.

Mheshimiwa Spika, tuboreshe viwanja vyetu katika viwango vya Kimataifa ili na sisi tuweze ku-*host* mashindano ya Kimataifa kama vile *Africa Cup* na mengineyo. Kiwanja kama cha Kirumba kikiboreshwa kitakidhi haja, hivyo kiboreshwe.

Mheshimiwa Spika, ili tuendelee lazima tuwekeze katika *Football Academy*. *TFF* wasimamie hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kuandaa mipango mizuri iliyooneshwa katika hotuba yake ya bajeti kwa kipindi kifupi tangu alipoteuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kutoa msisitizo kwa Serikali, umuhimu wa Wizara hii katika kujenga mwelekeo na nidhamu ya Taifa letu. Mafunzo kwa vijana katika kujenga maadili na mshikamano wa Kitaifa unategemea sana ufanisi wa Wizara hii. Hivyo bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya Wizara hii haiendani na uzito wa ajenda hii.

Mheshimiwa Spika, Taifa bila mshikamano ni vurugu, angalia yaliyotokea katika nchi za Maziwa Makuu; Uganda, Rwanda, Burundi, Congo DRC na Sudan; lakini pia Somalia. Hayo yote ni kutokana na kukosekana kwa mshikamano wa Kitaifa ambao ni wajibu wa Wizara hii kulisimamia. Naomba watendaji wa Wizara hii waweke mipango madhubuti na fedha za kutosha zitafutwe kuwajenga vijana kimaadili na kimshikamano.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kumekuwepo na wimbi la vijana kutopenda kazi, lakini wanataka maisha ya raha. Vijana wanaanza kucheza *pool* tangu asubuhi, nani anawalisha? Nchi itajengwa na nani? Waziri alifanyie kazi hili haraka kwani baadaye haya ndiyo yanakuwa magenge ya kufanya maandamano yakitumiwa na wachochezi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali kwa kuajiri Mkurugenzi wa Maendeleo ya Vijana. Ni matumaini yangu sasa vijana wanaokosa nafasi ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu wawekewe utaratibu wa kujenga uwezo wa kujiajiri kupitia vikundi vya ujasirimali na kupewa elimu ya biashara na mitaji. Pia wale wanaohitimu elimu ya juu wajengewe ushujaa wa kujiajiri na kujenga ajira kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, wasomi wetu wengi bado hawajiamini kuwa wanaweza kujiajiri; wote wanaomaliza shule wanatafuta ajira kwenye ofisi. Elimu ya ujasiriamali ianze kufundishwa katika shule zetu kuanzia shule ya msingi hadi vyuo vikuu. Kimsingi kila taaluma inaweza kujenga ajira, vipi mwenye digrii ya kilimo, mifugo, biashara, ualimu analia kukosa ajira? *Mindset* ya vijana wetu lazima ibadilishwe.

Mheshimiwa Spika, ili vijana wengi waweze kujishughulisha vema *program* ya *SIDO*, ipanuliwe sana kwani itakuwa na uwezo wa kutoa mafunzo kwa upana zaidi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni kutovu cha Kiswahili ulimwenguni. Hata hivyo, kama nchi hatuelekei kuitambua tunu hii. Nchi za Maziwa Makuu zina mweleko wa kuhitaji Kiswahili kwa mawasiliano yao, lakini hatuchukui juhudi za makusudi kuhamasisha kuanzisha vituo vya kufundisha lugha hii na ukalimani katika nchi za nje. Hiki ni chanzo kikubwa cha mapato kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ajabu utakuta nchi kama vile Kenya ndiyo inachangamkia fursa hizi wakati wako mbali kwa viwango. Uwoga wa wananchi wetu kujaribu nyanja pana Tanzania kama nchi inapaswa ipigie upatu matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi kwa nchi za Maziwa Makuu na *SADC*. Hii ni kwa sababu Kiswahili ndio lugha pekee ya asili inayojumuisha makabila na lugha nyingi wakati nyingine zote ni za kikoloni.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa vyombo vya habari unaweza kutumika vibaya na kuharibu Umoja wa Kitaifa. Hisia za vyombo vya habari sasa matukio ya maafa na uovu ndiyo habari, yale masuala ya maendeleo siyo habari! Vyombo visaidie Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Wizara kwa kusimamia shuguli za Wizara hii kwa makini. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wa Wizara hii. Katika kuchangia hoja hii binafsi nitajikita katika maswali ambayo yatahitaji majibu ya kina toka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwanza, vyombo vya habari katika nchi yetu vimeongezeka kwa kasi ya kutisha, kuna magazeti mengi, kuna redio nyingi, kuna magazeti mengi na hata sasa kuna Televisheni nyingi, lakini suala la kujiuliza ni hili, kwa nini magazeti mengi yanapotosha habari? Je, ni kwa makusudi au ni uelewa mdogo wa waandishi wetu? Je, Serikali inachukua hatua gani ili kurekebisha hali hii?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni huu, Serikali ilete Muswada wa vyombo vya habari ambao utaweka Sheria ya kuwabana au kuvibana vyombo vya habari vinavyopotosha taarifa kwa makusudi kwa lengo la kuwalinda na kulenga watu wa kundi fulani katika jamii yetu. Kuhusu elimu ndogo kwa wanahabari; je, Serikali imeweka utaratibu gani ili kuweza kuvibaini vyombo vya habari na wamiliki wa vyombo hivyo kuweza kutoa ajira kwa watu waliosomea tasnia ya habari kwa lengo la kuleta ufanisi katika sekta hii?

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na magazeti ya udaku au pendwa; magazeti haya kwa kiasi kikubwa yanakiuka maadili ya Mtanzania kwa kudhalilisha na kudanganya baadhi ya habari. Hata hivyo, haya magazeti yamesababisha baadhi ya wanafunzi wasisome vitabu vya hadithi, ushauri au tamthiliya. Je Serikali imejipanga vipi ili kuyadhibiti magazeti haya? Serikali haioni kwamba magazeti haya yanachangia kwa kiasi kikubwa kumomonyoka kwa maadili hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, kila siku kuna taarifa ya rushwa katika vyombo ya habari, swali la kujiuliza ni kwa vipi Serikali kupitia Wizara hii imelishughulikia vipi suala hili? Je, Waziri anafahamu kuwa kwa sasa tasnia ya habari inaongoza kwa rushwa, posho, ushabiki na hata udanyanyifu hapa nchini? Je, hali hii itaendelea mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, suala la ushabiki katika sekta hii ya habari hupotosha ukweli wa mambo katika nchi yetu, je, Wizara kupitia Serikali Kuu au hata vyombo vya usalama inadhibitije Wanasiasa uchwara wanaotumia vyombo vya habari kuendeleza malumbano katika nchi yetu? Baadhi ya vyombo vya habari hasa magazeti na Televisheni huchochea uchochezi katika nchi yetu. Hali hii inaweza kuhatarisha amani katika nchi yetu. Je, Serikali kupitia Wizara hii inatoa kauli gani?

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vingi vimezagaa mijini na si vijijini. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi ili kuhakikisha kuwa vyombo vya habari vinakusanya taarifa toka vijijini na kuarifu umma juu ya taarifa hizo? Vyombo vya habari vya watu binafsi vimejikita katika biashara, hali hii imepelekea baadhi ya watu kushindwa kuitoa taarifa muhimu katika nchi yetu. Je, Wizara ina mpango gani wa kudhibiti bei za matangazo na taarifa muhimu ili kuwe na kiwango maalum kinachotozwa kwa kila chombo?

Mheshimiwa Spika, napenda kuwasemea vijana kwamba, kwa nini katika nchi yetu hakuna Sera ya Vijana? Je, sera hii itaanza lini? Malengo ya sera hii yatakuwa ni yapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana na ajira, nukuu; kijana wa Afrika nina balaa?

- Chochote ninachokifanya kinanikatisha tamaa.
- Kikiwa deiwaka mpiga debe, kila siku nitaamkia korokoroni.
- Nikijiburudisha na gongo, ni kifo cha ajabu.
- Nikijiingiza kwenye ukahaba, natozwa kodi ya kichwa.
- Nikitaka kuwa changudoa, miwaya inanisubiri ininase.
- Nikitaka kuwanadi wagombea, wananitumia kama kondom.
- Nikitaka kuwa mkulima, ukame unanyemelea mazao.

- Nikitaka kuwa mwanamichezo, migogoro imejaa vilabuni.

Sasa nifanye nini ili nipate ajira?

Mheshimiwa Spika, swali, Wizara ina mkakati gani ili kuwaandaa vijana kujenga mazingira ya kujiajiri kuliko kutegemea ajira ambayo haipo?

Mheshimiwa Spika, vijana Watanzania walalamishi, ni kweli vijana wa Tanzania wanaongoza kwa ulalamishi, hakuna fikra! Hakuna maandamano yasiyo na tija. Je, Wizara imejiandaa vipi ili kuepuka kujenga Taifa na kizazi cha walalamishi katika nchi yetu? Je, Vijana wa Tanzania wana maadili yasiyo mema? Kama ndiyo kwa nini? Je, Serikali kupitia Wizara hii imejiandaa vipi kukabiliana na tatizo la mmomonyoko wa maadili katika nchi hii? Je, Wizara hii inashirikiana vipi na Wizara ya Elimu ili kufundisha somo la maadili mema mashuleni?

Mheshimiwa Spika, kwa nini hakuna jeshi la vijana hapa nchini? Kwa nini hakuna benki ya vijana hapa Tanzania? Je, kwa nini Serikali isianzishe kongamano la vijana nchi nzima angalau kila baada ya miaka mitano ili vijana wapate kufahamiana na kujadili matatizo yanayowakabili. Je, rasilimali za Taifa kama vile madini, wanyama, mito, misitu, bahari, maziwa na mabonde, zinawanufaishaje vijana wa Tanzania ili waweze kumiliki rasilimali za Taifa?

Mheshimiwa Spika, kupitia Wizara hii Serikali inakabilianaje na tatizo la madawa ya kulevya linalowaandama vijana hapa nchini? Naomba kuusemea utamaduni. Je, Wizara hii ina sera ya utamaduni wa Taifa? Je, kwa nini hatuna *cultural tourism* kama zilivyo nchi zingine za Afrika kama vile *South Africa?* Wizara hii inaienzije Fasihi ya Kiswahili ambayo ni sehemu kubwa ya ukombozi wa Mtanzania katika fani zote za siasa, uchumi na kijamii?

Mheshimiwa Spika, je, Wizara imefanya juhudi gani ili kuendeleza au kupiga vita baadhi ya mila na desturi za Mtanzania katika kipindi hiki cha Sayansi na Teknolojia? Je, Serikali kupitia Wizara hii inahakiki vipi Wahubiri wa dini mbalimbali hapa nchini ambao wanachochea vurugu na hivyo kuhatarisha amani katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, naomba kuisemea Sekta ya Michezo. Kwa nini tunaendelea kutumia makocha wa kigeni katika timu zetu na vilabu vyetu, je, kwa nini tusifundishe Watanzania wetu ili makocha wazalendo wa kufundisha timu zetu? Mbona migogoro haiishi kwenye vilabu vyetu? Hapa Tanzania kuna michezo ya aina mbalimbali, je, ni mchezo gani wa kujivunia? Wasanii wetu wanavuja jasho!

Mheshimiwa Spika, Serikali inawanusuru vipi wasanii wetu na waimbaji wa nyimbo mbalimbali toka mikononi mwa wadhamini/*promoters* ambao wanawanyonya kila kukicha? Je, shindano la *Miss* Tanzania linalinufaishaje Taifa letu? Kuna haja ya kuendelea kuwepo kwa shindano hilo? Je, waandaaji wa shindano hili hulipa kodi yoyote Serikalini? Kama hawalipi kwa nini na wataanza kulipa lini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dokta Fenella Mukangara kwa kuteuliwa kuwa Waziri kamili katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwani inagusa shughuli za vijana za kila siku hususan michezo na utamaduni. Cha kusikitisha sana Serikali inaichukulia Wizara hii kama sio muhimu katika jamii hasa kwa kutenga bajeti ndogo. Kuwasaidia vijana ni vyema Serikali ikawekeza sana katika eneo hili, katika nchi yetu yenye takribani asilimia 67-70, vijana lakini hawana ajira na hawajui hatma ya maisha yao na Serikali haioneshi njia au mwelekeo sahihi. Ni vyema sasa Serikali ikajipanga kutatua tatizo hili la ajira kwa kuwekeza kwenye mafunzo ya michezo, vifaa, walimu, madaktari na viwanja ili vijana waweze kuelekeza fikra zao katika cheo hiki.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Serikali inatakiwa kuangalia ni suala la uhaba wa Maafisa wa Utamaduni katika maeneo yetu. Hii imesababisha kabisa tuanze kupoteza mwelekeo wa kuuenzi utamaduni wetu na utamaduni wa nje umeanza kuchukua nafasi. Taaluma ya habari ni muhimu sana katika nchi yetu, ni vyema Serikali ikawasaidia sana waandishi wa habari ili waweze kuandika habari zilizo sahihi na zilizokuwa na maslahi kwa Taifa letu na Serikali itengeneze utaratibu wa kuwashughulikia waandishi wote wanaopotosha jamii.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kurudisha michezo mashuleni kwani itasaidia sana katika kuibua vipaji vya watoto wetu tangu wakiwa wadogo na hivyo kujenga Taifa lenye afya na uhai kimichezo kwani michezo ni ajira kubwa. Pamoja na nia njema ya Serikali tatizo kubwa lililopo ni viwanja vya michezo na walimu wa michezo. Kumekuwa na matatizo makubwa sana ya maeneo ya viwanja vya michezo mashuleni kutokana na sababu kwamba, shule nyingi hasa za Serikali zimekuwa zikisajiliwa bila kutilia mkazo kigezo cha kuwepo kwa viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kigezo hiki ni mojawapo ya shule kupata usajili, bado Wizara ya Elimu imekuwa haitilii maanani kigezo hiki katika kutoa usajili wa shule za Serikali. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuhakikisha kwamba kila shule inayopata usajili ni lazima ioneshe eneo lililotengwa kama kiwanja cha michezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutokuwepo kwa viwanja vya shule, kuna tatizo la walimu wa michezo mashuleni. Serikali haijafanya juhudi za makusudi za kuwasomesha walimu wa michezo na matokeo yake tumekuwa tukikodi makocha toka nje ya nchi ambao wamekuwa wakilipwa fedha nyingi sana za kigeni, Serikali iachane na mtindo huu wa kukodi Makocha toka nje na badala yake iwasomeshe wazawa na kuwapa motisha na mazingira mazuri zaidi ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la vyombo vya habari na utendaji kazi wake, kumekuwa na kilio kikubwa sana kwa wahariri wa magazeti na hata Televisheni kwamba hakuna uhuru wa habari na kwamba Serikali imekuwa ikipenda kusikia habari zile tu ambazo ni *positive* kwake lakini si zile ambazo ni *negative*.

Mheshimiwa Spika, hii imesababisha wananchi walio wengi kukosa haki yao ya Kikatiba ya kupata habari na kutoa maoni ya namna gani Serikali ifanye kazi, kama hakutakuwa na habari ambazo zinakosoa Serikali badala yake ziwe ni zile nzuri tu, Serikali itawezaje kujirekebisha na kufanya kazi yake sawa sawa na ya kuwaletea wananchi wake maendeleo? Ni vema sasa vyombo hivi vikapewa uhuru wa kutoa habari za aina zote ili mradi ziwe ni habari za kweli na zilizothibitishwa na zisiwe zile za uzushi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, kumekuwepo na kutoamini habari zinaandikwa na vyombo mbalimbali hususan magazeti na kuviona vyombo hivyo kama sio chanzo au vyanzo vizuri vya kuaminika vya habari. Je, ni vyombo vipi ambavyo ni vyanzo vizuri vya habari?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maadili ya vijana; kumekuwa na wimbi kubwa sana la kuporomoka kwa maadili ya vijana wa Kitanzania hasa kutokana na kuchochewa na matangazo, picha, filamu na kadhalika, toka nchi za nje hususan Marekani na Uingereza. Ni kwa nini Serikali imekaa kimya na haikemei pale ambapo kuna magazeti yanapotoa picha chafu ambazo siyo mfano mzuri kwa vijana wetu? Ni kwa nini Serikali inakaa kimya hata pale Televisheni zinaporusha matangazo yanayodhalilisha jinsia moja hususan wanawake?

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini pia Serikali haikemei mavazi ya nusu uchi yanayovaliwa na wasanii wa filamu za Kitanzania ambao kwa kweli wanatia aibu nchi yetu hasa watoto wadogo wanapoangalia filamu hizi. Wanaovaa nusu uchi ni wasichana, kwa nini Serikali haitoi mwongozo kwa mavazi yanayotakiwa kuvaliwa na waigizaji wa Kitanzania kulingana na mila za Watanzania, naomba majibu katika hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashindano ya *Big Brother Africa*; katika hotuba ya bajeti ya mwaka jana, Wizara iliahidi na kukemea kwa nguvu zote ushiriki wa vijana wa Kitanzania kwenye mashindano ya *Big Brother Africa!* Cha kushangaza, pamoja na mashindano haya kukiuka kwa kiwango kikubwa maadili ya Kitanzania, bado washiriki toka Tanzania wameendelea kwenda na Serikali imekaa kimya. Naitaka Serikali itoe tamko leo hii ni kwa nini mashindano haya bado yameendelea kuwakilishwa na vijana wa Kitanzania mpaka sasa?

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, habari; Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upotoshaji mkubwa wa vyombo vya habari, hii inajumuisha na vyombo vinavyomilikiwa na Serikali, hali hii ni hatari inaweza kuzusha tafrani katika jamii, ni vyema itungwe sheria ili kudhibiti vyombo vya habari vinavyopotosha jamii.

Mheshimiwa Spika, pili, michezo; kumekuwa na uzorotaji mkubwa kwenye Sekta ya Michezo, watoto wengi hawafundishwi elimu ya michezo wakiwa wadogo. Hivyo, inawashinda kuwa imara katika michezo kwa sababu wanajifunza ukubwani ni vyema elimu ya michezo itolewe toka watoto bado wawapo shule ya awali. Ukosefu wa makocha wazuri na waamuzi, Serikali kutoweka kipaumbele katika Mikoa ambayo Kihistoria imekuwa ikitoa wanamichezo shupavu na mahiri, hii ina *demoralize young stars* na kuona kuwa michezo hailipi na wala haina vivutio.

Mheshimiwa Spika, tatu, utamaduni katika nchi yetu unazidi kupotea, kupitia vyakula, mavazi, sherehe, harusi na misiba. Nasikitishwa sana na jinsi ambavyo utamaduni wa Watanzania unavyozidi kumong'onyoka hususan katika misiba. Watu wanajipamba kama wanakwenda harusini na pale ni sehemu ya majonzi, ilikuwa ni kawaida ya majirani kupeleka chakula msibani, lakini siku hizi wafiwa ndio wanalazimika kuwaandalia chakula wanaokuja kuhani, huu siyo hali hii haiashirii majonzi.

Mheshimiwa Spika, suala la vijana; kumekuwa na wimbi kubwa la vijana ambao hawana ajira na hii inasababishwa na vijana wengi kukosa sifa ya kuajiriwa kwa sababu ya mabadiliko ya teknolojia, athari hii inapelekea kuwa na wimbi kubwa la vijana lisilokuwa na ajira. Hivyo kupelekea vijana kushindwa kuunda familia mapema na hivyo vijana wengi kuamua kupata watoto nje ya mfumo usio rasmi.

Mheshimiwa Spika, hivyo kusababisha kuongezeka kwa *Single parents* na hata pia *dependence ratio* kwa kuwa watoto hawa wanaozaliwa wanabaki kulelewa na mabibi na mababu, hivyo Serikali ina mkakati gani wa kuwaandaa vijana wa Tanzania ili waweze kukabiliana na soko la Ajira.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na michezo, kwa mwaka uliopita iliomba kuidhinishiwa shilingi billioni 18.5, kwa mwaka huu wa fedha Wizara imeomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 19.3, kiwango ambacho kinaweza kuonekana ni kikubwa. Lakini bajeti hii ni finyu na haiwezi kutosheleza mahitaji yote ya Wizara, Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha za Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ukizingatia kwamba Wizara hii inashughulikia mambo mapana ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, utamaduni ni jambo muhimu linalohitaji kutunzwa. Taifa letu lina makabila mengi yenye tamaduni tofauti zenye umuhimu mkubwa, tuhakikishe tamaduni zetu tunazienzi, watoto wetu tuwafundishe ili na wao wazidumishe katika vizazi vyao.

Mheshimiwa Spika, lugha yetu ya Kiswahili haitumiki ipasavyo, katika Mashirika mbalimbali ya Kimataifa likiwepo Shirika la Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na kwingineko, inakadiriwa kwamba zaidi ya wazungumzaji milioni 500 wanaongea Kiswahili. Kuna umuhimu mkubwa wa

kukiendeleza Kiswahili na siyo kuwaachia wenzetu Wakenya ambao inasadikiwa kwamba katika vyuo vingi nchi za nje walimu watafsiri wa Kiswahili siyo Watanzania bali ni Wakenya.

Mheshimiwa Spika, nguvu ya vyombo vya habari inafahamika kwa wengi, vyombo vya habari vikitumiwa vibaya vina madhara makubwa na vikitumiwa vizuri vinaweza kusaidia katika kuendeleza jamii yetu ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TBC* ndicho chombo cha Umma cha utangazaji, chombo hiki kinafanya kazi nzuri sana lakini kwa mazingira magumu sana. Jengo ni chakavu, vifaa vimechoka na ni vichache fedha iliyotengwa ni shilingi milioni 500 itolewe kwa wakati ili *TBC* iweze kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi. Aidha, *TBC* itafute mbinu za kujiongezea kiasi hicho cha fedha kwa kuuza muda wa kurusha matangazo na vipindi ili kupunguza changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi hapa Tanzania wanaishi vijijini, wengi wao hawana uwezo wa kununua Televisheni, wapo ambao bado hawapati taarifa zozote kwa kupitia chombo chochote cha habari. Serikali iharakishe kutungwa kwa Sheria ya habari itakayosimamia tasnia ya habari nchini. Wahariri watapata uhuru wa kupata habari na wananchi haki yao ya msingi ya kupata habari, aidha, waandishi watazingatia taaluma, miiko ya utoaji habari na weledi.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zilizoendelea ukomo wa utumiaji wa mfumo wa analojia ni tarehe 17 Juni, 2015, kwa nchi za Afrika Mashariki, ukomo wa kutumia mfumo wa analojia ni tarehe 31 Desemba, 2012 na kuingia mfumo wa digitali. Hivi sasa kuna baadhi ya wafanyabiashara wanauza televisheni ambazo zinaweza kutumika tu katika mfumo wa analojia, hivyo wananchi watapata hasara kwani watashindwa kutumia televisheni hizo tutakapoingia katika mfumo wa digitali. Serikali iweke udhibiti wa hali hiyo kwani wananchi wengi wataumia.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuhamia mfumo wa digitali kwa kuharakisha majibu au maelezo ya Mheshimiwa Waziri hayaridhishi. Ni vema Serikali ikasubiri kidogo na kutoa elimu zaidi kwa wananchi.

**MHE. ANNA MARYSTELA J. MALLACK:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na michezo. Sote tunaelewa kwamba michezo ni kitu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu, kwani michezo ni burudani, michezo ni kuimarisha afya, michezo ni ajira. Tanzania tumekuwa tukibakia nyuma kimichezo, sababu hatujaweka kipaumbele kuanzia mashuleni. Naiomba Serikali iweke sehemu ya michezo kuwa ni lazima mashuleni na siyo hiari kwa mtu anayejisikia kucheza, michezo iwekewe kipindi shuleni kuanzia shule za awali (chekechea).

Mheshimiwa Spika, Serikali ihamasishe vijana wote kujiunga na michezo hata wale waliomaliza kusoma na kukaa mitaani bila shughuli ya kufanya kwa kutoa mashindano ngazi ya Kata, Tarafa hadi Wilaya. Hii itasaidia hata kwa vijana kutokaa bila shughuli ya kufanya na kuendekeza uzururaji na vitendo viovu kwa sababu muda mwingi watakuwa watu wa mazoezi, pia kutafuta vipaji kusiishie tu mikoa iliyoendelea watafute vipaji vya sanaa wazunguke Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye suala la vijana hapo ndiyo naguswa sana, maana hakuna kundi linaloteseka kama vijana. Tunapoongelea vijana tuangalie makundi yote ya vijana wapo vijana waliopo mitaani, wasio na ajira, wasio na mitaji, wasio na shughuli ya kufanya, wanaoishi bila kupata huduma muhimu za kijamii, wanaoishi bila kupata milo mitatu kwa siku, vijana wanatia huruma. Je, Serikali ina mpango gani na kundi la vijana wa aina hii ili wajikwamue katika umaskini uliokithiri?

Mheshimiwa Spika, ni miaka takribani saba sasa vijana waliahidiwa kuishi maisha bora kwa kila Mtanzania, lakini leo hii ni hawa hawa vijana tunawashuhudia wakiishi maisha duni. Hizi pesa za Mfuko wa Maendeleo unaotengwa katika kila Halmashauri zinamnufaisha nani? Inasikitisha sana vijana wanahangaika, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vijana mikopo ya masharti nafuu ili wajiajiri?

Mheshimiwa Spika, utamaduni ni suala pana sana, utamaduni wetu wa Kitanzania unafahamika kutokana na makabila yote ya Tanzania kupitia lugha, vyakula na mavazi, lakini Wizara itakubaliana na mimi kwamba Watanzania tunapoteza utamaduni wetu na zaidi tumebakia na utamaduni nadharia tu. Yote hii hutokana na tabia za kuiga tamaduni za nje kwani tunaiga mambo ambayo hayaendani na Taifa letu, mfano, mavazi.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wetu wa mavazi ni kufunika maumbile, lakini leo hii tunaiga mavazi ya hovyo ya kuvaa nguo za kubana maumbile na kuacha wazi maumbile ya ndani kama mapaja, matiti na kadhalika, kitu ambacho si utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyakula, tumekuwa tunasahau kula vyakula vya asili vyenye virutubisho kama mboga za majani, viazi vitamu, muhogo, maboga. Eti ukionekana kula vyakula vya mafuta mengi, pia vyakula vilivyotengenezwa kutoka nje tunaona ndiyo maendeleo, huko ni kuukana utamaduni wetu na siyo maendeleo bali ni ulimbukeni na una hasara yake.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia Wizara hii ilikomboe Taifa hili la Tanzania kwa kuuenzi utamaduni wetu kwa kutengeneza chombo cha kusimamia sanaa na utamaduni wetu wa Kitanzania ili ulindwe badala ya kupotea. Serikali pia ipige marufuku akinamama kutumia madawa ya kukuzia matiti na makalio na dawa hizo zikamatwe na wahusika wachukuliwe hatua kali sana.

**MHE. RIZIKI OMARI JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa umahiri wao wa kuendesha Wizara hii kwa umakini mkubwa sana. Wizara hii imebeba dhana nzima ya kujenga jamii iliyo bora hasa katika kulinda mila na tamaduni zetu, lakini kwa hakika filamu nyingi za maigizo zinazooneshwa kwenye *TV* zinawapevusha vijana wadogo kwani wanaonesha wazi kila kitu kinachoonesha mapenzi bila kuficha kitu, hii hali sio nzuri.

Mheshimiwa Spika, mavazi yanayovaliwa leo Tanzania hii siyo yanayoendana na mila na utamaduni wa Mtanzania kwa nini Serikali isiweke sheria ya mavazi? Mbona inawezekana, wakati wa uhai wa Mzee Karume kule Zanzibar mbona iliwezekana kukemea kuhusu mavazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waandishi wa Habari wa kujitegemea malipo yao ni duni na hii ni kwa vile hawana mikataba. Hivyo naiomba Wizara iingilie kati ili waweze kupata stahili zao. Waandishi wa Habari ambao bado hawajaajiriwa malipo yao huwa ni madogo sana na pia hutegemea na stori wanazoandika na *Media* nyingine hupima stori ndiyo huwalipa. Huu ni uonevu mkubwa unaofanywa na baadhi ya vyombo vya habari ambao ndio waajiri.

Mheshimiwa Spika, naziomba *media* ziweze kutenga fedha (fungu) kwa ajili ya kuwasomesha waandishi wa habari. Matumizi ya *Digital* kutoka *analog* mbona ni mapema mno kwa nini tunafanya haraka, mbona nchi nyingine wanaanza 2015, sisi tuna haraka ya nini, hatuoni kwamba hili litatuathiri sana na hasa tulio wanyonge? Kuna wafanyabiashara ambao wameagiza vifaa vya *Analog* karibuni tu, hivyo mzigo huo wanaufanyaje, kuna maskini walionunua *TV* zao hawana uwezo wala imani ya kuitupa ili anunue nyingine, tunawafanyaje watu wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naiomba Serikali itenge bajeti maalum kwa ajili ya timu ya Taifa ili kutoa kipaumbele kwa mchezo huu wa mpira.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Vijana na Michezo ni moja kati ya Wizara muhimu katika Serikali ambazo zinaleta maendeleo endelevu ya nchi. Hivyo, Wizara inahitaji kuwa makini katika kusimamia mikakati yake na Watendaji wake ambao baadhi yao ni wazembe katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira na vijana, ni jambo la kusikitisha ambalo linawaathiri vijana kisaikolojia kwa kukosa kazi, hasa wale wanaomaliza vyuo hurandaranda maofisini kutafuta kazi, lakini hawapati. Wengi wao wanaamini mara wamalizapo chuo, kazi ni za ofisini, wakati hilo si kweli hasa kutokana na asilimia kubwa ya vijana wana mwamko wa kupata elimu na nafasi za

Ofisi ni chache, Wizara inapaswa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Wizara ya kazi ili muwe na mikakati ya kufanya silabasi au mitaala ambao utakaoweza kuwasaidia vijana hawa kuwapa *skills* ili wakitoka vyuo waweze kujiajiri wenyewe, pia ni vyema Wizara ya vijana wakati umefika wa kutoa taaluma na kuwaeleza vijana kazi ni popote na yoyote.

Mheshimiwa Spika, suala la viwanda, ni moja ya sehemu ya kuwapatia vijana ajira, Serikali iwe na mikakati ya kufufua viwanda au hata kuiomba Wizara ya Biashara na Viwanda kuwahamasisha wawekezaji waje kufungua viwanda ili vijana wetu wapate kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo nayo ni moja kati ya vijana kupata nafasi ya ajira, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete anatilia mkazo sana michezo hasa ya mpira wa miguu na yupo tayari kutoa mshahara wa kocha kutoka nje ili aje afundishe mpira.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza Watendaji wa chini ndiyo wanaodhalilisha michezo hapa nchini na kuwakosesha vijana nafasi ya kuajiriwa huko nchi za nje. Mfano, mdogo tu hivi karibuni mchezaji mzuri wa Timu ya Twiga ameweza kupata nafasi ya kucheza timu ya nchi za nje ambayo inampa mchezaji nafasi nzuri ya kuongeza kipaji chake cha mpira, kupata kazi na pia kuisaidia nchi kupata kitu kidogo. Wizara inapaswa kulitilia mkazo jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la utamaduni; kila nchi ina utamaduni wake na ni vyema kuutukuza hasa ukiwa nje ya nchi ili kuliweka Taifa katika *symbol* nzuri. Tanzania bado hatuko tayari kuulinda na kuuhifadhi utamaduni wetu hasa utakapoona filamu za Kitanzania zilivyo. Wasanii wa Tanzania sasa wanafuata mila na tamaduni za nje hasa Nigeria na Ulaya. Filamu nyingi za Kitanzania za siku hizi huwa kuna utamaduni wa uchawi na dini ya Kikristo.

Mheshimiwa Spika, hili si zuri kwani inaonesha kwamba Tanzania mambo yao yote ni ushirikina, wakati siyo kweli au kila kitu huwa ni kwenda Kanisani na kuwatumia maaskofu, wakati hilo si kweli. Pia ni vyema Wizara pamoja na Baraza la Sanaa wakawaeleza wasanii umuhimu wa tamaduni zetu ili vijana wazielewe na wazishughulikie.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wasanii wanawake wanakwenda kinyume na tamaduni zetu hasa kutokana na mavazi, mwili wote ni uchi kuanzia kifua, utaona matiti yapo nje na nguo ipo kwenye makalio. Aibu kwa mtoto au kijana wa Kitanzania kuwa katika hali hiyo. Ukienda mbele zaidi makumbatiano yamekuwa makubwa, huwezi kukaa na watoto wako wakati unaangalia filamu hizi. Badala ya kuwafunza watoto mambo mema, sasa tunawapotosha kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muziki wa taarab; Utamaduni wa Taarab unapotoka, kuanzia waimbaji hadi watazamaji, tabia mbaya ya kukata mauno kwa waimbaji na watazamaji haifai, ni aibu. Taarab sasa haina tofauti na dansa.

Mheshimiwa Spika, Wizara inabidi itoe elimu juu ya tofauti ya taarabu na dansi. Lugha inayotumika katika mashairi nayo ni mtihani, hakuna maficho, ukiangalia taarabu za zamani mafumbo yamefumbika, hata kuyachambua hujui. Siku hizi matusi yapo waziwazi, Wizara ni vyema mkalikemea hili kwani linahatarisha watoto ambao wanaziimba nyimbo hizi.

Mheshimiwa Spika, suala la vazi la Taifa bado Tanzania hatukupata vazi la Taifa, namwomba Waziri alieleze Bunge kwa nini mpaka hii leo Tanzania hatuna vazi letu? Nashauri ni vizuri Serikali kukaa na kujaribu kuunda vazi la Kitaifa ili nasi tukiwa ndani au nje ya nchi tutambulike.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na viwanja vya michezo, tukiweka hali nzuri ya viwanja tutaweza kupata wachezaji wazuri na pia uchumi wa nchi utaongezeka na siyo viwanja vyetu kuwa kama vya Majimbo. Wizara itenge fedha maalum kwa kujenga viwanja vingine vya kuwa katika hali ya *standard* za Kimataifa, pia kuwa na bajeti maalum ya kuripea viwanja.

Mheshimiwa Spika, suala la vyombo vya habari; ni muhimu sana katika nchi, lakini baadhi yao havifuati maadili, magazeti, *TV,* zipo nyingi lakini hupotosha taarifa ili kupata kuuza magazeti

yao au kumfurahisha mtu fulani, ni vyema waandishi kutumia kalamu zao kwa kuandika habari za kweli ili nchi iwe katika utulivu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwekeze katika tasnia ya michezo, kuwe na vifaa vya michezo katika mashule na pia viwanja viwe vingi vizuri vya kutosha na kuwe na walimu wa michezo waliobobea kwa kila mchezo. Kadhalika Serikali iweke jengo la sanaa na kuweka vifaa mbalimbali vya mila na tamaduni za makabila mbalimbali ya Tanzania, pamoja na Wizara kutunga kitabu cha kueleza mila za Kitanzania na tamaduni zake ili vijana na watu kutoka nje wazifahamu.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Kwanza, ifanyike *study* kuona namna sekta ya muziki inavyoweza kutoa mchango katika pato la Taifa na uchumi kwa ujumla. Wizara itambue kuna wasanii wangapi na kazi zao na mapato yao kama njia ya kutengeneza mfumo wa kuifanya sekta hii kutambulika katika sekta za uchumi kama zilivyo sekta zingine. Ningependa kuona siku moja kwenye kitabu cha hali ya uchumi tunaoneshwa mchango wa sekta ya sanaa katika pato la Taifa na ajira ni kiasi gani, tengenezeni mfumo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uhuru wa habari uliopo, bado uhuru huu haujawekwa kwenye mfumo wa kisheria. Nashauri Serikali ikamilishe haraka sheria ya habari ili kufanya uhuru huu kuwa rasmi na kudumu. Lugha ni uchumi, Lugha ni teknolojia, nashauri mtengeneze mfumo kuhakikisha lugha ya Kiswahili inapata nafasi ya kutosha katika dunia ya sasa.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika mikutano ya Kimataifa kuna lugha mpaka sita zinatafsiriwa, lakini hakuna lugha hata moja toka Afrika, Kiswahili kinapaswa kuchukua nafasi hiyo na tuone fahari kuwa Waswahili badala ya kunyanyapaa lugha yetu na kuona fahari kutumia lugha ya mkoloni. Mikutano ya *common wealth, IPU-Inter Parliamentary Union*.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iongeze nafasi ya Vyama vya Siasa katika mbio za mwenge, Mwenge unapaswa kuendelea kuwa alama ya Taifa, mkifanya mkakati kuhakikisha mwenge unabeba dhana ya Utaifa kuliko Chama fulani mbio hizi zitaendelea kuwa chombo muhimu sana katika ujenzi wa misingi ya Utaifa na Taifa lenye historia duniani.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana ni muhimu sana, Serikali ikamilishe mchakato wa kuanzisha Baraza hili hasa katika kipindi cha sasa ambapo vijana wanagawanyika zaidi kwa misingi ya Vyama, dini na kabila. Hiki kitakuwa chombo muhimu sana katika kujenga Taifa lenye nguvu. Hali ya sasa ya kuanza kuibuka kizazi cha kizembe na uwajibikaji duni inaweza kufanyiwa kazi kama Baraza litaanzishwa na kujielekeza katika *philosophy* ya ujenzi wa vijana kama jeshi la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Wilaya mpya ya Uvinza kuna majengo makubwa mawili yanaitwa *centre* za vijana, lakini *centre* hizo hazifanyi kazi ingawa majengo ni mazuri. Nashauri Wizara itusaidie zana kama za ufundi stadi na teknolojia bora ya ushonaji na ufumaji kwa kuanzia ili vijana watumie vituo hivi kujipatia ujuzi badala ya kuacha majengo yachakae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja na naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote kwa hotuba nzuri inayotoa matumaini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa masuala ya vijana bado Serikali haijawapa kipaumbele kutokana hasa vijana wa vijijini na ndio wote hukimbilia mjini kuja kutafuta kazi. Ningeomba Wizara yako kuhamasisha vijana kubakia vijijini kwani wao ndio nguvu kazi ya kutegemewa, lakini pia Wizara kushirikiana na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kuhamasisha kwa upatikanaji ardhi ya kilimo, kupatiwa vitendea kazi na hata kuwapatia Maafisa Ugani kwa kila Kata ili iwe wepesi kufika vijijini kwa kutoa msaada.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa vyombo vya habari sasa imekuwa kero kwa jamii, tuchukulie taarifa iliyotoka kwenye magazeti pamoja na vyombo vya habari kwamba ‘’Tanzania tayari itaingia gizani” na suala hili limekanushwa na Waziri wa Nishati. Je, Wizara mnaliona hilo na tayari limekanushwa na Serikali na hao walioandika uchochezi huo wanafanywa nini? Tayari wamekwishaipotosha jamii ya Watanzania na kuwaathiri kisaikolojia.

Mheshimiwa Spika, kivazi cha utamaduni wa Mtanzania; Wizara ilikuwa na matangazo kuhusu kivazi cha Mtanzania rasmi, je, kivazi hicho kimefikia wapi mbona kimya au ndiyo ule usemi kimya kingi kina mshindo mzito? Ningeomba maelezo lini kivazi hicho kitatumiwa rasmi kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya, burudani na kufahamiana (undugu) hivi bado Wizara ina kazi kubwa kutafuta vipaji vya vijana wetu kwa kutembelea mashuleni kutafuta vipaji vya vijana kwa michezo mbalimbali kama mpira wa miguu, *netball, cricket, volleyball,* sarakasi na kadhalika. Kwani vipaji hivyo vipo katika shule zetu kuanzia msingi, sekondari hadi vyuo. Wizara lazima tuchacharike ili kuifanya Tanzania kuwa na vijana wenye vipaji bora ili kuifanya Tanzania na michezo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHERI KHATIBU AMEIR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyopo hapa juu. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uteuzi kwa kuongoza Wizara ya Habari. Wizara hii ni muhimu kwani ndio Wizara inayohabarisha mambo mbalimbali ndani ya nchi na nje. Napenda kuwaonya na kuwatahadharisha wale wanaopotosha ukweli wa baadhi ya taarifa au mambo na kufanyia kazi waajiri wanayodhamira potofu.

Mheshimiwa Spika, mfano, *ITV* sasa imekuwa sio chombo cha kutoa habari na kuwaelimisha watu bali kinafanyia kazi zaidi ya kupotosha baadhi ya mambo hasa tunapokuwa na chaguzi ndogo. Sikufurahi kwa mtindo uliokuwa na upendeleo wa chama fulani badala ya kudumisha wananchi wapige kura.

Mheshimiwa Spika, *TBC* hivi sasa haiko vizuri, yaelekea vyombo vyake na majengo vimechakaa. Hii ni TV ya Taifa lazima iwezeshwe iwe na uwezo zaidi kuliko *TV* za watu binafsi na watangazaji wawe na upeo wa utashi mkubwa wa kazi zao, lakini tatizo ni vifaa na kuwawezesha kimaslahi watangazaji wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vijana, Mheshimiwa Waziri hakujikita hasa na suala la maisha linalowakabili vijana. Naomba Wizara ijiimarishe zaidi kuinua ajira za vijana kupitia vijana na michezo. Michezo sasa ni ajira, naomba mfungue dirisha la vijana kuwasaidia kwa kuwahamasisha na kwa kuwapa vifaa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa hakuna tena riadha Tanzania, wakimbiaji hakuna, tumekuwa ni wasindikizaji wakati wote na hapawi na sura ya michezo na kuwepo kwa Wizara hii alimradi tuende tu. Nashauri Wizara ijipange tena Mawaziri mliopo ni vijana mna nguvu wasomi, mnaufumbuzi. Mnachotakiwa mtumie utaalam na muwe wabunifu.Watanzania wakichoka na nyie mtachoka jitahidini mvute kamba. Tunawatakia kazi njema na kutimiza malengo mliyojipangia.

**MHE. ASHA MOHAMED OMAR:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya habari kwa hatua nzuri ya habari na utangazaji kwa Shirika lake la *TBC* Taifa, *TBC* ni ya kuigwa kama mfano. *TBC* imejipanga vizuri kwa sababu kule Zanzibar Kisiwa cha Pemba *TBC* zote redio na *TV* zinapatikana vizuri sana mpaka vijijini kote Pemba.

Mheshimiwa Spika, wakati Zanzibar kuna *TV* yake lakini *TV* hii katika Kisiwa cha Pemba haipatikani wakati *TBC* inapatikana katika Kisiwa cha Pemba vizuri tu. Sasa naiomba Serikali itazame kwa jicho la huruma Shirika hili la Habari la *TBC* ili liweze kuelimisha jamii ya Watanzania kwa sababu tunajua kwamba matatizo mengi wanayo ikiwemo ufinyu wa fedha ya kujiendesha.

Tatizo lingine la *TBC* ni baadhi ya vifaa ambavyo vimechoka lakini pia jengo ambalo limejengwa limeachwa linachakaa bure halimaliziwi, kwa hiyo, Serikali tunaiomba lile jengo limaliziwe.

Mheshimiwa Spika, suala la utamaduni; utamaduni wetu wa Tanzania umepotea na unazidi kupotea, tunaiomba Serikali ipige vita mambo machafu wanayofanya vijana wetu wasanii ambao wanatukashifu sisi wanawake wenzao, tunaona haya kwa nini wanavaa nguo za maajabu uchi wa mnyama, mbona wasanii wa kiume wanavaa nguo zao vizuri. Kwa hali hii tutakuwa tunapoteza Taifa lenye heshima.

Mheshimiwa Spika, vijana ndio Taifa la leo na kesho. Hivyo, vijana wapewe kipaumbele, wapewe elimu ya ujasiriamali ili waweze kujikusanya pamoja na kujiajiri wenyewe, tuepukane na Taifa la vijana vibaka na wavuta unga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nashauri vijana wapewe elimu ya ujasiriamali ili waweze kujitegemea badala ya kuendelea kukaa vijiweni na kukimbilia mijini. Vijana wapewe mafunzo ya uzalendo wa nchi yao, maadili ya Kiafrika waache kuiga utamaduni usiofaa toka nje. Vijana wawezeshwe kwa kupewa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la habari. Waandishi wa Habari wawezeshwe kufika vijijini ili kutoa habari za vijijini. Waandishi wa habari waandike habari za kweli bila kufuata ushabiki wa vyama ikiwezekana kuwepo na waandishi wa habari ngazi ya Tarafa.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuhusu suala la utamaduni. Naiomba Serikali ijitahidi kuwa na utaratibu wa kushindanisha Tamaduni za vijijini ili kuinua vipaji vya wananchi wa vijijini. Utamaduni wa asili wa makabila yote, Serikali iendelee kuuhifadhi kuuendeleza na kushindanisha. Maafisa utamaduni wawepo hadi ngazi ya Kata.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuwasilisha hotuba nzuri na yenye mwelekezo wenye matumaini. Inasikitisha kuona uchakavu siyo tu wa majengo ya *TBC,* bali pia mitambo yake, misingi ambayo imepitwa na wakati, uchakavu wa mitambo hii huenda ndiyo inachangia usikivu hafifu wa *TBC* katika maeneo ya nchi na badala yake redio binafsi kama vile *redio one* kusikika vizuri zaidi, Serikali itenge fedha za kutosha kwa kuzingatia umuhimu wa *TBC* ili kununua mitambo ya kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba Wizara ilifahamishe Bunge hili manufaa ya Mkataba kati ya *TBC* na *Star media (Tanzania) Limited.*

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya michezo, Kimataifa Tanzania daima imekuwa ni msindikizaji tu kutokana kwa kutowekeza vya kutosha katika michezo kuanzia shule za msingi ili kuibua vipaji. Naishauri Serikali iwekeze vya kutosha ili kuinua kiwango cha michezo nchini kuanzia ngazi za shule za msingi.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwao na pia kwa hotuba nzuri waliyowasilisha hapa Bungeni leo na naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Sanaa ikiwezeshwa vizuri, inaweza kutoa ajira kwa watu wengi sana na kuongeza pato la Taifa kwa kuchangia kodi. Naishauri Serikali iwekeze kwenye vyombo kama *BASATA* na *COSOTA* ili hakimiliki ya wasanii ilindwe ipasavyo, lakini pia Sheria ya Hakimiliki irekebishwe ili kuzilinda ipasavyo haki hizo.

Mheshimiwa Spika, pia mfumo wa kodi kutokana na kazi za Sanaa kama mikanda na santuri uboreshwe. Leo hii filamu za Kiswahili zinaonekana duniani kote kupitia *cable TV* kama

*(Africa Magic Swahili).* Je, Tanzania tunafaidika vipi na ukuaji huu wa Sekta ya Sanaa? Serikali isiache sekta hii ikue yenyewe kivyake, iiongoze vizuri ili kila mdau afaidike (*win-win situation*).

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanapenda mchezo wa *football.* Je, Sisi kama Taifa tunaukuzaje mchezo huu? Napendekeza tuwekeze kwenye *training and nurturing of talents*. *For instance we could use the prisons* kama *training academics* kwa kuwa wao wana mtandao nchi nzima, wana mashamba na hivyo upatikanaji wa chakula na maeneo ya viwanja siyo tatizo sana.

Mheshimiwa Spika, tujaribu kwa Kanda moja baada ya nyingine, tufanye s*couting* ya watoto wenye vipaji na walelewe na kusomeshwa katika shule huku wakiwa kwenye hizi *soccer/sports academics*. Tutengeneze mfumo mzuri wa kupeleka vijana wetu kwenye vilabu vya nje ili watangaze nchi yetu Kimataifa na pia walete fedha za kigeni nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu na viongozi wanatukanwa sana na vyombo vya habari. Hatuwezi kusema tubane uhuru wa vyombo vya habari, la hasha! Sema tunaweza kutengeneza utaratibu mzuri zaidi wa kudhibiti tabia hii ya baadhi ya vyombo vya habari vilivyobobea katika kuchafua Serikali na viongozi. Utaratibu huu ni kama ifuatavyo (ninavyopendekeza). Kuwe na *press secretary* (pale maelezo) ambaye awe na nguvu kukitaka chombo kuthibitisha ama kusafisha jina la mtu aliyechafuliwa na kama akishindwa kuwe na adhabu mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Adhabu za faini, ama kuzuiliwa kutoa *a certain number of copies for a certain prescribed time;*

- Utaratibu wa sasa hauna *deterrent effect* ya maana kwenye *Media Houses* ndiyo maana wanaendelea kufanya makosa mbalimbali ya kiuandishi kwa makusudi tu; na

- Izingatiwe kuwa Vyombo vya Habari vina athari kubwa sana katika kulinda usalama, amani na utulivu wa Taifa. Tusizembee kwenye eneo hili la udhibiti, tutaangamia!

Mheshimiwa Spika, mwisho karibuni kwetu Nzega mwezi Novemba kuna Tamasha la Utamaduni wa Watu wa Nzega (Wanyamwezi na Wasukuma) linaloitwa *Mtukwao Festival (www. Mtukwao. Org).* Ahsanteni.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Pia natoa pongezi sana kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Michezo cha Mlaya kimekuwa hakipati *OC* kwa zaidi ya miaka miwili, hivyo kukifanya Chuo kiwe tegemezi na kishindwe kutekeleza majukumu yake. Je, ni kwa nini Serikali haipeleki pesa za *OC*?

Mheshimiwa Spika, kutokana na Chuo kupanuka, lipo tatizo la usafiri kwa Wanachuo wanapotaka kwenda kujifunza mafunzo nje ya Chuo. Serikali ina mpango gani wa kukipatia Chuo usafiri kama vile *Min Bus*?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mwaka 2012/2013 Wizara kupitia Chuo cha Michezo Malya, ilisema itaendesha mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ufundishaji Michezo na Stashahada ya Uongozi na Utawala wa Michezo kwa Wanachuo 40, Serikali inanihakikishiaje upelekaji wa pesa kwa ajili ya kukiendesha Chuo?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 kulikuwa na mchakato wa kuwa na Vazi la Taifa, napenda kujua mchakato huo umefikia wapi? Au ndio basi! Kwani hivi sasa sisikii matangazo kama ilivyokuwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiuliza mara kwa mara: Je, ni lini hasa Sheria ya Vyombo vya Habari italetwa Bungeni?

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Taifa ulijengwa kwa gharama kubwa, lakini kiwanja hicho sasa kimekuwa kama kiwanja cha mazoezi, gharama ya kukitunza ni kubwa tofauti na pesa inayolipwa kutokana na pesa za mazoezi ya timu za kwetu.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kitu gani kinachosababisha hadi leo uwanja huo kushindwa kupata Taasisi ya kuendesha? Serikali kwa nini inang'ang'ania kuendesha uwanja huo? Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, hivi *BMT* ipo? Kama ipo, inafanya nini? Kwani vyombo hivi havisikiki.

Mheshimiwa Spika, navipongeza Vyombo vya Habari vyote vinatekeleza wajibu wake kitaaluma. Uandishi wa habari, ni taaluma.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa habari, vijana, utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara kwa kuteuliwa kuwa Waziri mwenye dhamana wa Wizara hii, mimi binafsi nilifarijika sana, kwani ninatambua uwezo wake. Naendelea kujivunia kuwa wanawake tunaweza, tupewe nafasi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nilifurahi sana kuteuliwa kwa mdogo wangu kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Amosi Makalla. Pongezi hizi nazitoa, kwani nafahamu uwezo wake, uadilifu wake na umakini wake. Kwa kushirikiana na Katibu Mkuu na Watendaji wote ndiyo sababu hotuba ya bajeti hii ni nzuri sana na inaonyesha kuleta maendeleo na ufanisi katika Taasisi zote ambazo zipo kwenye Wizara hii na Mwenyezi Mungu awape afya, nguvu na uwezo wa kutekeleza majukumu yao barabara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi zake kubwa za kuwasaidia vijana kupata ajira, ingawa wimbi la vijana wengi wasomi bado wapo mijini na vijijini wakihangaika, hawana ajira na hata uwezo wa kujiajiri wengi wao hawana.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kuhakikisha vijana wanaondolewa kwenye utegemezi na uzururaji kwa kupatiwa ajira, kuwezesha mitaji na elimu ili wajiajiri? Nasubiri Majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna ukweli usiopingika kuwa Mfuko wa Vijana kwenye Halmashauri nyingi ambao unatokana na Halmashauri kutenga fedha asilimia tano kupitia pato lake na Serikali kuchangia kila mwaka. Halmashauri nyingi hazitengi kabisa au hutenga kidogo sana jambo ambalo linakwamisha azma ya kuwakwamua vijana. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu jambo hili? Nasubiri maelezo, pia nielezwe Serikali huchangia kiasi gani kwa kila Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ombi kuwa bado kuna Halmashauri ambazo hazina Maafisa Utamaduni na vijana, wakati wasomi wengi wapo. Naiomba Serikali kuimarisha Utamaduni, Habari na Michezo katika Halmashauri zote kutoa ajira mapema iwezekanavyo. Vilevile kuna tatizo la Maafisa Utamaduni kutokuwa na *OC* ya kujiendesha, jambo ambalo linawafanya Maafisa hawa kushindwa kutekeleza majukumu yao, pia kuwa ombaomba. Nategemea majibu yenye kutia moyo kuhusu Maafisa hawa na Watanzani kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza washabiki na wadau wa michezo nchi nzima kwa jinsi ambavyo wamekuwa mstari wa mbele kuchangia fedha na vifaa mbalimbali vya michezo kwa kuwaunga mkono wachezaji wa ngazi zote Vijijini, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla. Naomba moyo huu uendelee na Serikali itoe kauli ya kuwatia moyo. Vilevile watu husema, "mcheza kwao hutunzwa", naiomba Serikali sasa, umefika wakati kuanzisha Mfuko wa Michezo kwa kila Mkoa ili kuunga mkono nguvu na moyo wa kujitolea kwa wadau wote wanaojitolea kuchangia michezo ili kuondoa ugumu wa timu nyingi kushindwa kushiriki ligi mbalimbali. Nasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la kuimarisha utamaduni nchini, napenda kuipongeza Serikali jinsi inavyojitahidi sana kuimarisha utamaduni nchini kwa kuweka siku ya utamaduni ya Kitaifa.

Napenda kuiomba Serikali kuimarisha utamaduni kwa kuwawezesha wasanii na kuwapa motisha pamoja na kusimamia mashindano kuanzia ngazi za Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa ili kupata wasanii watakaoweza kulitangaza Taifa letu pamoja na kudumisha mila na kuwapa ajira wasanii wetu pamoja na kuwapa nafasi ya kwenda kutangaza nchi yetu nchi za nje. Nitafurahi kupata maelezo ya Serikali na wasanii wasikie wakiwemo vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii ndiyo yenye dhamana ya kuwasimamia vijana, napenda kujua ni namna gani inawasaidia vijana katika suala zima la vijana kupambana na Ukimwi wao wenyewe na kusaidia jamii kwa ujumla. Nasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuitahadharisha Serikali suala linalojitokeza kwa waandishi wa Habari kukiuka wajibu wao wa kutoa taarifa mbalimbali kwa jamii pamoja na kutoa elimu mbalimbali ya mambo yenye maslahi na Taifa, badala yake wanaanza kutumiwa kuchafua watu na Serikali kwa ujumla. Inawezekana ni tatizo na ufinyu wa uelewa na taaluma. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa semina, warsha, makongamano, mafunzo mafupi na kozi ndefu ndani na nje ya nchi? Ni uhakika, tukiwasaidia waandishi wetu watabadilika na hali hii ya kuchafua watu magazetini itatoweka.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba mishahara ya waandishi wa habari pamoja na stahili zao zitazamwe kama watumishi wengine ili kuondoa rushwa, pia kuwapa moyo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana timu yetu ya *Twiga Stars* kwa uwezo mkubwa iliyoonyesha kupitia mpira wa miguu. Naomba Serikali iwape ushirikiano na misaada ili timu hii iendelee kupeperusha bendera ya Taifa letu na iwe changamoto kwa wanawake wengine nchini. Vilevile salamu hizi ziwafikie wadau wote walioshiriki kusaidia timu hii bila kumsahau Mama Tunu Pinda - Mke wa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa aliyofanya kuchangisha fedha za kuwezesha mashindano ya *Netball* nchini Tanzania. Mungu ambariki sana na aendelee na moyo huo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ikumbuke kusaidia kukamilisha ujenzi wa Kiwanja cha Mpira cha Namfua Singida ambacho ni muhimu, ili ligi mbalimbali za Kanda na Taifa ziweze kuendelea kucheza Singida, kuleta pia raha ya michezo na kuinua michezo Singida, maana Mkoa wetu una vijana wenye vipaji vya michezo ya mpira, mbio na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii nikitegemea mchango wangu utapokelewa na kufanyiwa kazi.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, ajira ni tatizo kubwa hapa nchini. Vijana wengi waliohitimu Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo mbalimbali wana tatizo kubwa la ajira. Matokeo yake vijana wanahangaika kwa kukimbilia Mijini ili kutafuta ajira bila mafanikio. Aidha, wengine hulazimika kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu, ukahaba na mambo mengi yasiyofaa kama utumiaji wa madawa ya kulevya. Michezo ni sehemu ya ajira kwa vijana wetu hasa endapo itapewa kipaumbele kwa kutoa vifaa vya michezo na kuwa na wakufunzi wa michezo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara ishirikiane na Waheshimiwa Wabunge kwa kutoa vifaa vya michezo na kufanya utaratibu wa kutosha kuona michezo inadumishwa. Matokeo yake tutapata vijana wenye vipaji watakaoletea heshima Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Sekta ya Kilimo ikaboreshwa kwa kugawa ardhi kwa vijana na kuweka Vituo vya Kilimo ambavyo vitakuwa na wataalamu watakaosaidia vijana kulima kilimo cha kisasa. Ninashauri Vituo hivi vya Kilimo viwe na zana za kilimo ambazo zitasimamiwa na wataalamu wa kilimo. Vijana wapewe mashamba ambayo yamewekewa miundombinu ya umwagiliaji kwa vile hawana mitaji. Mwaka wa kwanza, wapewe mikopo kwa kupimiwa mashamba na mbegu, gharama za mikopo hiyo zilipwe wakati wa mavuno.

Mheshimiwa Spika, pia Sheria ya Sazi isimamiwe ili kila kijana afanye kazi badala ya kuzurura Mijini. Hii tukifanikisha, vijana watajiepusha na vitendo vya uhalifu ambavyo mwisho ya siku vijana wengi hujikuta wanatupwa jela badala ya kulijenga Taifa lao. Kwa vijana wa Mbarali wale ambao wamekosa ajira, baadhi nimejitahidi kutoa elimu namna wanavyoweza kujiajiri katika

Sekta ya Kilimo, kwa kuwataka waombe kupewa maeneo yanayofaa kwa kilimo katika vijiji vyao, Kata, Wilaya, hata nje ya Wilaya. Naomba kusaidiwa mikopo kwa vijana ili waweze kujiajiri wenyewe hasa kwenye Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kudumisha michezo Jimboni, nimeanzisha *Kilufi Cup* ambapo hushughulika na kuanzisha ligi kwa michezo ya mpira wa miguu *(football)* na mpira wa pete *(netball)* na tunahimiza michezo mingine. Michezo hiyo huanza ngazi ya vijiji, Kata na baadaye Wilaya. Napungukiwa na bajeti kwa ajili ya kununua vifaa vya michezo na uendeshaji wa michezo kwa ujumla. Mwaka 2011/2012 kiasi cha Shilingi milioni 15 zilitumika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuungwa mkono katika kupata vifaa vya michezo na fedha kidogo kwa uendeshaji michezo.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukurani. Ahsante sana.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja iliyoleta mbele yetu. Aidha baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea suala la kutosikika kwa Redio ya Taifa *(TBC)* pamoja na *Television* Wilaya mpya ya Kalambo. Ni mwaka wa pili mfululizo nikiwa Bungeni nikichangia kwa maswali, mchango wa kuzungumza na kwa kuandika, nikieleza jinsi ambavyo Jimbo langu la Kalambo na Wilaya mpya ya Kalambo wananchi wake kunyimwa haki yao ya msingi na ya kikatiba ya kupata habari hususan habari juu ya mambo ya nchi yao. Wilaya Mpya na Jimbo la Kalambo lenye jumla ya Kata 17, na jumla ya vijiji 126 kwa kiasi kikubwa inapakana na nchi za Zambia, *Congo DRC* na Burundi.

Mheshimiwa Spika, Matangazo ya radio na *Television* chini ya *TBC* yamekuwa hayawafikii wananchi katika maeneo yote ya Wilaya mpya na Jimbo langu la Kalambo, kama nilivyoainisha kuhusu jiografia ya Wilaya mpya ya Kalambo na ukizingatia umuhimu wa kupata habari na mawasiliano kwa umuhimu wa kiusalama.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, Wizara haijachukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba habari zinawafikia wananchi wa maeneo haya. Wananchi wa Jimbo na Wilaya mpya ya Kalambo wamekuwa wakilazimika kusikiliza *local radios* ambazo nyingi ni za akina wanaharakati zaidi na hivyo kuwa vichocheo zaidi vya kutaka kukipinga Chama kilicho madarakani pamoja na viongozi wake.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu makubwa kwamba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hotuba ya Wizara yake, atatoa jibu kuhusu adha hii ya wananchi kukosa habari za kuhusu nchi yao, kukosekana kwa mpango mkakati wa kuhakikisha elimu inatolewa kwa vijana kushiriki kukuza uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Spika, jitihada za makusudi imebidi zifanywe na Wizara ili jukumu lake la kuhakikisha kwamba kundi kubwa la nguvu kazi ambalo ni vijana wanawekewa mazingira ya kushiriki kwa vitendo katika kujenga uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza unapokwenda vijijini na kukuta kazi za kilimo zinafanywa na wazee pamoja na watu wa umri wa kuelekea uzeeni, haiingii akilini kwa vipi vijana wanakuwa hawako tayari kupenda kushiriki katika shughuli za kilimo. Ni wajibu wa Wizara kuhakikisha inatimiza wajibu wake wa kisera kwa kuwahakikishia vijana wanashiriki shughuli za uzalishaji mali.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kushukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi hotuba hii ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Suala la utamaduni katika nchi yetu naona kama limeachwa nyuma kwa sababu wale Maafisa wa Utamaduni waliopo Halmashauri, wamesahaulika kwa muda mrefu sasa. Sielewei kama

wamefutwa au la? Lakini inashangaza sana kuona zile ngoma tulizokuwa tunacheza kuanzia Shule za Msingi hazipo tena.

Mheshimiwa Spika, suala hili linasababisha vijana wengi na watoto wa Shule za Msingi na Sekondari kuishia kuimba *Bongo Flava* kwa sababu toka wanaanza Darasa la Awali mpaka wanamaliza hawajawahi kuona wanafundishwa ngoma au utamaduni wa Mtanzania. Naishauri Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Elimu ili waweze kurudisha suala la utamaduni mashuleni.

Mheshimiwa Spika, upande wa vijana sielewi ni kwanini katika Halmashauri zetu hatuna Ofisi wala Maafisa wa vijana. Kuna dhambi gani kuwa na Afisa vijana katika Halmashauri zetu? Naishauri Wizara ione umuhimu wa kuwa na Maafisa wa Vijana, vinginevyo vijana wataendelea kuwa na matatizo mengi na hawana mtu wa kuwaelimisha wala kuwasaidia kimawazo. Namaliza kwa kuishauri Wizara ione namna ya kudhibiti Vyombo vya Habari, hususan magazeti, kwa kuwa mara nyingine wamekuwa wanaandika habari ambazo zinachochea jamii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwa hotuba nzuri, lakini pia napongeza Wizara kwa kubuni dodoso kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ili wapate habari na hisia za Wabunge kuhusu changamoto za vijana, kwani changamoto hizi zinatofautiana kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Spika, hali ya vijana walisoma na wasiosoma ni *time bomb* ambalo ni lazima Serikali ifanye mikakati ya haraka kulishughulikia kulizima ili nchi iwe salama. Wengi wa vijana wamemaliza Darasa la Saba, wengi wako vijijini bila kuwa na shughuli ya kufanya. Serikali inapoteza nguvu kazi muhimu sana. Lakini pia unakuwa ni mzigo mzito kwa wazazi.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali isianzishe mashamba ambayo yatatayarishwa na Serikali kutumia nyenzo za kisasa, iwape mbegu na mbolea, lakini pia ihakikishe kilimo hicho ni cha umwagiliaji ili kuhakikisha wanavuna? Baada ya mavuno, Serikali itoe gharama zote na faida wachukue vijana ili kuweza kuendelea kujihudumia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe vijana hao wanalima mazao ya chakula na biashara. Hii itaweza kutoa ajira nyingi sana. Vijana wanapenda pia kupata burudani mbalimbali ili wasione kupungukiwa na starehe za ujana. Serikali kupitia Halmashauri na vijiji, ianzishe *club* mbalimbali ili vijana hao wabaki nchini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania iliweza kupambana na kutokujua kusoma na kuandika kwa watu wote hadi vijijini. Hivyo kwa vijana waliomaliza Darasa la Saba Serikali kwa kutumia utaratibu ule ule inaweza kuwapatia elimu vijana hao waliomaliza Darasa la Saba na masomo ya Sekondari ili kuongeza kiwango cha elimu.

Mheshimiwa Spika, mitaala yetu sasa hivi haiangalii kumtayarisha mwanafunzi aweze kujiajiri. Hili ni kosa ambalo Serikali lazima ilirekebishe. Vijana ni lazima watayarishwe kujiajiri, na hili liingie kwenye akili za vijana.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaohitimu Vyuo Vikuu ni wengi na hakuna ajira za kuwatosheleza wote. Lakini vijana hawa wana taaluma mbalimbali, pia kuna vijana wanaomaliza katika Vyuo mbalimbali vya *VETA*na vingine mbalimbali. Vijana hawa wamepata mafunzo ambayo wangeweza kujiajiri bila tatizo, lakini wengi hawana mtaji au vifaa vya kuanza kujiajiri, lakini pia hawana dhamana ya kuweza kukopa katika vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifanye utaratibu ili kuwapatia vijana hawa mitaji na vifaa ili wasihangaike kutafuta waanze vipi. Lakini pia kwa sababu hawana dhamana, vyeti vyao vitumike kama dhamana ya mitaji na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali itachukua hatua hizo, itaweza kuwaokoa vijana wengi sana wanaozurura, lakini pia Serikali itaongeza pato la Taifa kutoka kwenye michango mbalimbali watakayotoa vijana hao.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ilivyoianzisha Benki ya wanawake, nashauri pia ianzishe Benki ya vijana ambayo itapewa mtaji wa kutosha na iwe na matawi kwenye Mikoa yote ya Bara na Visiwani. Ingawa inaweza kuwa ngumu kuanza na matawi Mikoa na Wilaya zote, zinaweza kutumika Benki nyingine kwa kuweka dirisha la vijana kama wawakilishi wa Benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, michezo kwa nchi nyingi ni ajira nzuri kwa vijana. Lakini pamoja na ajira, michezo pia inaeneza jina la nchi na utamaduni duniani. Hapa kwetu tumepuuza michezo, kuitoa kwenye mashule yetu kwa kuonekana ni upotezaji wa muda. Natoa rai, michezo irejeshwe mashuleni, siyo tu kuruhusu watoto kucheza, lakini iibue vipaji kwa kupeleka Walimu wenye taaluma ya michezo mashuleni.

Mheshimiwa Spika, michezo pamoja na kujenga afya ya watoto, pia itapunguza kutoa muda usio na kazi kwa vijana na hivyo kutoa nafasi ya vijana kujihusisha kwenye vitendo viovu kama uvutaji wa bangi na uasherati. Michezo italeta pato kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, vitendo vya mmomonyoko wa maadili vinaongezeka kwa kasi kubwa sana kwa vijana wetu. Tumeondoka kabisa kwenye mila na desturi za Kitanzania, Serikali imekuwa ikiachia uingizaji wa tamaduni za nje zisizofaa bila kukemea, mizizi mibaya imeanza kuota ambapo kijana mdogo haoni vibaya kutukana hovyo mbele ya wakubwa na hata wakati mwingine kumtukana mkubwa bila kukemewa.

Mheshimiwa Spika, siyo vibaya kuiga utamaduni wenye tija kutoka nje, lakini siyo kuruhusu vijana kuiga tamaduni zinazoleta mmomonyoko wa tamaduni zetu na maadili mazuri. Serikali ni lazima ichuje sinema na michezo iliyoko kwenye vituo vyetu vya luninga ili sehemu zisizofaa ziondolewe.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kumekuwa na upotoshaji mkubwa sana wa habari mpaka unaposoma gazeti, mtu unatia shaka kwa habari unayosoma. Magazeti yamekuwa yakiandika habari nyingi aidha za uongo na baya zaidi ni pale wanapoandika habari za uchonganishi hasa kwenye siasa.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari sana, kwani madhara ya uchonganishi ni kuleta uhasama ambao unaweza kuleta fujo na hata vifo. Magazeti yamekuwa yakitumika kuchafuana kisiasa, lakini hata wale wanaotafutana kimaslahi katika biashara au ofisini. Suala hili ni lazima liwekewe sheria kali ili lisituingize Tanzania kama Taifa, katika majanga ya Kimbari. Naomba Sheria ya Habari ije haraka iwezekanavyo.

Jambo lingine ni kuwa, muda wa majadiliano Bungeni ni mdogo, Bunge liandae muda wa kutosha kwa bajeti kwa sababu bajeti ina masuala mengi sana, kwa sababu Idara zote, yaani Vijana, Habari na Michezo na Utamaduni vyote ni muhimu sana. Ingepaswa ingepata hata siku tatu ili Wabunge waweze kuchangia kwa kina. Kujadili kwa siku moja ni kuiona wizara siyo muhimu wakati inahudumia asilimia 60 ya wananchi na inaendelea kukua.

Mheshimiwa Spika, vijana ni umri gani mwisho? Naomba Serikali ieleze inapoongelea vijana inazungumzia umri upi? Hii ni muhimu ili basi iwe *standard* kwa sehemu zote kwenye sheria, mahospitali, siasa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza na naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara kwa kazi nzuri chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Naibu wake Mheshimiwa Amos Makalla, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi na Watendaji wote chini ya Wizara. Baada ya pongezi hizo, napenda kutoa mchango katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara hii kuwa na sehemu nne muhimu zinazoisimamia, lakini bado fedha inazotengewa ni ndogo, ingawa katika mwaka 2011/2012 Hazina imejitahidi kutoa fedha zote zilizokuwa zimepitishwa kwa ajili ya *OC* na kiasi cha asilimia 92.8 za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutenga fedha zaidi za bajeti ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu katika sehemu ya utamaduni, suala la lugha likiwemo, kwa vile ndiyo njia ya mawasiliano kati ya binadamu, pamoja na kwamba nchini tumeamua kuwa lugha rasmi ni Kiswahili na ya kufundishia katika elimu ngazi ya Sekondari na Vyuo Vikuu kuwa Kiingereza, lakini ifahamike kwamba jamii ya viziwi wanapata matatizo ya kushindwa kuwasiliana na kushindwa kumudu masomo kwa vile wao lugha yao ni lugha ya alama.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, kwa vile nchi sasa inapitia katika mabadiliko na maendeleo katika sekta mbalimbali ambayo wananchi wanapaswa kushiriki, mfano utoaji mapendekezo ya Katiba Mpya, Sensa, upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa, Upatikanaji wa elimu bora, kampeni mbalimbali na kadhalika, nashauri lugha ya alama sasa itambuliwe kuwa moja ya lugha rasmi nchini ili kuwezesha viziwi kuondokana na kikwazo cha mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, inatia faraja kuona nchi inajaribu kufufua michezo mbalimbali badala ya kusisitiza mchezo wa mpira wa miguu pekee yake. Hata hivyo, ni kwa kiasi gani Wizara inahusika na michezo ya watu wenye ulemavu nchini? Naomba maelezo ya Wizara kwa sababu nadhani kwa sehemu hii watu wenye ulemavu hawawezeshwi vya kutosha katika mazoezi ya michezo na kadhalika. Kwa mfano, katika michezo ya Olimpiki itakayoanza Uingereza hivi karibuni, kuna mchezaji mmoja tu mwenye ulemavu. Je, walisaidiwaje katika maandalizi?

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu naunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, msingi muhimu wa maendeleo ya vijana ni upatikanaji wa ajira na fursa za kujiajiri. Bado Serikali haijaweka mikakati ya dhati katika kushughulikia tatizo la ajira kwa vijana hapa chini. Hata hivyo, fursa zinazotengenezwa zimekuwa ni chache mno kuliko kasi ya ongezeko la vijana wanaohitaji ajira kila mwaka. Mikakati na shughuli zinazotekelezwa na Serikali kwa ajili ya kutengeneza ajira kwa vijana, bado haijaweza kuondoa vikwazo vinavyosababisha vijana washindwe kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Vijana ili iweze kutoa mikopo yenye masharti nafuu, jambo ambalo mpaka sasa hatujapata taarifa ya utekelezaji wake na pia Serikali ituambie, kuna mikakati gani ya kuwezesha utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana pindi benki hiyo itakapoanzishwa?

Mheshimiwa Spika, mchakato wa upatikanaji wa Vazi la Taifa umeonekana kuchukua muda mrefu, jambo ambalo linapelekea utumiaji wa fedha nyingi zaidi bila mafanikio. Hata hivyo, mchakato huu bado unahitaji kushirikiana na kuzingatia makabila na tamaduni mbalimbali zilizopo katika nchi yetu huku tukitambua kuwa nchi hii ina makabila mengi na tamaduni zake.

Mheshimiwa Spika, michezo ni ajira na husaidia katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo Serikali inahitaji kuwekeza zaidi katika michezo kuanzia ngazi za Wilaya hadi Taifa. Michezo kwa sasa inaonekana inapewa uzito kwa ngazi ya Taifa tu na kuacha kuinua vipaji katika ngazi za Wilaya. Tunahitaji kuwa na mkakati imara kwa kuwawezesha Maafisa Utamaduni wa Wilaya ili kuendeleza michezo mashuleni kwa ajili ya kuandaa na kuibua vipaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji kuangalia michezo mingine mbali na mpira wa miguu. Kwa sasa mpira huu wa miguu ndiyo unaonekana kupewa kipaumbele na kuacha michezo mingine kama *netball, volley ball* na kadhalika, ili kutoa nafasi kwa vijana wenye vipaji hivi kuonyesha na kuibua vipaji hivi. Serikali itueleze kuna mkakati gani wa dhati wa kuinua michezo mingine iliyosahaulika?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa vijana wa *Kigoma All Stars.* Wanamuziki wa kizazi kipya wanaotoka Mkoa wa Kigoma wametunga wimbo wa '*Leka Dutigite'* na kushukuru wazazi wao na kuutangaza kiutalii Mkoa wa Kigoma.

Napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya, akina Mwasiti, Linex, Diamond, Baba Levo, Abdul Kiba, Banana Zoro, Rachel, Queen Darken, Makomando na Ommy Dimples. Pia *Producer* Tuddy Thomas. '*Leka Dutigite'* umeweka hamasa kubwa na kuweka heshima ya Mkoa wa Kigoma kimuziki. Wizara ishirikiane na vijana kama hawa ili kukuza ajira kuongeza mapato na kuendeleza Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kampuni za Simu za Mkononi zinawanyonya sana wasanii, kwani kampuni hizi huchukua 75% - 80% ya mapato yote ya muziki ulio kwenye miito ya simu. Msanii ambaye ndio mwenye wimbo anapta asilimia 7% tu ya mapato hayo. Serikali iweke utaratibu ambao, mikataba ya huduma hii itakuwa inatenda haki kwa msanii. Kwa mfano, tuweke utaratibu ambao 50% ya mapato yatokanayo na '*ring tone*' yarudi kwa msanii. Biashara ya *ring tone* nchini ina jumla ya thamani ya Shilingi bilioni 42 kwa mwaka. Iwapo msanii atapata 50%, maana yake ni kwamba Serikali itapata kodi *(withholding tax)* ya angalau 10%, kwa hiyo, kuongeza mapato ya Serikali na pia mapato ya msanii.

Mheshimiwa Spika, urasimishaji wa kazi za wasanii *(stikers)* katika ukurasa 34 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Wizara inasema Waziri wa Fedha alitoa maelezo ya kina kwenye bajeti. Siyo kweli, maana hapakuwa na *detail*. Naomba pia ikumbukwe Wizara ya Fedha yenyewe haikuwa na mpango huu mpaka mimi niliposimama kidete kwenye Kamati ya Bunge ya Fedha na kutishia kuzuia bajeti kama kazi za wasanii hazitalindwa. Ndiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipoweka suala la *sticker* kwenye hotuba yake hata hivyo inaonyesha Serikali haijajiandaa, maana tulitaraji kwamba Wizara ingetoa utangulizi wa kutosha. Bado suala la *Distributors* wa kazi za wasanii ni muhimu sana kuliangalia na ninapendekeza kwamba Shirika la Posta nchini litumike kusambaza kazi za sanaa.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza Wizara ishauriane na Wizara nyingine kuhakikisha kwamba mfumo wa *sticker* unakuwa na manufaa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba juhudi za kutumia *stickers* maalum kwenye kazi za wasanii zilianza muda mrefu sana. Ni kweli kwamba wasanii wetu magwiji kama John Kitime na hata ndugu Joseph Mbilinyi wamehangaikia suala hili kwa miaka mingi. Ninawapongeza wote kwa juhudi hizo za kizalendo kabisa. Nampongeza pia aliyekuwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi kwa juhudi hizi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwenye mpira kuna *scorer* ili afunge magoli. Tuliyefunga goli hili, ni mimi kama Waziri wa Fedha na Mheshimia William Mgimwa kama Waziri wa Fedha. Jambo hili limeamuliwa kwenye Kamati ya Fedha baada kuingilia kati, Serikali haikuwa imepanga kutekeleza hili, mpaka tulipoingilia kati kwenye Kamati ya Fedha. Hatimaye sote tumefanikiwa, waliolianza jambo hili na tuliofunga magoli. Ni vyema rekodi hii ikawekwa sawa kwa faida ya vizazi vijavyo. *We make history.*

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Makadirio na Mapato ya Wizara yako kwa asilimia mia kwa mia. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanywa pamoja na ufinyu wa bajeti. Nina angalizo dogo tu *TBC* hasa wakati wa matangazo yake ya taarifa ya habari wakati wanatoa fursa ya kuonyesha na kuunganisha maelezo ya ziada huwa kunajitokeza tatizo la *Break* ndefu kabla ya kuonyesha kinachokusudiwa au wakati mwingine kulazimika kuendelea na taarifa inayofuata.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo na ninaishauri Wizara iisaidie *TBC* katika kujikwamua na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wao wote kwa hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2012/2013. Nawatakia utekelezaji wenye mafanikio. Pamoja na pongezi, napenda kuchangia yafuatayo kwa nia ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ianze mkakati wa kitaifa wa kujenga viwanja vya michezo vijijini. Aidha, upatikanaji wa vifaa vya michezo ni changamoto kubwa kutokana na gharama kubwa ya ununuzi. Naomba Serikali itoe ruzuku ya vifaa hivi hususan mipira na jezi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara itumie Mifuko ya Maendeleo ya Jimbo kupitishia hela za mikopo ya vijana. Mfumo huu utakuwa na mafanikio kutokana na kushirikishwaji wa wananchi kupitia Serikali za vijiji. Hivi sasa mfumo uliopo unatoa fursa kwa wadanganyifu kukopesha vikundi hewa.

Mheshimiwa Spika, nashauri vile vile Baraza la Vijana liwe na mfumo unaokwenda mpaka vijijini ili kuweza kupanua uwigo wa ushirikishwaji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara itumie mfumo uliopo wa uwakilishi, yaani Wabunge na Madiwani katika uhamasishaji wa uundwaji wa vikundi vya kiuchumi vya vijana pamoja na kuendesha na kuratibu mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana katika maeneo yao ya uwakilishi. Mfumo huu utasaidia sana katika kujenga misingi ya endelevu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya utamaduni imekuwepo kinadharia tu. Napenda kuishauri Wizara kuhamasisha Watanzania kuenzi utamaduni wetu kwa njia ya ngoma za matamasha ya kimila kama sherehe za kimila na desturi zinazoongozwa na kuratibiwa na Chifu Kingalu wa Mkoa wa Morogoro. Naomba Wizara itambue na kushiriki katika *events* hizi kwa hali na mali kama njia endelevu ya kuenzi utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nashauri Wizara iangalie namna ya kuwasaidia wanaocheza ngoma zetu ku-*record* kazi zao na wasaidiwe kupata masoko ya ndani na nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni nani mwenye jukumu la ku-*document historicali sites* ambazo ni kumbukumbu ya watawala wa kimila ambao waliwahi kutawala maeneo mbalimbali ya nchi hii? Je, kuna Machifu wangapi wanawake ambao waliwahi kutawala hapa Tanzania? Ni kwa nini Wizara hii haionyeshi juhudi ya kuweka hizi kumbukumbu wazi ili vizazi vya sasa na vijavyo viweze kupata *role models.*

Mheshimiwa Spika, Taifa linalofanya mazoezi linakuwa na wananchi wenye afya. Mfano mzuri wa Taifa ambalo lina mfumo wa mazoezi kwa raia wake wa rika zote ni China. Kutokana na mfumo wetu wa utawala, Tanzania inaweza kuanzisha mfumo wa kuhamasisha mazoezi ya namna yoyote ile kuanzisha ngazi ya vitongoji hadi Taifa. Naomba Wizara angalau ijenge dhamira ya kuanzisha mfumo huo kwa sababu hauhitaji gharama kubwa. Mazoezi yatapunguza sana matukio ya maradhi sugu kama kisukari, kiharusi, shinikizo la damu pamoja na unene usiokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba ni lini Serikali italeta sheria ya '*media*' ili kuwezesha Taifa kuwa na upashanaji wa habari wenye maadili. Hali ilivyo, kuna baadhi ya vyombo vya habari ambavyo vimeamua kuwa wanaharakati wa kupambana na Serikali badala ya kusaidia kudumisha amani na mshikamano miongoni mwa Watanzania. Kuna magazeti mengine ambayo yanapotosha sana malezi ya vijana. Naomba Serikali itafakari tena uwepo wa magazeti haya. Ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri atatoa majibu muafaka ya rai nilizozitoa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawatakia utekelezaji mwema wa bajeti ya mwaka 2012/2013.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilishsa mawazo yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *Radio Tanzania*, ni redio pekee ambayo watanzania wengi inaweza kuwafikia huko vijijini. Ni *Radio Tanzania* ambayo iko katika Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)*. Mikoa ya Kusini hata Mikoa mingine, redio hii ambayo ni tegemeo la Watanzania wengi huko vijijini haisikiki vizuri. Pamoja na juhudi zote zilizofanywa na Serikali ku-*invest* katika Shirika hili, naomba bado Serikali iendelee ku-*invest* zaidi ili redio hii sasa isikike vizuri kule vijijini wakati wote na vipindi vyote. Naomba ushauri wangu uzingatiwe, Serikali iongeze mitambo, minara na njia nyingine ambayo itaamsha matangazo ya radio hiyo kwenda mbali zaidi na kusikika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, mitambo ya *Television* ya Taifa iboreshwe vile vile ili matangazo yake yaweze kupatikana hadi katika Wilaya zetu na hata huko vijijini kwetu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ukiukwaji wa maadili ya utangazaji katika baadhi ya *Television* za watu binafsi na vyombo vingine vya habari kama vile magazeti na vijarida mbalimbali hapa nchini. Vyombo vya habari kutoa au kuandika lugha za matusi na uchochezi ambao unaweza kuleta athari katika jamii zetu na hata Taifa kwa ujumla, vyombo kama hivi ni vyema Serikali iendelee kuvithibiti na kuvichukulia hatua pale vinapokiuka maadili ya Sekta ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

Mheshimiwa Spika, ni hatari sana, kwa jinsi ambayo kwa sasa vyombo hivi vya habari vinavyoendesha shughuli zake kishabiki zaidi na kuwakoroga wananchi na Serikali yake huku Serikali yenyewe ikinyamaza bila kuchukua hatua thabiti za kisheria. Hili siyo sawa. Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Wizara hii bado ina kazi kubwa ya kufanya juu ya vijana wetu wa Kitanzania, na katika hili naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, michezo vijana wengi huko vijijini wa kike na kiume pamoja na watu wazima wana *interest* sana na suala la michezo. Tatizo kubwa wanalolipata ni upatikanaji wa vifaa vya michezo ikiwa ni pamoja na jezi, mipira, filimbi, raba na njaa, Ukosefu wa waalimu wa wataalam wengine wa michezo, ukosefu wa viwanja vya kufanyia michezo hiyo, pamoja na mazoezi na fedha taslimu za kuwasaidia huduma mbalimbali za michezo, hasa wanapokuwa katika Kambi za Michezo kwa ajili ya chakula na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipange bajeti ya kutosha na pesa au *allocation* ya kila Wilaya kwa sekta hii ya michezo iwafikie walengwa kwa kufanya kusudio lililopangwa. Bajeti ya michezo ni ndogo na pesa haiwafikii walengwa huko katika Wilaya zetu, na matokeo yake sekta hii imekuwa ombaomba kila mara inapokuwa na mashindano ya kawaida au ya kitaifa. Tafadhali Wizara izingatie haya.

Mheshimiwa Spika, utamaduni nao hali kadhalika una changamoto zake kama ilivyo kwenye michezo. Vikundi vingi vya utamaduni vinakosa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na fedha taslimu kwa ajili ya kuendesha shughuli hizi. Tafadhali Wizara iliangali hili pamoja na ukosefu wa fedha, sekta hii ya utamaduni inaathiriwa na wasanii hawa kufuata au kuiga tamaduni za wenzetu kutoka nje ya nchi hii badala ya kukazania maendeleo ya utamaduni na tamaduni zetu tulizozikuta tangu enzi za mababu zetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliangalie hili, utamaduni wa Kitanzania unapaswa kubaki utamaduni wa Kitanzania na makabila yake yote yaliyoko humu nchini na siyo kuchanganya hata na ka-*element* kadogo kutoka nchi nyingine. Utamaduni kutoka nchi za nje ambao hauendani na maadili ya Kitanzania na tamaduni zetu, Wizara hii inapaswa kuzuia kabisa usitumike hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, bado Wizara ina kazi kubwa ya ku-*create* ajira kwa vijana wake. Vijana wengi hawana kazi. Wizara *completely* inawajibika kwa vijana hawa. Wizara itengeneze mazingira ya ajira kwa vijana hawa, iwasaidie mitaji ya kufanya miradi mbalimbali aidha kwa vikundi ama mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutengeneza mazingira ya ajira na kutafuta mitaji, pia Serikali itoe mafunzo kwa vijana hawa aidha, kwa vikundi ama mmoja mmoja kwa ajili ya kuwaongezea uwezo wa kuendesha miradi yao. Kuna miradi mingi ambayo vijana hawa wanaweza wakajiajiri. Hata hivyo, kwa vijana ambao wamemaliza mafunzo yao ya Vyuo Vikuu, ni vyema wapewe ajira Serikalini na kupunguza idadi ya wafanyakazi wanaofanya kazi Serikalini kwa mikataba baada ya muda wao wa kustaafu kufika. Bado Serikali ina cha kufanya kuhusu ku-*provide* ajira kwa vijana pamoja na juhudi ambazo Serikali imeanza kuzionyesha, lakini bado ikaze buti kwa ajili ya vijana hawa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana hasa kwa kuwa na Idara ya Habari. Idara ya Habari ina wajibu wa kuhabarisha, kuhamasisha na kufurahisha. Lakini vyombo vya habari kwa sasa ndivyo vinavyoongoza kubadili maadili tuliyokuwanayo Watanzania. Ni muhimu Wizara ikaangalia juu ya kuvidhibiti vyombo ambavyo vinakiuka sheria na utaratibu wa maadili ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi uhuru mkubwa walionao unaipeleka nchi hii mahali pagumu pa uvunjifu wa amani. Ni vyema Serikali ivichunguze na kuvichambua vyombo vyote vya habari hasa Magazeti ambayo yanatoa habari ambazo ni za uchochezi na zenye malengo wa kisiasa kwa maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, wamiliki wa vyombo hivi vya habari ni vizuri Wizara ikawapa maelekezo juu ya kuchambua habari ambazo zinapaswa kutolewa katika jamii. Kumekuwa na vyombo ambavyo vinatoa matangazo ambayo yanabadili utamaduni na maadili ya nchi yetu. Ni vizuri Wizara iangalie na kuvichunguza vyombo hivi ili vitoe elimu kwa umma kuliko kutoa matangazo yasiyo na tija kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi hawafanyi kazi bila kuwa na mpango maalum wa kuwajengea uwezo. Taifa hili litakuwa na vijana wengi ambao wameathirika kisaikolojia kwa kukosa kazi. Lakini bado tunakuwa na vijana wezi, majambazi na Taifa la vijana wengi waliojaa Magerezani. Ninaishauri Serikali iimarishe Vyuo vya Ufundi vitakavyowasaidia vijana hawa waweze kujiajiri wenyewe kuliko ilivyo sasa, vijana wengi wanaomaliza mashule wakifikiri wataajiriwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, michezo ni eneo linaotangaza utamaduni wa Mtanzania na kulitangaza vyema Taifa hili. Wizara imeshindwa kuweka mpango maalum wa kuandaa timu zetu za Taifa katika michezo mbalimbali hapa nchini. Huwezi kuwa na timu nzuri ambazo hazina maandalizi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara iboreshe michezo mashuleni na kuandaa walimu wa michezo. Pia ni muhimu kuanzisha shule maalum za michezo zitakazolea na kuibua vipaji vya watoto ambao hatimaye wakitunzwa watatoa timu nzuri za Taifa katika michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara hii ni ndogo. Tunaomba iongezewe fedha ambazo zinaweza kupambana na changamoto zinazoikabili tasnia hii ya habari. Pamoja na kasoro hizo, tunaiomba Serikali iendelee kuongeza mishahara ya Waandishi wa Habari na Watangazaji kwani mishahara yao ni kidogo sana.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na uhai. Namwomba atujalie na mfungo mwema wa Ramadhani.

Pili, natoa mkono wa pole kwa wahanga wa meli ya *MV Skagit* iliyozama tarehe 18 Julai, 2012 wakati ikisafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar. Mwenyenzi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi, na awape afya njema wote walionusurika na wale waliopoteza watu wao awape subira. Amen.

Mheshimiwa Spika, naanza na ajira kwa vijana. Ajira kwa vijana ni muhimu sana kwa nchi yoyote yenye maendeleo duniani kwa sababu vijana ndiyo wachapakazi katika sehemu zote

muhimu. Vijana wana uwezo wa kuchapa kazi viwandani, mashambani, katika uvuvi na sehemu mbalimbali zinazohitaji nguvu na akili. Tanzania tunayo rasilimali watu ya vijana wengi waliosoma na wasiosoma, wengi wao wanazurura, Serikali imeshindwa kuwapatia ajira. Vijana wengi wamekusanyika Mijini wakifanya biashara za machinga, yaani biashara za mikononi ambazo tija yake ni ndogo sana hasa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana ni tatizo la Kitaifa. Vijana wengi hufanya kazi mbadala baada ya kukosa kazi ama ajira ya maana. Vijana hufuata mkumbo wa kujishughulisha na madawa ya kulevya, ulevi, wizi na utapeli na mengi mengineyo mabaya. Ni lazima Serikali ifanye juhudi za makusudi kuwawekeza vijana katika shughuli za maendeleo kama viwanda, kilimo cha kisasa, uvuvi wa kisasa, michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *Taifa Stars* ni timu ya Tanzania nzima, yaani Bara na Visiwani. Lakini uteuzi wake unaangalia upande mmoja tu wa Muungano, yaani Tanganyika, na vijana wa Zanzibar wanakosa fursa hii. Kama ni sahihi, hii ni dhuluma. Kwa hiyo, nataka kujua ni vigezo gani vinavyotumika kuteua timu ya Taifa? Je, *Taifa Stars* ya sasa hivi ina wachezaji wangapi kutoka Zanzibar? Je, Zanzibar hakuna vijana wanye uwezo kuchezea *Taifa Star*? Je, ili wachaguliwe *Taifa Stars* ni lazima wajiunge na timu za Tanzania Bara? Naomba majibu yenye tija.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, wachezaji wa Zanzibar wanacho kiwango kizuri tu na kigezo ni timu ya mafunzo ambayo imeshiriki Kombe la Kagame, imefanya vizuri pamoja na kutolewa robo fainali.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ikiongozwa na Waziri na Naibu Waziri kwa kuandaa hotuba nzuri na inayoeleweka. Ushauri wangu ni kuwa kutokana na ukosefu wa ajira, wapo vijana wanaojitahidi kuunda vikundi vya ngoma na filamu lakini hawana mitaji. Wapo ninaowafahamu katika Mkoa wa Mtwara, Serikali iwatafute vijana wa aina hii Tanzania nzima na iwatafutie wafadhili au mikopo, lakini pia isaidie kuwapa elimu jinsi ya kuboresha sanaa yao.

Mheshimiwa Spika, wimbi la madawa ya kulevya linazidi kuongezeka kutokana na wateja kuongezeka ambao ndiyo vijana wetu. Ni vyema sasa Serikali ikajikita katika kuhakikisha kwamba vijana wetu hawaendelei kuwa wateja. Walioathirika wapewe matibabu na ambao hawajajiunga na uteja waendelee kuelimishwa kuhusu madhara yake.

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri wangu, jamii ishauriwe kuchagua walezi wa vijana kwa kila Kata ambao pia Serikali itawatambua walezi hawa wahusike kukaa na vijana mara kwa mara kuwatia moyo na kuwapa ushauri juu ya mwenendo wa maisha. Pia wapate maoni ya vijana kuhusu jinsi ya kujikwamua kimaendeleo. Waelimisha rika pia wanaweza kutumia masuala yaliyojitokeza katika eneo husika kwa kuelimisha kwenye maeneo tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mkataba wa kuhifadhi utamaduni usioshikika, Serikali sasa ipitie mila na desturi chanya zinazowagusa vijana katika makabila mbalimbali iziboreshe, izieneze na kuzidumisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Fenella Mukangara - Waziri ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo, na Mheshimiwa Amos Makalla - Naibu Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nafasi zao.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuzungumzia maendeleo ya michezo na miundombinu. Ni ukweli kwamba Uwanja wa Taifa, Uwanja wa Uhuru na Uwanja wa Karume ni mafanikio makubwa. Hata hivyo, viwanja vingine nchini kama uwanja wa Jamhuri Dodoma, Jamhuri Morogoro, Sheikh Ameir Abeid Karume na vingine vina viwango duni kwenye sakafu za

majani ya kuchezea. Hakuna kazi ya makusudi ya kuboresha hali ya viwanja tangu vilivyojengwa. Uwepo wa viwanja vyenye viwango vya Kimataifa, inachangia maendeleo ya mpira wa miguu na uhamasishaji wa michezo mingine.

Mheshimiwa Spika, aidha, hapa Tanzania michezo ni mpira wa miguu tu. Hivi kuna mikakati gani ya kupanua uwigo na kuwa na jitihada ya makusudi kwenye michezo kama ya ngumi, riadha, netiboli, kikapu, kama ilivyo kwa nchi kama Kenya, Angola, Ethiopia, Msumbiji ambapo wametambua toka zamani kuwa vipaji vya watoto wetu haviko kwenye mpira wa miguu tu? Naishauri Serikali ije na Sera na mipango endelevu ya muda mfupi na wa kati wa kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Michezo kama cha Mallya, Kwimba ni mfano wa kuigwa na ni bora Vyuo vya namna hii vikaongezwa kiwango ili matunda ya Vyuo hivyo yaonekane wazi. Wanamichezo wa kiwango cha mabingwa wa dunia, wanaingiza kipato kupitia udhamini wa vifaa na vinginevyo; na tukiwa na wanamichezo wa ngazi hii, mapato yanayotokana na udhamini yanaweza kuchangia kwa kiwango fulani maendeleo ya Vyuo hivi vya michezo na jitihada nyingine za kuibua vipaji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lina umuhimu wa dharura ni kuangalia suala la maadili ya Mtanzania kwenye kazi za wasanii nchini. Nashauri kwamba suala la kubaini madaraja, *classification* ya kazi za wasanii ili zile kazi ambazo zina mambo ya watu wazima (*adult content)* zionyeshwe kwenye nyakati ambapo watu hawajakaa kwenye luninga wakiangalia vipindi hivyo na wakwe au wazazi wao. Aidha, watoto wa Tanzania wanaangalia baadhi ya vipindi vya Kitanzania ambavyo hawastahili kuviona kulingana na umri wao.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itoe maelezo kuhusu mipaka ya sheria hivi sasa, bila kuzingatia, kwamba kuna rasimu ya sheria mpya ya habari, kuhusu Uhuru wa Habari. Hivi ni wapi duniani ambapo hakuna wajibu wa taarifa zinazoandikwa na vyombo vya habari? Mimi ni mwathirika (*victim)* wa vyombo vya habari. Tangu nilipoulizwa humu Bungeni mwaka 2006 kuhusu vyombo vya habari kuwajibika kwa Watanzania kutoa habari kulingana na vipaumbele vya Kitaifa, Gazeti la Mwanahalisi mwaka 2011 liliripoti kwamba nilikwenda Afrika ya Kusini mwaka 2011 nikabadilisha jina, nikasafiri kwa siri kwenda kusaini mikataba ya kibiashara. Safari hiyo nilikuwa Mjumbe kwenye msafara wa Mheshimiwa Rais kwenye kikao cha *Tripartite* ya *SADC, EAC* na *COMESA*, Johannesburg na *TBC* walinionesha kwenye taarifa ya habari nikiwa na Mheshimiwa Rais na Mawaziri wengine.

Mheshimiwa Spika, nimepokelewa na Maafisa wa Ubalozi wetu, Mwanahalisi anasema hata Ubalozi ulikuwa haujui uwepo wangu Afrika ya Kusini. Hivi ni kweli kwamba gazeti la Mwanahalisi na magazeti mengine haya yakiandika taarifa za uongo kwa kujitengenezea mapato kwa kuwadhalilisha watu wengine, hawawezi kudhibitiwa, na wako juu ya sheria? Utaratibu huu ambao magazeti mengine kama Mwananchi, Tanzania Daima na kadhalika wanachafua watu bila kujali, utapata ufumbuzi lini? Utakoma lini?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza *Simba Sports Club* kwa kutwaa ubingwa na pia kwa kufikia hatua ambazo Tume nyingine za Tanzania zinaishia raundi ya kwanza kila mwaka katika mashindano ya Afrika. Kwa kufanya hivyo, *Simba Sports Club* ndiyo imedhihirika kuwa timu pekee inayowaletea faraja, fahari na starehe Watanzania wote bila kuzingatia tofauti zao za itikadi, dini, rangi kabila na kadhalika. Wote wanafarijika na mafanikio ya Simba *Sports Club*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia na kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa na mifumo rasmi juu ya ajira rasmi na zisizo rasmi. Vijana ndio 68% ya Watanzania na katika Kikao cha Hali ya Uchumi wa Taifa mwaka

2011 takwimu za ajira ni za mwaka 2006. Fanyeni tafiti za karibuni juu ya ajira, siyo kutumia takwimu za zamani.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuishauri Serikali iweke mfumo wa hifadhi ya jamii, hata kwa vijana wasio na ajira rasmi kama waendesha bodaboda. Hii imefanywa na Afrika Kusini na Katiba yao inatambua hivyo katika ibara ya 27 ya Katiba ya Afrika Kusini. Pia napenda kushauri vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu na Sekondari hawajui hatima yao juu ya tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, Taifa lisilo na utamaduni wake ni Taifa litakalosahaulika. Kwa sasa utamaduni wetu unapotea. Ukiangalia filamu, magazeti ya udaku, picha za ngono na kadhalika haya yote yanapoteza utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu kwa sasa halina Vazi la Taifa. Napenda kupata majibu ni lini Tanzania tutakuwa na Vazi la Taifa? Kwani imekuwa ni hadithi ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili ni sehemu ya utamaduni. Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza lugha hii? Tujiangalie tuathiri utandawazi, siyo tuathirike na utandawazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kupeleka Watanzania kusoma mambo ya michezo na sisi tuache kutegemea makocha wa kigeni. Tunapaswa kuwa na Watanzania wanaosomeshwa ili waje kufundisha timu zetu. Kuhusu viwanja vya michezo, Wilaya ya Kibondo haina kiwanja cha michezo. Napenda kuishauri Serikali itoe maagizo kwa Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Kibondo kutenga eneo la michezo na kujenga uwanja wa mpira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo mashuleni, napenda kuishauri Serikali iboreshe mashindano ya UMITASHUMITA yahusishe shule zote ili kuboresha michezo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii nami nitoe maoni yangu kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Serikali na kuishukuru kwa namna ambayo imeanza kushughulikia suala la sanaa za muziki, filamu na ufundi, hasa kwa uamuzi wa kuweka ushuru wa bidhaa za kazi za sanaa *(sticker)* kwenye muziki na filamu (*DVD, CD, VCD,* na kadhalika.) katika kuimarisha biashara na kuzuia *piracy*, hali ambayo imekuwa ikiwapotezea mapato wasanii wengi. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba katika mpango huu, ziingizwe pia kazi za sanaa za ufundi. Mfano, picha za kuchora, batiki na *Tie and Die,* vinyago, Tingatinga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, bidhaa hizi zinauzika sana nje na ndani ya nchi, mfano *TRA*, huzitoza kama magogo ya Maliasili. Hivyo, mapato ya kazi hizi na uhalali wa uhalisia wa kazi unapotea. Bidhaa hizi zinanunuliwa sana nchi za Scandavia, Ulaya, USA na na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iweke utaratibu au mfumo kwa wasanii kukopesheka, kwani mfumo wa ruzuku kwa wasanii haupo, sekta hii haitambuliki kama ni uwekezaji. Kuwe na dirisha la kukopesha wasanii.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara imekumbuka kuweka Shilingi milioni 50 kwa ajili ya kumaliza taratibu za kuleta Sheria ya *sticker* hapa Bungeni? Pia kwa ajili ya kanuni zitakazoanzisha mchakato wa matumizi ya *sticker!* Vile vile fedha za *Information Technology* ili kuweka sawa mfumo wa *TRA, BASATA, COSOTA* na Bodi ya Filamu Tanzania na iwe *linked* na *Bar Code* ambayo itasaidia mfumo mzima.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa mchakato wa Katiba mpya, wasanii wasiwekwe kando. Vyombo kama *BASATA*, Idara ya Sanaa, Mfuko wa Utamaduni na Vitivo vya Sanaa vitumike kukusanya na kuhamasisha wadau wa sanaa kutoa maoni yao yapelekwe Tume ya Kuratibu maoni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kwa upande wa *TBC. TBC* ni shirika ambalo linaelekea kubaya. Hali ya majengo ya *TBC* ni mabovu, yamechakaa, hali ambayo imesababisha hata utendaji wa kazi hauridhishi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, iangalie suala hili kwa makini.
Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iangalie na kuboresha maslahi ya Vyombo vya Habari vya Serikali na vya Binafsi, ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuandaa mazingira ya Vazi la Taifa lenye heshima na siyo kwenda nusu uchi.

Mheshimiwa Spika, utamaduni na mila potofu za baadhi ya jamii inayopelekea kutenda mambo yasiyoendana na matakwa ya ustawishaji wa desturi zinazotakiwa kuigwa na jamii, kurithisha maadili mema ya mavazi, ngoma na utamaduni mwingine.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Naomba nichangie mambo machache.

Mheshimiwa Spika, Tasnia ya Habari, sasa haifanyi kazi yake vizuri. Waandishi wengi sasa wanaweza kuandika habari ya uongo kwa masilahi fulani, lakini hawachukuliwi hatua. Pengine Sheria zinazosimamia Tasnia ya Habari hazitoi nafasi Waandishi wanaopotosha au kusema uongo kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano mingi sana ya vyombo vya habari kupotosha habari. Tena wakati mwingine kwa kudhalilisha na kukosesha watu ndani ya jamii. Naishauri Serikali, iziangalie Sheria za masuala ya habari ili kuongeza udhibiti na wanaopotosha au kusema uongo waadhibiwe ikiwa pamoja na vyombo vyao wanavyovitumikia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaiomba Serikali iiangalie Tasnia hii kwa jicho tofauti. Hali hii ya kupotosha na kuachwa bila adhabu, italisambaratisha Taifa kwa uchochezi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi za Wizara za kuwa na dhamira ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii iwatambulishe wananchi wa Maswa na Tanzania: je, upo mpango gani wa kupeleka Wataalamu wa kushauri yapi ndiyo maeneo ya mchakato wa kupata viwanja vya viwango vya Kitaifa na Kimataifa, hivyo viwe kisomo cha mafunzo ya kupata wanamichezo wa viwango vya Kitaifa na Kimataifa katika michezo yote maarufu kwa programu ya mwaka 2025 hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru kupata majibu ya mdomo yakiambatana na maandishi ya kunipa fursa ya kufuatilia. Vivyo hivyo, naarifu Chuo cha Michezo kipo Malya, eneo ambalo ni mpakani na Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara inaweza kutuma Walimu wa michezo ya vijana katika mipira ya miguu, riadha na baiskeli? Bila elimu, hakuna maarifa na ujuzi. Kwa hiyo, sasa naomba mwongozo wa kutekelezwa hivyo, uwe himizo la kujenga ufanisi katika Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Spika, je, maelezo ya nyongeza ni yapi? Yapo?

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri wa Michezo yupo tayari kuwa Mratibu wa Harambee ya kuchangisha vifaa vya michezo vya kusaidia Wilaya ya Maswa ipate vifaa vya kuchochea maendeleo ya kukuza michezo? Naomba majibu fanisi. Naomba maelezo ya nini Waziri afanyiwe, kuwa Mgeni Rasmi wa Harambe ya Kuchangisha Vifaa vya Michezo?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu kwa maandishi, hivyo nifuatilie utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono bajeti hadi nipate maelezo kwa hoja za mchango huu. Ahsante.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, timu zetu za Taifa zinafanya vibaya kutokana na Serikali kutokuwa na nia ya kusaidia. Serikali isikwepe jukumu hilo.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Waziri kwa Bajeti nzuri. Naiomba Wizara itusaidie sisi ambao tumepata Wilaya mpya kuanza vizuri masuala ya michezo, hususan Wilaya ya Kaliua. Tunaomba Wizara itusaidie kupata Afisa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara itushirikishe katika Mipango ya Kitaifa ya Michezo, ikiwemo na kutupatia wafadhili wa kutusaidia kujenga miundombinu kama vile viwanja vya mpira. Tunaomba Kaliua, iwe mfano.

Mheshimiwa Spika, mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri atamke, kuitambua *Simba Sports Club* kwamba, ndiyo Klabu pekee inayojitahidi kuliuza Jina la Tanzania katika uwanda wa mpira. Hili alitamke humu Bungeni na nchi isikie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Serikali, kwa mikakati mbalimbali ya kujenga misingi ya kuwaendeleza vijana. Vijana wana changamoto nyingi. Tunao vijana wanaomaliza Shule na Vyuo, lakini soko la ajira ni dogo na wengi wanabaki hawana ajira. Wapo vijana waliomaliza Elimu ya Msingi na wapo Mitaani, soko la ajira kwao ni duni sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali, inajitahidi kutoa nafasi za ajira, lakini ni wazi bado mikakati haijawa sawa. Nashauri kuwa, sasa kuwe na kambi maalum za mafunzo ya vijana na hasa wale ambao hawajapata fursa ya kisomo cha Vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Makambi haya yajikite katika elimu kwa vitendo, ujasiriamali, na wapewe mitaji itakayoratibiwa na taasisi husika, na ikiwekezana, basi kuwe na mtaji rasmi utakaozunguka kwa programu hii maalumu.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo kubwa la maeneo ya michezo ili kukuza vipaji vya michezo, stamina na afya kwa vijana wetu. Muda sasa umefika, Serikali kupitia Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji, zitenge maeneo ya michezo katika kila Kata na Miji; na hii iwe ni mpango kwa Mikoa na Wilaya zote Tanzania. Tukifanya hivi vijana wetu wataweza kutumia vyema muda wao wa ziada katika michezo na kujiepusha na vitendo viovu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uandishi na utoaji wa habari; tumekuwa tunashuhudia, na hususan, magazeti yetu ya ndani yakiandika vichwa vya habari vyenye maneno makali, mazito na ya kuuza magazeti, wakati ukweli wa habari yenyewe ni tofauti na kichwa cha habari yenyewe.

Nakumbuka kabisa tulivyofundishwa shuleni, kichwa cha habari yoyote sharti kiwe kifupi, lakini kinachobeba maana ya habari yote kwa ufupi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itupie macho suala hili na isimamie marekebisho ili uandishi uheshimu misingi ya taaluma hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Pili, niseme kwamba pesa zilizotengwa kwa bajeti mwaka 2012/2013 hazitoshi kabisa. Bajeti hiyo iongezwe, kwani Wizara ina Sekta nne; Habari, Michezo, Utamaduni na Vijana. Wizara, inahitaji fedha za kutosha iongezewe pesa.

Mheshimiwa Spika, njia ya kufundisha ufundi katika Shule za Msingi au Shule za Ufundi, inaleta ajira. Zamani kulikuwa na Shule za Ufundi katika Shule za Msingi. Kwa kufundisha ufundi Shule za Msingi, kutawapa ajira vijana ambao watakuwa nje ya mfumo wa Shule. Ufundi huo ni ufundi chuma, uashi na useremala na upishi.

Mheshimiwa Spika, zamani kulikuwa na shule hizo na watoto walikuwa wananufaika kwa kupata ajira. Tuanzishe tena. Mkoa wa Lindi, kulikuwa na shule 16, tunaomba zifufuliwe.

Mheshimiwa Spika, tunaomba uwanja wa michezo wa Lindi, ukarabitiwe. Uwanja huo ulianza tangu mwaka 1950. Zamani ulikuwa na taa za umeme na timu za Ulaya zilikuwa zinacheza hapo. Tunaomba ukarabatiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba wachezaji maarufu waenziwe tafadhali na wathaminiwe wanapokuwa wanastaafu. Lindi wanapenda sana michezo na wachezaji wengi wa Kitaifa wanatoka Lindi kama ifuatavyo: Ndugu Mohamedi Chuma (amechezea Taifa miaka 11), wengine ni Mohaji Muki, Akwitende, Mohamedi Muhi, Mohamedi Dini, Edfonce Amlima (aliwahi kuchezea timu ya Taifa na timu za nje huko Uarabuni), Omari Mahoti, Mohamedi Ngumba na wengineo. Tunaomba Serikali iwaenzi Wastaafu wa Michezo.

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza wachezaji wa Twiga Stars – Timu ya Wanawake, kwa kazi nzuri wanayofanya, hongera sana. Mimi zamani, mwaka 1964, nilikuwa nacheza mpira wa wanawake katika timu ya Shule, Sekondari ya Mtwara na nilikuwa *Centre Forward No. 9*, lakini wakati ule mpira wa miguu kwa wanawake haukuwa maafuru, haukuendelea. Sasa naomba mpira wa miguu kwa wanawake uendelezwe, kwani unapendwa na unaingiza pesa.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, wakati naiunga mkono hoja hii, napenda kusisitiza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba usikivu wa *TBC* uimarishwe. Suala la *migration* kutoka kwenye *analogue* kwenda *digital* lifanyike kwa umakini mkubwa. Kazi za sanaa za Wasanii mbalimbali zisimamiwe vizuri ili tuwanufaishe Wasanii na Taifa kwa ujumla. Aidha, napenda kusisitiza maadili kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, suala la Sheria Mpya ya Vyombo vya Habari ni muhimu likatiliwa mkazo. Sheria hii itungwe haraka iwezekanavyo, maana Sheria iliyopo ina upungufu mwingi na inatumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutamka kuwa naiunga mkono bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, michezo ni Afya, michezo ni chachu ya kukomaza akili, michezo hutoa burudani, hujenga na kukomaza mwili, ukakamavu na vile vile michezo hujenga nidhamu. Aidha, michezo huonesha uwezo na vipaji vya jamii. Kupitia Michezo na Tamaduni, jamii zimeweza kutangaza hulka na mambo mema ya jamii husika. Michezo huunganisha jamii, hujenga na kudumisha urafiki baina ya jamii mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tujiulize, pamoja na hazina ya utajiri huu unaopatikana kupitia michezo na utamaduni, ni kwa kiasi gani kama Taifa tunaenzi na kuthamini kwa dhati michezo na utamaduni? Iko wapi leo michezo yetu ya jadi? Imepotea, na inazidi kupotea! Sisi kama Taifa tunaridhika! Hatushtuki! Hatuna mikakati ya kufufua michezo na tamaduni zetu.

Mheshimiwa Spika, historia na tafiti mbalimbali zinaonesha kwamba machifu ndio walitumika kulinda na kurithisha mila, michezo na tamaduni zetu. Leo hii tujiulize, sisi kama Taifa, nani amechukua nafasi ya Machifu katika kulinda na kurithisha mila, michezo na tamaduni zetu? Je, ni Maafisa Utamaduni? Je, tumewawezesha kazi hiyo? Je, ni Baraza la Michezo la Taifa? Tunaridhika kama Taifa na kazi wanayoifanya?

Mheshimiwa Spika, umefika wakati sasa wa kuwa na kongamano la michezo ili tuweze kuibua mawazo mapya yatakayotuwezesha kuwa na Sera na Programu za Michezo zinazoendana na wakati tulionao sasa. Tuondoe kigugumizi katika kuandaa Sera Mpya ya Michezo.

Mheshimiwa Spika, lazima kama Taifa tujenge utamaduni wa Watanzania kupenda kushiriki michezo. Hii, siyo tu kwa faida za kiuchumi au kushinda mataji tu, bali iwe sehemu ya kuimarisha afya za wananchi wetu. Leo hii tunashuhudia kuongezeka kwa kiwango cha matatizo ya kiafya kutokana na wananchi kutoshiriki michezo na kazi zitoazo jasho. Wenzetu wa Mataifa ya Ulaya waliopata tatizo kama hili katika miaka ya 1980 – 1990 waliamua kwa makusudi kufanya michezo kuwa sehemu ya utamaduni wao, watu wakaanza kupenda kushiriki michezo kutokana na Serikali zao kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika michezo. Leo hii pamoja na mambo mengine, michezo imesaidia sana kuboresha afya za wananchi wao. Sisi tunajifunza nini kwa mafanikio yao?

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuhusu kuongeza ajira kupitia Wizara hii. Vijana wengi wako Mitaani na baadhi yao wana vipaji.

Mheshimiwa Spika, iko haja ya kuishauri Wizara ya Eimu, kuandaa Mtaala ambao utaendana na wakati kwa kutambua vipaji na kuvikuza, kuanzia Chekechea hadi Vyuo Vikuu. Kufanya hivyo, kutatatua tatizo la kufeli kimasomo kwa wengine kuendelea na masomo kuhusu vipaji vyao.

Mheshimiwa Spika, ninao mfano wa baadhi ya watoto ambao wameshindwa darasani, lakini kivitendo wameweza na kushinda michezo kama *kriket* na kadhalika. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi ni kwa nini wananchi walioko Mikoani kama Pwani na kwingineko hutaabika kupata Vituo vya Televisheni kwa kulipia ambapo ni haki ya kupata habari?

Mheshimiwa Spika, utamaduni wa Mtanzania ni jambo muhimu sana katika kudumisha amani, mshikamano na upendo na hakuna gharama kubwa kulinda Taifa letu. Ni vyema tukarejesha ngoma, nyimbo na vitendea kazi katika shule zetu na hasa zile tamaduni ambazo siyo potofu. Hii itasaidia watoto kujifunza utu na uzalendo kutoka utotoni na kuleta upendo na kuondoa ubinafsi wa kutolipenda Taifa na watu wake.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara hii itupie jicho Mkoa wa Morogoro na Wilaya zake, kuboresha viwanja vya michezo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri kwa kuteuliwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwepo na kituo cha pamoja cha taarifa za yanayojiri kwa vijana, lakini hasa kuanza utaratibu wa kuwaandaa vijana ili kujitegemea. Mfano, nchi ya India iliamua kufundisha watu wazima wapatao 2000 masuala ya ujasiriamali. Hii ilisaidia kuanzisha Mitaala ya Ujasiriamali na watoto kuanza kusoma kutoka shule na sasa ajira binafsi ziko nyingi India.

Mheshimiwa Spika, tujenge tabia ya kujenga ubunifu kulingana na *skills* zinazotakiwa, zinazogeuka biashara ili kuwawezesha vijana kuzipata na kujiwezesha nazo na kupata mianya ya biashara. Kwa mfano, kutengeneza zana za kazi rahisi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuiomba Wizara ikae na Vyama vya Michezo ili viweze kuimarisha eneo la utaalam ambao utaweza kujenga msingi wa kiufundi kwa michezo husika, kuanzia ngazi ya watoto wadogo watakaoweza kuunda timu za michezo kadhaa na hatimaye kuunda Timu za Kitaifa zenye kuleta mafanikio makubwa. Hivyo basi, kila chama cha michezo, kiimarishe Kitengo cha Utaalam (*Coaches*) na Wizara itoe tamko kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuonyesha namna nisivyoridhika na baadhi ya Vyombo vya Habari na Waandishi wa Habari ambao huacha maadili ya tasnia hii na kufanya mambo kinyume na maadili ya Taifa. Wizara itoe tamko la Waandishi wa Vyombo ambavyo vimeandika taarifa za kashfa kwa Kiongozi Mkuu wa Nchi na kuandika taarifa zinazolenga kugombanisha jamii na kupotosha umma.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wizara ikatoa tamko kuhusu hili. Ahsante.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, Sera ya Vijana ya Taifa imeeleza kuwa, kutaundwa Baraza la Vijana la Taifa. Baraza ambalo litakutanisha vijana wa makundi yote bila kujali itikadi zao za kisiasa au kidini.

Mheshimiwa Spika, ni miaka mingi imepita bila kuundwa kwa Baraza hili, na hakuna taarifa yoyote kutoka Serikalini, inayoeleza hatua iliyofikiwa katika mchakato wa kuundwa kwa Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara itueleze Waheshimiwa Wabunge na Vijana wote wa Tanzania, uundwaji wa Baraza hili umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, jambo gani linalozuia utekelezaji wa Sera? Vijana hawana sehemu wanayoweza kukutana na kujadili masuala ya Kitaifa, yanayowahusu na kutoa ushauri kwa Serikali. Vijana wameshindwa kupata habari zinazowahusu.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya uundwaji kwa Baraza la Vijana la Taifa, kama ilivyoahidiwa kwenye Sera ya Vijana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iendeleze Vyuo vya VETA. Kwa kuwa Serikali imeanzisha Shule ya Sekondari kila Kata, pia, iandae fungu la kuwawezesha vijana baada ya kumaliza Chuo wawezeshwe vifaa (vitendea kazi), mfano, spana za magari, mashine za *welding*, vifaa vya kujengea na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Wataalamu wa Wizara, wameandaa hotuba nzuri ambayo

imewasilishwa vizuri. Nampongeza pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambaye kwa niaba ya Kambi, amewasilisha maoni ya Upinzani ambayo inafaa Serikali iyazingatie katika kutekeleza mipango yake.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa leo, nitazungumzia utamaduni. Nitazungumzia utamaduni kwa sababu, kwa maoni yangu, maana yake na dhima yake havijaeleweka vizuri. Nitalizungumzia hili kila mara hadi wananchi wenzangu waelewe mambo haya. Ni vyema, maana na dhima yake hasa katika maendeleo ya kiuchumi na mengineyo vikaeleweka ili tupange mipango kwa kuyazingatia.

Mheshimiwa Spika, kwa fasili pana, utamaduni ni mambo yote ya kifikra na kimatendo, yanayoshikika na yasiyoshikika, ambayo mwanadamu amebuni, ameunda au kusanifu katika mapambano yake ya kuyateka maumbile ili atimize mahitaji yake ya msingi (chakula na kadhalika) na mahitaji mengine (burudani na kadhalika). Utamaduni hujumuisha amali zinazoshikika *(spiritual culture)*.

Mheshimiwa Spika, kila utamaduni huwa na vipengele vifuatavyo: Lugha, maarifa ya kisayansi na kiteknolojia na yasiyo ya kisayansi (ya kifani, mathalani imani, sheria, mila, maadili, Serikali, sanaa, sanaa – jadiya, dini, muziki na kadhalika), utamaduni wa amali zinazoshikika, ni pamoja na mavazi, majengo, vinyago, michoro, mapambo, ufinyanzi, ufumaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hoja ninayotaka kutoa ni kwamba, Serikali yetu, haijatambua umuhimu wa utamaduni na kuupa uzito unaostahili. Ndiyo maana Wizara hii, haipewi fedha ya bajeti ya kutosha kila mwaka. Swali ninalotaka sisi sote tujiulize na tulijibu ni hili: Je, bila kuwa na utamaduni imara, tunaweza kuendelea? Je, uchumi wetu unaweza kuendelea bila kusukumwa na utamaduni imara? Kwa nini maendeleo yetu yanasuasua katika miaka 50 iliyopita, wakati nchi nyingine tulizoanza nazo zimeshapiga hatua kubwa (mfano Cuba, Korea Kusini, na kadhalika)? Sababu za kiuchumi tu hazitoshi kuelezea tatizo letu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba, bila kuwa na utamaduni imara, utakaolea na kukuza uzalendo thabiti na utakaojikita kwenye maadili thabiti ya Utaifa, hatuwezi kupiga hatua za kikwelikweli za kimaendeleo. Siyo kwamba waasisi wa Taifa letu hawakufanya juhudi za kujenga misingi ya kitamaduni tunayoizungumzia, Mwalimu Nyerere alijitahidi kuikuza lugha ya Kiswahili, ingawa baadaye alikengeuka. Alituletea Azimio la Arusha ambalo lengo lake kuu pamoja na mengine lilikuwa kujenga misingi ya kujitegemea na maadili ya kijamii na ya kazi.

Mheshimiwa Spika, wakati wote alisisitiza uzalendo, maadili ya uchapakazi na daima alisisitiza kuwa, maendeleo yetu tutayaleta sisi wenyewe, na siyo mwingine. Lakini inaelekea kuwa somo halikufanikiwa kwa sababu, aliowafundisha na kuwakabidhi viwanda vilivyoanzishwa, ili tupige hatua ndio hao hao waliogeuka na kuvitafuna kwa manufaa yao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano michache ya nchi ambazo zina utamaduni imara, ambazo ziliendelea kwa muda mfupi tu. Sote tunafahamu kuwa, Japani ilishindwa vibaya katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia (1945). Aibu ya kushindwa haikuwafanya wawe wazembe, walichapa kazi na kilichowasaidia ni misingi imara ya kitamaduni. Wao baada ya miaka 25 tu, yaani 1970 walikuwa tayari ni Taifa tajiri linaloendelea haraka.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1980, ikazipita nchi nyingine za Ulaya, na kuwa nchi ya pili kiuchumi duniani. Mfano mwingine ni China, iliyojikomboa mwaka 1949. Hivi sasa ni nchi ya pili kiuchumi duniani. Imezipita nchi zote pamoja na Japan. Sifa pambanuzi za nchi hizi mbili zilizosaidia ni uzalendo thabiti, Utaifa imara na maadili madhubuti ya kazi. Sifa hizi zikiwepo hata utawala bora wa kiuchumi hauwezi kukumbana na matatizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa Serikali haijaupa uzito utamaduni na hali hii inafanya hata maendeleo mengine yasuesue. Ili hali hii ibadilike, hatua zifuatazo zichukuliwe:-

(1) Sera ya utamaduni ya mwaka 1997 irejewe ili masuala ya uzalendo, Utaifa, maadili ya jamii, na maadili ya uchapakazi yaliyokuwa katika tamaduni zote za asili yaingizwe;

(2) Sheria ya utamaduni itungwe ambayo itazingatia sera ya utamaduni na marekebisho yake, kanuni za utamaduni zitungwe baada ya sheria kupitishwa;

(3) Kwa hatua za muda mfupi, Idara za Utamaduni Mikoani na Wilayani zifanye kazi ya kukuza utamaduni kikwelikweli; na

(4) Sera ya lugha irejewe ili Kiswahili kipewe nafasi stahiki. Kiswahili ni kitambulisho chetu kikuu ndicho kitakachosaidia kujenga uzalendo halisi wa kitanzania.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, moja kati ya masuala muhimu katika uandishi, ni kufuata maadili ya uandishi "*ethics*", lakini inastaajabisha kuona maandishi yasiyofuata maadili.

Mheshimiwa Spika, nalazimika kuandika suala hili, hasa baada ya kufahamu kuwa kuna chombo ambacho kiko chini ya Wizara, mahsusi kwa ajili ya kusimamia kazi za uandishi iwe ni magazeti au vitabu.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha haki za binadamu cha mwaka huu wa 2012, pamoja na kuainisha ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu hapa nchini, ndani yake kimeweka picha iliyopigwa maiti, ilhali ikiwa haijasitirika.

Mheshimiwa Spika, maadili yetu Watanzania, yanazingatia kuheshimu binadamu akiwa hai, hata akiwa amekufa. Sasa Tume hii inayotetea Haki za Binadamu, hapa imekiuka maadili ya uandishi. Sasa Mheshimiwa Waziri, wakati anajumuisha, ningependa aniambie ni hatua gani Wizara hii ilichukua, juu ya Tume ya Haki za Binadamu?

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali iache utaratibu wa kutumia Walimu kuongoza Idara ya Utamaduni. Badala yake itumie Wataalamu waliosomea Idara hiyo. Mfano, Wilaya ya Meatu, Afisa Utamaduni *profession* yake ni Mwalimu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, ilete Muswada wa Vyombo vya Habari ili Bunge, litunge Sheria ambayo itasaidia kuondoa baadhi ya kero zinazowakabili Waandishi wa Habari. Leo, wapo wamiliki wa vyombo vya habari ambao wengi wao hawawalipi Waandishi mishahara yao, na hivyo kuwafanya waandishi wengi kukiuka maadili ya kazi zao na kulazimishwa kuandika habari ambazo zinahatarisha usalama kwa kulazimika kupewa rushwa na watu wenye nia mbaya.

Mheshimiwa Spika, waandishi wengi, hasa kwenye *Private Media,* hawana ajira. Nadhani kama Muswada huu utakuja Bungeni na kutungwa Sheria, itawasaidia zaidi Waandishi wa Habari, kwanza kwa kupata elimu bora na kufanya kazi zao kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, leo tunajisifu kwamba Tanzania ina uhuru wa vyombo vya habari, naamini kama huu tunaouita uhuru utatupeleka pabaya. Kama Serikali haitachukua hatua za haraka, Vyombo vya Habari vya Nchi hii vinaweza kutufikisha katika uasi (mauaji) kama vile ilivyokuwa Rwanda mwaka 1994, ambapo vyombo vya habari vilichangia kwa asilimia kubwa katika mauaji yale.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kushauri ni suala la Serikali kupitia *BMT*, kutafuta suluhu ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Pete (Netiboli), ambaye amesimamishwa kazi kwa muda mrefu, lakini hadi sasa hajarejeshwa kazini (Anna Kibira).

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia jambo lingine kuhusu michezo, ambapo kwa kweli, katika mpira wa miguu kumekuwa na unyonyaji mkubwa kwa klabu na wachezaji wake wanaoshiriki Ligi kuu ya Kandanda ya Tanzania Bara. Makato yanayochukuliwa na *TFF* ni makubwa mno. Mfano, katika uwanja Mkuu wa Taifa, yapo malipo ambayo hayaeleweki. *Club* zinapocheza kuna makato ya *VAT, BMT, TFF, DRFA*, ulinzi wa Polisi, kusafisha uwanja, Wachina na mengine mengi. Nashauri pawepo na mabadiliko katika makato ya michezo katika uwanja huu ili vilabu vifaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni lile wazo la kuwa na vazi la Taifa. Limeishia wapi?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara hii, ambayo ni muhimu kwa ustawi na mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kuitaka Wizara, kuchambua na kuongeza nguvu katika jukumu la ushauri na uhamasishaji. Katika jukumu la kuwaendeleza na kuwalea vijana; naishauri Wizara iongoze nguvu katika kushauri Wizara na sekta mbalimbali, katika kulea vijana. Jukumu la vijana kuwa na elimu ya michezo mashuleni litafanikiwa iwapo Wizara itazishauri Wizara za Elimu na TAMISEMI na kufanya kazi nao kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, Sekta hii ya michezo na utamaduni imekufa; na ni kwa Wizara hii kupiga filimbi, tutanyanyuka. Wizara inapashwa kuwa karibu, kushauri na kushawishi Ofisi za Waziri Mkuu na ile ya Ardhi, katika kuona vijana wanapendelewa kwa kupewa ardhi na kuwezeshwa kwa lengo la kuajiajiri. Hii ni mifano tu ambayo Wizara itasaidia kwa kushauri na kushawishi Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, la muhimu ambalo nataka nilisemee kwa pekee, ni fursa ya kuendeleza vijana kwa kutumia Kambi za JKT. Uamuzi wa kuanzisha Kambi hizi ni fursa nzuri ya kufufua michezo. Vijana wenye vipaji vya michezo na ujasiriamali, watambuliwe na kupelekwa katika Kambi hizo. Wakae huko kwa kipindi muafaka ili wapate elimu na ujuzi kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tukiweza kutumia kambi hizi kwa ufanisi, tutaweza kupunguza stadi kubwa ya vijana ambao wanaisubiri Serikali iwapatie ajira. Lakini pia hii ni nguvu kazi muhimu, hazina ambayo inabidi iandaliwe sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, bajeti hii ipite.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono bajeti ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kwa Wanahabari, bado lina utata mkubwa. Wengi wao wana ajira za muda, yaani zisizokuwa za kudumu. Wengi wao wamefanya kazi katika vyombo hivyo vya habari kwa miaka mingi. Je, Wizara hii imechukua hatua gani ili kuhakikisha Wanahabari hawa wanapata haki zao katika ajira?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni taarifa zimetoka katika Vyombo vya Habari kuwa, kuna utovu wa nidhamu, hadi kufikia kocha wa Timu ya Taifa ya Wanawake ya Mpira wa Miguu kujiuzulu.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusagana linafanywa bila kificho. Wale wanaojifanya wanaume, huwa mara kwa mara wanapingana na ushauri au adhabu zinatolewa kwa wale wanawake wao, hadi kusababisha vurugu na ukosefu wa nidhamu katika timu. Hii ni sababu kubwa ya kushindwa kwa timu hii katika mechi nyingi za Kimataifa na Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, namtaka Mheshimiwa Waziri achukue hatua za dharura ili kuondoa kadhia hii katika timu hii ya Taifa ya mpira ya akina mama.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze hotuba yangu wangu kwa kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukaranga; Naibu Waziri, Mheshimiwa Amos Makalla; Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mmomonyoko wa maadili ya Waandishi wa Habari, yasiyozingatia maadili ya Vyombo vya Habari. Wengi wao wamekuwa wakichochea migogoro na vurugu, kwani wanaandika habari za uongo na pia wanatumiwa na Vyama vya Siasa kuivuruga Serikali. Wamiliki wa vyombo kama wanafahamika, kwa nini Serikali isitoe onyo? Kwa sababu, vinaweza kuhatarisha amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ijaribu kusimamia maslahi ya wafanyakazi katika Vyombo vya Habari, kwani kuna baadhi ya vyombo hivi haviwatendei haki wanahabari hao.

Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili ni kitambulisho cha uraia wa Tanzania. Hii ni sambamba na kuwa, lugha ni utamaduni halisi wa Taifa hili. Kwa hiyo, tunaomba maeneo yafuatayo yazingatiwe:-

- Mahakama zitumie lugha ya Kiswahili katika kuendesha na kuandika hukumu;

- Usaili wa kazi utumike kwa Kiswahili kwani vijana wetu uwezo wanao, wanashindwa kupata kazi, kikwazo ni lugha ya Kiingereza;

- Mashuleni pia Kiswahili kitiliwe mkazo; na
- Vyeo mbalimbali vya majeshi yetu vitamkwe Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa sasa imefanikiwa kutoa wanamichezo mahiri na Sera ya Michezo kwa sasa, “Michezo ni Ajira.” Lakini hakuna mkakati wowote uliowekwa kuhakikisha Sera hii inatekelezwa. Kutokana na changamoto nyingi, baadhi yake ni viwango vya michezo ambavyo vilitengwa kwa ajili ya vijana wetu, Halmashauri imeshagawa kwa wananchi na kubadilisha matumizi.

Mheshimiwa Spika, Serikali, iliwahi kutoa tamko kuwa, wale wote waliojenga katika maeneo ya wazi, yaliyotengwa kwa ajili ya michezo wabomolewe, lakini mpaka leo hakuna hatua yoyote. Je, ni nini sasa msimamo wa Serikali katika hilo?

Mheshimiwa Spika, Serikali, ione umuhimu wa kuwekeza katika michezo, kwa kufungua *academy* za michezo ili kukuza vipaji na kuandaa timu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, *Twiga Stars* imekuwa ikifanya vizuri sana, lakini mpaka sasa Wizara haijaweza kuitengea hata fungu. Siku zote wamekuwa wakitembeza bakuli wanapokuwa na mashindano. Hii inawakatisha tamaa. Au kwa sababu, ni timu ya wanawake? Ni vizuri sasa itafutiwe kocha, pia ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, Vazi la Taifa, hivi limefikia wapi? Kwani kuna Kamati iliundwa kwa ajili ya kushughulikia hili suala, lakini majibu hatujapata. Naomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anajumuisha atujulishe. Tunasikia vibaya kuona nchi karibu zote za Afrika, zinatumbulika kwa mavazi ya nchi zao.

Mheshimiwa Spika, vijana ni kundi kubwa sana na lina tatizo kubwa sana la kupata ajira. Kundi hili, linatakiwa liandaliwe mazingira ya kujiajiri. Tunao wamanchinga, mafundi gereji, uchongaji na kadhalika. Sasa uwepo mkakati wa vijana hawa kuwezeshwa ili waweze kujiajiri na kwa wale wanaomaliza Vyuo Vikuu, tuangalie namna ya kuwapa ajira, kwani ni kundi kubwa. Pamoja na elimu waliyopata wanaishia kuwa wazururaji tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sana tumekuwa tukiambiwa kuwa, kuna mpango wa kuanzisha Benki ya Vijana, lakini jitihada hizi mbona hatuzioni? Tunaomba sasa Serikali, ituambie ina mpango gani juu ya hili suala? Tunataka vijana sasa, waweze kuwa na uwezo wa kukopesheka katika Benki yao.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri zetu kuna mafungu yametengwa kwa ajili ya vijana. Lakini, bado hakuna mpango mzuri wa kuweza kuwafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Wizara hii, jambo hili ilisimamie, ili vijana wasijiingize katika makundi mabaya ya wizi na ujambazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, siku hizi Uandishi wa Habari umekuwa kazi isiyo na utaratibu. Kila mtu anadhani anaweza kuandika habari. Suala hili limekuwa hivyo baada ya Serikali kuliacha hovyo hovyo bila kuliwekea kanuni na taratibu za Uandishi wa Habari. Aidha, waandishi wamekuwa wakipotosha umma kwa taarifa zao zisizokuwa na ukweli, bila kuzifanyia uhakiki, na Serikali, haichukui hatua zozote kwa Waandishi wanaopotosha habari. Hivyo, naishauri Serikali, kuweka kanuni zenye kuweka adhabu kwa Mwandishi yeyote atakayeandika au kuripoti habari au taarifa za uongo, basi hatua kali zichukuliwe kwa Mwandishi huyo, pamoja na kulifungia gazeti hilo.

Mheshimiwa Spika, michezo ya Shuleni, ni wazo zuri la Serikali kurejesha suala la michezo mashuleni, kwani utaratibu huo utaweza kuinua viwango vya michezo kwa watoto wetu. Hata hivyo, ili kuhakikisha lengo halisi la kukuza michezo nchini ni kuweka mipango mkakati madhubuti, itakayowezesha kufikia lengo husika.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napongeza kwa umahiri wa wachezaji wa timu ya *Twiga Stars*. Aidha, timu hiyo imeiweka nchi yetu ya Tanzania katika hatua nyingi mbele katika kuendeleza soka la wanawake nchini. Hivyo naishauri Serikali, iweke utaratibu mzuri wa uteuzi wa wachezaji hao wa *Twiga Stars* bila malalamiko. Vilevile Serikal, iwe inaanzisha timu za mipira ya miguu ya wanawake katika kila Kata, Jimbo au Wilaya ili kuweza kupata wachezaji bora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vazi la Kitaifa la Tanzania, naipongeza Serikali kwa kuanza mchakato wa kutafuta vazi rasmi la Tanzania, suala ambalo litaleta heshima ya nchi yetu. Hata hivyo, kwa kuwa hili ni suala muhimu sana, naiomba Serikali kuharakisha suala hili linamalizika mapema, kwani dunia itatuacha.

Mheshimiwa Spika, mikutano ya pamoja kati ya *TFF* na *ZFA* nimebaini kwamba, Vyombo hivi huwa havikutani mara kwa mara katika kujadili na kukuza soka letu la Tanzania. Hivyo, nazitaka Serikali zetu mbili, kuweka ratiba ya Mikutano hiyo kwa kila mwaka. Aidha, Mabaraza ya Michezo, yahusishwe zaidi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013, kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara – Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pia nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Amos Makalla, kwa weledi, imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu, Wizara hii ni roho ya ustawi wa nchi yetu. Hivyo, majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekelezaji. Ni heri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kuboresha na kuondoa upungufu unayojitokeza kila siku, maana sidhani kuwa ni busara kukosoa tu bila kutoa suluhisho.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba hii kujumuisha mengi, naomba nichangie machache kufuatana na hali halisi ya Jimbo la Kilwa Kaskazini na nchi kwa ujumla. Lipo tatizo kubwa sana katika Sera na Mwongozo wa Vyombo vya Habari, ambapo sasa imekuwa ni jambo la kawaida sana watu kuvitumia kuwaumiza na kuwadhalilisha wengine pasipo na ukweli. Uhuru

uliopindukia hauwezi kuleta tija kwa ustawi wa nchi yetu. Serikali ichukue hatua za uhakika katika kuthibiti hali hii, maana inaliweka Taifa letu rehani kwa manufaa ya wachache.

Mheshimiwa Spika, hali ya kiutendaji ya Shirika la Utanganzaji la Taifa *(TBC)* ni mbaya, ambapo inashindwa kujiendesha kwa kutokuwa na mtaji, lakini pia uchakavu mkubwa sana wa vifaa. Katika eneo la Kilwa, Ruangwa, Liwale na Rufiji, matangazo hayasikiki na hazitolewi sababu za msingi. Shirika la Magazeti *(TSN)*, nalo limekuwa likiyumba bila ya kuwa na Mtendaji Mkuu kwa kipindi kirefu sasa na haielezwi ni kwa nini mchakato huu haukamiliki.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa Serikali, imeshindwa kuwekeza katika michezo na kuiachia sekta binafsi ambayo kimsingi haina uwezo. Katika eneo hili inashangaza pia Serikali, kuzuia taasisi za umma kushiriki michezo. Ikumbukwe miaka ya nyuma taasisi za umma zilifanya vizuri, kama vile Reli, Bandari, *RTC, NASSACO*, Bora, Tumbaku na kadhalika. Kwa kiasi kikubwa ilileta ushindani mkubwa na kuweza kutoa matokeo mazuri kwa timu za Taifa katika mashindano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika michezo utasaidia sana kutoa ajira kwa vijana, ikizingatiwa sekta hii ikitiliwa mkazo inaweza kuwa kichocheo kikubwa sana kwa ukuaji wa uchumi kama wenzetu wa nchi jirani wanavyofanya. Serikali ifikirie kutoa vivutio *(incentives)* kwa wanaowekeza katika michezo kama sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, mashirika kama *Vodacom,* Serengeti, Bandari, *PPF, NSSF, TBL* na wengineo, wasijitoe katika uwekezaji kwenye michezo kwa kuanzisha timu, kliniki za michezo na viwanja vya michezo, ili kuwa mfano mzuri wa uendeshaji wa timu kwa kuzingatia ujuzi na uwezo wa kiuchumi walionao.

Mheshimiwa Spika, uibuaji wa vipaji katika michezo ni jambo muhimu hasa kwa michezo kama mpira wa miguu, kuogelea na baiskeli. Tunao vijana wengi sana ambao tukiwapa nyenzo na mbinu wanaweza kufanya vizuri sana katika michezo na kuipeleka mbele nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linahusu lishe duni kwa wanamichezo. Serikali, haiwezi kukwepa jukumu hili, ambapo Watalaamu, wametoa angalizo kuwa, uwezo kwa Wanamichezo wetu kuwa duni, inatokana na lishe duni pia. Naishauri Serikali, sasa iajiri Maafisa Lishe wa kutosha, ikiwa ni pamoja na kuhimiza elimu ya lishe kwa wanamichezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye jitihada za makusudi katika kuelimisha jamii kuhakikisha tatizo la watoto kushiriki katika sinema na maigizo yaliyokuwa juu ya umri wao. Nchi zote duniani haziweki wazi umri wa kuangalia filamu au muziki. Mfano mzuri ni Marekani, ambapo ni nchi iliyoendelea, lakini imeweka ukomo kwa kila umri.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii, kwa hotuba na mikakati mbalimbali waliyoiwasilisha katika Bunge lako Tukufu kupitia Hotuba hii ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Wizara hii, inayo dhamana kubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Sehemu kubwa ya wananchi wa Tanzania ni vijana ambao ni zaidi ya 50%. Mojawapo ya majukumu ya Wizara hii ni kuratibu na kusimamia masuala ya maendeleo ya vijana ili kuwawezesha kujiajiri na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri ameliomba Bunge lako liidhishe Shilingi bilioni 19.3, kati ya hizo Shilingi bilioni 3.0 tu ndiyo ameomba zitumike kwa kazi za maendeleo. Mchanganuo huu hauwezi hata kidogo kuwezesha utekelezaji wa majukumu ambayo Wizara imepangiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali iangalie mchanganuo wa bajeti yake. Siyo rahisi kuwezesha vijana kiuchumi au kuwawezesha kuajiri kama Serikali haifanyi tafiti za kutosha, ili

kuainisha fursa zilizopo ambazo vijana wetu wanaweza kunufaika nazo. Lakini pia naishauri Serikali kupitia Wizara hii, itenge fungu la kutosha ili kuwapatia mikopo vijana wetu waweze kuanzisha biashara ili kuwaondolea kero za maisha.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wanahitaji elimu ya stadi za maisha. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho ya hoja yake, aniambie Wizara yake imejipanga vipi ili kuwapatia vijana elimu ya stadi za maisha? Vijana wetu ndio nguvu kazi ya Taifa, lakini kama hapatakuwa na mkakati mahsusi wa kuwaendeleza, watabaki bila matumaini na mwisho wa siku watajiingiza kwenye mambo yasiyokubalika kwa sababu ya kukata tamaa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Sera ya Vyombo Vya Habari itumike ipasavyo. Mwenendo wa baadhi ya Vyombo vya Habari haukubaliki, kwani vimekuwa vikishabikia upande wa upinzani na kuwachonganisha wananchi dhidi ya viongozi walioko madarakani. Kwa uelewa wangu wa dini, viongozi wote wamechaguliwa na Mungu. Navishauri vyombo vinavyokiuka matakwa ya Sera ya Habari, Sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya utamaduni ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Nchi za Magharibi na Ulaya Mashariki, zimenufaika sana na mchango wa tasnia ya sanaa. Mfano, taasisi kama *Hollywood* imetumika kutoa elimu kwa umma, lakini pia filamu ambazo zimetengenezwa na wasanii wa *Hollywood* zimechangia mapato ya nchi na ajira kwa waigizaji. Naishauri Serikali yetu, ijenge Vyuo vya Sanaa, sambamba na kukijengea uwezo Chuo cha Kaole kule Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya michezo ni muhimu kwa kujenga umoja wa wanamichezo, kutoa ajira kwa wanamichezo, pia ni chanzo kizuri cha mapato kwa wanamichezo na nchi kwa ujumla. Naishauri Serikali iwekeze katika michezo ili Taifa liweze kuwa na wanamichezo mahiri ambao watalileteasifa Taifa letu. Aidha, naiomba Serikali yangu, pamoja na juhudi za kuleta makocha kutoka nje, nashauri ijenge vyuo ambavyo vitatoa elimu ya michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri kwamba fedha ambazo zinatengwa kila mwaka kwa Wizara hii ziongezwe ili kukidhi utekelezaji wa majukumu ambayo Wizara hii imepangiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha leo na kuweza kuchangia hoja hii. Kwanza, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kuchangia kuhusu Vyombo vya Habari kama vile *TV* na *Radio*. Navipongeza vyombo vyote vya habari hapa nchini kwa jinsi wanavyoweza kutupasha habari na matokio mbalimbali yaniyotokea nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na vyombo vyetu vya habari *Radio* na *TV*, kusoma habari za ndani ya nchi na nje ya nchi, mimi naona zina kasoro ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, karibu *television* zote zinatoa habari wakati mmoja, saa 2.00 usiku na saa 12.00 asubuhi, wakati wananchi wote hawawezi kuwepo kwa wakati huo. Ili kwenda vizuri na usomwaji wa habari, ni bora habari kutoka Televisioni kama vile *ITV, STAR TV, TBC1, TBC Radio,* na *Radio One* ziwe zinatofautiana kusoma taarifa za habari japo kwa saa, ili wananchi wakikosa saa 2.00 wawahi saa 3.00 usiku.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa vijana hawana viwanja vya michezo kutokana na viwanja vya michezo kama viwanja vya mpira kuvamiwa na wananchi au Serikali kwa kujenga nyumba. Kwa hiyo, naishauri Serikali kusimamia vizuri viwanja vya michezo ili vijana wetu waweze kuwa na viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wasanii wetu hasa wa michezo ya kuigiza kwenye *television* na *radio,* wameegemea sana michezo ya mapenzi au ya uchawi jambo ambalo siyo zuri sana.

Kwa sababu watoto au vijana wanaotazama michezo hiyo huwa wanasoma na baadhi yao kuvutika na kuiga. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kuelimisha wasanii wetu kujikita kutoa elimu juu ya nchi yetu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuwakusanya vijana na kuwapa elimu ya kuwa na vikundi vya biashara ili wapatiwe mkopo na kuweza kujiari kibiashara ili kuondoa matatizo ya vibaka Mitaani.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsanteni sana.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwajenga Wizara hii iwe katika amani nzuri ya nchi yetu. Hata hivyo napenda nichangie machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wanahabari wetu wengi wanapenda kutoa habari kutegemea na matukio, yaani wanapenda zaidi kuripoti matukio bila kuyafanyia utafiti wa kina. Katika hili, ni bora kuwa na wanahabari waliojikita katika jamii mbalimbali ili msomaji wa habari ile afaidike zaidi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya magazeti yamejikita katika Vyama fulani vya Siasa kiasi kwamba msomaji asiyeunga mkono Chama kile, anajenga taswira kuwa kinachoongelewa humo ni propaganda tu ya Chama fulani. Kama inawezekana, ingekuwa vizuri yasioneshe picha hiyo wazi wazi hata kama wamiliki wa gazeti hili ni waumini wa Chama fulani.

Mheshimiwa Spika, bado nchi yetu haijfanya vizuri katika michezo. Kwa ujumla tumekuwa na washiriki zaidi kuliko washindani, hadi katika michezo ya Kimataifa. Nashauri ziwepo Shule nyingi tukianza na mitaala ya michezo katika mashule yetu, aidha, vilabu vya mpira wa miguu, pete na riadha na kadhalika. Kuwe na Shule za *Academy* kwa vijana ambao watakomazwa katika aina mbalimbali za michezo. Ni vyema mashule yakaandaa mashindano ya aina mbalimbali ya michezo ili kuibua vipaji huko Vijijini na Wilayani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina utamaduni mpana kwa kuwa na makabila zaidi ya 120. Hata hivyo, ni fahari kubwa kuwa na utamaduni wetu umeunganishwa na lugha ya Kiswahili. Naomba lugha ya Kiswahili ikuzwe zaidi na ivuke mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema utamaduni wa makabila mbalimbali ukatunzwa na kuenziwa sana. Lakini wakati huo huo utamaduni potofu upigwe vita ili kuendana na wakati uliopo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Serikali mbali ya kuridhia, mkataba wa vijana Afrika, ningependa kujua Serikali imejipanga vipi kutekeleza maazimio hayo ya mkataba huo. Kuondoa tatizo la ajira kwa vijana, vijana kutumia kilimo kujikwamua na umasikini, kumilikishwa ardhi na kuhakikisha vijana wanapata elimu bora itakayowafanya wapate soko la ajira hasa ukizingatia tupo kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakabiliana vipi na changamoto zinazolikabili Taifa kwa baadhi ya vyombo vya habari kukiuka maadili ya vyombo vya habari, kujihusisha na siasa kwa kutumika na baadhi ya Vyama vya Siasa kuchafua baadhi ya wanasiasa kwa maslahi binafsi?

Mheshimiwa Spika, pia vyombo vya habari vimekuwa vikiwanyonya Wanandishi wa Habari kwa kuwalipa pesa kidogo, hivyo kuchangia waandishi wengi kukiuka maadili na kuandika habari zisizo za ukweli kwa kutumiwa na watu wenye maslahi binafsi ili kupata rushwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inaviwezesha Vyama vya Soka ngazi ya Wilaya na Mikoa ili viweze kufanya kazi kwa ufasaha na kuendeleza kuibua vipaji na Taifa liendelee kuwa na timu nzuri ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imejipanga vipi kusaidia timu ya mpira wa miguu ya wanawake? Tumeshuhudia kumekuwa na mashindano mbalimbali ya kuibua vipaji vya mpira wa miguu kwa wanaume kama Kopa Coca Cola?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuanzisha michuano mbalimbali katika ngazi ya Wilaya na Mkoa ili tupate timu nzuri ya mpira wa miguu kwa wanawake?

Mheshimia Spika, naomba Serikali iendelee kushughulikia tatizo la wizi wa kazi za wasanii.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa vazi la Taifa limefikia wapi?

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pia nampongeza Mheshimiwa Fenella Mukangara kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii na Mheshimiwa Amos Makalla kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata ufafanuzi katika masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, je, Wizara ina mipango na mikakati gani mahsusi ya kuwasaidia vijana wa kike?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mipango ya Wizara na mikakati yao ya kuwajengea uwezo vijana, inaonekana msisitizo mkubwa umewekwa kwa vijana wa kiume. Hii inawezekana kuwa ni kwa sababu vijana wa kiume ndio wanaoshinda vijiweni kufanya fujo na kushiriki katika shughuli za kuvuruga amani na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kuwa, pia vijana wengi wa kike nao hawana shughuli za kufanya katika kukabiliana na changamoto za maisha licha ya kwamba huwezi kuwaona wamekaa vijiweni. Hivyo ningependa kupata maelezo ya mikakati na mipango mahsusi ya Wizara inayolenga vijana wa kike hasa waliopo Vijijini ili waweze kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali na masuala mengine ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, je, ni kwa nini timu ya Taifa ya soka la wanawake wa Twiga *stars*, haipewi umuhimu kama timu ya mpira wa miguu ya wanaume *(Taifa Stars)?* Inasikitisha kuona timu hii haipewi fedha za kutosha wakati wa maandalizi ya Kambi na hasa inapojiandaa kushiriki mashindano mbalimbali ya Kitaifa, licha ya ukweli kuwa timu hii imeweka rekodi nzuri sana katika soka la wanawake Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, soka la wanawake licha ya kuwa ni ajira kwa vijana na burudani, linaweza kutumika sana katika kusaidia jitihada za Serikali za kukuza usawa wa jinsia na haki za wanawake. Kitendo cha wasichana kucheza vizuri mpira wa miguu ambao wengi wanadhani kuwa hii ni fani ya wanaume, ujumbe mkubwa unaopelekwa kwa jamii ni kuwa, wasichana na wanawake wana uwezo wa kufanya vizuri zaidi katika kazi na fani nyingine zinazodhaminiwa kuwa ni za wanaume peke yao.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa Mheshimiwa Waziri kwa kuwa naye ni mwanamke, atawekeza nguvu zake katika kuisaidia *Twiga stars* ili iwe kwenye hadhi sawa kama timu ya *Taifa Stars*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara na Mikoani.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ualimu Butimba kinatoa Stashahada katika fani za Michezo, Muziki, Sanaa za Ufundi na Sanaa za Maonyesho. Taaluma inayotolewa katika fani hizo hapo Chuoni ni ya hali ya juu na hivyo ni vyema wahitimu hawa wakatumika pia kusaidia kuwaandaa

vijana wenye vipaji katika fani hizo ili waweze kujiajiri kupitia fani hizo ambazo zinatoa ajira nyingi sana duniani kote. Hili linawezekana kwa Wizara hii kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika kuwabaini wahitimu wenye *interest* za kuendeleza fani zao kwa vijana wetu wa ngazi zote za elimu.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano uliokuwepo kati ya Chuo cha Ualimu Butimba na Chuo cha Sanaa Bagamoyo uendelezwe kwa kuandaa matamasha ya pamoja na kutumia matamasha haya kubadilishana uzoefu, changamoto na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa *TBC* haipatikani Musoma, hadi uwe na *dish* au king'amuzi. Tatizo ni nini? Tunaomba isikike, maana siyo wote wanaoweza kuwa na vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza matangazo yanayodhalilisha akina mama yaondolewe kwenye *TV* zetu, mfano ni lile la '*always*' humfanya mwanamke ajisikie vibaya hasa anapokuwa na watoto, wakwe na kadhalika. Liondolewe tafadhali.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Kazi njema.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme naunga mkono hoja, lakini hata hivyo ningependa maoni yangu yafanyiwe kazi kwa haya machache tu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uhuru wa Habari na maadili yake hapa Tanzania inatumika vibaya sana. Maadili katika tasinia ya habari yanakiukwa sana. Habari ni kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha. Lakini cha ajabu, sasa hivi imekuwa habari zinakuwa tu ni za kishabiki katika aidha kuchafuana au kujengana kwa sababu za kibinafsi, kisiasa, ilimradi tu gazeti liuzwe au *Television* na Radio isikike na ionekana bila kuzingatia maadili *(ethics)* ya kazi katika tasnia hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara itoe suluhisho ina mkakati gani katika kuhakikisha ina-*control media* iliyojaa *ethics* za tasnia. Nahitaji kupata majibu ya kina na uhakika katika kujenga na kuimarisha nchi yetu kwenye tasnia hii ya jamii tunayoizunguka, kwani *media* ni nyenzo muhimu katika jamii yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya. Akili pia hufanya kazi vizuri endapo michezo imezingatiwa katika viungo vya mwili. Lakini kitu cha ajabu sana, kwanza makocha wa timu zetu za Tanzania kwa nini wanakuwa ni *expatriates*? Ni sababu zipi zinazopelekea kuwalipa licha ya kuwa ni kubwa lakini tangu wameanza kufundisha timu zetu za nyumbani *impact* yake imekuwa ni ipi? Hatuna makocha wa hapa hapa Tanzania kuwajengea zaidi uwezo wa kufanya shughuli hizo? Kwa mara nyingine tena nahitaji kupata maelezo ya kina?

Mheshimiwa Spika, michezo sasa hivi hapa nchini kwa nini imeshuka viwango tofauti na zamani? Wizara inifafanulie, ina mkakati gani kwa sasa katika kuinua vipaji vya wanamichezo wetu Tanzania? Kwani vipaji hivyo vimefifia kabisa tofauti na mwanzo ambapo vijana walikuwa wanang'amuliwa vipaji vyao tangu enzi wakiwa mashuleni, wadogo na hivyo kuwaendeleza kama wafanyavyo wenzetu wa nchi nyingine katika kuendeleza na kukuza michezo.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wamekuwa wakirandaranda Mitaani, hivyo kuishia kufanya matendo yasiyoendana na utamaduni wa Mtanzania. Serikali ina mkakati gani kuondokana na hilo na kudumisha yale yaliyo mema kwa nchi yetu? Nini tuna cha kujivunia katika kukuza utamaduni wetu? Naomba kupatiwa maelezo ya kina juu ya hili tafadhali.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kujua Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha Kiswahili kinakuwa ni lugha moja ya Afrika hasa ukizingatia historia yake katika nchi nyingine za Afrika, Tanzania ikiwa ndiyo chambo?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOZA ABEDI SAIDY:** Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kuchangia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kuwa tunatambua umuhimu wa Wizara hii muhimu ambayo inajiajiri yenyewe, hasa nikianza na michezo.

Mheshimiwa Spika, michezo ni ajira, michezo ni afya, michezo ni ujuzi, hivyo Serikali inatakiwa kuwa makini kwani suala hili ni moja la kurejesha heshima ya nchi kupitia michezo kimaadili na ukakamavu kwa vijana wa Taifa la kesho.

Mheshimiwa Spika, napendekeza michezo irejeshwe kuanzia Shule za Msingi, kwani hata kipindi cha mwaka 2011 nilichangia habari hii. Bado michezo huko Wilayani haijachangamka kama inavyotakiwa hasa nikizingatia mafunzo ya Baraza la Michezo la Taifa *(BMT)* kuwezeshwa, mafunzo mafupi kwa walimu 3000 nchini kote; sasa suala la kujiuliza; mafunzo haya yameshafanyika katika Manispaa na Halmashauri za Miji ili wapange viwango vya wataalamu wa michezo kwa viwango stahiki (madaraja) kushiriki michezo?

Mheshimiwa Spika, tuangalie mpango wenyewe, kweli unaelimisha watu kama vijana kwenye michezo bila kitendea kazi na bila kuwawezesha vijana? Wanajituma wanakwenda kwenye michezo, wana njaa wamekuwa omba omba; kwani unapoanzisha jambo, unategemea upate. Sasa utapataje vijana wenye vipaji huko Vijijini hata viatu vya michezo hawana? Huo siyo utendaji, bali ni kujaribu jambo. Serikali bado haina nia ya dhati ya michezo.

Mheshimiwa Spika, hii inasababisha vijana kusambaa ovyo kutafuta sehemu zenye ajira ya michezo kwa kulipwa, kwa kuona nchini hakuna pato. Kijana wa Kiafrika amekuwa hana thamani nchini? Kwani wengi huenda nchi kama Msumbiji na kupata matatizo bila kuchukuliwa hatua za kuwadhibiti kimichezo. Kama vile kuuza *CD* za utamaduni wa asili nchini, makongamano yasiishie Mijini, yaende na Vijijini pia.

Mheshimiwa Spika, habari ni kivumisho cha upatikanaji wa taarifa. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze suala la *TBC,* Shirika kubwa la Utangazaji Tanzania kuwa na vyombo vichache kama vile kamera na kadhalika: Je, ni lini Serikali itaboresha Shirika hili muhimu? Mheshimiwa Waziri akifanya majumuisho yake, atuambie hivi vyombo vya *digital* ametwambia vitarusha matangazo yake, hivyo vingine vyote vitasitishwa. Je, wale kule Vijijini wenye redio za wakulima watapataje habari na kwenye *television* zao za zamani? Watazipeleka wapi? Je, Serikali haioni watu wake siyo wote wenye uwezo huo, na hakuna maeneo mengi umeme?

Mheshimiwa Spika, Shirika la BASATA linafanya kazi zake wapi? Hivi ni Mijini tu? Huku Wilayani watatembelea lini hasa? Vile vile *COSOTA,* chama hakimiliki bado hakuna haki na usawa katika sanaa kwenye malipo ya muziki, kwani kutofanya hivyo, chombo hiki hakimpi fursa mtoto wa kimasikini kupata ajira binafsi kupitia sanaa. Taifa pia halipati pato kwa kuuza na kutoza ushuru kwa kuuza *CD* ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie hayo yote ambayo hali imekuwa ngumu, kwani mradi wa *digital* mpaka sasa ni Mikoa saba tu na muda ni mdogo mno. Je, Serikali inaonaje kuongeza muda, kwani wananchi wapewe elimu na kutambua umuhimu wa maendeleo ya chombo hicho?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Sasa nitamwita Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Anapewa dakika 15.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii nami niweze kuchangia katika hoja yetu hii tuliyonayo leo ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Kwanza, nianze kama Watanzania wengine kutoa pole kwa wenzetu wote wale wahanga ambao walipatwa na ajali. Pia natoa pole na rambirambi kwa wale wote ambao wamepoteza marehemu.

Mheshimiwa Spika, la pili, nami nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumshukuru Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo. Nataka niseme tu kwamba, sitamuangusha na kwamba, amepatia kwani wote nyie ni mashahidi, mimi ni nahodha wa timu ya Bunge *Sports Club* na kwa mantiki hiyo, nataka kusema kwamba kuniweka katika Wizara hii ni kwamba, upele umepata mkunaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine kwa namna ya pekee niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Mvomero kwa namna ambavyo wananipa ushirikiano na kwa namna ambavyo walionesha imani yao kubwa sana. Nisingekuwepo leo hata kuteuliwa kuwa Naibu Waziri kama wao wasingenipa heshima ya kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Mvomero. Nataka niwahakikishie kwamba, nawawakilisha vyema, nawashukuru kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nataka niwaambie tu kwamba kwa mwaka huu wa fedha nimefuatilia mambo mengi makubwa likiwemo suala la barabara yetu ya Dumila – Magole- Turiani – Mziha na itakamilika kama ilivyopangwa. Lakini pia miradi mikubwa ya maji katika Jimbo ikihusisha Mvomero na Turiani nayo tumepata fedha na miradi mikubwa ya umeme inayoendelea ni jitihada za Serikali kuhakikisha tunaendelea kupata umeme na mawasiliano katika maeneo ambayo tulikuwa na matatizo makubwa ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, la tatu niishukuru sana familia yangu, mke wangu Grace James na watoto wangu kwa kunipa ushirikiano kwa muda wote katika nafasi yangu ya Ubunge na Unaibu Waziri. Najua wamenikosa kwa muda mrefu, lakini ndiyo majukumu yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine niishukuru sana Kamati ya Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama na Makamu wake Juma Nkamia na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, rafiki yangu Joseph Mbilinyi kwa maelekezo na ushirikiano wanaotupa katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru sana Wabunge kwa michango yenu mingi mizuri. Mmechangia wengi, kwa maandishi wako karibu 126 na kuzungumza atakuja kuwataja Waziri. Mmesema mambo mengi lakini tunashukuru kwa michango na maelekezo yenu.

Mheshimiwa Spika, hatuna nafasi kubwa sana ya kujibu hoja zote, nitapitia baadhi ya maeneo na Waziri atapata nafasi ya kujibu baadhi ya maeneo. Hata hivyo, napenda niseme kwamba michango yote niliyoiangalia mingi ni ya pongezi, changamoto na maelekezo.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme, nawaahidi kwamba tutayafanyia kazi yote mliyoyasema. Mimi ni mwenzenu nilikuwa kule nyuma mtaa wa *V.I.P (VIP street* pale), naelewa Wabunge wakati mwingine tunasema, ndiyo kazi ya Bunge kuisimamia Serikali na nataka niseme kwamba, hata Wazungu wanasema ukiwa unalijua tatizo na hutaki kuonesha njia ya kutatua tatizo wewe pia ni tatizo. Kwa hiyo, kwa michango yenu mingi mizuri, mnataka tuondokane na matatizo hayo. Sisi tumeipokea.

Mheshimiwa Spika, tupeni muda, nimeteuliwa Mei mpaka sasa nina miezi karibu mitatu, kwa yale yote yaliyofanywa huko nyuma, ni Serikali hii, lakini na sisi ndiyo tunaingia. Kwa hiyo, tupeni muda ili tuweze kukamilisha hizo kazi. Kuna wengine wamesema Wizara ifutwe, isifutwe ili sisi tuliopewa kazi hii sasa tuoneshe uwezo wa kuyasimamia hayo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sasa nijielekeze kwenye hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nimesema kwamba ziko nyingi lakini nitazungumzia baadhi tu ya hizo hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo suala lililozungumziwa hapa na Wabunge karibu watatu linalohusu viwanja vya CCM kwamba vitarudishwa lini Serikalini. Nataka niseme tu kwamba, niliwahi kujibu swali hapa, lakini na michango yenu yote inaonesha dhahiri kwamba tunatambua mmiliki wa viwanja hivi vyote ni Chama cha Mapinduzi na kama hivyo ndivyo kwa sababu haya mambo yote

yamethibitishwa na kesi ya mwaka 2010 Na. 16 ambayo aliifungua Wakili Mbogolo. Katika kesi hiyo ilithibitishwa pasipo mashaka yoyote kwamba viwanja vyote vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba michango yenu yote mliyoitoa hapa juu ya ubovu wa viwanja, kuchakaa na namna gani ya kuviboresha CCM nao wamesikia. Lakini ni hiari yao watakapoamua kama ni kurejesha viwanja au la, wao ndiyo wamiliki sahihi. Hata hivyo, michango hiyo inapokelewa na wenyewe watatafakari kuona kwamba, kama inawezekana kwa hiari yao kurejesha viwanja hivyo Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa timu ya Olimpiki iliyopo London kwamba, wako kule wanaishi kwa shida sana, hawajalipwa posho zao. Nataka niseme tu kwamba, timu ipo salama na waliondoka hapa mimi ndiye niliyewaaga, nilihakikisha wamelipwa posho zao za kujikimu kwa siku 15. Hata habari hizi za leo tulipowapigia simu wamesikitika sana kwamba, kauli hizi zinaweza zikavunja moyo wachezaji walioko huko na kwamba Olimpiki wao wamegharamia malazi, safari na usafiri wa ndani. Kwa hiyo, wako salama hawana tatizo. Hata usiku wa leo Mkurugenzi wa michezo atafika kumalizia posho zingine zilizobaki ili waendelee kuwa salama. Nataka kuwahakikishia Wabunge juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kuhusu kwamba kwa nini kituo cha michezo hakikujengwa mpaka sasa toka mwaka 2006 na kwamba hili linatoa mianya kwa mmiliki ambaye ni Katibu Mkuu wa *TOC* kuendelea kufaidika yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba, mwaka 2006 hawa Olimpiki walitoa ofa ya kujenga kituo cha michezo kati ya Kenya, Zambia na Tanzania. Kwa bahati mbaya sana Tanzania ilikuwa haijajiandaa haikuwa na viwanja vyenye hati na Kenya pia ilikuwa hivyo hivyo, kituo hicho kikajengwa Zambia. Kwa hiyo, si kwamba jambo hili limefanywa kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuhusu ubadhirifu kwamba, hii Kamati ya Olimpiki kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha. Nataka niwahakikishie tu kwamba, baada ya kupokea maelezo haya ndani ya Bunge na nje ya Bunge maana yupo kijana anaitwa Gideon Bayo naye amelalamika mpaka kwenye magazeti kwamba kuna ubadhirifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi kama kiongozi nilitaka kusikiliza pande zote. Nilimpigia simu Gideon Bayo nikaambiwa hebu nisaidie zipo tuhuma hizi *email* yangu hii hapa, simu yangu hii hapa, hebu nitumie ubadhirifu wote niambatanishie na vielelezo vyote. Sasa alichokifanya nina *email* yake hapa, ameniambia tu, unajua nilisema tu baada ya kujitoa kwenye Uchaguzi, nilikuwa na hasira. Kwa hiyo, nataka kukueleza tu je, unafahamu kwamba kuna fedha *dollar* 100,000 huwa zinakuja Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, akashindwa kuthibitisha zile tuhuma alizokuwa anazitoa kwenye magazeti na *email* yake ninayo na maelezo yote ninayo hapa. Lakini pia nikamwomba Mkurugenzi wa Michezo kufuatilia jambo hili, naye akatafuta taarifa, lakini zaidi nilifuatilia kupata taarifa kutoka Olimpiki *solidarity*. Wenyewe wameleta taarifa kwamba tulifanya ziara Tanzania mwaka 2009 na tunakutumia taarifa, tukapata taarifa zao kwamba Tanzania kuhusu suala la usimamizi wa fedha unaendelea vizuri na ndiyo maana wameendelea kutusaidia. Kwa hiyo, pia *TOC* wanakaguliwa hesabu zao, wanazo hati safi. Kwa hiyo, maelezo ya Mkurugenzi wa Vijana, maelezo ya *TOC*, maelezo ya fedha zinakotoka huko yamethibitisha pasipo mashaka kwamba hawa hesabu zao zipo vizuri. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, nije suala la gawio la viwanja la asilimia mbili kwa Manispaa ya Temeke. Ni kwamba mapato ya Uwanja wa Taifa awali yalikuwa ni asilimia 20 kwenda Serikalini. Hatimaye tukasikiliza tukapunguza ikawa asilimia 10 ndiyo inakwenda Serikalini na asilimia mbili inakwenda *TFF* kuwagawia wadau wao ambao ni Vyama vya Mpira wa Miguu vya Mkoa na kwa Dar es Salaam asilimia mbili inakwenda Chama cha Mpira, Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo kwamba kwa nini Temeke haipati, lakini *DFLA* wao wanapata mgao huo wa asilimia mbili.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu hoja aliyoitoa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Kwa muda mrefu kumekuwa na maneno mengi kuhusu *studio* ambayo inaitwa *Martha and Studio*. Hii ni *Studio* ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa kwa kikundi cha Fleva *Unit,* aliitoa kwa nia nzuri kuwasaidia kwamba mtu ambaye amerekodi miziki kule akienda pale kuiweka katika kiwango kizuri basi atumie *studio* hii.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na nia nzuri ya Mheshimiwa Rais toka mwaka 2009 aliwapa *studio* hiyo, lakini zaidi aliwalipia hata pango milioni 9,600,000/=. Zaidi ya hapo wakataka wasaidiwe mtaalam wa kufunga *studio* hiyo. Zile fedha za pango alizotoa Mheshimiwa Rais mpaka sasa zimekwisha na wanaomba fedha za pango wakati *studio* bado haijaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba, pamoja na nia nzuri ya Mheshimiwa Rais ya kukabidhi hawa Fleva *Unit studio* hii ili iwasaidie wasanii, nia nzuri ya Mheshimiwa Rais bado haijaonekana. Sasa na kwa kuwa jambo hili limesemwa semwa sana mimi sichelewi na Wizara kuona kwamba tunamshauri Rais na tutashauri kwamba *studio* hii pamoja na nia nzuri aliyokuwa nayo, sasa irejeshwe Serikalini hasa BASATA ili vijana wengi zaidi waweze kufaidika na *studio* hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ilikuwa pia kwamba *THT* wamepewa ofisi ya Serikali, hapana. Ni kwamba *THT* wanazo Ofisi zao zipo Ada *Estate,* pale wanasaidiwa pango na Mradi wa Malaria wana Mkataba nao. Kwa hiyo, sehemu ya pango inalipwa na wale watu wa Malaria na sehemu ya pango wanalipa wao. Lakini tunaendelea kufuatilia Mradi wa Malaria unachangia kiasi gani katika pango hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kuhusu kazi za wasanii kwamba tayari Serikali sasa kupitia Waziri wa Fedha wameridhia kwamba kuanzia mwezi Januari, 2013 kutakuwa na *sticker* na baadaye *barcode* kuhusu kazi za wasanii. Nataka kuwahakikishia tu kwamba, Serikali imejipanga kuona kwamba utekelezaji wa jambo hili unatekelezwa kama ilivyokusudiwa na tunaandaa taratibu nzuri ikiwemo kuwahusisha wadau na mipango ya kuona kwamba taarifa zinapatikana na kuwalinda wasanii kuhusu usambazaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishe na niseme kupitia Bunge hili Tukufu kwamba ule muda wa kuiba kazi za wasanii umefika mwisho. Wale wote wajanja wa Dar es Salaam na maeneo mengine. Nataka niseme kama kulikuwa na hizo kazi mnaweza kudurufu mitambo hiyo muisalimishe haraka sana na kama kuna watu ambao wao wanaweza kuwa ni wajanja zaidi wataendelea. Mimi nataka niwahakikishie tunawajua, nawapongeza akina Alex Msama kwa kazi nzuri wanayoifanya. Serikali itahakikishia kwamba inawapa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, wale wezi wote wa mjini nataka niwahakikishie kwamba, Wizara hii imepata Waziri kijana, mimi mwenyewe nataka niwahakikishie kama kuna watu wapo wapo Mjini tutawaingilia kwenye ma-*godown* yao katika maneneo yoyote. Kuona kazi zile wanazozifanya kwa sababu niwambie tu kama Mjini mimi mwenyewe nimekatwa kitovu changu pale *Ocean Road*, nimekulia Kawe *line Police.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wajanja wote wa Mjini nataka niwaambie kwamba *operation* baada ya Bunge hili kumalizika tutaianza kwa kila kichochoro kuona kwamba, tunakamata na tutachukua hatua kali sana kwa watu hao wanaochezea kazi za wasanii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi sana, lakini nataka niseme tu kwamba Waziri atakuja naye kuyasema. Hatua za kuwawezesha Tasnia za filamu za muziki na sanaa kwa jumla kuchangia pato la Taifa limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Wizara itashiriki kikamilifu katika mchakato wa kurasimisha Tasnia za filamu za muziki ambao utawawezesha wadau wote wa sekta kupata mapato stahiki na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimshukuru sana Waziri Fenella Mukangara kwa ushirikiano mkubwa anaonipa, watendaji wakuu wa Wizara, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano na Maafisa wote na Wakurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Na kitovu kilichopo Dar es Salaam. Mheshimiwa mtoa hoja! Nakushawishi wakati unajibu hoja jibu moja moja usipoteze muda kwa kutaja majina yao.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru kwa dhati kwa kuongoza kwa umakini mkubwa kabisa mjadala huu wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao maswali na maelekezo mbalimbali waliyotoa kuhusiana na Hotuba ya Bajeti ya Makadirio na Matumizi ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli niseme tu kwa kifupi kwamba pongezi zilikuwa ni nyingi sana na kwa kiasi kikubwa zimetupa moyo kuonesha kwamba kazi tunaifanya vizuri na tutaendelea kuifanya vizuri. Tumepokea michango mingi ya kutosha na kwa kiasi kikubwa ni darasa kwangu pamoja na Naibu Waziri wangu.

Mheshimiwa Spika, muda ni mdogo sitoweza kujibu kila mmoja peke yake. Kwa hiyo, nataka niseme lingine pia kwamba wamezungumza kikubwa kabisa kuhusu bajeti kuongezwa. Kwa hiyo, nataka niliseme hapa kwamba, tutatumia ile bajeti tuliyonayo na mtusaidie tuweze kuipitisha halafu mwaka kesho tuweze kuifikiria kwa mapana zaidi.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji walikuwa ni wengi tumepata wachangiaji kwa mchango wa maandishi 144 na wachangiaji wa kusema kwa kauli 10. Sasa naomba niwataje waliochangiaji kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Mariamu Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Hussein Nassoro Amar, Mheshimiwa Lucy Philemon Owenya, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Gosbet Blandes, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Mchungaji Daktari Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Amina Abdallah Amour. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile wapo Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Daktari Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa Desderius John Mipata na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wamechangia Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Daktari Mary Mwanjelwa,

Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mheshimiwa Neema Hamid, Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis na Mheshimiwa Abuu Jumaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Daktari Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Magdalena K. Sakaya, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Anna MaryStella Mallack, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa *Engineer* Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Thuwayba Idrissa Muhamed, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Joshua Nassari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile wapo Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Kapteni John Chiligati na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wapo Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Daktari Titus Kamani, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Philipo A. Mulugo, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba na Mheshimiwa Juma Sururu Juma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini; Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati Vijijini; Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa na Rais; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mbunge wa Tumbatu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna Mheshimiwa Magale John Shibuda, Mbunge wa Maswa Magharibi; Mheshimiwa Profesa Juma Athuman Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi; Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini; Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa na Mheshimiwa Dustan Kitandula, Mbunge wa Mkinga.

**SPIKA:** Naomba mtulie, msiongee, sio mahali pa kuongea na saa hizi sio wakati wa kuongea humu ndani.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ezekiea Wenje, Mbunge wa Nyamagana; Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Margareth Sitta, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Charles Mwijange, Mbunge wa Muleba Kaskazini; Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini; Mheshimiwa Meshack Opululwa, Mbunge wa Meatu; Mheshimiwa Mbarouk Ali, Mbunge wa Wete; Mheshimiwa Profesa Kahigi, Mbunge wa Bukombe na Mheshimiwa Munde Tambwe, Mbunge Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile wapo Mheshimiwa Sarah Msafiri Ally, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge wa Sengerema; Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho; Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mbunge wa Nachingwea; Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini; Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini; Mheshimiwa Daktari Augustino Mrema, Mbunge wa Vunjo na Mheshimiwa David Ernest Silinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mbunge wa Mbozi Magharibi; Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mbunge wa Mtambile; Mheshimiwa Daktari Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga; Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa endelea tu muda unapita.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nataka nisahihishe jina la Mheshimiwa…

**SPIKA:** Mheshimiwa yako mengi tu huwezi kusahihisha. Yako mengi sana, endelea kusoma hivyo hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza kuna jina moja nimelikosa kwa kuwa nilitamka labda nipatiwe hiyo *list.* Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni; Mheshimiwa Tauhida Galos Nyimbo, Mbunge wa Viti Maluum; Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Daktari Getrude Rwakatare, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini; Mheshimiwa George Mkuchika, Mbunge wa Newala na kuna jina moja hapa nililikosa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO**: Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mbunge wa Viti Maalum na kuna jina lingine. *I miss a one name.*

**SPIKA:** Endelea muda hautoshi.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, aliyechangia mwingine kwa maandishi ni Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha na Mheshimiwa Engineer Gerson Hosea Lwenge, Mbunge wa Njombe Magharibi. *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri naomba uendelee maana umeshachukua dakika 20.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Wale wengine nimeshawaingiza.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwashukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Napenda pia nianze kwa kusema kwamba, naishukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa maelekezo mbalimbali yenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara na hivyo kuleta mafanikio yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, nataka pia niahidi kuwa maoni na mapendekezo yote yaliyotolewa tutayazingatia. Yale yote ya muda mfupi katika uwezo wetu tutayafanyia kazi mara moja na mengine tutayaweka katika mpango wetu wa maendeleo wa mwaka mmoja na ule wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, vile vile nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake iliyoibua masuala mbalimbali mengi yakiwa ni ya kutukumbushia vitu ambavyo tulikwishaahidi, lakini pia ambavyo tumekwishavifanyia kazi kwa nafasi kubwa tu ya kutosha. Ameweza kuchangia na tunataka kusema kwamba amechangia kuhakikisha kwamba tunaendelea kujenga Wizara yetu na kuzisimamia vizuri sekta hizi muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tangu mwanzo hoja ni nyingi zilizojitokeza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini napenda nichukue nafasi hii nianze kwa kugusia chache. Nitakachofanya sitoweza hata itakapofika kwenye hoja moja moja sitoweza kugusia ile hoja moja

na kutaja watu wote. Kuna hoja zingine utakuta zimechangiwa na watu 27, wengine 15 na wengine hata 45. Sasa kwa ujumlajumla nataka nizungumzie hoja chache tu kabla sijaingia katika hoja zile ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, kero moja ni ile ukosefu wa ajira. Hili limejitokeza sana na linaulizwa kuna mikakati gani ya kuhakikisha kwamba tunaondoa kero hii. Kwanza nianze kwa kuwashukuru Wabunge kwa kuliona hili nililitegemea kwa kiasi kikubwa, Wizara tulilitegemea kwamba ni kero ambayo ni kubwa inatukabili wote kama Watanzania, lakini kama vijana Wizara ambayo tunayoiongoza na vijana wengi wamo pia humu ndani ya Bunge tulitegemea sana hii ije.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kama ilivyojitokeza wakati wa hotuba yangu, jukumu la Wizara yangu kama Wizara yenye dhamana ya kushughulikia Maendeleo ya Vijana ni pamoja na kusimamia na kuhakikisha kero hii ya ukosefu wa ajira inayotukabili kwa vijana inayolikabili Taifa letu tunalishughulikia kikamilifu. Niseme tu, kwamba sisi kama Wizara tumejipanga kwa makusudi kubuni na kutekeleza mipango mbalimbali ya kuwatayarisha na kuibua njia mbalimbali za kuwapatia vijana wetu ajira.

Mheshimiwa Spika, tunasisitiza na kuelekeza kwa vitendo kwamba vijana wenyewe ni muhimu wawe ni washiriki wakuu kwa maana ya kuwatayarisha, kujiajiri na lakini vilevile kujitayarisha na kuweza kuwajibika. Sasa tumejipanga vipi, kwa kutumia nafasi tuliyonayo ndani ya Serikali. Tunahakikisha kila Wizara inafanya jitihada za makusudi za kutoa kipaumbele kwa vijana pale panapotokea fursa za ajira na hasa katika mipango ya Wizara mbalimbali. Lakini pia tunaendelea kubuni mbinu mbalimbali zinazopelekea kuhakikisha kujenga mazingira ya upatikanaji wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, katika hili Wizara yangu imeanza kwa kushirikiana kwa karibu na TAMISEMI na nataka niseme hapa mbele yenu Waheshimiwa Wabunge kwamba huu ni mkakati wa makusudi wala sio ule ambao wengi wamesimama hapa wanasema mmepanga mikakati na mikakati imekuwa mikakati. Huu ni mkakati thabiti na mtaona matokeo yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kujipanga kutekeleza majukumu yake vizuri tunaendelea kuhimiza Mikoa, Wilaya na Halmashauri za Wilaya nchini kuajiri Maafisa Vijana, Michezo, Utamaduni na Maafisa Habari ili wawe chachu ya kusaidia maendeleo ya vijana kupitia fursa za utamaduni, michezo na nyingine nyingi zilizoko katika maeneo ya ndani ya jamii zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa sekta ya Wizara yangu ni sekta mtambuka kama nilivyosema tangu mwanzo na sekta zote ni kisima cha ajira, ndiyo maana tunaendelea kujipanga vizuri tukishirikiana na Wizara mbalimbali na wadau wengine kuibua na kutumia fursa hizi mbalimbali kwa lengo la kukabiliana na changamoto la ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia sekta zetu za utamaduni, michezo na habari tunasimamia kujenga mtazamo chanya na sahihi kwa vijana wetu katika masuala ya utamaduni na hili nitalizungumzia kama mojawapo ya hoja ambazo zimejitokeza, lakini pia michezo na habari ikiwa ni pamoja na kuzitumia kama nafasi za kuwatayarisha vijana na kuibua ajira mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tunapoangalia vijana kama rasilimali mojawapo katika mlengo wa kutaka kupata ajira tunazungumzia vijana chini ya sekta yangu kwa maana ya kuwa na rasilimaliwatu, vijana ambao waliotulia, vijana wazalendo wenye kupenda kazi na wenye kuweza kuajirika na kujiajiri. Hili ni lengo kubwa kabisa ambalo Wizara yangu kwa kupitia sekta ya vijana, habari pamoja na utamaduni tunajikita kuhakikisha kwamba tunawatayarisha vijana.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Wizara yangu inashughulikia na kuhimiza Mikoa na Wilaya kuwashirikisha vijana katika shughuli mbalimbali kama nilivyosema kwa lengo la kuwawezesha vijana wenyewe kuwajibika katika kubuni, kuthubutu na kujihusisha katika masuala mbalimbali ya kujiletea maendeleo ikiwa ni pamoja na kujitolea kwa njia mbalimbali. Pia tunaangalia hata kwa vijana ambao ni wasomi na pia wale ambao wasiokuwa wasomi. Vijana waliopo tayari tunawafikia na mipango ya kuendelea kuwafikia wengine ipo kupitia vituo vyetu kama tulivyozungumza katika hotuba yetu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeona hata wachangiaji hapa wameweza kuzungumza kazi nzuri inayofanywa katika ngazi za Wilaya na katika ngazi za Halmashauri mbalimbali. Mfano mzuri umetolewa hapa kuhusu Mheshimiwa Mwantumu Mahiza pale Mkoa wa Pwani. Iko pia mifano mbalimbali ya mwitikio wa vijana katika kujikita katika mikakati mbalimbali ya utekelezaji wa kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni moja kwa moja (*direct)* mwitikio wa mipangilio mbalimbali ambayo inasimamiwa na Wizara. Vijana wako Arusha, Mwanza na hasa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani, naweza kutoa hiyo mifano bila hata kusita. Mifano hii inaonesha kuwa wote tukijipanga kwa dhati kabisa kuwasaidia vijana kuwashirikisha wenyewe maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla yanaweza kupatikana kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kimsingi kupitia muundo wetu wa Maafisa Vijana, Utamaduni, Michezo, Habari wapo Mikoani, Wilayani na TAMISEMI kwa ujumla tumeweza kushirikiana na kufuatilia utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa vijana na wananchi mbalimbali. Popote pale walipo napenda tu nichukue nafasi hii niseme kwamba, kazi kama kazi zipo zinatuzunguka kila mahali. Kama kero zinatuzunguka kila mahali, ile peke yake ni fursa ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachojipanga kama Wizara ni kuhakikisha tunajitahidi kila namna ya kubadilisha mtazamo wa vijana wetu na wananchi kwa ujumla. Kwamba tunapoziangalia kero tuziangalie kama fursa za kazi, lakini tunapoangalia vijana kama nguvukazi ambayo iko tayari, nguvukazi nyingine ambayo ni wasomi, nguvukazi ambayo tunasema imekaa bila ya kuajiriwka au bila ya kuajiriwa, basi tujitahidi kwa namna yoyote ile tujipange kuhakikisha kwamba tunawapa vijana nafasi, lakini pia tunawatengeneza vijana wenye kutambua wajibu wao kwamba wana jukumu kubwa kabisa la kujitafutia maendeleo wakiwa wanasaidiwa na Serikali kama tulivyosema.

Mheshimiwa Spika, kikubwa kabisa ambacho napenda nimalize suala la ajira la vijana ni kwamba, kimsingi ajira nyingi zinatokana na sekta binafsi. Kwa hiyo basi, kupitia Wizara yangu pamoja na maelekezo mengine mengi ambayo tunayazungumzia ni kuhakikisha kwamba tunawapanga vijana wawe na mtazamo chanya kwa masuala ya sekta binafsi. Watambue kabisa kwamba tunahitajika kuwa na mahusiano mazuri na wawekezaji na ni muhimu kuangalia aina ya uwezekaji pamoja na kuwatayarisha na wao kama wao kuwa rasilimaliwatu wa kuweza kuwekeza katika hao wawekezaji watakapokuja, lakini pia kuchangia kwa hali na mali katika suala zima la sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika hili Wizara yangu kupitia vituo mbalimbali vya vijana tunazo programu mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya vijana, tunatoa mafunzo mbalimbali ya stadi za maisha na kazi zikiwemo mafunzo ya ujasiriamali ambayo yanawapa nafasi vijana kuajirika na kuweza kujiajiri wenyewe. Nilifurahi hapa kuna Mbunge mmoja aliweza kutamka na kutaja fursa mbalimbali za kuwatayarisha vijana kuweza kuajirika na ambavyo imeweza kuwafikia vijana mbalimbali katika Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii niseme kwamba nafasi ya kuwatayarisha vijana kuweza kuajirika ni nafasi ambayo Wizara yangu inaifanyia kazi kwa bidii. Lakini pia inaona ni suala ambalo ni muhimu, ni suala ambalo lilichangiwa na zaidi ya Wabunge 45 wakigusia kwa dhati kabisa kuhusu suala la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda niongezee hapa kama nilivyosema kwamba, Wizara yangu inashirikiana na Wizara nyingine. Fursa za kazi zipo katika mipango mbalimbali ya Wizara tofautitofauti ukianza na Wizara ya Viwanda na Biashara, nafasi kubwa za kazi kwa vijana kwa ngazi mbalimbali. Ukifuatilia karibu mipango ya uzalishaji ambayo tunazungumzia sasa hivi umuhimu wa kuweza kuanzisha viwanda mbalimbali, Wizara yangu inasimamia kwa karibu kuhakikisha kwamba Wizara ya Viwanda inabeba vijana mbalimbali katika masuala yao ya kuanzisha viwanda.

Mheshimiwa Spika, lakini vile viwanda ambavyo tunataka tulenge ni katika masuala ya mazao yaani viwanda vidogo vidogo vinavyotokana na mazao pamoja na ufugaji, basi tuwe

tayari tumekwishawatayarisha kwanza vijana wenye kupenda masuala ya kulima ili kusudi wawe tayari wenye ku-*benefit* moja kwa moja katika mpangilio huu.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara yangu msukumo wake katika Wizara hii ni kuhakikisha kwamba vijana tulionao wanachukua jukumu halisi kabisa la kuhakikisha kwamba wanasimama imara katika suala la uhakika wa chakula. Kijana ambaye si mgonjwa, ana nguvu zote, ambaye amesoma ana zaidi ya miaka 18, mashamba mengi yapo.

Mheshimiwa Spika, tukaona sisi tumejitahidi kabisa kupitia vituo vyetu vya vijana, kwamba vijana wale ambao wako tayari ambao hata pamoja na kuhakikisha kwamba tunawahimiza waingie katika masuala ya kilimo, wale ambao wako tayari tutasimama nao imara kuhakikisha kwamba uhakika wa chakula kwanza wa kuanzia na wao vijana nao na iwe kama ndio kaulimbiu ya kijana. Kijana ambaye halimi, hafanyi kazi kwa sababu fursa nyingi zinamzunguka basi atambue pia na tatizo la chakula linaweza kuja kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo na Uvuvi pia ni sehemu nyingine ambayo tunafanya kazi nayo kwa karibu kuhakikisha kwamba masuala ya ufugaji na hivi vyote ninavyovitaja ni vitu ambavyo vimekwishaanza kufanya kazi katika Wilaya mbalimbali vikishirikiana na Wizara yangu, lakini kwa msukumo wa kupitia chini ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ya Uchukuzi tunahimiza kabisa masuala ya kuhakikisha usafiri wa ndege, meli na treni upo, lakini suala la ndege kwa sababu lile litafungua na fursa mbalimbali ambazo tunawahimiza vijana kuingia katika fursa mbalimbali za kuweza kuanzisha vibiashara tofauti tofauti ambavyo kwa kiasi kikubwa vitahitaji masuala ya uchukuzi ambayo ni ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, masuala ya utalii na maliasili, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara zote kwa kiasi kikubwa napenda nichukue nafasi hii niseme kabisa kwamba, ni Wizara ambazo tunashirikiana, lakini tukitambua kabisa kuna umuhimu wa kupanga mipangilio yao huku wakihakikisha kwamba wanagusa vijana katika suala la ajira.

Mheshimiwa Spika, nilizungumzia Wizara yangu na sekta mbalimbali kwamba ni kisima cha ajira kama tukijipanga vizuri. Tumekuwa muda wote tunazungumzia sekta ya habari kama vile ni suala ambalo linagusa tu uandishi wa habari. Sekta ya habari ina vitu vingi, unaweza ukashughulikia masuala mengi katika maeneo yanayohusiana na sekta ya habari.

Mheshimiwa Spika, upangaji wa habari kwa maana (*organization of information)*, kusimamia au kushughulikia uendeshaji wa teknolojia za habari, (*handling of information technology*) zote hizi ni fursa mbalimbali za ajira. Rasilimali asinifu kwa habari kwa maana (*information resources)*, vyanzo vya habari huduma (*information resources* na *services),* mifumo ya habari (*information system)* na uandishi wa habari.

Mheshimiwa Spika, vyote hivi ni fursa mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa vijana wengi ambao ni wasomi unaweza ukawakuta wamemaliza shahada zao za kwanza wanaweza kwenda za pili wakazamia katika hizi nafasi zingine ambazo kwa kiasi kikubwa zinahitaji ustadi mkubwa wa *profession.* Katika masuala ya sanaa kuna fursa mbalimbali za kazi katika masuala ya filamu, muziki, ngoma, masuala ya kuchora, zote hizi ni fursa mbalimbali na katika hili walichangia zaidi ya wachangiaji 45.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia kwa haraka haraka na kwa jumla jumla ni kuhusu kuporomoka kwa maadili ya wananchi na mahusisho zaidi kuhusu vyombo vyetu vya habari. Hili limechangiwa na wachangiaji wengi zaidi ya kumi. Kwa kiasi tunapozungumza utamaduni wa maadili yetu kwa Watanzania tunafahamu kuwa Mtanzania ni mtu mwenye upendo, ushirikiano, mwenye kutii sheria, mwenye kupenda amani, uvumilivu, kujitolea, kujitegemea, mwenye umoja ambaye yuko tayari kujinyima ili wengine wapate. Hili lilifanyika wakati wa kupigania uhuru na hili tunalifahamu.

Mheshimiwa Spika, anayepewa nafasi halafu akikimbilia kujikimu, halafu akakimbia mwenyewe, mara nyingi inakuwa si rahisi kuweza kutambulika kama Mtanzania halisi. Ndiyo maana mpaka sasa hivi, leo mabibi na wengi tunakaa majumbani mwetu na mashangazi na wajomba zetu na nini. Yote hii inaonesha kabisa maadili tuliyonayo ni mazuri kwa muda mrefu. Lakini sasa kuporomoka kwa maadili kunaonekana katika viashiria mbalimbali na si kwa vijana tu katika jamii nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ndani ya jamii yetu humu Bungeni Spika anaweza akazungumza mara tatu, tatu, mtu anaambiwa kaa lakini bado anaambiwa lile lile na viongozi vijana ambao ni *role model*, unaonekana waziwazi, wakati mwingine unakaa unajiuliza hivi vijana wa kule nje wanatuonaje. Nataka niliseme wazi bila kusita kabisa ndani ya jamii kulalamika, matusi, kejeli kwa viongozi, chuki, uchochezi, kukosa uvumilivu baina ya kundi moja kwa lingine, madai juu ya madai mbalimbali, utegemezi, kutopenda kujitolea, kutosaidia, ubinafsi, kutotii Sheria za mamlaka mbalimbali na uvunjifu wa amani. Haya sasa hivi naona yanaanza kubebwa kama vile ndiyo maadili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nichukue nafasi hii kama nilivyopewa nafasi ya kusimamia vijana na hili nataka niliseme kwa jamii nzima. Huu sio utamaduni wetu.

**SPIKA**: Nasema mtu asiyehusika ndiye anasema Waziri si anyamaze tu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nataka niseme yote niliyoyataja hapo ni viashiria vya kuporomoka kwa maadili. Matamshi ya kujenga yamekuwa adimu siku hadi siku, tunayasoma katika magazeti, tunayaona katika televisheni, tunayasikia wakati mwingine kutoka kwa viongozi na wakati mwingine yanaumiza hasa ukiona yanatoka kwenye viongozi wengine ambao ni vijana ambao tunawategemea, lakini hata kwa viongozi wengine ambao ni *role models* wa kueleweka na kuweza kuheshimika.

Mheshimiwa Spika, hii ni kazi yetu sote tushirikiane kukemea na kulifanyia kazi hili. Tuache kushabikia kama vile Serikali ndiye yenye wajibu au kuhusika peke yake katika kutatua kero mbalimbali na wengine kubakia au kutazama au kuchochea. Maadili yapo chini ya sekta ya utamaduni, hivyo Wizarani yangu inaendelea kwa hali na mali kufikia jamii kupitia vyombo vya habari na madhehebu ya dini kuhimiza maadili mema wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii kwa wale ambao wamechangia kwa uchungu kabisa kuhusu maadili kuporomoka kwamba Wizara iko pamoja nao na tunajitahidi kwa hali na mali kuhakikisha maadili yale ya upendo, ushirikiano ya kuweza kutofautiana bila kutoana macho na kadhalika tunayarudisha kwa hali na mali kwa sababu kimsingi Taifa lenye kukaa kila dakika ukigeuka ni maadili ya ovyo ovyo si Taifa ambalo ni *health*. Taifa ambalo ni *health* ni Taifa tulilokuwa nalo kama zamani. Kwa hiyo, nataka nichukue fursa hii Wizara yangu katika kudhibiti suala la maadili katika mambo mbalimbali pamoja na filamu tumekemea hivyo vitu na tunazo sekretarieti mbalimbali za kuweza kusimamia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande wa vijana na kwa upande wa jamii kwa ujumla tunataka kuhimiza hilo na Wizara yangu inafanya kazi kwa karibu na viongozi wa dini pamoja na viongozi mashuhuri kwenye jamii kuhakikisha kwamba tunarudi kwenye mstari mzuri wa kuheshimiana. Vijana tuheshimu wazee pamoja na viongozi na tutambue kabisa unapokuwa kiongozi *whether* ni kijana au mtu mzima uongozi ni dhamana na kuna namna fulani ambayo unategemea ku-*behave* kama kiongozi.

Mheshimiwa Spika, suala la usikivu wa *Radio* ya *TBC* ni suala lingine ambalo limezungumziwa na limejitokeza kwa kiasi kikubwa na wachangiaji wengi. Kimsingi *TBC* inasikika nchi nzima, hata hivyo, kutokana na uchakavu wa mitambo na Wabunge wengi wamelizungumzia kwa kiasi kikubwa, kukatikakatika mara kwa umeme na ufinyu wa bajeti baadhi ya sehemu za nchi zimekuwa hazipati matangazo hayo.

Mheshimiwa Spika, hili nataka nichukue nafasi hii, nikiri kwamba hili ni kweli na sehemu chache ambazo *TBC* haisikiki na haiwezi kuonekana na wakati mwingine unaona kabisa

tunahangaika. Tatizo la usikivu wa matangazo, nataka niseme lilitokea baada ya mtambo mkubwa wa Kunduchi kuharibika, baada ya kupokea umeme mwingi kuliko kawaida na kuweza kuunguza baadhi ya vifaa vyake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mpaka sasa bado tunaendelea kurekebisha sehemu mbalimbali za kuhakikisha ule mtambo unarudi katika hali yake thabiti, kazi hii inafanywa na Wizara ikishirikiana na *TBC*. Nataka nichukue nafasi hii niwashukuru Ubalozi wa Japan ambao wamekubali kutupatia vipuri hivyo ili mtambo huo uweze kufanya kazi na mafundi wa *TBC* wapo wanajitahidi kila siku waweze kuturushia matangazo yetu kama mnavyoona. Hata matangazo haya ya Bunge yanarushwa kila mahali.

Mheshimiwa Spika, ziko sehemu chache ambazo kwa kusema kweli hayasikiki na kwa wakati mwingine hayaonekani na nataka nichukue nafasi hii niseme kwamba, bado tunajitahidi. Aidha, ili kuhakikisha matangazo ya *TBC* yanamfikia kila Mtanzania popote alipo nchini Serikali inaendelea na mpango wake wa kufunga mitambo ya Radio ya *FM* katika Miji Mikuu ya Mikoa yote nchini kadri fedha zinavyopatikana na baada ya hapo katika miji yote ya Wilaya.

Hadi sasa *TBC* imefunga mitambo ya *FM* katika Mikoa 24 kwa upande wa *Television TBC* tayari imefunga mitambo yake katika Mikoa 12 na katika mfumo wa digitali, matangazo ya *television* yanaonekana katika Mikoa saba ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza na Tanga na hivi karibuni Mkoa wa Morogoro nao utaongezeka.

Mheshimiwa Spika, matangazo haya ya *television* yanarushwa pia kupitia *satellite* ambao Watanzania wengi wenye ungo kwa maana ya *dish* na *satellite* wanaweza kuyapata popote pale walipo hapa nchini kupitia njia ya *satellite* na king'amuzi cha *DSTV Channel* 143.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda nilizungumzie harakaharaka na kwa ujumla ni baadhi ya uandishi usiofuata ueledi na uliojaa uchochezi, uzushi na chuki. Katika nchi yetu tasnia ya habari imekuwa tangu mwaka 1992 na nataka nilizungumzie hili kama suala ambalo linatugusa. Kwa sababu magazeti yanapoandika vitu vingine ambavyo havina mwelekeo moja kwa moja unakuwa umemgusa mwananchi, halafu inakuwa ni shida kuanza kuhangaika kujaribu kunyamazisha au kujaribu kufuatilia vitu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kama nilivyozungumza ndiyo ukiukwaji wenyewe wa maadili unauona moja kwa moja katika vitu ambavyo vinawafikia wananchi. Tumeshuhudia ongezeko kwa vyombo vya habari nchini hasa baada ya Serikali kuruhusu Sekta binafsi kuanzisha magazeti ya kila siku, vituo vya *Radio* na Televisheni. Mathalani ongezeko la magazeti yanayotoka kila siku kama nilivyozunguza katika hotuba yangu ni mawili na kumi na tano kwa siku.

Lakini pia tuna vituo vya Radio 86 na uanzishwaji wa Vituo vya televisheni ambavyo vimefikia zaidi ya 26. Ongezeko hilo la vyombo vya habari halikwenda sanjali na ongezeko la watumishi wenye weledi katika taaluma ya habari. Kwa hiyo, kukawa na ombwe kubwa la watumishi wenye weledi katika vyombo hivyo hali iliyosababisha kuandikwa na kutangaza habari zisizozingatia maadili ya taaluma zikiwemo za uchochezi, uhasama, uzushi, udini, ukabila na hivyo kuhatarisha hata amani ya nchi na mshikamano wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kuwepo kwa tatizo hili na imechukua hatua mbalimbali. Kwanza tumekuwa tunahakikisha tunawaita wahariri na kuwaelimisha juu ya wajibu wao kwa Taifa na wale wanaokaidi kuandikiwa barua za onyo na endapo hawajajirekebisha hatua ya kufungiwa kwa muda na ikishindikana kufutwa katika daftari la usajili.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kuwashauri walioathirika na habari hizi mbovu, habari potofu kuchukua hatua za kimahakama, lakini pia kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa habari kutoa elimu kwa waandishi wa habari na watangazaji wa habari pamoja na wamiliki wa vyombo vya habari ili waelewe vizuri wajibu wao kwa jamii na Taifa.

Mheshimiwa Spika, tunalotaka ni kuhakikisha kwamba, tunajenga Taifa lenye muonekano mzuri, kuhakikisha kwamba Watanzania wanatambua kwamba hii Tanzania ni yao na hakuna mtu

mwingine atakayeijenga na hakuna Tanzania itakayojengwa kwa kuwa kila siku unaikejeli na kutoa matusi wakati ukiwa hata huna sababu maalum ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika hili nashukuru kwamba tunalo Baraza la Habari la Tanzania *(MCT)*, vyuo vikuu tunashirikiana navyo vinavyofundisha mambo ya habari na Baraza la Vyuo Vikuu *(TCU)* na Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* katika kuandaa mitaala ya taaluma ya uandishi wa habari na ustadi wa habari.

Mheshimiwa Spika, aidha Wizara yangu inawaomba wamiliki wa vyombo vya habari binafsi kuhakikisha kwamba wanaajiri watu wenye ustadi na ueledi wa habari na kuwalipa stahiki zao kamilifu. Tunaambiwa kwamba, kuna ambao wapo tayari kupokea ndogondogo mradi akuchafue. Sasa tunasema kama unalipwa vizuri una haja gani ya kukaa na kwenda kuchafua mtu kwa kupata ndogondogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nihimize kabisa wenye vyombo vya habari binafsi pamoja na vile vya umma kuhakikisha kwamba wale tunaowaajiri ni wana ustadi na weledi wa habari, lakini pia wanalipwa mafao yao vizuri ili waweze kuweka na ku-*enjoy* na kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimeshukuru kuna Mheshimiwa mmoja hapa amelizungumzia vizuri sana kwa maneno, lakini katika maandishi imejitokeza sana mpaka inaogopesha. Pia nataka niseme kwamba, kama vyombo vingine vitoe pia kipaumbele katika kugharamia mafunzo ya watumishi wao.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kuwataka waandishi na watangazaji wa habari kuhakikisha kuwa habari wanazoandika na vipindi wanavyoandaa vinazingatia taaluma pamoja na kuweka mbele maslahi ya Taifa letu na uzalendo, uhuru na haki inayosimamia viendane na wajibu wa kupata habari, lakini pia kutoa hiyo habari.

Mheshimiwa Spika, kimsingi tunajipanga na kuendelea kuboresha misingi ya kufanya kazi ikiwa ni pamoja na kutayarisha Sheria ya Habari na Kanuni mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tunamlinda huyu mwananchi pamoja na mtoa habari zinazohusu uchochezi, chuki, uzushi na habari zisizojali tija kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia hapa kwa uchungu kabisa kwamba ni muhimu kabisa mtu atakayesimama wanasema ni *self appointed spokes person* wa wananchi basi uwe ukweli unazungumzia wananchi na wamekutuma kweli. Isije ikawa ni wewe una nafasi ya kuweza kufikia magazeti na vyombo vya habari, basi unapewa nafasi ya kuendelea kuchafuachafua na ukategemea tutaacha tu kimyakimya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali tuko tayari kulifanyia hilo kazi kwa karibu kabisa kwa sababu tunakokwenda huko masuala ya habari ni masuala muhimu na tumeona kabisa nchi zinachafuka kutokana na habari za uchafuzi ambazo zinaweza zikaleta vurugu. Nichukue nafasi hii niombe hata viongozi wenye tabia za kutumia nafasi zao kupitia vyombo vya habari na waandishi wa habari kutoa matamshi yasiyo na busara yenye kueneza hofu, chuki na uwezekano wa kuleta migongano na hofu kwa wananchi na vyombo vya dola basi waache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nichukue nafasi hii nizungumzie suala la urasimishwaji wa muziki, hili limeshazungumziwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka nizungumzie masuala ambayo sikuyagusia. Suala la maboresho ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Hili limezungumzwa na watu saba na napenda niseme kwamba, ni kweli fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana zinazotolewa hazitoshi kulingana na mahitaji halisi ya idadi ya vijana waliopo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali inajitahidi kuongeza pesa katika Mfuko huo kulingana na bajeti inayotengwa kila mwaka. Vile vile Wizara inaendelea kuhimiza Halmashauri za Wilaya kuhakikisha kwamba zinatenga asilimia kumi ya mapato yake kwa ajili ya kuendeleza

vijana kwa maana tano kwa vijana na tano kwa wanawake kwa ajili ya kuendeleza vijana na wanawake katika Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa inahusu Baraza la Vijana. Waheshimiwa Wabunge nane walizungumzia suala hili na napenda niseme kwamba ushauri wao umepokelewa, mapendekezo ya kutunga Sheria ya uandaaji wa Baraza la Vijana la Taifa umekamilika na kuwasilishwa ngazi ya ushauri na hatimaye uamuzi. Pindi mchakato huu utakapokamilika Baraza litaundwa kwa mujibu wa Sheria itakayotungwa.

Mheshimiwa Spika, lingine walizungumzia kuhusu vijana watambuliwe na huyu ni Mheshimiwa Vicent Nyerere wa Musoma. Huyu nimemtaja kwa sababu yupo peke yake. Niseme kwamba, Wizara kuwatambua vijana sasa hivi, kweli hili ni jambo la msingi na nataka niseme kwamba, mpaka sasa hivi tunaendelea na mchakato tuliokuwa tumekwishaanza, tunaendelea kuwatambua kidogokidogo kwa maana ya ku-*update* taarifa mbalimbali zinazohusu vijana kwa kuboresha *kanzidata* iliyopo kwa maana ya *Youth Database* kupitia kwenye dodosa ambalo kwanza limesambazwa kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini pamoja na viongozi mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge msilione hilo dodoso mmeletewa kutupatia taarifa mkadhani ndiyo tunaanza, hii ni kazi tu, tunataka kuhakikisha kwamba na ninyi hapo mlipo je mnatambua vijana wenu kule walipo na makundi yao mbalimbali? Sisi Kiwizara tuko tayari na tumekuwa tunafanya hilo, tunachotaka ni kuhakikisha tunawakutanisha karibu na vijana wenu ambao mnajua kuwatetea vizuri.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni baadhi ya shule za sekondari zibadilishwe kuwa vituo vya *VETA* ili kutoa elimu ya ujasiliamali. Hili limezungumzwa na wachangiaji wanne. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kila Wilaya inakuwa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi kwa lengo la kuwasaidia vijana ambao hawakupata nafasi ya kuendelea na elimu ya juu wapate mafunzo ya ujasiriamali yatakayowasaidia kujiajiri wenyewe. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuwahimiza vijana kujiunga na vyuo vilivyopo na vitakavyoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili la kuhusu uzalendo na kuhusu maadili kwa vijana. Hili nadhani nimekwisha kulizungumzia, Maafisa Vijana kupelekwa Wilayani, hili nimelizungumzia katika suala la ajira. *Combination* iliyopo na mkakati ambao tumeupanga kuhakikisha kwamba tunafanya kazi maafisa TAMISEMI, lakini kuhakikisha kwamba tuna Afisa Vijana, Maafisa Michezo na Maafisa Utamaduni lakini vile vile na Maafisa Habari. Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Aziza Hilal, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Serikali ianzishe Benki ya Vijana kama ilivyo Benki ya Wanawake na hii imezungumzwa na wachangiaji kama wanne. Nakubaliana na ushauri uliotolewa hata Wizara imeshaanza mchakato wa kuandaa Benki ya Taifa ya Vijana kwa lengo la kuwa na chombo cha fedha ambacho kitatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana. Kwa mwaka huu wa fedha Wizara itatafuta mshauri mwelekezi ili aweze kuwashauri vijana namna nzuri ya kuanzisha na kuendesha Benki hii.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba, hili tayari limekwishaanza na katika nafasi ya kuhangaika tumekwishaeleza kwamba kama tunataka kuanzisha Benki ambayo itakuwa *run commercially* tunahitaji si chini ya bilioni 16. Kwa hiyo, tayari tumeshaanza huo mchakato wa kuanza kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii Wabunge wote tulioko hapa tutakapowafuata kuomba kutuelekeza namna nzuri ya kuweza kuanzisha hii Benki mtusaidie kutuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifungue vituo Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya Tanga vya vijana. Nataka niseme kwamba vituo vimefunguliwa. Tunavyo vile vitatu, lakini pia tuna vituo vya michezo na tutaendelea kuvifungua kadri tunavyoweza.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema tunafanya kazi kwa kushirikiana na Wizara nyingine tumesikia hapa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wana vile vituo mbalimbali ambavyo vinaweza vikatoa mafunzo huko. Kwa hiyo na sisi tunategemea tunaendeleza vile vituo vyetu na vile vituo ambavyo tayari Wizara ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Wizara zingine tutashirikiana navyo kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme hapa Dodoma, Mwanza, Mbeya, Tanga, maombi yaliyoombwa na watu kama wanne tutafanya kazi kwa karibu kuhakikisha kwamba vijana walioko katika sehemu hizo wanafaidika na hivyo vituo vingine kwa kupitia Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, je, michango ya mbio za mwenge wa uhuru ni hiari au lazima. Hili nilivyokuwa najibu hoja ya Kambi ya Upinzani shughuli za mwenge kugharamiwa na Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA**: Kengele ya pili Mheshimiwa.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Kama mnavyofahamu nyongeza ya muda wa Spika haipo. Katibu!

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 96-WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO**

Kif. 1001 - *Admin. and HR. Management*... ... ... Sh. 2,744,555,500/=

**MWENYEKITI:** Simameni tu kwa kujipendezesha, mpo wengi lakini *time* haitoshi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Katika mchango wangu nilimwomba Waziri kwamba Sera ya uwekezaji haimtambui sana msanii na kazi zake hasa katika kupata mikopo, naomba Waziri atusaidie kwa sababu kazi zetu zinapokuwa zimekwama hata *studio* msanii anakosa dhamana yoyote ya kwenda kuchukua fedha labda benki ili kutoa kazi yake na kuweza kuiuza ili aweze kurudisha. Naomba Waziri atusaidie.

**MWENYEKITI:** Mtasaidia mkiwa *brief* na wote mnaouliza muwe *brief* na Waziri awe *brief*. Waziri majibu!

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mlata kuhusu uwezekano wa Serikali kuwasaidia Wasanii wasiokuwa na kipato. Tumezungumzia hapa suala hili la urasimishaji kazi za wasanii. Lakini pia wakati tunahangaika na suala hilo, Wasanii wapo katika mashirikisho katika masuala yao kujiunga katika shirikisho, huko ndiko wanakotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya masuala wanayoyazungumza wajiunge katika *SACCOS* na wakijiunga katika *SACCOS* zao za kisanii mbalimbali wanaweza wakafaidika katika Mfuko wa Vijana ambao tunauzungumzia. Wasanii kama kikundi wakiwa chini ya *SACCOS* wanaweza kufaidia chini ya hilo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia suala liliripotiwa jana katika gazeti la *The Citizen,* kuhusiana na namna ambavyo Makampuni ya Simu yanavyowanyonya wasanii katika *ring tones*, ambapo Makampuni ya Simu katika jumla ya mapato ya *ringtones* yanapata asilimia sabini na tano mpaka themanini na msanii anapata asilimia saba tu ya fedha ambazo zinakusanywa katika *ringtones*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atoe kauli ni namna gani ambavyo tunahakikisha kwamba kijana ambaye anahangaika kwenda studio, anarekodi wimbo, anaimba, wimbo ule unauzwa kwenye Kampuni za Simu, lakini anapata asilimia saba tu ya mapato na Kampuni ya Simu inapata asilimia themanini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali kuhusu jambo hili.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hilo alilolizungumzia Mheshimiwa Zitto hata mimi nimeliona katika gazeti, lakini ni suala ambalo tumeshapata habari zake na tunalishughulikia, lipo katika mikono ya *TCRA* sasa hivi. Kwanza kuweza kuangalia hizo kampuni ambazo zimepelekea mpaka msanii anapata hiyo *percent* ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nirudie kusema kwamba, kwa kupitia huu urasimishaji wa kazi za Wasanii na kupitia mashirikisho yao haya yote yanaweza yakatatuliwa. Lakini pia kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na kupitia *TCRA* tutaanza kulishughulikia hilo kwa karibu ili kuhakikisha kwamba nchi yetu haipotezi mapato pamoja na wasanii pia hawanyimwi haki zao.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia mapato kwa Halmashauri ya Temeke kutokana na Uwanja wa Taifa. Katika majibu ya Waziri anasema Chama cha Mpira, Mkoa wa Dar es Salaam kinapata asilimia mbili ya mapato hayo, lakini sisi tunazungumzia Halmashauri ya Temeke.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza wakati natoa majumuisho ni kwamba, mapato yale asilimia kumi huenda Serikalini na *TFF* hufanya kazi na wadau wakiwepo Vyama vya Michezo vya Mikoa. Kwa maana hiyo, asilimia mbili wanapata Chama cha Mpira wa Miguu, Mkoa wa Dar es Salaam. Huo ndiyo utaratibu uliopo sasa, lakini kama ni ushauri tunaweza tukaufanyia kazi kama Wizara.

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikumbusha hoja ya mwaka jana ya kusimamishwa kwa Katibu Mkuu wa CHANETA kwa sababu au kwa tuhuma za kushirikiana na Chama cha Netiboli cha Zanzibar, jambo ambalo sisi wengine tunaona kwamba kwa kufanya hivyo alikuwa anaimarisha Muungano na kupunguza kero za Muungano. Sasa ni takribani miaka mitatu kiongozi huyo amesimamishwa uongozi kwa tuhuma hiyo, lakini hakuna *effort* yeyote inayofanyika kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua Wizara na Baraza la Michezo wamefikia wapi katika kulishughulikia suala hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa kifupi maana yake hatuwezi kuendesha kesi hapa.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ufafanuzi wa suala la Katibu Mkuu wa CHANETA lililotolewa na Mheshimiwa Missanga ni kwamba, Wizara yetu ilipokea suala hili na inaendelea kulishughulikia na wamefikia katika hatua nzuri, tutatoa taarifa. Lakini mazungumzo yanaendelea kuona kwamba, jambo hili linaisha, hata Kamati imetoa maelekezo ya kushughukia suala hili.

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi, niliuliza kuhusu Jimbo la Igalula lilikuwa na Mfutakamba Igalula *Super League Cup*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mfutakamba tusaidie, zungumzia jambo la sera, ukisema Igalula Mfutakamba *Cup* mbona hatuwezi. (*Kicheko*)

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema sera ya michezo. Kwa hiyo, katika sera ya michezo hawa vijana wapo katika vikundi lakini pia vipaji ni karibu vijana 30 wanaweza kwenda kwenye hizi timu (B), je, Wizara inaweza kutusaidia vipi ili waweze kwenda kwenye majaribio katika klabu za Yanga *Sports Club*, Simba *Sports Club* na maeneo mengine kwa sababu vipaji vyao vinahitaji kuendelezwa.

**MWENYEKITI:** Wakati wa mshahara wa Waziri hatuzungumzii vitu vya mtu, hajui Waziri.

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nataka kufahamu kuhusiana na ushiriki wa vyombo vya habari hususan katika maeneo ya vijijini. Kwa takribani sasa miaka hamsini, vyombo vya habari vimekuwa vikiripoti zaidi taarifa za mijini karibu kwa asilimia 90 na maeneo ya vijijini taarifa hizo zimekuwa hazifiki kwa sababu kumekuwa na changamoto mbalimbali. Nataka kufahamu mkakati wa Wizara wa namna gani wamejipanga kuhakikisha taarifa zinawafikia wananchi wa vijijini katika mwaka huu wa fedha.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada inazofanya Wizara yetu ni pamoja na kuona kwamba *TBC* inaweza kuwa na mtandao mkubwa na kufika mpaka maeneo ya vijijini na ninyi ni mashahidi, Wabunge wengi wamechangia kuhusu *TBC* kuwa na usikivu mpaka maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni haki yao wananchi wote kupata habari. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, Wizara imepokea na tutaendelea kushughulikia na kuwahamasisha Waandishi wa Habari kuwapatia habari wananchi wa maeneo yote bila kubagua mjini na vijijini.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilipenda kujua ukubwa wa tatizo la ajira kwa vijana. Kwa sababu tuna miaka hamsini tangu tupate uhuru, ni aibu mpaka leo kwamba Serikali inaendelea kusema kwamba, kuna watu wameajiriwa Wizara fulani, ningependa *specifically* muwe na takwimu kwenye mkono, ni vijana kiasi gani hawana ajira, wangapi wana ajira kwa sababu hamuwezi ku-*plan* kama hamna takwimu.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi siwezi kuwa na *exactly data* kwamba vijana wangapi wameajiriwa Wizarani na Vijana wangapi hawajaajiriwa. Nimesema sasa hivi tunajitahidi kuhakikisha tunaweka *statistics* zetu sawasawa kwa upande wa Tanzania na itatusaidia zaidi wakati wa sensa inayokuja ili kuweza kujua vijana wako wangapi na kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, *data* zilizopo ni zile za nyuma sana na tunachofanya ni kujazia kidogo kidogo na hatuwezi kusema *percent* ishirini au *percent* sabini. Ahsante.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Bunge lililopita la Aprili tuliridhia Mkataba wa Vijana Afrika, lakini nimekuwa na masikitiko kwamba katika hotuba ya Waziri hajagusia kama Wizara wana mikakati gani ya kuhakikisha tunatekeleza mkataba huo. Kwa uzuri zaidi katika Wizara ambazo zimeshapitisha bajeti yake ikiwemo Ardhi na Kilimo imeoanisha ni jinsi gani ambavyo imeweka mikakati ya kuwasaidia vijana kuhusiana na Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa Wizara hii ndiyo inatakiwa kuwa *coordinator* na *issues* zote za vijana kwenye Wizara nyingine. Sijui Wizara imejipangaje kuhakikisha haya mambo ambayo yameahidiwa kwenye Bunge hili Tukufu la ule mkataba unashughulikiwa ipasavyo.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nazungumzia suala la Mkataba wa Afrika wa Vijana kwamba lengo mojawapo ni kuanzisha Baraza la Vijana, lakini pia ikiwa ni kupanga vitu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vijana wanakingwa katika masuala ya UKIMWI na vitu vingine vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba tayari kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje tumekwishapeleka ujumbe Afrika *(AU)* kuhakikisha kwamba wanatuweka katika *list* kwamba tumeridhia mpaka Bungeni, lakini pia suala la kutayarisha Baraza la Vijana, liko tayari katika ngazi ya juu ambayo ni ngazi mojawapo itakayotusaidia katika lile Baraza la Vijana kuhakikisha kwamba mambo mbalimbali yanayohitajika ndani ya ule mkataba yanatekelezeka.

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa Kanuni ya 104, Kanuni Ndogo ya (2), nalazimika kuingia kwenye *guillotine*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*… … … … … Sh. 251,109,600/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*… … … … … … Sh. 434,534,000/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit*… Sh. 131,006,700/=
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*… … Sh. 288,344,800/=
Kif. 1006 *Internal Audit Unit*… … … … … … … Sh. 188,691,600/=
Kif. 1007 *Information and Comm. Tech. Unit*… … Sh.76,775,100/=
Kif. 1008 *Legal Service Unit*… … … … … … ... Sh.4,164,429,300/=
Kif. 6001 *Culture Development Division*… … … Sh. 3,055,399,000/=
Kif. 6002 *Youth Development Division*… … … Sh. 1,184,379,200/=
Kif. 6004 *Sports Development*… … … … … …Sh. 1,721,838,100/=
Kif. 7003 *Information Services*… … … … … … Sh. 6,084,953,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 96- WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO**

Kif. 1001 - *Administration and HR. Management*… … … … Sh.0/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*… … … … … … … … … … Sh.0/=
Kif. 6001 - *Culture Development Division*… … … Sh.961,600,000/=
Kif. 6002 - *Youth Development Division*… … … ..Sh. 300,000,000/=
Kif. 6004 - *Sports Development*… … … … … …Sh.1,330,000,000/=
Kif. 7003 - *Information Services*… … … … … … Sh. 550,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*
*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo na Taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 mafungu kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yeyote, Hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana,*
*Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2012/2013*
*Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara na kwamba mpaka sasa hivi wana miezi michache tu toka wameteuliwa kushika Wizara hii na mafundisho mliyowapa watayashika vizuri, wengine mliandika vizuri, mwaka mwingine watafanya vizuri zaidi. Naomba niwapongeze pia watalaam wa Wizara hii kwa msaada waliowapa katika kufanya kazi yenu nzuri. Tunawatakia kheri.

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo moja tu linatoka ofisini kwangu ambalo linasema onesho la kuzima moto. Linasema niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Kampuni ya Ikweta SUMA *JKT Company Limited*, inategemea kuanza kuunganisha magari ya kuzima moto aina ya *ZEAL* na *URA* katika kiwanda cha Ruvu JKT Mlandizi, kampuni imeagiza gari moja la aina hiyo kwa ajili ya kufanya mafunzo na mazoezi ya jinsi ya kutumia teknolojia hiyo.

Hivyo basi, Wabunge wote mnakaribishwa kwenye onesho la kuzima moto kwa kutumia gari aina ya *ZEAL***,** kesho tarehe 25 Jumatano saa saba na nusu mchana katika kiwanja cha shule ya Sekondari ya Dodoma. Lengo kubwa ni kuwawezesha Wabunge kuona magari hayo ya zimamoto ili waweze kuweka *order* kwa ajili ya Halmashauri zao. Magari hayo yatasaidia kuokoa majanga ya moto katika Taifa letu. Kwa hiyo, kesho saa saba na nusu mnakaribishwa kwenye maonesho.

Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa…

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanaongea*
*badala ya kumsikiliza Spika)*

Waheshimiwa Wabunge, mbona mnaongea sasa vipi? Mtakwenda kuangalia kama yanawafaa, basi ni vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi tuliyofanya siku ya leo, katika kuvumiliana Waziri hapa ameeleza kwamba Taifa letu limezoea kukubaliana na kuvumiliana. Kwa hiyo, utakuta tumepunguza muda wetu wa kazi kwa sababu ya kuwezesha shughuli zingine za ibada ziendelee kufanyika na ndiyo amani tunayoipata, hii inatokana na wenzetu hawa wanaofanya ibada. Kwa hiyo tuwe na tabia ya kuvumiliana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.03 Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 25 Julai 2012, Saa Tatu Asubuhi)*